

FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARIMIWA

UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!

PITIO LA AGANO JIPYA

MATHAYO - UFUNUO

NA BOB UTLEY,
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFAIRI
(UTAFASILI WA BIBLIA)

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS
2000 (Imehaririwa 2007)

ORODHA YA YALIYOMO

Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia.....	i
Somo la Ufunguzi	01
Utangulizi wa Mathayo	03
Utangulizi wa Marko	09
Utangulizi wa Luka	16
Utangulizi wa Yohana	25
Utangulizi wa Matendo ya Mitume	34
Utangulizi wa Warumi	45
Utangulizi wa 1 Wakorintho.....	50
Utangulizi wa 2 Wakorintho	58
Utangulizi wa Wagalatia	65
Utangulizi wa Waefeso	70
Utangulizi wa Wafilipi	80
Utangulizi wa Wakolosai.....	87
Utangulizi wa Barua kwa Wathesalonike.....	97
Utangulizi wa Nyaraka za Kichungaji:1 na 2 Timotheo na Tito.....	107
Utangulizi wa Tito	115
Utangulizi wa Filemoni.....	117
Utangulizi wa Waebrania.....	120
Utangulizi wa Yakobo.....	126
Utangulizi 1 Petro	131
Utangulizi wa 2 Petro.....	139
Utangulizi wa 1 Yohana.....	145
Utangulizi wa 2 Yohana na 3 Yohana	151
Utangulizi wa Yuda	153
Utangulizi wa Unabii wa Agano la Kale.....	159
Utangulizi wa Ufunuo	169

Kiambatisho cha Kwanza	181
Kiambatisho cha Pili	190
Kiambatisho cha Tatu	194

MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIO THIBITIKA

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11).

Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa. Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihita digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliunganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko. Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtazamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru, lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia!


Hivyo ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:

- (1) Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
- (2) Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
- (3) Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
 - a. Aina ya uwasilishaji (aia ya fasihi) inachaguliwa kuelezea ujumbe
 - b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
 - c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
 - d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
 - e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
 - f. Maneno yaliyochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Jifunze ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-historia wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu).

Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:



lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1)

shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya “mwitikio wa msomaji” (unamaanishwa nini kwangu). Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali.

Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: “Biblia inaangazia zaidi katika fasihi”. Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao.

Tunlazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

- (1) muundo wa kihistoria
- (2) mazingira ya fasihi
- (3) muundo wa kisarufi (vipashio)
- (4) matumizi ya maneno ya kisasa
- (5) vifungu sambamba vyenye kuhusiana

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasihi wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri.

Mizunguko mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasihi ufuatao:

- (1) Mzunguko wa kwanza wa usomaji
 - (a) Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti, kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
 - (i) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
 - (ii) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
 - (iii) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
 - (b) Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
 - (c) Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
 - (d) Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
 - i. Agano la kale
 - 1) Simulizi za waebrania
 - 2) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
 - 3) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
 - 4) Alama za siri za ki-sheria
 - ii. Agano jipya
 - 1) Simulizi (Injili, matendo)
 - 2) Hadithi za mafumbo (Injili)
 - 3) Barua/nyaraka

(2) Mzunguko pili wa usomaji

- (a) Soma kitabu kizima tena, ukitaifuta kufahamu mada muhimu au masomo.
- (b) Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
- (c) Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

(3) Mzunguko wa tatu wa usomaji.

- (a) Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
 - (b) Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
 - (i) Mwandishi
 - (ii) Tarehe
 - (iii) Wapokeaji
 - (iv) Kusudu mahsusi la uandishi
 - (v) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
 - (c) Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
 - (d) Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji
- (4) Mzunguko wa nne wa usomaji
- (a) Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
 - (b) angalia fasihi au muundo wa kisarufi
 - (i) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
 - (ii) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
 - (iii) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
 - (c) Taja vipengele vifuatavyo:-
 - (i) Istilahi muhimu
 - (ii) Istahili zisizo za kawaida
 - (iii) Muundo muhimu wa kisarufi
 - (iv) Maneno magumu, ibara, na sentesi
 - (d) Angalia njia muhimu zilizosambamba
 - (i) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
 - a) Vitabu vya thiolojia
 - b) Biblia za marejeo
 - c) Itifaki
 - (ii) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
 - (iii) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
 - (e) Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
 - (i) Soma biblia
 - (ii) Ensiklopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
 - (iii) Tanguzi za biblia
 - (iv) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama “uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi”.

Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki. Mtu hawezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!

Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji #3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee

aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema “asema Bwana” lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni “zetu” na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Biblia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafsiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafsiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

- (1) Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
- (2) Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
- (3) Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
- (4) Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
- (5) Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

- (1) Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *Scripture Twisting*, IVP, kr. 17-18

“Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni.”

- (2) Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti)* Uk.75:

Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.”

- (3) H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:

“Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.”

Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya “Mzunguko wa usomaji #3” angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
 - a. United Bible Society Greek Text. Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
 - b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
 - c. The New King James Version (NKJV)
 - d. The New Revised Standard Version (NRSV)
 - e. Today’s English Version (TEV)
 - f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuwiwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo.

Kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa “mada ya sentensi” au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuwiwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
 - a. Mazingira ya fasihi
 - b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
 - c. Habari za kisarufi
 - d. Usomaji wa neno
 - e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
 - a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa “Upokeaji wa Maandiko halisi”.
 - b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
 - c. The Today’s English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
 - d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi Kiyunani, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
 - a. Tofauti za mswada
 - b. Maana ya maneno mbadala
 - c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi
 - d. Maandiko tata yenye mana zaidi ya mbili
Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
7. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa sura hiyo.

Juzuu za Mwongozo wa Masomo (*Study Guide Commentary Volumes*) sasa zinapatikana:

- Vol. 0 Semina juu ya “Waweza Kuelewa Biblia”
 Vol. 1 Mtangulizi wa Kwanza wa Kikristo; Mathayo

- Vol. 2 Injili Kama Ilivyoandikwa na Marko: Marko na 1 & 2 Petro
- Vol. 3A Mwana Historia Aitwaye Luka: Injili Kama ilivyoandikwa na Luka (inapatikana mnamo 2003)
- Vol. 3B Mwana Historia Aitwaye Luka: Kitabu cha Matendo ya Mitume (inapatikana 2003)
- Vol. 4 Nyaraka na Barua za Wanafunzi Wapendwa: Injili ya Yohana, 1, 2 na 3 Yohana
- Vol. 5 Injili Kama Ilivyoandikwa na Paulo: Warumi
- Vol. 6 Nyaraka za Paulo kwa Kanisa lenye Misukosuko: 1 & 2 Wakorintho (inapatikana 2002)
- Vol. 7 Barua za kwanza za Paulo: Wagalatia na 1 & 2 Wathesalonike
- Vol. 8 Nyaraka za Paulo akiwa Gerezani: Wakolosai, Waefeso, Filemoni na Wafilipi
- Vol. 9 Safari ya Nne ya Paulo ya Umisionari: 1 Timotheo, Tito na 2 Timotheo
- Vol. 10 Ukuu wa Agano Jipya: Waebrania
- Vol. 11 Ndugu wa Kiukoo wa Yesu Wazungumza: Yakobo na Yuda
- Vol. 12 Tumaini katika Nyakati Ngumu—Pazia la Mwisho: Ufunuo
- Vol. 1AOT Namna Yote Yalivyoanza: Mwanzo 1-11

SOMO LA UFUNGUZI

I. MAANA ZA MANENO YATUMIKAYO MARA KWA MARA

A. MAJINA YA MUNGU

1. Bwana (YHWH /Kurios)
2. Mungu (Elohim /Theos)
3. Mwana wa Adamu
4. Mwana wa Mungu
5. Mwokozi
6. Yesu
7. Kristo

B. MAJINA YA MAANDIKO NA FASIRI

1. Andiko la Kimasoreti
2. Tafsiri ya Biblia ya Kiebrania ya Agano la Kale kwenda katika Kiyunani
3. Targums
4. Vulgate(Tafsiri ya Kiyunani)
5. Peshitta
6. Magombo ya Bahari ya Chumvi

C. FAHARASA YA MANENO (ANGALIA KIAMBATISHO CHA KWANZA)

D. UKOSOAJI WA KIMAANDIKO (ANGALIA KIAMBATISHO CHA PILI)

E. ISTILAHU ZA KISARUFI ZA KIYUNANI ZILIZO NA ATHARI KATIKA UFASIRI (ANGALIA KIAMBATISHO CHA TATU)

II. MPANGILIO WA MUDA WA MSINGI WA AGANO JIPYA

III. RAMANI YA MSINGI YA KARNE YA KWANZA YA ULIMWENGU WA MEDITERANIA

A. Vyanzo vya Maji

- | | |
|--------------------------|---------------------|
| 1. Bahari ya Mediterania | 4. Bahari ya Aegean |
| 2. Bahari Nyeusi | 5. Mto Nile |
| 3. Bahari ya Adriati | 6. Mto Yordani |

B. Nchi zilizotajwa katika Agano Jipya

- | | |
|-------------|---------------|
| 1. Misri | 10. Galatia |
| 2. Yudea | 11. Pamphilia |
| 3. Samaria | 12. Licia |
| 4. Dekapoli | 13. Asia |
| 5. Galilaya | 14. Bithynia |
| 6. Shamu | 15. Pontus |
| 7. Foenike | 16. Akaya |
| 8. Kilikia | 17. Makedonia |

9. Kapadokia

18. Illirikum

19. Italia

C. Visiwa vilivyotajwa katika Agano Jipya

1. Kipro
2. Krete
3. Patmo
4. Siliki
5. Malta

D. Miji Mikuu

1. Iskandria
2. Memphis
3. Yerusalemu
4. Antiokia
5. Tarso
6. Efeso
7. Pergamo
8. Korintho
9. Athene
10. Rumi
11. Thessalonike

UTANGULIZI WA MATHAYO

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Mpaka wakati wa Mageuzi Injili ya Mathayo ilifikiriwa kuwa injili ya kwanza (na bado ndivyo ilivyo kwa kanisa Katoliki la Kirumi).
- B. Ilinakiliwa zaidi, ikinukuliwa zaidi kama Injili katika Katekismusu na liturujia ya kwanza na kanisa kwa ajili ya karne mbili za kwanza.
- C. William Barclay katika *The First Three Gospels*, ukur. 19, alisema “Wakati tunapogeukia Mathayo, tunageukia kitabu ambacho kinaweza kuitwa nyaraka moja muhimu kuliko zote katika Imani ya Mkristo, kwa kuwa ndani yake tuna ukamilifu na simulizi iliyopangwa katika mfumo mzuri na mafundisho ya Yesu.” Hii ni kwasababu kilikuza mafundisho ya Yesu katika njia ya maudhui. Kilitumika kufundishia waongofu wapya (wote wawili Wayahudi na Mataifa) juu ya uzima na ujumbe wa Yesu wa Nazareti.
- D. Inatengeneza daraja la kimantiki kati ya Agano Jipya na Agano la Kale, kati ya waaminio wa Kiyahudi na waaminio wa Mataifa. Kilitumika Agano Kale katika ahadi/mbinu za kutimiliza kama ilivyofanyika katika mahubiri ya mwanzo ya Matendo ya Mitume *kerygma*. Agano la Kale linanukuliwa zaidi ya mara hamsini na kuelezwa mara nyingi zaidi. Pia, majina mengi na ufanano unaotumika juu ya YHWH anatumika kwa Yesu.
- E. Hivyo, makusudi ya Injili kulingana na Mathayo yalikuwa uinjilisti na uanafunzi, vipengele pacha wa Agizo Kuu (28:19-20).
 - 1. Walitakiwa kusaidia waongofu wapya wa Kiyahudi kwa kuwafahamisha wao juu ya maisha ya Yesu na mafundisho,
 - 2. Walitakiwa kufanya wanafunzi wote Wayahudi waaminio na Mataifa waaminio kwa namna watakiwavyo kuishi kama Wakristo.

II. UANDISHI

- A. Ingawa nakala za awali za Kiyunani za Agano Jipya (200-400 B.K.) zina maelezo “kulingana na Mathayo,” kitabu chenyewe hakina jina.
- B. Desturi mfanano za kanisa la kale ni kwamba Mathayo (pia ajulikanayo kama Lawi, kama vile Marko 2:14; Luka 5:27,29), mtoza ushuru (kama vile Mt. 9:9; 10:3) na mwanafunzi wa Yesu, aliandika Injili.
- C. Mathayo, Marko na Luka zinafanana sana:
 - 1. Wao mara kwa mara wanakubaliana katika mfumo juu ya nukuu ya Agano la Kale ambao unapatikana katika andiko la Kimasoteri wala Tafsiri ya Agano la Kale la Kiebrania kwenda Kiyunani,
 - 2. Wao mara kwa mara wanamnukea Yesu katika muundo wa kisarufi usio wa kawaida, hata kwa kutumia maneno nadra ya Kiyunani,
 - 3. wao mara kwa mara wanatumia tungo na hata sentensi za maneno sawia ya Kiyunani,

4. kidhahiri ukopaji wa kibayana umetokea.

D. Nadharia kadhaa zimekua kuhusu uhusiano kati ya Mathayo, Marko na Luka (Vitabu vya Injili Fupi).

1. Desturi zinazofanana za kanisa la kwanza ni kwamba Mathayo (Lawi), mkusanya ushuru na mwanafunzi wa Yesu, aliandika Injili. Mtume Mathayo alichukuliwa bila kujulikana kuwa mwandishi mpaka wakati wa Mageuzi.
2. Karibia 1776 A. E. Lessing (na baadaye Gieseler katika 1818), aliweka nadharia na jukwaa la mdomo katika ukuaji wa Injili (“kuona kwa pamoja”). Alielezea kwamba walikuwa wote wategemezi wa desturi za kwanza za kinywa ambazo waandishi walizirekebisha kwa ajili ya hadhira zao waliolengwa:
 - a. Mathayo: Wayahudi
 - b. Marko: Warumi
 - c. Luka: Mataifa

Kila moja ilikuwa ikihusiana na kituo tofauti cha kijiografia cha Ukristo

- a. Mathayo: Antiokia, Shamu
 - b. Marko: Rumi, Italia
 - c. Luka: Kaisaria Baharini, Palestina
 - d. Yohana: Efeso, Asia Ndogo
3. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa J. J. Griesbach aliweka nadharia kwamba Mathayo na Luka waliandika simulizi tofauti za maisha ya Yesu, zikiwa kila moja inajitegemea kila moja peke yake. Marko aliandika Injili fupi akijaribu kuleta upatanishi kati ya simulizi hizi mbili.
 4. Mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja H. J. Holtzmann alileta nadharia kwamba Marko ilikuwa Injili ya kwanza kuandikwa na kwamba wote Mathayo na Luka alitumia muundo wake wa Injili pamoja na nyaraka tofauti ikijumuisha misemo ya Yesu iitwayo Q (Lugha ya Kijerumani *quelle* au “chanzo”). Hii iliitwa nadharia ya “chanzo cha pili” (pia ilipitishwa na Fredrick Schleiermacher mnamo 1832).
 5. Baadaye B. H. Streeter alikuja na nadharia na kurekebisha “chanzo cha pili” kwa nadharia iitwayo “chanzo cha nne” nadharia ambayo ilipewa jina “Luka kwanza” pamoja na Marko pamoja na Q.
 6. Nadharia hapo juu ya uundaji wa Vitabu Injili ni madhania pekee. Hakuna ushahidi wa kihistoria wala wa maandiko halisi aidha ya chanzo “Q” au ya “Luka kwanza.” Uanazuoni wa kisasa haujui namna gani Injili zilikuzwa wala nani aliyeziandika (ukweli ni huo huo juu ya sheria ya Agano la Kale). Hata hivyo kukosa huku kwa taarifa hakuathiri mtazamo wa kanisa juu ya uvuvio wao au uaminifu kama nyaraka ya kihistoria pamoja na nyaraka ya imani pia.
 7. Kuna ufanano wa dhahiri katika muundo na maneno kati ya injili lakini kuna tofauti tofauti za kuogofya. Tofauti ziko wazi na zinafanana kwa usimulizi wa shuhuda wa macho. Kanisa la kwanza halikusumbuka na utofautiano wa simulizi hizi za ushuhuda wa macho wa maisha ya Yesu. Inaweza kuwa kwamba hadhira kusudiwa, staili ya mwandishi na lugha tofauti tofauti ilihusika (Kiaramu na Kiyunani) simulizi kwa kinachoonekana kuwepo kwa utofautiano. Lazima isemwe kwamba waandishi hawa waliovuviwa, wahariri au watunzi walikuwa na uhuru wa kuchagua, kupanga, kuasilisha na kuweka muhtasari matukio na mafundisho ya maisha ya Yesu (kama vile *How to Read the Bible for All Its Worth* cha Fee na Stuart, ukur. 113-148).

- E. Kuna desturi ya kanisa la kwanza kutoka kwa Papias, askofu wa Hierapolis (130 B.K), ambayo iliandikwa katika Eusebius' *Historical Ecclesiasticus* 3:39:16, kwamba Mathayo aliandika Kiaramu katika Injili yake. Hata hivyo, wanazuoni wa kisasa wamekataa desturi hii
1. Kiyunani cha Mathayo hakina tabia ya ufasiri kutoka kiaramu
 2. kuna mbinu za kimaneno za Kiyunani (kama vile 6:16; 21:41; 24:30)
 3. nukuu nyingi zaidi za Agano la Kale zinatoka katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiebrania katika Kiyunani (LXX) wala maandiko ya Kiebrania ya Kimasoteri
- Inawezekana kwamba 10:3 ni dokezo la uandishi wa Mathayo. Linaongeza "mkusanyaji wa kodi" kwenye jina lake. Maoni haya ya kujitegemea hayapatikani katika Marko. Mathayo pia hakuwa akijulikana katika Agano Jipya au kanisa la kwanza. Kwanini desturi nyingi zimekuzwa kwa jina lake na Injili hii ya kwanza ya Kitume?

III. TAREHE

- A. Kwa namna nyingi tarehe ya Injili inaunganisha tatizo la Injili. Ni injili gani iliyoandikwa kwanza na nani amekopa kwa nani?
1. Eusebius, katika *Historical Ecclesiasticus*, 3:39:15 alisema Mathayo alitumia Marko kama mwongozo wa muundo.
 2. Augustine, hata hivyo alimuita Marko "mfuasi wa kambi" na mfupishaji wa Mathayo.
- B. Mjongeo mzuri zaidi ungekuwa kujaribu kuweka mipaka ya tarehe inayowezekana
1. Lazima iliandikwa kabla ya mwaka 96 B.K au 115
 - a. Clement wa Rumi (96 B.K) alielezea Injili ya Mathayo katika barua yake kwa Wakorintho.
 - b. Ignatius (110-115 B.K.), Askofu wa Antiokia, alinukuu Mathayo 3:15 katika barua yake *To the Smyrneans*, 1:1
 2. Swali gumu zaidi ni mapema namna gani ingeandikwa?
 - a. Kidhahiri baada ya matukio yaliyoandikwa ingekuwa kati ya miaka ya 30
 - b. wakati mwingine ilitakiwa kupita mahitaji yake, utungwaji na mzunguko
 - c. Kuna uhusiano gani wa sura ya 24 na uharibifu wa Yerusalemu mnamo mwaka 70 B.K.? Sehemu ya Mathayo inamaanisha mfumo wa utoaji sadaka ulikuwa bado unaendelea (5:23-24; 12:5-7; 17:24-27; 26:60-61). Hii inamaanisha tarehe kabla ya mwaka 70 B.K.
 - d. ikiwa Mathayo na Marko viliandikwa wakati wa huduma ya Paulo (48-68 B.K.) kwanini hakuwahi kuwarejerea? Irenaeus ananukuliwa na Eusebius katika *Historical Ecclesiasticus* 5:8:2, kusema kwamba Mathayo aliandika Injili yake wakati Petro na Paulo walikuwa Rumi. Petro na Paulo waliuwawa wote wakati wa utawala wa Nero ambao uliishia mnamo mwaka 68 B.K
 - e. Dhanio la wanazuoni wa kisasa la mwanzoni kabisa ni mwaka 50 B.K
- C. Wasomi wengi wanaamini kwamba Injili nne zina uhusiano zaidi wa vituo vya Kijiografia vya Ukristo kuliko waandishi wa kidesturi. Mathayo inaweza kuwa imeandikwa kutokea Antiokia ya Shamu, kwasababu ya mambo yake ya kanisa la Kiyahudi/Kimataifa mnamo mwaka wa 60 B.K. au angalau kabla ya mwaka 70 B.K.

IV. WAPOKEAJI

- A. Kama uandishi na tarehe ya Injili havina uhakika, hivyo pia wapokeaji wake. Inaonekana kuwa bora zaidi kuhusiana kwa wote Wayahudi waaminio na Mataifa. Kanisa huko Antiokia ya Shamu ya karne ya kwanza inashabihiana na wasifu huu zaidi.
- B. Origen ananukuliwa Eusebius katika *Historical Ecclesiasticus* 6:25:4, kwamba kiliandikwa kwa ajili ya Wayahudi waaminio.

V. UANISHI WA KIMUUNDO

- A. Namna gani Injili hii imeundwa? Mtu anaweza kutafuta kusudio la mwandishi wa asili aliyevuviwa kwa kuchambua muundo wa kitabu kizima.
- B. Wasomi wamependekeza miundo kadhaa
 - 1. safari za kijiografia za Yesu
 - a. Galilaya
 - b. kaskazini mwa Galilaya
 - c. Perea na Yudea (wakati akisafiri kuelekea huko Yerusalemu)
 - d. katika Yerusalemu
 - 2. Vipengele vitano vya kimaudhui vya Mathayo. Vinatambuliwa kwa tungo inayojirudia rudia “Na wakati Yesu alikuwa amemaliza vitu hivi” (kama vile 7:28; 11:1; 13:53; 19:1; 26:1). Wasomi wengi wanaona vipengele hivi vitano kama jaribio la Mathayo kumuelezea Yesu kama “Musa mpya,” pamoja na kila kipengele kikiwa na ufanano na moja ya vitabu vitano vya (Mwa., Kut., Hes., Kumb.)
 - a. muundo usiosawia ambao unacheza kati ya simulizi na sehemu za mahubiri
 - b. mfumo wa kithiolojia/kimaisha ambao unachukua tungo inayojirudia rudia “kutokea muda huo Yesu alianza. . .” (kama vile 4:17; 16:21) hivyo kugawa kitabu katika sehemu tatu (1:1-4:16; 4:17-16:20; na 16:21-28:29)
 - c. msisitizo wa Mathayo wa vifungu vya utabiri wa Agano la Kale kwa matumizi ya maneno ya msingi “kutimilizwa” (kama vile 1:22; 2:15,17,23; 4:14; 8:17; 12:17; 13:35; 21:4; 27:9 na 27:35).
- C. Ile “injili” ni aina ya uwasilishaji ya kipekee ya kifasihi. Vyenyewe sio simulizi za maisha. Sio simulizi za kihistoria. Vina ubaguzi kithiolojia, vikiwa na muundo wa aina ya kifasihi. Kila waandishi wa Injili walichagua kutoka matukio ya maisha na mafundisho ya Yesu ili kumuwasilisha Kwake kipekee kwa hadhira wake waliokusudiwa. Injili zilikuwa machapisho ya kiinjilisti.

VI. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

- 1. Masihi, 1:1
- 2. Bikra, 1:23,25
- 3. Immanueli, 1:23
- 4. Mama jusi, 2:1
- 5. Mnazareti, 2:23
- 6. Tubuni, 3:2
- 7. Kiri, 3:6
- 8. Mafarisayo, 3:7
- 9. Masadukayo, 3:7

10. "akaondoa viatu Vyake," 3:11
11. "Huyu ndiye Mwanangu Mpendwa," 3:17
12. "juu ya hekalu," 4:5
13. "Sheria au Manabii," 5:17
14. "talaka," 5:31
15. "mahali pa kuwekea Miguu," 5:35
16. sinagogi, 6:2
17. "mlango mwembamba," 7:13
18. mwandishi, 8:19
19. "mwenye kupagawa na pepo," 8:28
20. "kuketi mezani," 9:10
21. viriba, 9:17
22. wapiga filimbi, 9:23
23. mitume, 10:2
24. nira, 11:29,30
25. "ulimwengu huu wa sasa wala ujao," 12:32
26. mfano, 13:3
27. magugu, 13:25
28. "desturi za wazee," 15:2
29. kuzimu, 16:18
30. akageuka sura, 17:2
31. hupagawa, 17:15
32. "watozao nusu-shekeli," 17:24
33. dinari, 20:2,9
34. Hosanna ikimaanisha "tuokoe sasa," Kiaramu, "nguvu za kifalme kwa" , 21:9
35. "utungu," 24:8
36. "chukizo la uharibifu" 26:64
37. talanta, 25:20
38. "baraza zima," 26:59
39. "kuja mawinguni kwa mbingu," 26:64
40. "Konde la Damu," 27:8
41. Praitorio, 27:27
42. "Golgotha," 27:33
43. "baadhi yao waliona shaka," 28:17

VII. WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

1. Zerubabeli, 1:12
2. Herode, 2:13
3. Mwana wa Daudi, 9:27
4. Mwana wa Adamu, 10:23
5. Mtumishi wangu, 12:18
6. Beelzebuli, 12:24
7. Herodia, 14:6
8. Simoni Bar-yona, 16:17
9. "makuhani wakuu na wazee," 21:23

10. Maherodia, 22:16
11. Rabbi(Mwalimu), 23:7
12. Kayafa, 26:3
13. Pilato, 27:2
14. Barabba, 27:16
15. Maria Magdalena, 27:56
16. Yusufu wa Arimathaya, 27:57

VIII. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Betlehemu, 2:1
2. Jangwa la Yudea, 3:1
3. Galilaya, 3:13
4. Nazareti, 4:13
5. Kapernaumu, 4:13
6. Sodoma na Gomora, 10:15
7. Bethsaida, 11:21
8. Sidoni, 15:21
9. Kaisaria Filipi, 16:13
10. Mlima Mzeituni, 21:2
11. Gethsemane, 26:36

IX. MASWALI YA MJADALA

1. Kwanini vizazi vya Mathayo na Luka vinatofautiana?
2. Tamari, Rahabu, na Ruthu wana vitu gani vinavyofanana?
3. Eliya na Yohana Mbatizaji wana vitu gani vinavyofanana?
4. Nini maana ya “ufalme wa mbinguni”?
5. Ni nini hasa ambacho Shetani alikuwa akimjaribu Yesu kufanya jangwani?
6. Elezea 5:17 kwa maneno yako mwenyewe.
7. Elezea 5:48 kwa maneno yako mwenyewe.
8. Elezea 7:6 kwa maneno yako mwenyewe.
9. Kwanini 8:5-13 sio kawaida na yenye umuhimu hivyo?
10. Elezea 10:38 kwa maneno yako mwenyewe.
11. Elezea 10:19 kwa maneno yako mwenyewe.
12. Kwanini Yesu aliponya siku ya Sabatho?
13. Kwanini kukufuru ni kwenda kinyume na Roho? (12:31-32)
14. Uotaji wa mbegu unahusiana vipi na uzaaji matunda katika mfano wa mpanzi? (13)
15. Elezea 13:44 kwa maneno yako mwenyewe.
16. Elezea 15:11 kwa maneno yako mwenyewe.
17. Elezea 16:20 kwa maneno yako mwenyewe.
18. Elezea 18:8 kwa maneno yako mwenyewe.
19. Je kila mwamini ana malaika mlinzi?
20. Elezea 19:17 kwa kuhusianisha na Yesu kuwa Mwana wa Mungu.
21. Elezea 21:18-19 kwa maneno yako mwenyewe.
22. Kwa nini Yesu alizungumza kwa ukali kwa waandishi na Mafarisayo katika sura ya 23?
23. Ni nini umuhimu wa 24:36?

UTANGULIZI WA MARKO

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Kanisa la kale siku zote walipuuzia kunakiri, kujifunza na kufundisha Marko katika rejea za Mathayo na Luka kwasababu waliona Marko kama toleo la “pitio la msomaji” (yaani, injili iliyofupishwa), mtazamo ambao hasa ulisemwa na Augustine.
- B. Marko mara kwa mara hainukuliwi na kanisa la kale la Kiyunani au wapingaji wa karne ya pili (walinzi wa imani).
- C. Tokea kukua kwa mjongeo wa kisasa wa kihistoria-kisarufi kwa ufasiri wa Kibiblia. Wote Mathayo na Luka wanatumia katika uwasilishaji wao wa maisha ya Yesu na umuhimu wake. Hivyo Marko inakuwa nyaraka ya kimsingi, ya kwanza rasmi inayosimulia maisha ya Yesu.

II. AINA YA UWASILISHAJI

- A. Injili sio simulizi za maisha za kisasa au historia. Ni maandiko ya kibaguzi ya kithiolojia yaliyotumika kumtambulisha Yesu kwa hadhira mbali mbali na kuwaleta katika imani kwake. Zenyewe ni simulizi za “habari njema” za maisha ya Yesu kwa makusudi ya uinjilisti (kama vile Yohana 20:30-31).
- B. Marko inazungumzia mazingira manne tofauti tofauti ya kihistoria na makusudi manne ya kithiolojia
 - 1. maisha na mafundisho ya Yesu
 - 2. maisha na huduma ya Petro
 - 3. mahitaji ya kanisa la kwanza
 - 4. makusudi ya kiinjilisti ya Yohana Marko
- C. Injili nne ni za kipekee katika fasihi ya Mashariki ya Karibu na Uyunani-Rumi. Waandishi waliovuviwa walikuwa na jukumu la kuongozwa na Roho ya kuchagua mafundisho ya Yesu na matendo ambayo kwa uwazi yalifunua tabia Yake na/au kusudi.

Walipanga maneno haya na matendo katika njia mbali mbali. Mfano mmoja ungekuwa kulinganisha Mahubiri ya Mathayo katika Mlima (Mt. 5-7) pamoja na Mahubiri ya Luka katika uwanda. Inakuwa dhahiri kwamba Mathayo vili jaribu kukusanya mafundisho yote ya Yesu katika hubiri moja ndefu, wakati Luka alisambaza mafundisho haya haya katika Injili yake. Kitu hiki hiki kingeweza kusemwa juu ya Mathayo kuweka miujiza ya Yesu pamoja wakati Luka anaeneza katika Injili yake nzima.

Hii inamaanisha uwezo wa waandishi wa Injili sio tu wa kuchagua na kupangilia mafundisho ya Yesu bali pia kuyaasilisha kwa ajili ya makusudi yake ya kithiolojia (soma Fee na Stuart's *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 113-134). Wakati ukisoma Injili mtu lazima aendelee kuuliza hoja ya kithiolojia waliyokuwa wakijaribu kuielezea waandishi hawa. Kwanini wajumuishe tukio hili hasa, muujiza na somo?

- D. Injili ya Marko ni mfano mzuri wa Koine ya Kiyunani kama lugha ya pili ya watu wa ulimwengu wa kimediterania. Lugha mama ya Marko ilikuwa Kiaramu (kama milivyokuwa kwa Yesu na Wayahudi wote katika karne ya kwanza). Ladha ya Kisemiti ni tabia ya Injili ya Marko.

III. UANDISHI

- A. Yohana Marko kidesturi amekuwa akitambuliwa na mtume Petro katika uandishi wa Injili hii. Kazi yenyewe (kama Injili zote) haina jina.
- B. Ushahidi mwingine wa simulizi ya ushuhuda wa macho wa Petro haiandiki matukio maalumu matatu ambayo Petro mwenyewe alihusika.
1. kutembea kwake juu ya maji (kama vile Mt. 14:28-33)
 2. yeye kuwa msemaji huko Kaisaria Filipi kwa ajili ya Imani ya Kumi na Mbili (kama vile Mt. 16:13-20), katika Marko pekee 8:27-30 na “juu ya mwamba huu” na vifungu vya “funguo za ufalme” vimeondolewa.
 3. kupatikana kwa kodi ya hekalu kwa ajili yake mwenye na Yesu (kama vile Mt. 17:24-27)
- Yawezekana upole wa Petro ulimchochea kutosisitiza matukio haya katika mahubiri haya .
- C. Desturi za kale za Kanisa
1. I Clement, ikiandikwa toka Rumi mnamo mwaka 95 B.K, alielezea Marko (kama inavyoandikwa kwa *Shepherd of Hermes*).
 2. Papias, askofu wa Hierapoli (mnamo mwaka 130 B.K.), aliandika *Interpretation of the Lord's Sayings*, ambayo inanukuliwa na Eusebius (275-339 B.K.) katika barua yake *Ecclesiastical History* 3.39.15. Alielezea kwamba Marko alikuwa mfasiri wa Petro aliyenukuu kwa uhakika, lakini sio kwa mtiririko, kumbukumbu ya Petro ya Yesu. Inavyoonekana Marko alichukua na kuasilisha mahubiri ya Petro na kuwapanga katika uwasilishaji wa Injili. Papias alidai kupokea taarifa hii kutoka kwa “wazee,” ambayo iliyorejea kwa Mtume Yohana.
 3. Justin Martyr (150 B.K.), katika kunukuu Marko 3:17, inaongeza kwamba inatoka kwa kumbukumbu za Petro.
 4. Dibaji ya Anti-Marcionite kwa Marko, iliyoandikwa mnamo mwaka 180 B.K., inatambua Petro kama shuhuda wa macho wa Injili ya Marko. Pia inataja kwamba Marko aliandika Injili kutokea Italia baada ya kifo cha Petro (kidesturi katika Rumi mnamo mwaka 65 B.K.).
 5. Irenaeus, aliandika mnamo mwaka 180 B.K., anamtaja Yohana Marko kama mfasiri wa Petro na mtunzi wa kumbukumbu zake baada ya kifo chake (kama vile *Contra Haereses* 3:1:2).
 6. Clement wa Iskandria (195 B.K.) anaelezea kwamba wote waliosikia Petro akihubiri katika Rumi alimuuliza Marko kuandika mahubiri haya.
 7. Ie Muratorian Fragment (yaani uidhinishaji), iliyoandikwa mnamo mwaka 200 B.K. kutoka Rumi, ingawa andiko limekamilika, inaonekana kukiri kumbukumbu za mahubiri ya Petro.
 8. Tertullian (200 B.K.) katika *Against Marcion* (4:5) inasema Marko amechapisha kumbukumbu ya Petro.
 9. Katika *The Expositor's Bible Commentary* Vol. 8, ukur. 606, Walter Wessel anatengeneza maoni ya kushangaza kwamba desturi za kanisa la kwanza zinatoka katika vituo vya makanisa tofauti tofauti kijiografia
 - a. Papias kutoka Asia Ndogo
 - b. Dibaji ya Anti-Marcion na Muratorian Fragment
 - c. Irenaeus (kama vile *Adv. Haer.* 3.1.1) kutoka Lyons huko Ufaransa. Desturi za Irenaeus pia zinapatikana katika Tertullian (kama vile *Adv. Marc.* 4.5) kutoka Afrika kaskazini na

Clement wa Iskandria, Misri (kama vile *Hypotyposeis* 6 ikinukuliwa Eusebius, *Eccl. His.* 2.15.1-2; 3.24.5-8; 6:14:6-7). Huu utofautiano wa kijiografia unatoa sifa kwa uaminifu wake kwasababu ya desturi pana ya ukubalifu katika Ukristo wa mwanzo.

10. Kulingana na Eusebius' *Eccl. His.* 4:25, Origen (230 B.K) katika *Commentary on Matthew* (hakuna fasiri ijulikanayo juu ya Marko na Yeyote mpaka karne ya tano) anasema Marko aliandika Injili kama Petro alivyoeleza kwake yeye.
11. Eusebius mwenyewe anajadili Injili ya Marko katika *Eccl. His.* 2.15 na kusema Marko aliandika mahubiri ya Petro kwa ombi la wale walioyasikia ili kwamba yawe yakisomwa katika makanisa yote. Eusebius anajikita katika desturi hii katika maandiko ya Clement wa Iskandria.

D. Tunajua nini kuhusu Yohana Marko

1. Mama yake alikuwa mwamini aliyejulikana huko Yerusalemu na ambaye kanisa lilikutana nyumbani mwake (yawezekana usiku wa Karamu ya Bwana, kama vile Marko 14:14-15; Mdo. 1:13-14; Mdo. 12:12). Alikuwa mtu asiye na jina aliyekimbia kutoka Gethsemane (Marko 14:51-52).
2. Alikuwa amesindikizwa na Mjomba wake Barnaba (kama vile Kol. 4:10) na Paulo Antiokia kutokea Yerusalemu (Mdo. 12:25).
3. Alikuwa mwenza wa Barnaba na Paulo katika safari yao ya kwanza ya kimisionari (Mdo. 13:5), lakini alirudi nyumbani ghafla (Mdo. 13:13).
4. Baadaye Barnaba alitaka kumchukua Marko katika safari yake ya pili ya kimisionari, lakini hii ilisababisha kutoeleweka kwa ajabu kati ya Barnaba na Paulo (Mdo. 15:37-40).
5. Baadaye aliunganishwa na Paulo na kuwa rafiki na mhudumu mwenza (Kol. 4:10; II Tim. 4:11; Filemoni 24).
6. Alikuwa mwenza na mhudumu mwenza pamoja na Petro (1 Pet. 5:13), yawezekana huko Rumi.

- E. Elimu yake binafsi ya maisha ya Yesu inaonekana kuthibitishwa na 14:51-52, ambapo jamaa anakimbia uchi kutoka Gethsemane mara baada ya kukamatwa kwa Yesu. Maelezo haya yasiyo kawaida kabisa yanaonekana kuaksi tajiriba binafsi ya Paulo.

IV. TAREHE

- A. Injili ni simulizi ya ushuhuda wa macho na ufasiri wa maisha, matendo na mafundisho ya Yesu yanayoonekana kuchukuliwa kutoka katika mahubiri ya Petro. Yalikusanywa na kutungwa na kusambazwa baada ya kifo chake, ndivyo pia isemavyo Dibaji ya Anti-Marcionite na Irenaeus (ambao wanaongeza pia baada ya kifo cha Paulo). Petro na Paulo waliuwawa kama wafia dini chini ya utawala wa Nero (54-68 B.K.) huko Rumi (desturi za kanisa). Tarehe kamili hazijulikani lakini ikiwa ni kweli, hivyo yawezekana tarehe ya Marko ilikuwa kati ya miaka ya sitini.
- B. Inawezekana kwamba Dibaji ya Anti-Marcionite na Irenaeus hairejerei kifo cha Petro bali kuondoka kwake (yaani, kutoka) kutoka Rumi. Kuna baadhi ya ushahidi wa kidesturi (yaani Justin na Hippolytus) kwamba Petro alitembelea Rumi wakati wa utawala wa Claudius (41 mpaka 54 B.K.), (Eusebius' *Eccl. His.* 2.14.6).

- C. Inaonekana kwamba Luka anahitimisha Matendo ya Paulo bado yuko gerezeni katika miaka ya sitini. Ikiwa ni kweli kwamba Luka alitumia Marko katika Injili yake, hivyo lazima itakuwa kiliandikwa kabla ya Matendo ya Mitume na, hivyo mapema zaidi kuliko mwanzoni mwa sitini.
- D. Uandishi na tarehe ya Marko kwa namna yoyote haiathiri kweli ya Injili ya kihistoria, kithiolojia na kiinjilisti (au yeyote). Yesu, si mwandishi wa kibinadamu, ndiyo msingi!
- E. Inashangaza kwamba hakuna Injili mojawapo (hata Yohana, iliandikwa mnamo mwaka 95-96 B.K) inarejerea au inaeleza uharibifu wa Yerusalemu (kama vile Mt. 24; Marko 13; Luka 21) mnamo mwaka 70 B.K. na kamanda wa Kirumi, baadaye Mfalme, Titus. Marko yawezekana iliandikwa kabla ya tukio hili. Hata inawezekana kwamba Mathayo na Luka viliandikwa kabla ya hukumu kuu juu ya Dini ya Kiyahudi. Inatakiwa isemwe tarehe kamili kwa ajili ya utungwaji wa Vitabu vya Injili hazijulikani kwa wakati huu (kama ilivyo uhusiano wao wa kifasihi kwa zenyewe).

V. WAPOKEAJI

- A. Marko anaunganishwa na Rumi na waandishi wa kanisa la kwanza
 - 1. 1 Petro 5:13
 - 2. Dibaji ya Anti-Marcionite (Italia)
 - 3. Irenaeus (Rumi, kama vile *Adv. Haer.* 3.1.2)
 - 4. Clement wa Iskandria (Rumi, kama Eusebius *Eccl. Hist.* 4.14.6-7; 6.14.5-7)
- B. Marko haiweki bayana kusudi lake katika kuandika Injili. Kunawezekana kukawa na nadharia kadhaa.
 - 1. kipande cha maandiko cha kiinjilisti (kama vile 1:1) kikiandikwa hasa kwa Warumi (kama vile 1:15; 10:45)
 - a. vipengele vya Kiyahudi vikifasiriwa (kama vile 7:3-4; 14:12; 15:42)
 - b. maneno ya Kiaramu yakifasiriwa (kama vile 3:17; 5:41; 7:1,34; 10:46; 14:36; 15:22,34)
 - c. matumizi ya maneno mengi ya Kilatini kama vile, mnyongaji, 6:27; sextanus, 7:4; sensa, 12:14; nusu-pesa, 12:42; praitorio, 15:16; akida, 15:39; maandalio, 15:42)
 - d. lugha jumuishi kuhusiana na Yesu
 - (1) lugha jumuishi ikihusiana na wale wa Palestina (kama vile 1:5,28,33,39; 2:13; 4:1; 6:33,39,41,55)
 - (2) lugha jumuishi ikihusiana na watu wote (kama vile 13:10)
 - 2. mateso yakifuata moto katika Rumi mnamo mwaka 64B.K., ambalo Nero aliwalaumu Wakristo, akianzisha wimbi la mateso kwa waaminio. Marko mara kwa mara anataja mateso (kama vile mateso ya Yesu 8:31; 9:39; 10:33-34,45 na mateso ya wafuasi wake 8:34-38; 10:21,30,35-44).
 - 3. kuchelewa kwake kwa Kurudi Mara ya Pili
 - 4. kufa kwa mashuhuda wa macho wa Yesu, hasa mitume
 - 5. kuinuka kwa uzushi ndani ya makanisa ya Wakristo yaliyokuwa yameenea
 - a. Wana dini ya Kiyahudi (Wagalatia)
 - b. Walimu wa uongo (1 Yohana)
 - c. muunganiko wa a. na b. (yaani, Wakolosai na Waefeso; 2 Pet. 2)

VI. UANISHAJI WA MUUNDO

- A. Marko kimeundwa kwa namna ambayo Juma la mwisho la maisha ya Yesu ni shabaha zaidi ya moja ya tatu ya kitabu. Umuhimu wa kithiolojia wa Juma la Mateso iko wazi.
- B. Kwakuwa Marko, kulingana na desturi za kanisa, ilichukuliwa na mahubiri ya Petro, (yaani yawezekana katika Rumi) inakuwa wazi kwanini hakuna simulizi ya kuzaliwa zilizojumuishwa. Marko anaanzia ambapo uzoefu wa Petro unaanzia, Yesu akiwa ni mtu mzima tayari na inahusiana kithiolojia na ujumbe wa Yohana Mbatizaji juu ya Toba na imani katika kuandaa kazi ya Masihi. Mahubiri ya Petro lazima yalitumia dhana za “Mwana wa Adamu” na “Mwana wa Mungu.” Injili inaaksi thiolojia yake yesu mwenyewe ya utu wa Yesu. Mwanzoni alikuwa mwalimu mkuu na mponyaji, lakini baadaye akawa Masihi! Masihi huyu hakuwa anatarajiwa kutawala kama kamanda wa Kijeshi bali Mtumwa atesekaye (kama vile Isaya 53).
- C. Uaninishi wa kimsingi wa kijiografia wa Marko unashirikishwa na Vitabu vingine vya Injili (yaani, Mathayo na Luka)
1. huduma ya Galilaya (1:14-6:13)
 2. huduma nje ya Galilaya (6:14-8:30)
 3. safari ya Yerusalemu (8:31-10:52)
 4. juma la mwisho katika maeneo ya Yerusalemu (11:1-16:8)
- D. Hata inawezekana kwamba muundo wa Marko unafuatisha utaratibu wa msingi wa mahubiri ya kwanza ya Kitume (yaani, Mdo. 10:37-43, kama vile C. H. Dodd’s *New Testament Studies* ukur. 1-11). Ikiwa hii ndiyo kweli hivyo Injili zilizoandikwa ni hitimisho la kipindi cha desturi za kinywa (yaani, *kerygma*). Dini ya Kiyahudi ilichukulia mafundisho ya kinywa kuwa kuu kwa maandiko ya kuandikwa.
- E. Marko na wasifu na simulizi za haraka (yaani, “ghafila,” kama vile 1:10) ya maisha ya Yesu. Marko haiweki kumbukumbu vipindi virefu vya mafundisho kutoka tukio mpaka tukio (yaani, matumizi ya kurudiwa “ghafila”). Injili ya Marko inamfunua Yesu na matendo Yake. Hata hivyo, simulizi hii ya haraka inatengenezwa na maelezo ya ushuhuda wa macho (yaani Petro).

VII. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. ubatizo wa toba, 1:4
2. akivaa singa za ngamia, 1:5
3. kama hua, 1:10
4. siku arobaini, 1:13
5. ufalme wa Mungu umekaribia, 1:15
6. sinagogi, 1:23
7. kufuru, 2:7
8. waandishi, 2:6
9. viriba, 2:22
10. mifano, 4:2
11. vazi, 5:27
12. chachu ya mafarisayo, 8:15
13. rudi nyuma yangu shetani, 8:33
14. akageuka, 9:2

15. kuzimu (Gehenna), 9:47
16. nyumba ya sala kwa mataifa yote, 11:17
17. denari, 12:15
18. pasaka, 14:1
19. nardo, 14:3
20. kikombe hiki, 14:36
21. saa imefika, 14:41
22. Siku ya Maandalizi, 15:42
23. siku ya kwanza ya Juma, 16:2

VIII. WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

1. Simoni, 1:16
2. Zebedayo, 1:20
3. roho mchafu, 1:23
4. Lawi, 2:14
5. biathari, 2:26
6. Mkananayo, 3:18
7. Beelzebuli, 3:22
8. Legioni, 5:9
9. Mfalme Herode, 6:14
10. Herodia, 6:17
11. Msirofoinike, 7:26
12. Bartimayo, 10:46
13. Kaisari, 12:14
14. chukizo la uharibifu, 13:14
15. wateule, 13:20
16. Kristo wa uongo, 13:22
17. makuhani wakuu, 14:1
18. Abba, 14:36
19. Baraza, 14:55
20. Barabba, 15:7, 11
21. Simoni Mkirene, 15:21
22. Salome, 15:40
23. akida, 15:45

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Yudea, 1:4
2. Yerusalemu, 1:4
3. Mto Yordani, 1:5
4. Nazareti, 1:9
5. Galilaya, 1:9
6. Kapernaumu, 1:21
7. Idumaya, 3:8
8. Tiro, 3:8
9. Sidoni, 3:8

10. Wagerasi, 5:1
11. Dekapoli, 5:20
12. Bethsaida, 6:45
13. Dalmanutha, 8:10
14. Yeriko, 10:46
15. Mlima Mzeituni, 11:1
16. Gethsemane, 14:32

X. MASWALI YA MJADALA

1. Ubatizo wa Roho ni nini? (1:8)
2. Nini mahitaji ya agano jipya? (1:15)
3. Kwa nini wasikilizaji wa Yesu walishangazwa na mahubiri yake? (1:22)
4. Kwanini Yesu hakuruhusu mapepo kuzungumza? (1:34)
5. Kwanini Yesu aliwaambia walioponywa wasiwaambie wengine? (1:43)
6. Kwanini Yesu alishutumiwa kwa kukufuru katika sura ya 2?
7. Elezea 2:17 kwa maneno yako mwenyewe.
8. Kwanini Yesu aliponya siku ya Sabato mara nyingi mara kwa mara?
9. Kwanini Yesu alifundisha kwa mifano? (3:10-13)
10. Elezea mfano wa udongo kwa maneno yako mwenyewe (4:3-9).
11. Kwanini Yesu hakufanya miujiza mingi katika mji wake mwenyewe alipozaliwa? (6:4-6)
12. Kwanini Yesu alitembea juu ya maji katika sura ya 6?
13. Elezea unabii wa Isaya katika 7:6-7.
14. Elezea 7:15 kwa maneno yako mwenyewe.
15. Kwanini Marko ananukuu maneno ya Yesu ya Kiaramu?
16. Elezea 8:38 kwa maneno yako mwenyewe.
17. Kwanini Mafarisayo wanamuuliza Yesu juu ya talaka katika sura ya 10?
18. Kwanini wanafunzi walishangaa (10:26) juu ya kile Yesu alichosema katika 10:25?
19. Kwanini Yesu alipanda juu ya mwana punda katika sura ya 11?
20. Kwanini Yesu alisafisha hekalu katika sura ya 11?
21. Kwanini 11:28 ni swali muhimu sana?
22. Kwanini mfano mwanzoni mwa sura ya 12 ni wenye nguvu na unarejerea kwa nani?
23. Amri gani iliyo kuu zaidi kuzidi zote katika Agano la Kale?
24. Kwanini 13:30 ni ngumu sana kuifasiri?
25. Elezea 15:34 kwa maneno yako mwenyewe.

UTANGULIZI WA LUKA

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Luka ni injili ndefu kuliko zote. Luka-Matendo ya Mitume (ikiwa mtu atakataa Waebrania kama nyaraka ya Paulo) inajumuisha kurasa nyingi zaidi za karatasi kuwahi kufanywa na mwandishi yeyote wa Agano Jipya na ni Mkristo Mmataifa wa kizazi cha Pili cha wakristo!
- B. Luka anaandika Koine ya Kiyunani iliyo bora zaidi kuliko waandishi wengine wa Agano Jipya kukiwa na utofauti mkubwa wa mwandishi wa Waebrania. Kiyunani inavyoonekana ilikuwa lugha yake mama. Alikuwa mtu mwenye elimu kubwa sana na Tabibu (kama vile Kol. 4:14).
- C. Luka anaelezea upendo wa Yesu na kujali kwa wale ambao viongozi wa Kiyahudi hawakuwahi hata kutambua:
 - 1. wanawake (mfano, Maria, Elizabeti, Anna, Maria na Martha, n.k)
 - 2. masikini (kama vile Heri za Luka, Luka 6:20-23 na mafundisho juu ya mali, kama vile 12:13-21; 16:9-13,19-31)
 - 3. watu waliotengwa na kuchukiwa kijamii, kikabila na kidini
 - a. wanawake wasio na maadili (kama vile 7:36-50)
 - b. Wasamaria (kama vile 9:51-56; 10:29-37; 17:11-16)
 - c. viwete (kama vile 17:11-19)
 - d. watoza ushuru (kama vile 3:12-13; 18:9-14;19:1-10)
 - e. wahalifu (kama vile 23:35-43)
- D. Luka anaandika kumbukumbu zenye ushuhuda wa macho za Maria (yaani sura mbili za kwanza za Matendo ya Mitume) na pia uzao unaowezakuwa ni wake (yaani 3:23-38). Injili ya Luka inaandika mambo yanayomgusa Yesu kwa wote Wayahudi na Mataifa.

II. MWANDISHI

- A. Desturi za kanisa la kwanza zisizokuwa na jina
 - 1. Irenaeus (175-195 B.K., *Against Heresies*, 3.1.1; 3.14.10) anasema hasa kwamba Luka iliandika katika kitabu cha Injili iliyohubiriwa na Paulo.
 - 2. Dibaji ya Anti-Marcion juu ya Luka (175 B.K.) inasema kwamba Luka alikuwa mwandishi wa Injili.
 - 3. Tertullian (150-160-220/240 B.K. katika *Against Marcion* 4:2,3; 4: 5,3) anasema kwamba Luka aliandika chapisho ya injili ya Paulo
 - 4. Muratorian Fragment (180-200 B.K.) inataja jina Luka kama mwandishi na kumuita tabibu mwenza wa Paulo. Pia linasema kwamba aliandika masimulizi yake kwa kusikia kilichokuwa kinasemwa tu (ikimaanisha, aliwahoji mashuhuda).
 - 5. Origen, alinukuliwa na Eusebius kutoka katika fasiri yake juu ya Mathayo (*Hist. Eccl.* 6.25.6), anaelezea uandishi wa Luka wa Injili.
 - 6. Eusebius (*Hist. Eccl.* 3.4.2,6-7) pia anakiri uandishi wa Luka wa Injili zote za Luka na Matendo ya Mitume.
- B. Ushahidi wa ndani wa uandishi wa Luka

1. Injili hii kama kazi nyingine nyingi za Kibiblia, haina jina
2. Ikiwa Luka-Matendo ya Mitume ni seti mbili za juzuu, ambayo inaonekana kuwa kweli kutokana na utangulizi wake unaofanana, hivyo sehemu za “sisi” za Matendo ya Mitume (kama vile 16:10-17; 20:5-16; 21:1-18; 27:1-28:16) inamaanisha simulizi ya ushuhuda wa macho wa shughuli za umisionari wa Paulo.
3. Utangulizi wa Luka (kama vile 1:1-4) unadai kwamba Luka alifanya utafiti simulizi za ushuhuda wa macho ili aweze kuandika maisha ya Yesu yenye mjongo wa kihistoria ambalo linaonyesha alikuwa mwamini wa kizazi cha pili. Utangulizi wa Luka pia unachukua Matendo ya Mitume. Luka na Matendo ya Mitume kwa sehemu fulani kidogo vinaingiliana katika muda (yaani matukio ya baada ya ufufuo).

III. MTU AITWAYE LUKA

A. Dibaji ya Anti-Marcion juu ya Luka (175 B.K.)

1. mzaliwa wa Antiokia ya Shamu
2. tabibu
3. alikuwa hajaoa
4. mfuasi wa Paulo
5. aliandika kutokea Akaya
6. alikufa akiwa na miaka 84 huko Boeotia

B. Eusebius wa Kaisaria (275-339 B.K.) katika *Hist. Eccl.* III.4.2

1. kutokea Antiokia
2. mmisionari mwenza wa Paulo
3. aliandika Injili na Matendo ya Mitume

C. Jerome (346-420 B.K. huko *Migna* XXVI. 18)

1. aliandika kutokea Akaya
2. alikufa huko Boeotia

D. Alikuwa mtu mwenye elimu ya juu

1. ana sarufi nzuri ya Kiyunani cha Koine
2. misamiati mikubwa (hasa ya kidaktari na mambo ya usafiri wa majini)
3. mbinu za kitafiti (kama vile 1:1-4)
4. inawezekana alikuwa tabibu (kama vile Kol. 4:14). Pia maoni mabaya ya Marko juu ya matabibu katika Marko 5:26 inaondolewa katika ufanano wa Luka 8:43. Luka anatumia maneno yanayohusiana na utabibu, kuponywa, magonjwa, n.k. angalau mara 300 (kama vile W. K. Hobart, *The Medical Language of Luke*, au bora kuliko, A. Harnack, *Luke the Physician*).

E. Alikuwa ni mtu wa Mataifa

1. Paulo anaonekana kutofautisha katika orodha yake ya wasaidizi katika Kol. 4:10-11 (yaani “wale waliotahiriwa”) na wasaidizi wengine (yaani Epafra, Luka na Dema).
2. Katika Matendo ya Mitume 1:9 Luka anasema “katika lugha zao wenyewe,” akirejerea Kiaramu ambayo anamaanisha kuwa haikuwa lugha yake.
3. Katika Injili yake Luka anaondoa mkanganyiko pamoja na Mafarisayo juu ya Sheria ya Kiyahudi ya Kinywa.

- F. Katika watu wote kuwa mwandishi wa Injili ndefu zaidi na, pamoja na Matendo ya Mitume, mwandishi wa sehemu kubwa ya Agano Jipya, inashangaza kwamba mtu ajulikanaye kidogo tu, asiyeshuhuda wa macho (yaani asiye Mtume) Mtu wa Mataifa angechaguliwa. Bado hii ni desturi isiyofahamika ya kanisa la kwanza, ya watu walio wanamapinduzi!

IV. TAREHE YA KUANDIKWA

- A. Hakuna mtu anayejua hasa uhusiano kati ya (1) madokezo ya utafiti wa asili wa Luka (yaweze kana ilifanyika wakati Paulo alikuwa gerezani huko Kaisaria [kama vile Mdo. 23-26 na hasa 24:27]); (2) andiko lake la mwisho (yaani, Injili ya Luka kama tunavyojua ikitumia Marko na “Q”); na (3) mzunguko wa Luka – Mdo. (kwenda au kwa ajili ya Theophilo).
- B. Lazima ilikuwa kabla ya 95 B.K. ikiwa I Clement ana nukuu au uelewa usio sahihi kutoka Matendo ya Mitume na Matendo ya Mitume inafuatia Injili
1. Mdo. 13:22 - I Clement, 18:1
 2. Mdo. 20:36 - I Clement, 2:1
- C. Matendo ya Mitume lazima iwe kabla ya uharibifu wa Yerusalemu (70 B.K.) na kamanda wa Kirumi, Titus
1. hakuna kutajwa kwa vifo vya
 1. Mtume Yakobo (62 B.K.)
 2. Mtume Paulo (64-67 B.K.)
 2. Mahubiri ya Stephano katika Matendo ya Mitume 7 hayajumuishi uharibifu wa Hekalu ambayo kwa nguvu ingezeleza hukumu ya Mungu juu ya Dini ya Kiyahudi
 3. Paulo anatembelea Yerusalemu katika Matendo ya Mitume 21 na Luka, ikiwa aliandika baada ya mwaka 70 B.K., linaweze kana ingetajwa katika uharibifu wa Yerusalemu katika Injili yake
- D. Ikiwa Luka alitumia Injili ya Marko kama uainisho na/au Luka aliandika karibu na muda wa utafiti wake katika Palestina, hivyo miaka ya baadaye ya hamsini na sitini mwanzoni (pamoja na Matendo ya Mitume ikiandikwa mapema baada wakati Paulo akiwa bado gerezani huko Rumi, 62-63 B.K.).

V. WAPOKEAJI

- A. Kinaandikwa kama wakfu kwa Theophilo (kama vile Luka 1:1-4; Mdo. 1:1). Kuna nadharia kadhaa juu ya utambulisho wake:
1. mfanyakazi wa serikali ya Kirumi kwasababu Luka anamuita “mtukufu” katika Luka 1:3 na anatumi ajina hilo kwa Felix (kama vile Mdo. 23:26; 24:3) na Festo (kama vile Mdo. 26:25)
 2. mwangalizi mwenye mali nyingi (Theofilo lilikuwa jina lililozoeleka kati ya Wayahudi na Wayunani) waliomsaidia kulipia gharama za kuandika, kunakili na kusambaza Luka na Matendo ya Mitume.
 3. Jina lake linamaanisha “Mungu alipenda,” “mpenzi wa Mungu,” hivyo inaweze kana kuwa rejea ya siri kwa baadhi ya Wakristo
- B. Injili ya Luka inalenga kwa Mataifa
1. kinaelezea desturi za Kiyahudi
 2. Injili ni kwa watu wote (kama vile 2:10)

3. kinanukuu nabii zote ambazo zinarejerea kwa “wote wenye mwili” (kama vile 3:5-6 ambayo ni nukuu kutoka Isaya 40)
4. kizazi kinarudi nyuma mpaka Adamu (yaani wanadamu wote, kama vile 3:38)
5. mifano mingi ya upendo wa Mungu kwa Mataifa (mfano Luka unavutwa kwenye mipaka ya wale walioalikwa katika karamu ya ki-Masihi, 13:29)
6. mifano ya Agano la Kale, inatangaza upendo wa Mungu kwa Mataifa (kama vile 2:32; 4:25-77)
7. Agizo Kuu la Luka - msamaha unahubiriwa kwa mataifa yote (kama vile 24:47)

VI. MAKUSUDI YA UANDISHI WA KITABU CHA LUKA

A. Injili zote ziliandikwa kwa makundi fulani ya watu yaliyokusudiwa kwa kusudi la Uinjilisti (kama vile Yohana 20:30-31)

1. Mathayo kwa ajili ya Wayahudi
2. Marko kwa ajili ya Warumi
3. Luka kwa ajili ya Mataifa
4. Yohana kwa ajili ya Mataifa

Luka kipekee anataja umisionari wa Sabini (kama vile 10:1-24). Kwa ajili ya Walimu wa Kiyahudi, 70 ilikuwa ni hesabu ya kuashiria lugha za ulimwengu (kama vile Mwa. 10). Kwa Yesu kutuma wahubiri 70 kuhubiri habari njema, hii ingezungumzwa kwamba Injili ni kwa ajili ya watu wote.

B. Makusudi mengine yakini

1. kuzungumzia Ujio wa Mara ya Pili uliochelewa
 - a. Luka 21 ni sawa sawa na lakini kidogo tofauti na Mt. 24, Marko 13, kuhusiana na kurudi kwa Kristo na mwisho wa ulimwengu.
 - b. Hata hivyo Luka anazungumzia uinjilishaji wa ulimwengu ambao unachukua muda kwa kanisa kutimilizika (kama vile 24:47).
 - c. Pia Luka (kama Paulo) kinasisitiza kwamba ufalme wa Mungu upo hapa sasa (kama vile 10:9, 11; 11:20; 17:21) pamoja na hapo baadaye.
 - d. Muhtasari mzuri wa maoni na mijadala ya wanazuoni wa Kibiblia unaweza kuonekana katika toleo la Anchor Bible, vol. 28, kur. 231-235.
2. kuelezea Ukristo kwa wafanyakazi wa serikali ya Kirumi (kama inavyofanya matendo ya Mitume)
 - a. neno “mtukufu” katika utangulizi
 - b. Luka 23 ina Pilato akisema, “sioni kosa lolote alilolitenda mtu huyu” (kama vile 23:4, 14-15, 22)
 - c. Wafanyakazi wa serikali katika Matendo ya Mitume wanawasilishwa kwa fahamu mzuri na Paulo anahutubia kwa wafanyakazi wa Kirumi kuonesha heshima kwao na wanaitikia vizuri juu ya kurudi kwake (kama vile Mdo. 26:31-32)
 - d. Akida wa Kirumi, wakati wa usulubishaji msalabani pia anatoa ushuhuda mzuri juu ya Yesu (kama vile Luka 23:47)

C. Kuna baadhi ya maudhui ya kithiolojia ya kipekee ambayo yanafanya kazi katika makusudi ya maandiko ya Luka

1. Luka anaonyesha kujali kwa kipekee kwa makundi fulani ya watu.
 - a. masikini na matajiri (mfano Heri za Luka, Luka 6:20-23)
 - b. Watu waliotengwa katika jamii

- (1) Wanawake wasio na maadili (kama vile Luka 7:36-50)
 - (2) Wasamaria (kama vile Luka 9:51-56; 10:29-37)
 - (3) Wenye njia za ukaidi (kama vile Luka 15:11-32)
 - (4) Wakusanya kodi (kama vile Luka 19:1-10)
 - (5) viwete (kama vile Luka 17:11-19)
 - (6) wahalifu (kama vile Luka 23:39-43)
2. Luka anataja Hekalu katika Yerusalemu. Injili inaanza na Wayahudi na Maandiko yao (yaani Yesu kutimiliza unabii wa Agano la Kale), lakini wanamkataa (kama vile 11:14-36) na anakufa Mkombozi kwa ulimwengu mzima (kama vile 10:1-24) na kuweka hekalu lao pamoja na Yeye mwenyewe (kama vile??).

VII. VYANZO VYA INJILI YA LUKA

A. Nadharia kadhaa zimependekezwa kuhusiana na uhusiano kati ya Mathayo, Marko na Luka (Vitabu vya Injili)

1. Desturi sare ya kanisa la kwanza ni kwamba Luka, tabibu mtu wa Mataifa na mmisionari mwenza wa Mtume Paulo ndiye aliyeandika Injili.
2. Mnamo mwaka 1776 A. E. Lessing (na baadaye Gieseler mnamo 1818), alitoa nadharia jukwaa la kinywa katika ukuaji wa Vitabu vya Injili (“kuona kwa pamoja”). Alielezea kwamba vyote vilikuwa vikitegemea katika desturi za kale za kinywa ambazo waandishi walirekebisha kwa ajili ya hadhira wao wenyewe waliowalenga
 - a. Mathayo:Wayahudi
 - b. Marko:Warumi
 - c. Luka:Mataifa

Kila kimoja kilihusiana na kituo tofauti cha kijiografia cha Ukristo

 - a. Mathayo:Antiokia, Shamu au Yudea
 - b. Marko:Rumi, Italia
 - c. Luka:Kaisaria pembezoni mwa Bahari, Palestina au Akaya
 - d. Yohana:Efeso, Asia Ndogo
3. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa J. J. Griesbach alitoa nadharia kwamba Mathayo na Luka waliandika simulizi tofauti za maisha ya Yesu ambazo kila moja inajitegemea kiukamilifu tofauti na nyingine. Marko aliandika Injili ya muhtasari akijaribu kuingia kati ya simulizi hizi mbili.
4. Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa H. J. Holtzmann alikuja na nadharia kwamba Marko ilikuwa injili ya kwanza na kwamba Mathayo na Luka walitumia muundo wa Injili yake pamoja na nyaraka za kutenganisha zilizo na semi za Yesu ziiwazo Q (Kijerumani *quelle* au “chanzo”). Hii ilipewa jina, nadharia ya “chanzo cha pili” (iliyoungwa mkono na Fredrick Schleiermacher mnamo mwaka 1832).

Baadhi wanadhania kwamba orodha hii kutoka kwa Yesu iliyo na muundo kama fasihi za hekima za Agano la Kale inaweza kuwa kile ambacho Papia amekiandika kwamba Mathayo ndiye aliyeandika. Tatizo ni kwamba hakuna nakala hata moja nya orodha hii ya misemo iliyodumu. Ikiwa kanisa lilifurahia Injili sana, waliwezaje kupoteza orodha ya misemo ya Mwanzilishi wa Imani iliyotumika katika Mathayo na Luka?

5. Baadaye, B. H. Streeter alikuja na nadharia iliyorekebisha wa “chanzo cha pili” ambayo aliita “chanzo cha nne” ambayo ilipendekeza “proto Luka” pamoja na Marko ikiwa na Q.

6. Nadharia hapo juu za uundaji wa Vitabu vya Injili ni nadharia tu. Hakuna ushahidi wa maandiko wa kihistoria wala wa uhakika wa aidha chanzo "Q" au "Luka kwanza." Uanazuoni wa kisasa hautambui namna gani Injili zilikuzwa wala nani aliyeziandika (ndivyo ilivyo juu ya sheria za Agano la Kale na Manabii wa Zamani). Hata hivyo ukosefu huu wa taarifa hauathiri mtazamo wa kanisa juu ya uvuv wao na uaminifu kihistoria pamoja na nyaraka za imani.
 7. Kuna ufanano wa dhahiri katika muundo na mpangilio wa maneno kati ya Injili, lakini kuna tofauti nyingi pia za kutisha. Tofauti ni kawaida katika simulizi za mashuhuda wa macho. Kanisa la kwanza halikusumbuka na utofautiano wa simulizi hizi tatu za maisha ya Yesu ya ushuhuda wa macho. Inaweza kuwa kwamba hadhira lengwa, mbinu ya mwandishi na tofauti za lugha katika simulizi zilijumuishwa (Kiaramu na Kiyunani) kwa tofauti hizi zinazoonekana. Lazima iwekwe wazi kwamba waandishi hawa waliovuviwa, wahariri au watunzi walikuwa na uhuru wa kuchagua, kupangilia, kuasilisha na kuweka kwa muhtasari matukio na mafundisho ya maisha ya Yesu (kama vile *How to Read the Bible for All Its Worth* by Fee na Stuart, kur.113-148).
- B. Luka kibayana anadai kwamba alifanya utafiti (kama vile Luka 1:1-4) katika maisha ya Yesu kwa jicho la ushuhuda wa macho. Kufungwa kwa Paulo huko Kaisaria pembezoni mwa Bahari huko Palestina kulimruhusu Luka kupata muda na kuwapata watu hawa. Sura za 1-2 kunaweza kuaksi kumbukumbu za Maria (kama vile Sir William Ramsay, *Was Christ Born at Bethlehem?*) kama uzao ulivyo wa sura ya 3.
- C. Vyanzo kadhaa vya kanisa la kwanza vinataja kwamba Luka alikuwa mmisionari mwenza asafiriye na Mtume Paulo. Baadhi ya vyanzo vya kale pia vinaelezea kwamba Injili ya Luka iliathiriwa na mahubiri ya Paulo. Haiwezi kupingwa kwamba umisheni wa ulimwengu wa injili unabainishwa kama utimilifu wa unabii katika Luka, Mdo na maandiko ya Paulo.

VIII. UPEKEE WA LUKA

- A. Sura mbili za kwanza ni za kipekee kwa Luka na zinaweza kuwa zimetokea kwa Mariamu, kama ilivyo 3:23-28.
- B. Miujiza ya kipekee kwa Luka
1. kijana wa mjane wa Naini akifufuliwa, 7:12-17
 2. mwanamke mgonjwa katika Sinagogi akiponywa siku ya Sabato, 13:10-17
 3. mwanaume mgonjwa akiponywa siku ya Sabato, 14:1-6
 4. wakoma kumi wakiponywa, na mmoja tu Msamaria akirudi kushukuru, 17:11-18
- C. Mifano ya upekee kwa Luka
1. Msamaria mwema, 10:25-37
 2. rafiki aliyekazana, 11:5-13
 3. mpumbavu tajiri, 12:13-21
 4. sarafu iliyopotea, 15:8-10
 5. wana wawili, 15:11-32
 6. wakili dhalimu, 16:1-8
 7. mtu tajiri na Lazaro, 16:19-31
 8. hakimu dhalimu, 18:1-8

9. Mfarisayo na Raia, 18:9-14

D. Mifano katika Luka ambayo pia katika Mathayo imetumika ki-utofauti

1. 12:39-46 (Mt. 24:43-44)
2. 14:16-24 (Mt. 22:2-14)
3. 19:11-27 (Mt. 25:14-30)

E. Simulizi zingine za kipekee

1. matukio ya sura mbili za kwanza
2. Zakayo, mtoza ushuru, 19:1-10
3. Yesu anapelekwa kwa Herode na Pilato kuchunguzwa, 23:8-12
4. watu wawili wakiwa njiani kwenda Emmau, 24:13-32

F. Viashiria vya kipekee zaidi katika Luka vinapatikana katika 9:51-18:14. Hapa Luka hategemei juu ya Marko au "Q" (yaani, misemo ya Yesu yawezekana iliyoandikwa na Mathayo). Hata matukio au mafundisho yanayofanana yanawekwa katika muundo tofauti. Maudhui unganishi ya sehemu hii ni "njiani kwenda Yerusalemu" (kama vile 9:51; 13:22, 33; 17:11; 18:31; 19:11,28) ambayo hasa ni safari Yake kwenda msalabani.

IX. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. tasa, 1:7
2. ukombozi, 1:6;8
3. pembe ya wokovu, 1:69
4. sensa, 2:1
5. zelote, 6:15
6. ufalme wa Mungu, 6:20
7. wapiga filimbi, 7:32
8. watumishi wa Sinagogi, 8:49
9. Mwana wa Adamu atateswa, 9:22
10. Msamaria, 10:33
11. Ole wenu! 11:42, 43, 44, 47, 52
12. tubuni, 13:3, 5
13. mlango mwembamba, 13:24
14. kubeba msalaba wake mwenyewe, 14:27
15. udhalimu, 16:11
16. Sheria na Manabii, 16:16
17. kifua cha Ibrahimu, 16:22
18. jiwe la kusagia, 17:2
19. mpaka muda wa mataifa utimilizwe, 21:24
20. Baraza la wazee, 22:66
21. Paradiso, 23:43

X. WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. Theophilo, 1:3
2. Zakaria, 1:5

3. Malaika wa Bwana, 1:11; 2:9
4. Gabrieli, 1:26
5. Kirenio, 2:2
6. Anna, 2:36
7. Tiberio, 3:1
8. Mtawala Herode, 3:1, 19
9. Kayafa, 3:2
10. Naamani, 4:2
11. Malkia wa Kusini, 11:31
12. Zekaria, 10:51
13. Lazaro, 16:23
14. Zakayo, 19:2
15. Yusufu, 23:50
16. Cleopa, 24:18

XI. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Galilaya, 1:26
2. Nazareti, 1:4
3. Betlehemu, 1:4
4. Iturea, 3:1
5. Bethsaida, 9:10
6. Korazini, 10:13
7. Tiro, 10:13
8. Kapernaumu, 10:15
9. Samaria, 17:11
10. Sodoma, 17:29
11. Yeriko, 19:1
12. Emmau, 24:13
13. Bethania, 24:50

XII. MASWALI YA MJADALA

1. Nini umuhimu wa Mungu kufunua kuzaliwa kwa Yesu kwa wachungaji kwanza?
2. Nini umuhimu wa kauli ya Yesu katika 2:49?
3. Kwanini kizazi katika Luka kinarudi nyuma mpaka kwa Adamu?
4. Ni kwa namna gani wanafunzi walikuwa wakivunja sheria katika 6:1-5? Ni sheria gani walikuwa wakivunja?
5. Elezea maneno ya Yesu katika 6:46.
6. Kwanini Yohana aliona shaka juu ya Yesu kama Masihi aliyehaidiwa katika sura ya 17:18-23?
7. Kwanini Wagerasi walimtaka Yesu kuondoka?
8. Elezea kwa maneno yako mwenyewe maana ya 9:62.
9. Wakati gani shetani alianguka kutoka mbinguni? (10:18)
10. Kwanini Wayahudi waliwachukia Wasamaria?
11. Je 12:41-48 inamaanisha kiwango cha adhabu au mamlaka za kuzimu?
12. Elezea 13:28-30 kwa maneno yako mwenyewe.
13. Nini makusudi ya mfano wa mwana mpotevu katika 15:11-32?

14. Elezea 16:18 kwa maneno yako mwenyewe lakini kuwa na hakika ya kufasiri kwa ufahamu wa mazingira nyake ya kihistoria.
15. Je 17:34-35 inakubaliana na kunyakuliwa kwa siri? Kwanini au kwanini sio?
16. Kwanini 20:2 ni swali muhimu hivyo?
17. Wakulima wa mizabibu 20:10 ni wakina nani?
18. Je Yuda aliwajibika kwa matendo yake kwa mujibu wa 22:3?
19. Kwanini 23:20 kuwa mstari muhimu mpaka kuandikwa na Luka?

UTANGULIZI WA YOHANA

I. MAELEZO YA UTANGULIZI

- A. Mathayo na Luka inaanza na kuzaliwa kwa Yesu na ubatizo Wake, lakini Yohana anaanza kabla ya uumbaji.
- B. Yohana anawasilisha Uungu kamili wa Yesu wa Nazareti kutoka mstari wa kwanza wa sura ya kwanza na anarudia msisitizo huu katika injili yake yote. Vitabu vya Injili vinafunika kweli hii mpaka baadaye katika uwasilishaji wake (“Siri ya Kimasihi”).
- C. Inavyoonekana Yohana alikuza injili yake kwa ufahamu wa ukiri wa msingi wa Vitabu vya Injili. Anajaribu kuweka mbadala na kufasiri maisha na mafundisho ya Yesu kwa ufahamu wa mahitaji ya kanisa la kwanza (baadaye katika karne ya kwanza).
- D. Yohana anaonekana kuweka muundo wa uwasilishaji wake wa Yesu Masihi kuzunguka
 1. miujiza saba/ishara na fasiri zake
 2. mazungumzo ishirini na saba na/au majibizano pamoja na mtu mmoja mmoja
 3. siku fulani za ibada na karamu
 - a. sabato
 - b. pasaka (kama vile sura za 5-6)
 - c. Hema za kukutanikia (kama vile sura za 7-10)
 - d. Hanukkah (kama vile 10:22-39)
 4. Kauli za “Mimi Ndimi”
 - a. zinazohusiana na Jina la Mungu (YHWH)
 - 1) Mimi Ndimi (4:26; 8:24,28; 13:19; 18:5-6)
 - 2) Ibrahimu hajakuwako, Mimi Niko (8:54-59)
 - b. ikiwa na vielezi vya nomino
 - 1) Mimi ndimi Mkate wa Uzima (6:35, 41, 48, 51)
 - 2) Mimi ndimi nuru ya ulimwengu (8:12)
 - 3) Mimi ndimi mlango wa Kondoo (10:7, 9)
 - 4) Mimi ndimi Mchungaji mwema (10:11, 14)
 - 5) Mimi ndimi ufufuo na uzima (11:25)
 - 6) Mimi ndimi njia, kweli na uzima (14:6)
 - 7) Mimi ndimi mzabibu wa kweli (15:1, 5)
 - E. Tofauti kati ya Yohana na Injili zingine
 1. Ingawa ni kweli kwamba kusudi la msingi la Yohana ni la kithiolojia, matumizi yake ya historia na jiografia ni la usahihi zaidi na lenye maelezo ya ndani. Sababu sahihi kwa tofauti kati ya Vitabu vya Injili na Yohana haijulikani
 - a. huduma ya kwanza ya Yudea (kutakaswa kwa mapema kwa Hekalu)
 - b. mtiririko na tarehe za maisha ya Yesu ya Juma la mwisho
 2. Ingekuwa msaada kuchukua muda kujadili tofauti za kidhahiri kati ya Yohana na Vitabu vingine vya Injili. Naomba kumnukuu George Eldon Ladd kutoka *A Theology of the New Testament* juu ya tofauti:

- a. “Injili ya nne ni tofauti sana na vitabu vingine vya Injili kwamba swali lazima likabiliwe kiukweli ikiwa inatoa taarifa sahihi wa mafundisho ya Yesu au ikiwa imani ya Mkristu imerekebisha desturi ambayo historia imemezwa katika ufasiri wa kithiolojia” (ukur. 215).
- b. “Suluhu inayokaribia karibu kabisa ni kwamba mafundisho ya Yesu yanaelezwa katika nahau ya Johannine. Ikiwa hii ni suluhu sahihi, na ikiwa tunatakiwa kuhitimisha kwamba Injili ya nne imefichwa au kueleweka katika nahau ya Yohana, swali hili muhimu linafuata: Ni kwa kiasi gani thiolojia ya Injili ya nne ni ya Yohana kuliko ile ya Yesu? Ni kwa kiasi gani mafundisho ya Yesu yamekuwa ya Yohana kabisa kiasi kile tulicho nacho ni ufasiri wa ki-Yohana kuliko uwakilishaji wa mafundisho yenyewe ya Yesu mwenyewe?” (ukur. 215).
- c. Ladd pia anamnukuu W. F. Albright kutoka “Recent Discoveries in Palestine and the Gospel of John” katika *The Background of the New Testament and Its Eschatology* kilicho haririwa na W. D. Davies na D. Daube

“Hakuna tofauti kubwa ya msingi katika mafundisho ya Yohana na Vitabu vingine vya Injili; ulinganifu kati yao unalalia katika ufahamu wa desturi katika vipengele kadhaa ya mafundisho ya Kristo, hasa yale yanayoonekana kufanana na mafundisho ya Wa-Essene kwa ukaribu zaidi.

Hakuna chochote kabisa cha kuonesha kwamba mafundisho yoyote ya Yesu yameharibiwa au kufanywa ya uongo, au kwamba vipengele vya msingi vipya vimeongezwa kwake. Kwamba mahitaji ya kanisa la kwanza yalichagiza uchaguzi wa vitu kwa ajili ya kujumuishwa katika Injili tunayokubaliana nayo, lakini hakuna sababu ya kudhania kwamba mahitaji ya kanisa ndiyo yaliyosababisha mavumbuzi au marekebisho ya umuhimu wa kithiolojia.

Moja kati ya madhanio ya kigeni kabisa ya ukosoaji wa wa wasomi wa ya Agano Jipya na wana thiolojia ni kwamba ufahamu wa Yesu ulikuwa na ukomo kwamba ulinganifu wowote unaonekana kati ya Yohana na Vitabu vingine lazima ulitokana na tofauti kati ya Wakristo wanathiolojia wa kwanza. Kila mwenye fikra kubwa na haiba anafasiriwa tofauti na rafiki zake tofauti na wasikilizaji wake, ambao huchagua kile kinachoonekana kuwa cha kupendeza zaidi au cha kuzaa kutoka katika vile walivyoviona na kusikia” (kur. 170-171).

- d. Na tena kutoka kwa George E. Ladd:

“Tofauti kati yao sio kwamba Yohana ni kitabu cha kithiolojia na vingine sio, lakini vyote ni vya kithiolojia ila kwa namna tofauti tofauti. Historia iliyofasiriwa inaweza kuwakilisha kwa ukweli zaidi kweli za mazingira kuliko mambo ya nyakati ya matukio tu. Ikiwa Yohana ni ufasiri wa kithiolojia, ni ufasiri wa matukio ambayo Yohana anashawishiwa kwamba yalitokea katika historia. Kidhahiri sio kusudio la Vitabu vya Injili kutoa taarifa ya *ipsissima verba of* (maneno halisi) Yesu wala historia na matukio yaliyomtokea katika maisha. Ni taswira ya Yesu na muhtasari wa mafundisho yake. Mathayo na Luka wanajiskia huru kupanga upya nyaraka katika Marko na kutoa taarifa ya mafundisho ya Yesu kwa uhuru fulani. Ikiwa Yohana alitumia zaidi uhuru kuliko Mathayo na Luka, ni kwasababu alitamani kutoa taswira ya mvuto wa ndani na wenye uhalisia wa Yesu” (kur. 221-222).

II. MWANDISHI

- A. Injili haipewi jina lakini inatoa dokezo la uandishi wa Yohana

1. mwandishi shuhuda wa macho (kama vile 19:35)
 2. Tungo “mwanafunzi apendwaye” (wote wawili Polycrates na Irenaeus wanamtaja kwamba alikuwa Mtume Yohana)
 3. Yohana, mwana wa Zebedayo, hakuwahi kutajwa kwa Jina
- B. Mazingira ya kihistoria ni dhahiri kutoka kwenye injili yenyewe, hivyo, jambo la uandishi sio jambo kuu katika ufasiri. Ukiri wa mwandishi aliyevuviwa ndio wa msingi!
- Uandishi na tarehe za Injili za Yohana haziathiri uvuvio bali ufasiri. Wafasiri wanatafuta mazingira ya kihistoria, mazingira ambayo yalisababishwa kitabu kuandikwa. Je mtu awekza kulinganisha Yohana na nadharia ya u-pili (1) nyakati mbili za Kiyahudi; (2) mwalimu wa haki aitwaye Qumran; (3) Dini ya Zoroastrian; (4) Fikra za walimu wa Ujuzi; au (5) mtazamo wa kipekee wa Yesu?
- C. Mtazamo wa kifestari wa kale ni kwamba Mtume Yohana, mwana wa Zebedayo ni chanzo cha kibinadamu cha ushuhuda wa macho. Hii lazima ifafanuliwe kwasababu vyanzo vya nje vya karne ya pili vinaonekana kuunganisha vingine katika uzalishaji wa Injili:
1. Waaminio wenza na wazee wa Ki-Efeso walimtia moyo Mtume aliyekuwa katika hali ya uzee kuandika (Eusebius anamnukuu Clement wa Iskandria)
 2. Mtume mwenza, Andrea (toleo la Muratorian Fragment, 180-200 B.K., kutoka Rumi)
- D. Baadhi ya wasomi wa kisasa wamefikiria mwandishi mwingine wakijikita katika madhanio kadhaa juu ya staili na mada za Injili. Wengi hudhania tarehe ya mwanzoni mwa karne ya pili (kabla ya 115 B.K.):
1. kiliandikwa na wanafunzi wa Yohana (marafiki wa Yohana wenye ushawishi) waliokumbuka uandishi wake (J. Weiss, B. Lightfoot, C. H. Dodd, O. Cullmann, R. A. Culpepper, C. K. Barrett)
 2. kiliandikwa na “mzee Yohana,” (moja wa viongozi wake wa mwanzo kutoka Asia walioshawishiwa na thiolojia ya Mtume Yohana na misamiati yake) kutokea katika vifungu tata katika Papias (70-146 B.K.) akinukuliwa na Eusebius (280-339 B.K.)
- E. Ushahidi wa Yohana mwenyewe kama chanzo cha msingi kwa nyaraka za Injili
1. ushahidi wa ndani
 - a. mwandishi alijua mafundisho ya Kiyahudi na taratibu na kushirikisha mtazamo wao wa kiulimwengu wa Agano la Kale
 - b. mwandishi aliifahamu Palestina na Yerusalemu katika miaka yao ya hali ya 70 B.K.
 - c. mwandishi anadai kuwa shuhuda wa macho
 - 1) 1:14
 - 2) 19:35
 - 3) 21:24
 - d. mwandishi alikuwa mshirika wa kundi la Mitume, kwahiyo anaufahamu wa
 - 1) maelezo ya muda na mahali (usiku wa kukamatwa)
 - 2) maelezo ya hesabu (mabalasi 2:6 na samaki wa 21:11)
 - 3) maelezo ya kina ya watu
 - 4) mwandishi alijua maelezo ya matukio na mrejesho kwao
 - 5) mwandishi anaonekana kurejerewa kama “mwanafunzi apendwaye”
 - a) 13:23,25

- b) 19:26-27, 34-35
 - c) 20:2-5,8
 - d) 21:7, 20-24
- 6) mwandishi anaonekana kuwa sehemu ya wanafunzi wa karibu zaidi na Yesu pamoja na Petro
- a) 13:24
 - b) 20:2
 - c) 21:7
- 7) Jina Yohana, mwana wa Zebedayo, halikuwahi kutokea katika injili hii, jambo linaloonekana kuwa si kawaida kwasababu alikuwa mshirika wa Kundi la Mitume walio karibu na Yesu
- e. ushahidi wa nje
- 1) Injili inajulikana kwa
 - a) Irenaeus (120-202 B.K.) aliyekuwa na uhusiano wa karibu na Polycarp, alimfahamu Mtume Yohana (kama vile Eusebius' *Historical Eccleasticus* 5:20:6-7) - "Mwanafunzi aitwaye Yohana aliyependa kuegama kifuani Pake na yeye mwenyewe aliitoa Injili huko Efeso, Asia" (*Haer*, 3:1:1, ilinukuliwa na Eusebius' *Hist. Eccl.* 5:8:4).
 - b) Clement wa Iskandria (153-217 B.K.) - "Yohana aliyehimizwa na rafiki zake na akivuviwa ki-Mungu na Rohu, aliandika Injili ya kiroho" (Eusebius' *Historical Eccleasticus* 6:14:7)
 - c) Justin Martyr (110-165 B.K.) katika toleo lake la *Dialogue with Trypho* 81:4
 - d) Tertullian (145-220 B.K.)
 - 2) uandishi wa Yohana ulielezwa na mashuhuda wa hapo mwanzo
 - a) Polycarp (70-156 B.K., aliandikwa na Irenaeus), aliyekuwa askofu wa Smirna (155 B.K.)
 - b) Papias (70-146 B.K., akiandikwa na Utangulizi wa Anti-Marconite kutoka Rumi na Eusebius), aliyekuwa askofu wa Hierapoli huko Filigia na kutoa taarifa kuwa mwanafunzi wa Mtume Yohana

F. Sababu zinazotumiwa kuona mashaka wa uandishi wa kidesturi

1. muunganiko wa injili pamoja na maudhui ya walimu wa ujuzi
2. udhahiri wa kiambatisho cha sura ya 21
3. Tofauti za kimtiririko pamoja na Vitabu vya Injili
4. Yohana asingerejerea yeye mwenyewe kama "mwanafunzi apendwaye"
5. Yohana wa Yesu anatumia misamiati tofauti na aina ya uwasilishaji kuliko Injili zingine

G. Ikiwa tutachukulia kuwa alikuwa nia Yohana Mtume, hivyo tunaweza kuwaza nini juu ya mtu huyu?

1. Aliandika kutokea Efeso (Irenaeus anasema "alitoa Injili kutoka Efeso")
2. Aliandika wakati alikuwa mzee (Irenaeus alisema aliishi mpaka utawala wa Trajan, 98-117 B.K.)

III. TAREHE

A. Ikiwa tutadhania ni Mtume Yohana

1. Kabla ya mwaka 70 B.K, wakati Yerusalemu ilipoharibiwa na Kamanda wa Kirumi (baadaye Mfalme), Titus
 - a. Katika Yohana 5:2, “Na huko Yerusalemu penye mlango wa kondoo pana birika, iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha, nayo ina matao matano...”
 - b. matumizi ya kurudia rudia ya jina la hapo awali “wanafunzi” kuashiria kundi la kinabii
 - c. vipengele vya baadaye vya walimu wa ujuzi vimegundulika katika magombo ya Bahari ya Chumvi, ambayo yanaonesha yalikuwa sehemu ya lugha ya kithiolojia ya karne ya kwanza
 - d. hakuna kutajwa kwa uharibifu wa Hekalu na mji wa Yerusalemu mnamo mwaka 70 B.K.
 - e. mwana akiolojia maarufu wa ki-Marekani W. F. Albright anatangaza tarehe ya Injili mnamomiaka ya mwishoni mwa 70 au 80 mwanzoni
2. baadaye katika karne ya kwanza
 - a. thiolojia iliyokuzwa ya Yohana
 - b. kuanguka kwa Yerusalemu hakutajwi kwasababu kulitokea miaka ishirini hapo kabla
 - c. matumizi ya Yohana ya aina ya tungo na msisitizo
 - d. desturi za hapo kabla za kanisa
 - 1) Irenaeus
 - 2) Eusebius

B. Ikiwa tutachukulia “Yohana Mzee” hivyo tarehe ingekuwa karibia na karne ya pili kati. Nadharia hii ilianza na kukataliwa kwa uandishi wa Mtume Yohana iliyotolewa na Dionysius (kwa sababu za kifasihi). Eusebius, aliyekataa uandishi wa Mtume Yohana wa Ufunuo kwa sababu za kithiolojia, alijiskia alikuwa amepata “Yohana” mwingine kwa wakati sahihi na katika sehemu sahihi katika nukuu za Papias (*Historical Eccleasticus* 3:39:5,6), ambaye anaorodhesha “Yohana” wawili (1) Mtume na (2) Mzee (presbyteri).

IV. WAPOKEAJI

- A. Kiasili kiliandikwa kwa makanisa ya Jimbo la Kirumi la Asia Ndogo, hasa Efeso.
- B. Kwasababu ya mwonekano wake mwepesi na kina cha simulizi hili la maisha na watu wa Yesu wa Nazareti kwa wote waamini wa Mataifa na vikundi vya walimu wa ujuzi.

V. MAKUSUDI

- A. Injili yenyewe inataja makusudi yake ya kiinjilisti, 20:30-31
 1. kwa wasomaji wa Kiyahudi
 2. kwa wasomaji wa Mataifa
 3. kwa wasomaji walimu wa uongo wanaokua
- B. Kinaonekana kuwa na msukumo wa toba
 1. dhidi wafuasi wafia dini wa Yohana Mbatizaji
 2. dhidi ya wasomaji walimu wa uongo wanaokua (hasa hitimisho); mafundisho haya ya uongo ya walimu wa uongo pia yanaunda historia ya nyuma kwa vitabu vingine vya Agano Jipya:
 - a. Waefeso
 - b. Wakolosai
 - c. Nyaraka za Kichungaji (1 Timotheo, Tito, 2 Timotheo)
 - d. 1 Yohana (1 Yohana inafanya kazi kama nyaraka za ziada kwa ajili ya Injili)

- C. Kuna uwezekano kwamba kauli ya makusudi ya 20:31 inaweza kueleweka kama kutia hamasa juu ya ustahimilivu sawasawa na uinjilisti kwasababu ya matumizi endelevu ya NJEO YA WAKATI ULIOPO. Kwa namna hii, Yohana kama Yakobo wanatengeneza uwiano juu ya msisitizo wa thiolojia ya Paulo kwa baadhi ya makundi katika Asia Ndogo (kama vile 2 Petro 3:15-16). Inashangaza kwamba desturi za kanisa la kwanza linamtaja Yohana pamoja na Efeso, sio Paulo (kama vile F. F. Bruce's *Peter, Stephen, James and John: Studies in Non-Pauline Christianity*, kur. 120-121).
- D. Dibaji (sura ya 21) inaonekana kujibu maswali hasa ya kanisa la awali
1. Yohana anaweka mbadala wa Simulizi za Injili. Hata hivyo anajikita katika huduma ya Yudea, hasa Yerusalemu.
 2. maswali mawili yanawekwa katika kiambatisho, sura ya 21
 - a. urejesho wa Petro
 - b. urefu wa Yohana
 - c. kuchelewa kurudi kwa Yesu
- E. Baadhi wanamuona Yohana kama akiondoa msisitizo wa nadharia ya Sakramenti kwa makusudi ya kupuuzia na kutoandikwa au kujadili sheria zenyewe licha ya fursa kamilifu za kimuktadha katika sura ya 3 (kwa ubatizo) na sura ya 6 (kwa Ekaristi au Karamu ya Bwana).

VI. AINISHO LINALOJIKITA JUU YA

- A. Dibaji ya kifalsafa/kithiolojia (1:1-18) na Hitimisho la uhalisia (sura ya 21)
- B. ishara za miujiza Saba wakati wa huduma ya Yesu kwa watu (sura za 2-12) na tafsiri zake:
1. kubadili maji kuwa divai katika sherehe ya Kana (2:1-11)
 2. uponyaji wa mwana wa afisa wa mahakama huko Kapernaumu (4:46-54)
 3. uponyaji wa kiwete katika birika la Siloamu huko Bethsaida, Yerusalemu (5:1-18)
 4. kulisha watu zaidi ya 5,000 huko Galilaya (6:1-15)
 5. kutembea juu ya Bahari ya Galilaya (6:16-21)
 6. Uponyaji wa kipofu wa kuzaliwa huko Yerusalemu (9:1-41)
 7. kufufuliwa kwa Lazaro huko Bethania (11:1-57)
- C. usaili na mazungumzo ya mtu mmoja mmoja
1. Yohana Mbatizaji (1:19-34; 3:22-36)
 2. Wanafunzi
 - a. Andrea na Petro (1:35-42)
 - b. Philipo na Nathanaeli (1:43-51)
 3. Nikodemo (3:1-21)
 4. Mwanamke wa Samaria (4:1-45)
 5. Wayahudi huko Yerusalemu (5:10-47)
 6. mkutano huko Galilaya (6:22-66)
 7. Petro na Wanafunzi (6:67-71)
 8. Ndugu wa Yesu (7:1-13)
 9. Wayahudi huko Yerusalemu (7:14-8:59; 10:1-42)

10. wanafunzi katika chumba cha juu (13:1-17:26)
11. kukamatwa kwa Wayahudi na mashitaka (18:1-27)
12. Shitaka la Kirumi (18:28-19:16)
13. mazungumzo baada ya ufufuo, 20:11-29
 - a. pamoja na Mariamu
 - b. na Mitume Kumi
 - c. pamoja na Thomaso
14. ufunguzi na ufungaji wa Petro, 21:1-25
15. (7:53-8:11, hadithi ya mama mzinzi, haikuwa kiasili sehemu ya Injili ya Yohana!)

D. Siku fulani za kuabudu/siku za karamu

1. sabato (5:9; 7:22; 9:14; 19:31)
2. pasaka (2:13; 6:4; 11:55; 18:28)
3. karamu ya Hema la Kukutania (sura za 8-9)
4. Hanukkah (sherehe za mianga, kama vile 10:22)

E. Matumizi ya kauli “Mimi Ndiye”

1. “Mimi Ndiye” (4:26; 6:20; 8:24,28,54-59; 13:19; 18:5-6,8)
2. “Mimi Ndiye Mkate wa Uzima” (6:35,41,48,51)
3. “Mimi ni nuru ya ulimwengu” (8:12; 9:5)
4. “mimi ni mlango wa kondoo” (10:7,9)
5. “Mimi ndiye Mchungaji Mwema” (10:11,14)
6. “Mimi ndiye ufufuo na Uzima” (11:25)
7. “Mimi ndimi njia, kweli na uzima” (14:6)
8. “Mimi ndimi mzabibu wa kweli” (15:1,5)

VII. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. neno, 1:1
2. amini, 1:7
3. “ulimwengu ulifanyika kwa Yeye,” 1:10
4. “Neno likawa mwili,” 1:14
5. kweli, 1:17
6. nabii, 1:21
7. mwana kondoo wa Mungu,” 1:29
8. “kama hua,” 1:32
9. Rabbi, 1:38
10. “Hakika, hakika,” 1:51
11. “malaika wa Mungu wakipanda na kushuka,” 1:51
12. “mabalasi sita,” 2:6
13. “mtawala wa Wayahudi,” 3:1
14. “kuzaliwa upya,” 3:3
15. “Mwana wa Adamu lazima ainuliwe,” 3:14; 12:34
16. “uzima wa milele,” 3:16
17. “Mimi ndimi mkate wa uzima,” 6:35,48
18. “Sikukuu za vibanda,” 7:2

19. "Una pepo," 7:20; 8:48; 10:20
20. utawanyiko (nje), 7:35
21. "Yesu alikuwa bado hajatukuzwa," 7:39
22. "Yeye Ibrahimu asijakuwako, Mimi niko," 8:58
23. "wakamtoa nje ya Sinagogi," 9:22
24. "mlango wa kondoo," 10:7
25. "sikukuu ya kutabaruku," 10:22
26. kukufuru, 10:36
27. "akatafuta mwana kondoo, akakaa juu yake," 12:14
28. "saa," 12:23
29. "kisha baadaye shetani alimwingia," 13:27
30. "amri mpya," 13:34
31. "mahali pa kukaa," 14:2
32. "kukaa ndani yangu," 15:4
33. "akainua macho yake kuelekea mbinguni," 17:1
34. "Mungu wa Pekee wa kweli," 17:3
35. "kabla ya misingi ya ulimwengu," 17:24
36. akampiga mijeledi, 19:1
37. Gabatha, 19:13
38. Golgotha, 19:17
39. "walimwomba pilato miguu yao ivunjwe," 19:31
40. siku ya kiyahudi ya maandalio," 19:42

VIII. WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. Yohana, 1:6
2. Mwana wa Mungu, 1:34
3. Masihi, 1:41
4. Kefa, 1:42
5. Nikodemo, 3:1
6. Nabii, 7:40
7. Lazaro, 11:2
8. Pacha, 11:16
9. Yuda Iskariote, 13:2
10. Msaidizi, 14:26
11. Malko, 18:10
12. Anna, 18:24
13. Mariamu wa Klopa, 19:25

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Galilaya, 1:43
2. Nazareti, 1:45
3. Kana, 2:1
4. Kapernaumu, 2:12
5. Ainoni karibu na Salimu, 3:23
6. Samaria, 4:4

7. Tiberia, 6:1
8. Betlehemu, 7:42
9. Bethania, 11:1
10. Kedroni, 18:1
11. Bahari ya Tiberia, 21:1

X. MASWALI YA MJADALA

1. Kwanini Yohana 1:1 ni muhimu sana?
2. Kwanini Ubatizo wa Yohana haukuwa ule uliozoeleka?
3. Je kuzaliwa mara ya pili kuna maanisha nini?
4. Ni namna gani “kuamini” na “kutii” kunahusiana katika 3:35?
5. Mstari wa 4:24 una maanisha nini?
6. Kwanini Yohana 5:4 iko katika mabano?
7. Je 9:2 ina maanisha kuvaa mwili tena? Ikiwa sio, elezea kwanini?
8. Elezea mbinu ya kifasihi ya ukinyume wa 9:41
9. Elezea 10:34-35 kwa maneno yako mwenyewe.
10. Kwanini Yesu aliwaosha wanafunzi miguu katika sura ya 13? Ni nini mazingira ya sura za 13-17?
11. Kwanini Yohana 14:6 ni muhimu sana?
12. Kwanini Yohana 14:23 ni muhimu sana?
13. Elezea Yohana 15:16.
14. Yohana 17 inaitwa “maombi ya Kuhani Mkuu Yesu.” Anaomba kwa ajili ya watu watatu au makundi tofauti, wataje.
15. Elezea majibishano kati ya Yesu na Pilato katika Yohana 18:33-38
16. Je wanafunzi walipokea Roho katika 20:22 au wakati wa Pentekoste katika Matendo ya Mitume 1?
17. Kwanini Yohana 20:31 muhimu?

UTANGULIZI WA MATENDO YA MITUME

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Matendo ya Mitume inaunda muunganiko muhimu kati ya simulizi za maisha ya Yesu (Injili), mahubiri yao katika Matendo ya Mitume, ufasiri wao na kutumika kwake katika nyaraka za kitume za Agano Jipya.
- B. Kanisa la awali lilikuza na kushirikishana makusanyo mawili ya maandiko ya Agano Jipya: (1) Injili (Injili nne) na (2) Mitume (yaani, nyaraka za Paulo). Hata hivyo kwa uvumi za elimu ya Kristo za karne ya kwanza, thamani ya mkitababu cha Matendo ya Mitume kikadha dhahiri. Matendo ya Mitume kinafunua maudhui haya na kusudi la mahubiri ya kitume (*kerygma*) na matokeo ya kushangaza ya injili.
- C. Usahihi wa kihistoria wa Matendo ya Mitume umesisitizwa na kuthibitishwa na gunduzi za kisasa za akiolojia, hasa kwa kuhusiana na jina la wafanyakazi wa kiserikali wa Kirumi (mfano, *stratēgoi*, 16:20,22,35,36 [pia lilitumika juu ya kiongozi wa hekalu, Luka 22:4,52; Mdo. 4:1; 5:24-26]; *politarchas*, 17:6,8; na *prōtō*, Mdo. 28:7, kama vile A. N. Sherwin-White, *Roman Society and Roman Law in the New Testament*). Luka anaandika mivutano ndani ya kanisa la awali, hata mapigano kati ya Paulo na Barnaba (kama vile Mdo. 15:39). Hii inaaksi maandiko yenye uwiano sawa, usio wa ulali yaliyofanyiwa tafiti ya kihistoria.
- D. Jina la Kitabu linapatikana kwa utofauti kidogo wa miundo katika maandiko ya Kiyunani ya kale:
1. Maandiko κ (Sinaiticus), Tertullian, Didymus, Eusebius yana "Matendo ya Mitume" (ASV, NIV)
 2. Maandiko B (yaani, Vaticanus), D (yaani, Bezae) katika mchango wake, Irenaeus, Tertullian, Cyrian, Athanasius yana "Matendo ya Mitume" (KJV, RSV, NEB)
 3. Maandiko A² (yaani, marekebisho ya kwanza ya Alexandrinus), E, G, Chrysostom yana "Matendo ya Mitume Watakatifu"
- Inawezekana kwamba neno la Kiyunani *praxeis*, *praxis* (yaani, matendo, njia, tabia, kazi, shughuli) vinaaksi aina ya uwasilishaji wa kifasihi ambayo inaashiria maisha na matendo ya watu mashuhuri au wenye ushawishi (yaani, Yohana, Petro, Stephano, Philipo, Paulo). Kitabu kwa asili kinaweza kuwa hakina jina (kama Injili ya Luka).
- E. Kuna desturi za kipekee mbili za Matendo ya Mitume. Ile fupi ni yak i-Iskandria (MSS P⁴⁵, P⁷⁴, κ , A, B, C). Familia ya kimagharibi ya kimaandiko (P²⁹, P³⁸, P⁴⁸ na D) inaonekana kujumuisha maelezo mengi zaidi. Haijajulikana ikiwa yanatoka kwa mwandishi au yalikuwa maingizo ya baadaye yaliyofanywa na waandishi, wakijikita katika desturi za kanisa la kwanza. Wanazuoni wengi zaidi wa maandiko wanaamini kwamba maandiko ya magharibi yana maongezeko ya baadaye kwasababu (1) yanalainisha au yanajaribu kuweka hali isiyo ya kawaida au maandiko magumu; (2) yanaongeza maelezo ya nyongeza; (3) anaongeza tungo bainishi kuisitiza Yesu kuwa Kristo; na (4) hayanukuliwi na waandishi wa aina yoyote wa kale wakati fulani katika karne tatu za kwanza (kama vile F. F. Bruce, *Acts: Greek Text*, kur. 69-80). Kwa mjadala mrefu zaidi waweza kusoma A *Textual Commentary on the Greek New Testament* cha Bruce M. Metzger, kilichochapishwa na the United Bible Societies, kur. 259-272.

Kwasababu ya hesabu kubwa ya maongozoko ya baadae, fasiri hii haitajishughulisha na mibadala yote ya kimaandiko. Wakati utofauti wa kimaandiko utakapokuwa wa msingi katika kufasiri, ndipo itakapobidi na kulazimu tu fasiri hii kuijadili.

II. MWANDISHI

A. Kitabu hakina jina, lakini Luka linatumika zaidi.

1. Sehemu za upekee na za kushangaza za “sisi”, 16:10-17 (safari ya kimisionari ya pili huko Filipi); 20:5-15; 21:1-18 (mwisho wa safari ya kimisionari) na 27:1-28:16 (Paulo alipeleka Rumi kama mfungwa) inamaanishwa kwa msisitizo kwamba Luka ndiye mwandishi.
2. Muunganiko kati ya Injili ya tatu na Matendo ya Mitume ni dhahiri wakati mtu anapolinganisha Luka 1:1-4 na Matendo ya Mitume 1:1-2.
3. Luka, tabibu wa Mataifa, anatajwa katika Kol. 4:10-14, Filemoni 24, na 2 Timotheo 4:11 kama mwenza wa Paulo. Luka ndiye mwandishi wa Mataifa pekee katika Agano Jipya.
4. Shuhuda asiyetajwa wa kanisa la kwanza alisema.
 - a. Muratorian Fragment (180-200 B.K kutoka Rumi anasema, “kilitungwa na Luka, Tabibu”)
 - b. Maandiko ya Irenaeus (130-200 B.K.)
 - c. maandiko ya Clement wa Iskandria (156-215 B.K.)
 - d. maandiko ya Tertullian (160-200 B.K.)
 - e. maandiko ya Origen (185-254 B.K.)
5. Ushahidi wa ndani wa staili na misamiati (hasa misamiati ya kidaktari) inathibitisha Luka kuwa mwandishi (yaani, Sir William Ramsay na A. Harnack.

B. Tuna vyanzo vitatu vya taarifa kuhusu Luka.

1. Vifungu vitatu katika Agano Jipya (Kol. 4:10-4; Filemoni 24; 2 Tim. 4:11) na Kitabu cha Matendo chenyewe.
2. Dibaji ya karne ya pili ya Anti-Marcion juu ya Luka (160-180 B.K.)
3. Mwana historia wa kanisa la kwanza wa karne ya nne, Eusebius, katika chapisho lake *Ecclesiastical History*, 3:4, anasema “Luka kwa kabila, mzaliwa wa Antiokia na kwa kazi, ni tabibu, aliyejenga kufahamiana hasa na Paulo na akiongozana na mitume waliobakia kwa uchache sana, ametuachia sisi mifano ya uponywaji wa nafsi alioupata kutoka kwao katika vitabu viwili vilivyovuviwa, Injili na Matendo ya Mitume.”
4. Huu ni wasifu uliunganishwa wa Luka.
 - a. Mtu wa mataifa (anatajwa katika Kol. 4:12-14 pamoja na Epafra na Dema kama wasaidizi na sio wasaidizi wa Kiyahudi)
 - b. kutoka aidha Antiokia ya Shamu (ikiwa Dibaji ya Anti-Marcion kwa Luka) au Filipi ya Makedonia (yaani, Sir William Ramsay juu ya Matendo ya Mitume 16:19)
 - c. tabia (kama vile Kol. 4:14, au angalau mtu mwenye elimu ya juu)
 - d. alifanyika mwongofu wakati wa umri wa utu uzima wa kati baada ya kanisa kuanzishwa huko Antiokia (Dibaji ya AntiMarcion)
 - e. Mwenza wa kusafiri wa Paulo (sehemu za Matendo ya Mitume ya “sisi”)
 - f. Hakuwa ameo
 - g. aliandika Injili ya tatu na Matendo ya Mitume (utangulizi unaofanana na staili sawa na misamiati)
 - h. alikufa umri wa miaka 84 huko Boeotia

C. Ukosoaji wa uandishi wa Luka

1. Mahubiri ya Paulo akiwa Mlima Mars huko Athene anatumia vipengele vya kifalsafa vya Kiyunani na maneno kutengeneza msingi unaofanana (kama vile Mdo. 17), lakini Paulo, katika Rum. 1-2, anaonekana kuchukua “msingi unaofanana” (yaani, asili, shuhuda wa ndani wa kimaadili) kama si jambo muhimu.
2. Mahubiri ya Paulo na maoni katika Matendo ya Mitume yanamchukua yeye kama Mkristo wa Kiyahudi anayemuangalia Musa kwa umakini, lakini nyaraka za Paulo zinashusha Sheria kama jambo lenye tatizo na la kupita.
3. Mahubiri ya Paulo katika Matendo ya Mitume hayana shabaha ya kimatukio ya siku za mwisho kama vitabu vyake vya kwanza vinavyofanya (yaani, 1 na 2 Wathesalonike).
4. Maneno haya ya ulinganifu, staili na msisitizo yanavutia lakini hayatoi hitimisho. Wakati baadhi vigezo hivyo hivyo vinatumika kwa Injili, Yesu wa Vitabu vya Injili wanazungumza tofauti sana na Yesu wa Yohana. Bado wasomi wachache wangepata kwamba vyote viwili vinaaksi maisha ya Yesu.

D. Wakati wa kujadili uandishi wa Matendo ya Mitume ni muhimu sana tujadili vyanzo vya Luka kwasababu wasomi wengi (yaani, C. C. Torrey,) wanaamini Luka alitumia chanzo cha nyaraka Kiaramu (au desturi za kinywa) kwa sura nyingi kumi na tano za kwanza. Ikiwa hii ni kweli, Luka ni mhariri wa nyaraka hii, si mwandishi. Hata katika mahubiri ya baadaye ya Paulo, Luka anatoa tu muhtasari wa maneno ya Paulo na sio masimulizi ya kinywa. Matumizi ya Luka ya vyanzo ni kama muhimu kuwa na swali kama uandishi wake wa kitabu.

III. TAREHE

- A. Kuna mjadala mkuba sana na kutokukubaliana kuhusu muda wa kuandikwa kwa Matendo ya Mitume, lakini matukio yenyewe yanachukua kutokea mnamo mwaka 30-63 B.K. (Paulo aliachiliwa kutoka gerezani huko Rumi mnamo miaka ya kati ya 60 na kukamatwa upya na kuhukumiwa chini ya Nero yawezekana katika mateso ya mnamo mwaka 65 B.K.).
- B. Ikiwa mtu alidhanja asili ya toba ya kitabu kuhusu Serikali ya Kirumi hivyo tarehe (1) kabla ya mwaka wa 64 B.K. (mwanzo wa mateso ya Nero ya Wakristo katika Rumi) na/au (2) ikihusiana na mapinduzi ya Kiyahudi ya mwaka 66-73 B.K.
- C. Ikiwa mtu akilinganisha Matendo ya Mitume na Injili ya Luka katika mpangilio, hivyo tarehe kwa kuandikwa kwa injili kulichagiza tarehe ya kuandikwa kwa Matendo ya Mitume. Tokea kuanguka kwa Yerusalemu mikononi mwa Titus mnamo mwaka 70 B.K. (yaani Luka 21), lakini haelezewi, inaonekana kuwa katika tarehe kabla ya mwaka 70 B.K. Ikiwa ndivyo, basi Matendo ya Mitume, ikiandikwa kama matokeo, lazima iwekwe mnamo miaka ya 80.
- D. Ikiwa mtu atasumbuka na umalizikaji wa ghafla (yaani Paulo akiwa bado gerezani katika Rumi, F. F. Bruce), hivyo tarehe inayofanana na mwisho wa kifungo cha kwanza cha Kirumi cha Paulo mnamo mwaka 58-63 B.K, inapendelewa.
- E. Baadhi ya tarehe za kihistoria zinazofanana na matukio ya kihistoria inayoandikwa katika Matendo ya Mitume.
 1. kusambaa kwa njaa chini ya Claudius, Mdo. 11:28, 44-48 B.K.

2. kifo cha Herode Agrippa 1, Mdo. 12:20-23, 44 B.K. (kipupwe)
3. baraza la Sergius Paulus, Mdo. 13:7, alipoteuliwa mnamo mwaka 53 B.K.
4. kuondolewa kwa Wayahudi kutokea Rumi kulikofanywa na Claudius, Mdo. 18:2, 49 B.K. (?)
5. ujumbe wa baraza la Gallio, Mdo. 18:12, 51 B.K. au 52 (?)
6. ujumbe wa baraza la Felix, Mdo. 23:26; 24:27, 52-56 B.K. (?)
7. kuondolewa kwa Felix kwa kuwekwa Festo, Mdo. 24:27, 57-60 B.K. (?)
8. Wafanyakazi wa kirumi wa Yudea
 - a. Waendesha mashitaka
 - (1) Pontio Pilato, 26-36 B.K.
 - (2) Marcello, 36-37 B.K.
 - (3) Marullus, 37-41 B.K.
 - b. Mnamo mwaka 41 B.K. mbinu za kimashataka za utawala wa Kirumi ulibadilishwa kuwa mfano wa kwanza. Mfano wa Kirumi, Claudius, alimteua Herode Agrippa I mnamo mwaka 41 B.K.
 - c. Baada ya kifo cha Herode Agrippa I, 44 B.K., mbinu ya kimashataka ilianzishwa upya mpaka mwaka 66 B.K.
 - (1) Antonius Felix
 - (2) Porcius Festus

IV. MAKUSUDI NA MUUNDO

- A. Kusudi moja la kitabu cha Matendo ya Mitume ilikuwa kuandika ukuaji wa ghafla wa wafuasi wa Yesu: kutoka mizizi ya Kiyahudi kwenda kuwa huduma ya kiulimwengu; kutoka kujifungia chumba cha juu mpaka jumba la Kifalme la Kaisari
 1. Utaratibu huu wa kijiografia unafuata Matendo ya Mitume 1:8, ambayo ni Agizo Kuu la Matendo ya Mitume (Mt. 28:19-20).
 2. upanuzi huu wa kijiografia unaelezewa kwa njia kadhaa.
 - a. Kwa kutumia miji mikuu na mipaka ya kitaifa. Katika Matendo ya Mitume kuna nchi 32, miji 54 na visiwa 9 vya Mediterania vinavyotajwa. Miji mitatu ni Yerusalemu, Antiokia na Rumi (kama vile Mdo. 9:15).
 - b. kwa kutumia watu wa msingi. Matendo ya Mitume inaweza kugawanywa katika nusu mbili: huduma za Petro na Paulo. Kuna zaidi ya watu 95 wanaotajwa katika Matendo ya Mitume, lakini wakubwa ni: Petro, Stefano, Philipo, Barnaba, Yakobo na Paulo.
 - c. Kuna miundo miwili au mitatu ya kifasihi ambayo inatokea kwa kurudia rudia katika Matendo ya Mitume ambayo inaonekana kuaksi jaribio la kiufahamu la mwandishi katika muundo:

(1) kauli za kimuhtasari	(2) kauli za ukuaji	(3) matumizi ya hesabu
1:1 - 6:7 (huko Yerusalemu)	2:47	3:41
6:8 - 9:31 (huko Palestina)	5:14	4:4
9:32 - 12:24 (mpaka Antiokia)	6:7	5:14
12:25 - 15:5 (mpaka Asia Ndogo)	9:31	6:7
16:6 - 19:20 (mpaka Uyunani)	12:24	9:31
19:21 - 28:31 (mpaka Rumi)	16:5	11:21,24
	19:20	12:24
		14:1
		19:20

- B. Matendo ya Mitume kidhahiri kwa kuelewa vibaya kulikogubika kifo cha Yesu kwa kosa la uhaini. Inavyoonekana, Luka anaandika kwa Mataifa (Theophilo, yawezekana mfanyakazi wa Kirumi). Anatomia (1) hotuba ya Petro, Stephano, na Paulo kuonesha mikakati ya Wayahudi na (2) mtazamo chanya wa wafanyakazi wa serikali wa Kirumi juu ya Ukristo. Warumi hawakuwa na kitu cha kuwatia hofu juu ya wafuasi wa Yesu.
1. hotuba ya viongozi wa Kikristo
 - a. Petro, 2:14-40; 3:12-26; 4:8-12; 10:34-43
 - b. Stefano, 7:1-53
 - c. Paulo, 13:10-42; 17:22-31; 20:17-25; 21:40-22:21; 23:1-6; 24:10-21; 26:1-29
 2. mawasiliano na viongozi wa kiserikali
 - a. Pontio Pilato, Luka 23:13-25
 - b. Sergius Paulus, Mdo. 13:7,12
 - c. hakim mkuu wa Filipi, Acts Mdo. 16:35-40
 - d. Gallio, Mdo. 18:12-17
 - e. Asiarchs wa Efeso, Mdo. 19:23-41 (hasa mstari wa 31)
 - f. Claudius Lysias, Mdo. 23:29
 - g. Felix, Mdo. 24
 - h. Porcius Festus, Mdo. 24
 - i. Agrippa II, Mdo. 26 (hasa mstari wa 32)
 - j. Publius, Mdo 28:7-10
 3. Mtu anapolinganisha mahubiri ya Petro na ya Paulo, ni dhahiri kwamba Paulo ndiye mgunduzi, lakini mtangazaji mwaminifu wa kweli za Injili za Kitume. *Kerygma* iliyoungwa!
- C. Luka sio tu aliulinda Ukristo kabla ya serikali ya Kirumi, lakini pia alimtetea Paulo mbele ya kanisa la Mataifa. Paulo kwa kurudia rudia aliwakabili makundi ya Kiyahudi (yaani, wafia dini wa Kiyahudi Wagalatia, wale “mitume wakuu” wa 2 Kor. 10-13; na makundi ya Walimu wa uongo (yaani nadharia ya elimu ya uongo ya Wakolosai na Waefeso). Luka anaonesha hadhi ya Paulo kwa kufunua kwa usahihi moyo wake na thiolojia katika safari zake na mahubiri.
- D. Ingawa Matendo ya Mitume ilikusudiwa kuwa kitabu cha kimafundisho, hakiandiki kwa ajili yetu viashiria vya mahubiri ya kwanza ya Mitume ambayo C. H. Dodd ameyaita “the *Kerygma* (mafundisho ya kwanza ya kanisa)” (yaani kweli ya msingi kuhusu Yesu). Hii inatusaidia sisi kuona kile walichokihisi kuwa vitu muhimu vya injili, hasa pale walipolinganisha kifo cha Yesu na ufufuo.

MADA MAALUMU: MAFUNDISHO YA KANISA LA KWANZA

Kuna maoni mengi kuhusu Ukristo. Siku zetu hizi ni siku za wingi wa dini, kama ilivyokuwa karne ya kwanza. Binafsi, kwa pamoja nayajuisha na kuyakubali makundi yote yale yanayodai kumfahamu na kumwamini Yesu Kristo. Wote hatukubaliani kuhusu hili au lile lakini kimsingi ukristo ni kumhusu Yesu. Hata hivyo, kuna makundi yanayodai kuwa wapo wakristo ambao wanaonekana “kufanana.” Ni kwa vipi naweza kuelezea tofauti?

Sawa, kuna njia mbili:

- A. Kitabu kinachoweza kusaidia kujua kile makundi ya madhehebu ya kisasa yanaamini

(kutoka katika maandiko yao) *The Kingdom of the Cults* na Walter Martin.

B. Hotuba ya makanisa ya awali, hasa wale kupitia Mtume Petro na Paulo katika kitabu cha Matendo, wanatupatia maelezo ya msingi kwa vipi waandishi wa karne ya kwanza waliovuviwa waliueleza Ukristo kwenye makundi. “matamko” haya ya awali au “mafundisho” (ambacho kitabu cha matendo ni mhutajari wake) yanaendana na neno la Kiyunani *Kerygma*. Ufuatao ni ukweli halisi wa injili kuhusu Yesu katika Matendo ya Mitume:

1. Kutimiliza nabii nyingi za Agano la Kale- – Mdo. 2:17-21,30-31,34; 3:18-19,24; 10:43; 13:17-23,27; 33:33-37,40-41; 26: 6-7,22-23
2. Alitumwa na YHWH kama alivyoahidi- Mdo. 2:23; 3:26
3. Miujiza iliyotendeka kuthibitisha ujumbe wake na kudhihilisha huruma ya Mungu- – Mdo. 2:22; 3:16; 10:38
4. Waliofunguliwa, wasiomilikiwa- Mdo. 3:13-14; 4:11
5. Kusulubishwa – Mdo. 2:23; 3:14-15; 4:10; 10:39; 13:28; 26:23
6. Alifufuliwa kuja uzimani- Mdo. 2:24,31-32; 3:15,26; 4:10; 10:40; 13:30; 17:31; 26:23
7. Ameinuliwa mkono wa kulia wa Mungu Baba- Mdo. 2:33-36; 3:13,21
8. Atakuja tena mara ya pili – Mdo. 3:20-21
9. Alichaguliwa kuwa hakimu- Mdo. 10:42; 17:31
10. Akamtuma Roho Mtakatifu- Mdo. 2:17-18,33,38-39; 10:44-47
11. Mwokozi wa kila aminiye- Mdo. 13:38-39
12. Hakuna mwingine aliye mwokozi- Mdo. 4:12; 10:34-36

Hapa kuna baadhi ya njia za kukubali kwenye hizi nguzo za ukweli:

1. Tubu – Mdo. 2:38; 3:19; 17:30; 26:20
2. Amini – Mdo. 2:21; 10:43; 13:38-39
3. Ubatizwe – Mdo.2:38; 10:47-48
4. Mpokee Roho – Mdo. 2:38; 10:47
5. Yote yatakujilia- Mdo.2:39; 3:25; 26:23

Mpango huu ulitumika kama tamko la kanisa la mwanzo, ingawa waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaweza kuacha sehemu au wakasisitiza wengine hasa katika maandiko yao. Injili yote ya Marko kwa karibu inafuata dhana ya mafundisho. Marko kiutamaduni anaonekana kama kuitengeneza hotuba ya Petro, iliyohubiriwa huko Roma, katika injili iliyoko kwenye maandishi. Injili zote za Mathayo na Luka zinafuata muundo wa Marko.

- E. Frank Stagg katika fasiri yake, *The Book of Acts, the Early Struggle for an Unhindered Gospel*, anaeleza kusudi kuwa kimsingi upelekwaji wa ujumbe kuhusu Yesu (yaani injili) kutoka katika Dini ya Kiyahudi ya mkazo ya kitaifa kwa ujumbe wa ulimwengu kwa wanadamu wote. Fasiri ya Stagg inajikita katika makusudi ya Luka katika maandiko ya Matendo ya Mitume. Muhtasari mzuri na uchambuzi wa nadharia tofauti tofauti inapatikana katika ukurasa wa 1-18. Stagg anachagua kujikita katika neno “isiyofichwa” katika 28:31, ambayo sio njia ya kawaida ya kuhitimisha kitabu, kama ufunguo wa kuelewa msisitizo wa Luka katika kuenea kwa Ukristo kwa kushinda vikwazo vyote.
- F. Ingawa Roho Mtakatifu anatajwa zaidi ya mara hamsini katika Matendo ya Mitume, sio “Matendo ya Roho Mtakatifu.” Kuna sura kumi na moja ambapo Roho hatajwi. Anatajwa zaidi mara kwa mara katika nusu ya kwanza ya Matendo ya Mitume ambapo Luka ananukuu vyanzo vingine (yaweze kana kiasili iliandikwa katika Kiaramu). Matendo hajimzungumzii Roho kama ambavyo Injili zinavyomzungumzia Yesu! Hii haijakusudiwa kushusha nafasi ya Roho, bali kutulinda kutoka katika kujenga thiolojia ya Roho kimsingi au kiukamilifu katika Matendo ya Mitume.

- G. Matendo ya Mitume haijakusudiwa kufundisha fundisho (kama vile Fee na Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 94-112). Mfano wa hili unaweza kuwa jaribio kujikita msingi wa thiolojia ya uongofu kutoka Matendo ya Mitume ambayo imekusudiwa kushindwa. Mpangilio na viashiria vya uongofu vinatofautiana katika Matendo ya Mitume; hivyo, utaratibu gani ni wa kitabia wa kawaida? Sharti tutazame Nyaraka kwa ajili ya msaada wa kimafundisho.

Hata hivyo, inafurahisha kwamba baadhi ya wasomi (yaani, Hans Conzelmann) wameona Luka kimakusudi wakiweka mtazamo mpya wa kithabiti wa matukio ya siku za mwisho wakati wa karne ya kwanza pamoja na mjongeo wa huduma ya subira kwa Kurudi kwa Mara ya Pili kwa Yesu kulikochelewa. Ufalme uko hapa katika nguvu sasa, ukibadilisha maisha. Kanisa linatenda kazi sasa kwa kufanyika shabaha, sio tumaini la matukio ya siku za mwisho.

- H. Kusudi lingine la Matendo ya Mitume laweza kuwa sawasawa na Rum. 9-11, kwanini Wayahudi walimkataa Masihi wa Kiyahudi na kanisa linakuwa linaundwa zaidi na watu wa Mataifa? Sehemu kadhaa katika Matendo ya Mitume kiasili ulimwenguni kote yanashangiliwa. Yesu anawatuma ulimwenguni kote (kama vile 1:8). Wayahudi wanamkataa lakini Mataifa wanamwitikia Kwake. Ujumbe wake unafika Rumi.

Inawezekana kwamba kusudi la Luka ni kuonesha kwamba Ukristo wa Kiyahudi (yaani, Petro) na Ukristo wa Mataifa (yaani, Paulo) wanaweza kuishi kwa pamoja na kukua pamoja! Hawako katika mashindano bali wameungana katika uinjilishaji wa ulimwengu.

- I. Kadiri kusudi linavyohusika, nakubaliana na F. F. Bruce (yaani, *New International Commentary*, kur. 18) kwamba kwakuwa Luka na Matendo ya Mitume vilikuwa kiasili juzuu moja, kwamba dibaji ya Luka (yaani, 1:1-4) inafanya kazi pia kwa Matendo ya Mitume. Luka licha ya kuwa si shuhuda wa macho wa matukio yote, kwa uangalifu aliyatafiti na kuyaandika kwa usahihi, akitumia mfumo na muundo wake mwenyewe wa kihistoria, kifasihi na kithiolojia.

Hivyo, Luka katika Injili zote mbili na simulizi, anataka kuonyesha uhalisia wa kihistoria na uaminifu wa kithiolojia (kama vile Luka 1:4) wa Yesu na kanisa. Inaweza kuwa kwamba shabaha ya Matendo ya Mitume ni maudhui ya utimilizwaji (yaani, isiyofichwa, kama vile 28:31, ambapo ni neno la mwisho la kitabu). Maudhui haya yanabebwa na kuzungumzwa mbele kwa maneno kadhaa tofauti tofauti na tungo (kama vile Walter L. Liefeld, *Interpreting the Book of Acts*, kur. 23-24). Injili sio jambo lililofikiriwa fikiriwa mara mbili, mpango B, au jambo jipya. Ni mpango wa kale wa hapo kabla wa Mungu (kama vile Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29).

V. AINA YA UWASILISHAJI

- A. Matendo ya Mitume kwa Agano Jipya ni kile Yohua-2 Wafalme vilivyo kwa Agano la Kale, simulizi za kihistoria. Simulizi za kihistoria za kibiblia ni za kweli japo shabaha haipo katika mtiririko au kumbukumbu za kina na undani wa kutosha wa matukio. Inachagua matukio kadhaa ambayo yanaelezea Mungu kuwa ni nani, sisi ni nani, tunavyopatanishwa na Mungu, namna gani Mungu anatumia tuishi naye.
- B. Tatizo katika kutafsiri simulizi za kibiblia ni kwamba waandishi huwa hawaweki katika maandiko (1) nini yaliyo makusudi yao, (2) nini iliyo kweli kuu, au (3) kwa namna gani tunaweza kuiga vitu hivi vilivyoandikwa. Msomaji anahitaji kufikiri kwa kupitia maswali yafuatayo:
1. Kwanini tukio hili linaandikwa?

2. Ni kwa namna gani linahusiana na nyaraka ya Biblia iliyopita?
3. Nini kweli kuu ya kithiolojia?
4. Je kuna umuhimu kwa muktadha wa kifasihi? (Tukio gani linaloanza au kufuata? Je somo hili limeshughulikiwa mahali pengine?)
5. Muktadha wa kifasihi ni mkubwa kiasi gani? (Wakati fulani kiasi kikubwa cha masimulizi yanaunda maudhui ya kithiolojia au kusudi.)

C. Simulizi za kihistoria hazitakiwi kuwa chanzo kimoja tu cha fundisho. Mara kwa mara vitu vinaandikwa ambavyo ni vidogo kwa makusudi ya mwandishi. Simulizi ya kihistoria inaweza kuelezea kweli zilizoandikwa mahali pengine katika Biblia. Kwasababu tu kitu fulani kilitokea haimaanishi ni mapenzi ya Mungu kwa waamini wote wa nyakati zote (mfano, kujiua, kuwa na wake wengi, vita vitakatifu, kushika nyoka, n.k).

D. Mjadala bora zaidi wa kimuhtasari juu ya namna gani ya kufasiri simulizi za kihistoria upo katika toleo la Gordon Fee na Douglas Stuart's *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 78-93 na 94-112.

VI. ORODHA YA VITABU VINGINE VYA MAZINGIRA YA KIHISTORIA

Vitabu vipya vinavyoweka Matendo ya Mitume katika mazingira ya karne ya kwanza vilizalishwa na washiliaji wa msimamo wa kigezo cha Desturi. Mjongeo huu wa kati wa kitaaluma hakika umesaidia katika uelewa wa Agano Jipya. Mrandano huu unahaririwa na Bruce M. Minter.

- A. *The Book of Acts in Its Ancient Literary Setting*
- B. *The Book of Acts in Its Graeco-Roman Setting*
- C. *The Book of Acts and Paul in Roman Custody*
- D. *The Book of the Acts in Its Palestinian Setting*
- E. *The Book of Acts in Its Diaspora Setting*
- F. *The Book of Acts in Its Theological Setting*

Pia vingine vinavyoweza kusaidia ni:

1. A. N. Sherwin-White, *Roman Society and Roman Law in the New Testament*
2. Paul Barnett, *Jesus and the Rise of Early Christianity*
3. James S. Jeffers, *The Greco-Roman World*

VII. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "kwa dalili nyingi," 1:3
2. "siku arobaini," 1:3
3. "ufalme wa Mungu," 1:3
4. "wingu likampokea," 1:9
5. "wapata mwendo wa sabato," 1:12
6. "konde la Damu," 1:19
7. "kura," 1:26
8. "Pentekoste," 2:1
9. "wakajazwa na Roho Mtakatifu," 2:4
10. "kusema kwa lugha nyingine," 2:4
11. "waongofu," 2:10; 13:43

12. "shauri na kusudi la Mungu," 2:23
13. "kuzimu," 2:31
14. "mkono wa kuume wa Mungu," 2:33
15. "tubuni," 2:38; 3:19
16. "kuumega mkate," 2:42,46
17. "saa ya kusali," 3:1
18. "akiomba sadaka," 3:2
19. "tao la Sulemani," 3:11; 5:12
20. "Mtakatifu na Mwenye Haki," 3:14
21. "nyakati za kuburudishwa," 3:19
22. "watu wasio na elimu, wasio na maarifa," 4:13
23. "akalala," 7:60
24. "Njia," 9:2
25. "wakawawekea mkono," 9:12 (cf. 8:17)
26. "kikosi," 10:1
27. "Wakristo," 11:26
28. "kuagua," 16:16
29. "na nyumba yake yote," 16:33
30. "Waepikureo," 17:18
31. "Wastoiko," 17:18
32. "Areopago," 17:22
33. "Wayahudi wapunga pepo," 19:13
34. "uganga. . . vitabu," 19:19
35. "vihekalu vya fedha vya Artemi," 19:24

VIII. WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

1. Theophilo, 1:1
2. wanawake, 1:14
3. Matthiya, 1:23
4. Masadukayo, 4:1; 5:17
5. Anna, 4:6
6. Kayafa, 4:6
7. "watawala na wazee wa watu," 4:8
8. Anania, 5:1; 9:10
9. Safira, 5:1
10. Gamalieli, 5:34
11. Stefano, 6:5
12. Sauli, 7:58; 8:1; 9:1
13. Philipo, 8:5
14. Dorkasi, 9:36
15. Kornelio, 10:1
16. Agabo, 11:28; 21:10
17. Yutiko, 20:9

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Yerusalemu, 1:8
2. Yudea, 1:8
3. Samaria, 1:8
4. Wa-Parthia, 2:9
5. Kapadokia, 2:9
6. Ponto, 2:9
7. Asia, 2:9
8. Firigia, 2:10
9. Pamfilia, 2:10
10. Misri, 2:10
11. Libia, 2:10
12. Kirene, 2:10
13. Wakreta, 2:11
14. Nazareti, 2:22
15. Alexandria, 6:9
16. Kilikia, 6:9
17. Dameski, 9:2
18. Kaisaria
19. Yafa, 9:36
20. Foinike, 11:19
21. Kipro, 11:20
22. Tarso, 11:25
23. Sidoni, 12:20
24. Filipi, 16:12
25. Beroya, 17:10
26. Athene, 17:16
27. Korintho, 18:1

X. MASWALI YA MJADALA

1. Ni kwa namna gani 1:6 inafunua ukosefu wa maarifa ya Mitume?
2. Ni kwa namna gani 1:8 inahusiana na Mt. 28:19-20?
3. Orodhesha sifa za mtume (1:22).
4. Kwanini “upepo” na “moto” vinahusianishwa na Roho? (2:2-3)
5. Elezea muujiza wa 2:8.
6. Petro anasema unabii wa Yoeli umetimilizwa. Ni kwa namna gani unaweza kuelezea 1:17 na 19-20?
7. Ni nini umuhimu wa kithiolojia wa Yesu kuitwa “Bwana” na “Kristo”? (2:36)
8. Je 2:44 ni mamlaka ya kibiblia ya ujamaa? (kama vile 4:34-35)
9. Elezea maana ya 3:18.
10. Elezea namna gani Agano la Kale katika 4:11 inahusiana na Yesu
11. Je kujazwa kwa Roho siku zote kunahusianishwa na kushuhudia katika Matendo ya Mitume?
12. Orodhesha sifa za “Saba” katika Matendo ya Mitume 6. Je walikuwa mashemasi?
13. Kwanini Sauli alikasirishwa sana na Wakristo? (8:1-3)
14. Je 8:15-16 inatoa mpangilio wa matukio ya wokovu kwa waamini wa kisasa?
15. Ni nini makusudi ya ndimi katika 10:44-48?

16. Kwanini Paulo kwanza alihubiri katika masinagogi ya maeneo ya karibu na kwake? (13:5)
17. Ni nini kilitokea huko Listra ambacho kilisababisha Paulo na Barnaba kuchana mavazi yao? (14:8-18)
18. Nini yalikuwa makusudi ya Baraza la Yerusalemu katika Mdo.15?
19. Kwa nini Paulo na Barnaba wapingana? (15:36-41)
20. Kwanini Roho alimkataza Paulo asiende Asia? (16:6)
21. Kwanini viongozi wa mji walikuwa wana huzuni katika 16:35-40?
22. Ni kwa namna gani Prisila na Akila walimsaidia Apollo? (18:24-28)
23. Kwanini 20:21 ni mstari muhimu?
24. Ni nini maana ya 21:9?
25. Kwanini Paulo alifungwa huko Yerusalemu katika Mdo. 21?
26. Elezea 23:6-7 kwa maneno yako mwenyewe.

UTANGULIZI WA WARUMI

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Warumi ni kitabu cha mtume Paulo cha mfumo wa hali ya juu na mafundisho yenye mantiki ya Mtume Paulo. Kiliathiriwa na hali ya mambo ya Rumi, hivyo basi ni nyaraka za “mara moja.” Wakati mwingine hutokea kwamba kwa sababu Paulo aliandika nyaraka. Hata hivyo ni maandiko makuu ya Paulo yasiyopendelea upande wowote, katika njia ya Paulo ya kuhusika na tatizo (inawezekana kuwaonea wivu kati ya Wayahudi waaminio na uongozi wa mataifa) ulikuwa ni uwakilishi wa wazi wa injili na kuhusisha maisha ya kila siku.
- B. Uwasilishaji wa Paulo katika injili kwenye Warumi una matokeo ya uzima wa kanisa katika kila nyakati:
1. Augustine aliamini katika mwaka wa 386 B.K kwa kusoma Warumi 13:13-14.
 2. Ufahamu wa Martin Luther juu ya wokovu ulibadilika kabisa katika mwaka wa 1513 B.K kama alivyolinganisha Zab. 31:1 na Rum. 1:17 (kama vile. Hab. 2:4).
 3. John Wesley aliamini katika mwaka wa 1738 B.K kwa kuyasikiliza mahubiri ya Luther katika utangulizi wa kitabu cha Warumi.
- C. Kufahamu kitabu cha Warumi ni kuufahamu Ukristo! Nyaraka ina muundo wa maisha na mafundisho ya Yesu msingi wa kweli kwa ajili ya kanisa kwa nyakati zote.

II. UANDISHI

Paulo bila shaka alikuwa ni mwandishi. Mfano moja wa salamu yake unapatikana katika 1:1. Kwa ujumla inakubalika kwamba “mwiba katika mwili” wa Paulo ulikuwa ni tatizo la macho, hivyo basi, hakuandika nyaraka zake mwenyewe, lakini alimtumia mwandishi, Tertio (kama vile 16:22).

III. TAREHE

- A. Inaelekea tarehe ya uandishi wa kitabu cha Warumi ni mwaka wa 56-58 B.K. Hiki ni mojawapo ya vitabu vichache vya Agano jipya ambavyo vinaweza kuwa na tarehe sahihi. Hili limefanyika kwa kulinganisha Mdo. 20:2 na kuendelea na Warumi 15:17 na kuendelea. Kitabu cha Warumi inawezekana kiliandikwa huko Korintho kuelekea mwisho wa safari ya tatu ya umisionari wa Paulo, muda mfupi kabla hajaelekea Yerusalemu.
- B. Inawezekana mtiririko wa maandiko ya Paulo ulifuatwa na F. F. Bruce na Murry Harris na mabadiliko kidogo.

<u>Kitabu</u>	<u>Tarehe</u>	<u>Mahali kilipoandikwa</u>	<u>Uhusiano katika Matendo ya mitume</u>
1. Wagalatia	48	Antiokia Shamu	14:28; 15:2
2. I Wathesalonike	50	Korintho	18:5
3. II Wathesalonike	50	Korintho	
4. I Wakorintho	55	Efeso	19:20
5. II Wakorintho	56	Masedonia	20:2
6. Warumi	57	Korintho	20:3
7.-10. Nyaraka za kifungoni			
Wakolosai	mwanzoni miaka ya 60		
Waefeso	mwanzoni miaka ya 60	Rumi	
Filemoni	mwanzoni miaka ya 60		
Wafilipi	mwishoni mwaka wa 62-63		28:30-31
11.-13. Safari ya nne ya umisionari			
I Timotheo	63 (au mwishoni,	Makedonia	

Tito II Timotheo	63 lakini kabla ya 64 B.K. 68)	Efeso (?) Rumi
---------------------	-----------------------------------	-------------------

IV. WAPOKEAJI

Nyaraka inaelezea hitimisho lake Rumi. Hatufahamu ni nani mwanzilishi wa kanisa huko Rumi:

- A. Yumkini ikawa ni baadhi ya watu waliotembelea Yerusalemu katika siku ya Pentekoste na wakaamini na kurudi makwao na kuanzisha kanisa (kama vile Mdo. 2:10);
- B. inaweza kuwa ni wanafunzi waliokimbia mateso katika Yerusalemu baada ya kifo cha Stefano (kama vile Mdo 8:4); au
- C. Inawezekana ni waamini kutokana na safari za umisionari wa Paulo waliosafiri kwenda Rumi. Paulo kamwe hakuwahi kulitembelea kanisa hili, lakini aliazimia kwenda (kama vile. Mdo 19:21). Alikuwa na marafiki wengi huko (kama vie. Rum. 16).

Ni dhahiri mpango wake ulikuwa ni kutembelea Rumi akielekea Spania (kama vile Rum. 15:28) baada ya safari yake ya Yerusalemu na “zawadi ya upendo.” Paulo alihisi huduma yake katika Mediterania mashariki ilikuwa imekamilika. Alitafuta maeneo mapya (kama vile. 16:20-23). Matunda ya nyaraka kutoka kwa Paulo akiwa Uyunani kwenda Rumi inaonekana yana Fibi, kutoka Kenkrea, aliyesafiri katika njia hiyo (kama vile Rum. 16:1). Kwa nini nyaraka hii, iliandikwa katika mitaa ya nyuma ya Korintho kwenye karne ya kwanza na mtengeneza hema wa kiyahudi, ina umuhimu? Martin Luther anakiita “kitabu kikuu katika Agano jipya na injili halisi.” Uthamani wa kitabu hiki unapatikana katika ukweli kwamba ni maelezo ya kina sana ya injili kwa mwalimu wa sheria aliyeamini, Sauli wa kutoka mji wa Tarso, kuitwa kuwa mtume wa mataifa. Nyaraka nyingi za Paulo ni thabiti zilizofunikwa kwa maeneo maalumu, lakini sio kwa Warumi. Ni utaratibu wa uwakilishi wa maisha marefu ya imani ya mtume.

Je unatambua, jumuiya ya kikristo, kwamba maneno ya kiufundi yanayotumika leo kuelezea “imani” (“haki,” “shutuma,” “kukubali,” na “utakatifu”) yanatoka katika Warumi? Muombe Mungu akufungulie nyaraka hii ya kushangaza kwako kama tunavyotafuta pamoja kwa mapenzi yake kwa ajili ya maisha yetu leo!

V. KUSUDI

- A. Kujitokeza kwa ajili ya msaada wa safari yake ya umisionari kwenda Spania. Paulo aliona kazi yake ya kitume mashariki mwa Mediterania imekamilika (kama vile. 16:20-23).
- B. Kuelezea tatizo katika kanisa la Warumi kati ya Wayahudi waaminio na Wamataifa waaminio. Hii inawezekana kuwa ni matokeo ya kuondolewa kwa Wayahudi wote kutoka Rumi na mwishowe kurudishwa kwao. Hivyo basi viongozi wa Kiyahudi wa kikristo waliwekwa tena na viongozi wa kikristo wa mataifa.
- C. Kujitambulisha yeye mwenyewe kwa kanisa la Warumi. Kulikuwa na upinzani mwingi kwa Paulo tangu alipokuwa myahudi mwaminifu katika Yerusalemu (baraza la Yerusalemu la Mdo. 15), kutoka kwa wayahudi wasio waaminifu (Uyahudi kwa Wagalatia na II Kor. 3, 10-13), na kutoka kwa Wamataifa (Wakolosia, Waefeso) walio jaribu kuunganisha injili na chaguo lao la nadharia au falsafa.
- D. Paulo alishutumiwa kuwa ni mzushi hatari, aliyeongeza kutokujali mafundisho ya Yesu. Kitabu cha Warumi kilikuwa ni njia yake ya utaratibu wa kujilinda yeye kwa kuonyesha kwa namna gani injili yake ilikuwa ya kweli, akitumia Agano la kale na mafundisho ya Yesu (injili).

VI. MAELEZO YA MUHTASARI

- A. Utangulizi (1:1-17)
 1. Salamu (1:1-7)

- a. Mwandishi (1-5)
 - b. Hitimisho (6-7a)
 - c. Salamu (7b)
2. Tukio (1:8-15)
 3. Dhamira (1:16-17)
- B. Mahitaji ya Haki ya ki-Ungu (1:18-3:20)
1. Kukataliwa kwa Wamataifa ulimwenguni (1:18-32)
 2. Unafiki wa Wayahudi au maadili ya upagani (2:1-16)
 3. Hukumu kwa Wayahudi (2:17-3:8)
 4. Shutuma Ulimwenguni (3:9-20)
- C. Haki ya Ki-Ungu ni nini (3:21-8:39)
1. Haki kwa njia ya imani pekee (3:21-31)
 2. Msingi wa haki: Ahadi ya Mungu (4:1-25)
 - a. Kusimama katika haki ya Ibrahimu (4:1-5)
 - b. Daudi (4:6-8)
 - c. Uhusiano wa Ibrahimu katika tohara (4:9-12)
 - d. Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu (4:13-25)
 3. Kupata haki (5:1-21)
 - a. Mwelekeo wa jambo: upendo usio stahili, furaha isiyo sawa (5:1-5)
 - b. msingi wa kusudi: upendo wa ajabu wa Mungu (5:6-11)
 - c. taipolojia ya Adamu/Kristo: dhambi ya Adamu, utoaji wa Mungu (5:12-21)
 4. Haki ya kiroho ni jambo la lazima katika haki binafsi (6:1-7:25)
 - a. kuwa huru mbali na dhambi (6:1-14)
 - (1) kusudi la kudhaniwa (6:1-2)
 - (2) Maana ya ubatizo (6:3-14)
 - b. Mtumwa wa shetani au mtumwa wa Mungu: uchaguzi wako (6:15-23)
 - c. Ndoa ya mwanadamu kwa sheria (7:1-6)
 - d. sheria ni njema, lakini dhambi huzuia mema (7:7-14)
 - e. mapambano ya ndani ya mema na mabaya kwa waaminio (7:15-25)
 5. matokeo dhahiri ya haki ya ki-Ungu (8:1-39)
 - a. uzima katika Roho (8:1-17)
 - b. Ukombozi wa uumbaji (8:18-25)
 - c. Msaada thabiti wa Roho (8:26-30)
 - d. hukumu ya ushindi wa haki kwa imani (8:31-39)
- D. Kusudi la ki-Ungu kwa wanadamu wote (9:1-11:32)
1. kuchaguliwa kwa Israeli (9:1-33)
 - a. mrithi halisi wa imani (9:1-13)
 - b. ufalme wa Mungu (9:14-26)
 - c. mpango wa Mungu ulimwenguni unahusisha wapagani (9:27-33)
 2. Wokovu wa Israeli (10:1-21)
 - a. Haki ya Mungu dhidi ya haki ya mwanadamu (10:1-13)
 - b. Rehema ya Mungu inamlazimisha mjumbe, kwa ajili ya wito ulimwenguni (10:14-18)
 - c. Israeli inaendelea na mashaka katika Kristo (10:19-21)
 3. kutokufanikiwa kwa Israeli (11:1-36)
 - a. mabaki ya kiyahudi (11:1-10)
 - b. wivu wa kiyahudi (11:11-24)
 - c. upofu wa kitambo kidogo wa Israeli (11:25-32)
 - d. sifa za Paulo juu ya Mungu (11:33-36)

- E. Matokeo ya kipawa cha haki ya kiroho (12:1-15:13)
1. wito wa utakaso (12:1-2)
 2. matumizi ya vipawa (12:3-8)
 3. Mahusiano ya waaminio na waaminio wengine (12:9-21)
 4. Mahusiano na mamlaka (13:1-7)
 5. Mahusiano na jirani (13:8-10)
 6. Mahusiano na Bwana wetu (13:11-14)
 7. Mahusiano na ushirika wa wanajumuiya wa kanisa (14:1-12)
 8. Matokeo yetu kwa wengine (12:13-23)
 9. Mahusiano katika kumfanana Kristo (15:1-13)

- F. Hitimisho (15:14-33)
1. Mipango binafsi ya Paulo (15:14-29)
 2. Mahitaji kwa ajili ya maombi (15:30-33)

- G. Nyongeza ya maneno (16:1-27)
1. Salamu (16:1-24)
 2. Baraka (16:25-27)

VII. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. mtume, 1:1
2. "ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili," 1:3
3. watakatifu, 1:7
4. haki, 1:17
5. hasira ya Mungu, 1:18
6. kutubu, 2:4
7. "hakuna upendeleo kwa Mungu," 2:11
8. kutahiriwa, 2:25
9. "mausia ya Mungu," 3:2
10. haki, 3:4
11. upatanisho, 3:25
12. "mfurahi katika dhiki pia," 5:3
13. "tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake," 5:9
14. "kipawa cha haki," 5:17
15. "yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi," 6:7
16. kutakaswa, 6:19
17. "Roho wa Mungu anakaa ndani yenu," 8:9
18. Abba, 8:15
19. saburi, 8:25
20. aliowajua, 8:29
21. aliwachagua, 8:29
22. akawatukuza, 8:29
23. "mkono wa kuume wa Mungu," 8:34
24. "mamlaka . . .uwezo," 8:38
25. kufanywa mwana, 9:4
26. maagano, 9:4
27. "jiwe likwazalo," 9:33
28. kukiri," 10:9
29. kuamini, 10:4,11
30. matawi ya asili, 11:21

31. siri, 11:25
32. Amina, 11:36
33. mkifuata ukarimu, 12:13
34. laana, 12:14
35. "aitii mamlaka iliyo kuu," 13:1
36. "tuyavue. . .kuzivaa," 13:12
37. "dhaifu wa imani," 14:1
38. "sisi tulio na nguvu," 15:1

VIII. WATU WA KUWATAMBUA KI-MUHTASARI

1. Ibrahimu, 4:1
2. mababu, 9:5
3. Esau, 9:13
4. Baali, 11:4
5. Fibi, 16:1
6. Priska na Akila, 16:3
7. Yunia, 16:7 (KJV, Yunia)
8. Tertio, 16:22

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Rumi, 1:7
2. Kenkrea, 16:1

X. MASWALI YA MJADALA

1. Kwa nini 1:16 ina tabia za uandishi wa Paulo?
2. Ni kwa njia gani mbili wanadamu wote humtambua Mungu? (yaani, Sura 1-2)
3. Ni kwa namna gani 1:26-27 inaelezea jambo la mapenzi ya jinsi moja kwa sasa?
4. Ni kwa namna gani 2:6 inasimulia Gal. 6:7?
5. Katika sura ya 3 kifungu cha 9-18 ni mfuatano wa dondoo za Agano la kale. Je zote zina rejelea ukweli wa kithiolojia?
6. Kwa nini 4:6 ni ya muhimu sana?
7. Elezea 4:15 kwa maneno yako.
8. Ni nini 5:8 inakisema kuhusu Mungu?
9. Ni kwa namna gani 5:18 na 19 zinafanana?
10. Elezea utendaji wa kujiingiza kwenye shutuma wa 6:11.
11. Warumi 6:23 inaitwa injili katika gamba la kokwa, kwa nini?
12. Elezea tofauti iliyopo kati ya "hali mpya ya Roho" na "hali ya zamani ya andiko."(7:6)
13. Ni nani sura ya 7 inamwelezea?
14. Ni nini ambacho 7:7-12 inasema juu ya kusudi la sheria ya Agano la kale?
15. Ni kwa namna gani 7:19 inatumika kwa maisha yako?
16. Eleza 8:22 kwa maneno yako mwenyewe.
17. Je! Isaya 8:26-27 inaongelea juu ya kunena kwa lugha mpya?
18. Ni kwa namna gani 8:28 inasimuliwa 8:29?
19. Ni nini lengo la kipengele cha fasihi, sura ya 9-11?
20. Elezea 10:4 kwa maneno yako mwenyewe.
21. Elezea 11:7 kwa maneno yako mwenyewe.
22. Elezea 11:26 kwa maneno yako mwenyewe.
23. Je! Vipawa vilivyotajwa katika sura ya 12 bado vinafaa na kutumika?
24. Elezea 12:20 kwa maneno yako mwenyewe.
25. Elezea 14:14 kwa maneno yako mwenyewe.
26. Elezea 14:23 kwa maneno yako mwenyewe.

UTANGULIZI WA I WAKORINTHO

(USHAURI WA KIUTENDAJI KWA KANISA LENYE KUTAABIKA)

I. UPEKEE WA I WAKORINTHO

- A. Hii ilinakiliwa mara nyingi na makasisi wa kanisa la kale kipindi cha mwanzo kuliko maandiko mengine ya Paulo yenye kuonyesha umuhimu na matumizi yake.
- B. Katika Muratorian Fragment, ambayo ilikuwa orodha ya vitabu vya kisheria kutoka Rumi (200 B. K), hiki kinaorodheshwa kama maandiko ya kwanza ya Paulo ambayo pia yanaonyesha umuhimu wake.
- C. Paulo anaweka utofauti katika barua hii ya kiutendaji kati ya maoni yake binafsi na amri za Bwana. Hata hivyo, hiki kinajikita katika maarifa ya mafundisho ya Yesu katika kila jambo. Kama angeliyafuatisha maneno ya Yesu. Huyu aliyaamini mawazo yake ambapo pia alivuviwa na kupewa mamlaka katika hayo (kama vile 7:25, 40).
- D. Kanuni ya mwongozo wa Paulo kwa ushirika wa kanisa ni ule uhuru binafsi wa waamini, lakini pia ni kipimo cha jukumu la kipimo chao, kanuni hii haikujikita katika sheria, bali katika pendo. Afya na ukuaji wa kanisa zima hupelekea upendeleo binafsi au kipaumbele (kama vile 12:7).
- E. Barua hii (kandokando na II Wakorintho) inatupatia mtazamo wa awali katika kuliangalia kanisa la Agano Jipya, muundo wake, njia, na ujumbe. Hata hivyo, pia lazima ikumbukwe kwamba kanisa hili lilikuwa likipitia msukosuko, halikuwa na ufanano wa kusanyiko.

II. MJI WA KORINTHO

- A. Chochoro za kuelekea eneo la uvuvi kandokando ya eneo la kusini hasa karibia na Uyunani (yaani, Rasi ya Malea) zilikuwa hatari sana. Hivyo, safari fupi sana ya nchi kavu ilikuwa ya muhimu. Eneo la kijiografia la Korintho sehemu ya nchi kavu yapata maili nne kati ya Ghuba ya Korintho (yaani, Bahari ya Adriatic) na Ghuba ya Saronic (yaani, Bahari ya Aegean) yote haya yaliufanya mji huu kuwa wa uvuvi wa kibiashara, biashara (kubobea katika aina mbalimbali za uhunzi na aina ya kipekee ya shaba), na kituo cha kijeshi. Katika siku zile za Paulo mji huu ulikuwa wa kifasihi ambapo tamaduni za Mashariki na Magharibi zilikutana.
- B. Pia mji wa Korintho ulikuwa kituo kikubwa cha kitamaduni cha ulimwengu wa Uyunani-Rumi kwa sababu ilianzishwa Michezo ya ki-Isthmia kwa mwaka mnamo mwaka 581 K.K. (katika Hekalu la Poseidon). Ni Michezo ya Olimpiki pekee iliyokuwa huko Athene, kila baada ya miaka minne, hii iliwaweka katika ulinganifu na umuhimu (Thucydides, *Hist.* 1.13.5).
- C. Katika mwaka 146 K. K. mji wa Korintho uliingizwa katika maasi (yaani, Umoja wa Achaia) dhidi ya Rumi na uliangamizwa na Generali wa Kirumi Lucius Mummius na idadi kubwa ya Wayunani walipelekwa utumwani. Kwa sababu ya umuhimu wa kiuchumi na kijeshi mji huu ulijengwa upya kwa vyo vyote vile mnamo mwaka 46 au 48 K.K. na Julius Kaizari. Huu ulikuwa koloni la Kirumi ambapo askari wa Kirumi waling'atuka. Mji huu uliuga mji wa Rumi katika usanifu wa majengo na utamaduni na ulikuwa kituo cha kiutawala cha Kirumi (yaani, Senatorial) jimbo la Akaya mnamo mwaka 27 K.K. Huu ulikuja kuwa Jimbo la Kifalme mnamo mwaka 15 B.K.
- D. Eneo la Korintho ya Kale lililokuwa limezungushiwa ngome, lililokuwa limeinuka umbali wa hatua 1880 juu ya uwanda, lilikuwa eneo la hekalu la Aphrodite. Kwa hekalu hili lililoingiza makahaba wapatao 1,000 (Strabo, *Geography*, 8.6.20-22). Kuitwa jina la "wa Kikorintho" (yaani, *Korinthiazesthai*,

lililoanzishwa na Aristophanes [450-385 K.K.] lilikuwa sawa na kupotea, maisha ya maasi. Hili hekalu, kama hekalu maarufu la mji, liliharibiwa katika tetemeko yapata miaka 150 kabla ya kuwasili kwa Paulo, kama ilivyokuwa kwa mara nyingine mnamo mwaka 77 B.K. Haijulikani kama dhehebu la ustawi liliendelea katika siku zile za Paulo. Kwa kuwa Warumi, mnamo mwaka 146 K.K., waliuangamiza mji na kuwaua au kuwatumikisha wenyeji wake wote, mvuto wa mji wa Kiyunani ulikuwa umefifizwa na utawala wa koloni la Kirumi (Pausanias, II.3.7). Mukstadha wa utamaduni wa Kirumi badala ya utamaduni wa Kiyunani, ulitengeneza tofauti muhimu katika kuifasiri I Wakorintho.

III. MWANDISHI

- A. Ni katika mji huu ambapo Mtume Paulo alifanya ziara ya pili ya umisheni; maelezo yake yanapatikana katika kitabu cha Matendo ya Mitume 18:1-21. Kupitia maono Bwana alimfunuliwa Paulo kuwa wengi wangeliamini na pasingekuwa na kufaulu kwa upinzani wa huduma yake (kama vile Matendo 18:9-10).
- B. Mkakati wa ziara ya Paulo ulikuwa ni kupanda kanisa katika miji midogo iliyokuwepo nyakati zake, kwa kuwafahamu waongofu wapya, kuwatembelea wachuuzi, na mabaharia wangelieneza injili kadri walivyokuwa wakisafiri. Jambo hili lilikuwa juu ya kanisa mama kuchukua jukumu la uinjilishaji na uanafunzi wa eneo hili.
- C. Paulo aliwakuta Akila na Prisila, pia wakiwa wanawaamini watengeneza mahema au wawamba ngozi wa Kiyahudi, ndani ya Korintho. Hawa walilazimishwa na utawala wa Klaudio kwenda nje ya Rumi mnamo mwaka 49 B.K. (Orosius, *Hist.* 7:6:15-16) dhidi ya taratibu au jadi zo zote za Kiyahudi (kama vile Matendo 18:2). Paulo aliwasili Korintho akiwa peke yake. Wote Sila na Timotheo walikuwa katika utendaji huko Makedonia (kama vile Matendo 18:5). Huyu alivunjika moyo sana (kama vile Matendo 18:9-19; I Kor. 2:3). Hata hivyo, alitunzwa na kuendelea kukaa ndani ya Korintho miezi kumi na minane (kama vile Matendo 18:11).
- D. Uandishi wa Paulo wa kitabu hiki unaonyeshwa na Clement wa Rumi, aliyeandika barua kwa Wakorintho 95/96 B.K. (*I Clement* 37:5; 47:1-3; 49:5). Uandishi wa tabia ya Paulo wa barua hii kamwe haukuwahi kutiliwa mashaka, hata na wanazuoni wa ukosoaji wa sasa.

IV. TAREHE

- A. Tarehe ya Paulo kuitembelea Korintho umegunduliwa na maandishi ya Mfalme Klaudio yaliyopatikana huko Delphi, ambayo yanabainisha tarehe ya ugavana wa Galio kama wenye kuanza mnamo mwezi wa Saba mwaka 51 B.K, 52 (kama vile Matendo 18:12-17), ambao ungeifanya tarehe ya kuwasili kwa Paulo kuwa mwaka 49-50 B.K.
- B. Tarehe ya barua ya Paulo kwa wakati mwingine ingekuwa katikati ya miaka ya 50. Huyu aliandika barua hii kutoka Efeso ambapo alihudumu kati ya miaka miwili (kama vile Matendo 19:10) na miaka mitatu (kama vile Matendo 20:34).
- C. Mtiririko yakini wa maandishi ya Paulo kwa kuwafuatisha F. F. Bruce na Murry Harris kwa nyonggeza ndogondogo:

<u>Kitabu</u>	<u>Tarehe</u>	<u>Eneo la Maandiko</u>	<u>Ufunuo wa kitabu cha Matendo</u>
1. Wagalatia	48	Ashuru Antiokia	14:28; 15:2
2. I Wathesalonike	50	Korintho	18:5
3. II Wathesalonike	50	Korintho	
4. I Wakorintho	55	Efe	19:20
5. II Wakorintho	56/57	Makedonia	20:2

6. Warumi	57	Korintho	20:3
7. -10. Barua za gerezani			
Wakolosai	miaka ya 60	Rumi	
Waefeso	miaka ya 60	Rumi	
Filimoni	miaka ya 60	Rumi	
Wafilipi	mnano mwaka 62-63	Rumi	28:30-31
11.-13. Safari ya Nne ya Umisheni			
I Timotheo	63 (au baadaye,	Makedonia	
Tito	63 lakini kabla ya	Efeso	(?)
II Timotheo	64 68 B.K)	Rumi	

(Huenda Paulo alikamilisha kazi hii mnamo mwaka 65 B.K).

V. MPOKEAJI WA BARUA

- A. Wapokeaji wa barua hii lilikuwa kanisa la muda mrefu lililoundwa na Mataifa kadhaa. Idadi kubwa ya Korintho ilikuwa imechanganyikana kwa rangi na kitamaduni. Tunafahamu kutokana na utafiti wa mambo ya kale na Maandiko (kama vile Matendo 18:4-8) kwamba kulikuwa na sinagogi ndani ya Korintho.
- B. Askari wa Kirumi waling'atuka baada ya kukamilisha miaka ishirini ya huduma ya kijeshi. Korintho ulikuwa mji huru, koloni la Kirumi, na makao makuu ya jimbo la Kirumi la Akaya.
- C. Barua hii inaonekana kuyaakisi makundi kadhaa ndani ya kanisa: (1) wasomi wa Kiyunani waliendelea kujivunia mapokeo yao ya kifalsafa na walikuwa wakijaribu kuunganisha ufunuo wa Kikristo pamoja na desturi hizi na mapokeo ya kisomi; (2) walezi wa Kirumi na wasomi wa kijamii; (3) Mataifa ya waamini wa Kiyahudi waliokuwa wakijizuia anasa na waliokuwa wakitawaliwa na dhana ya "woga wa mungu", waliokuwa wakiudhuria katika sinagogi; na (4) idadi kubwa ya watumwa waliokoka.

VI. KUSUDI LA BARUA

- A. Paulo aliyasikia matatizo yaliyokuwa yakiendelea huko Korintho kutokana na vyanzo vinne
1. watu wa Kloe, 1:11
 2. barua kutoka katika kanisa iliyokuwa ikiuliza maswali, 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12
 3. ziara binafsi kutoka Stefana, Fortunato, na Akaiko, 16:17. Inawezekana kwamba barua (#2) ililetwa na watu hawa (#3).
- Inafurahisha kwamba Murry Harris amekifupisha kitabu cha I Wakorintho kinachojikita katika Paulo kuzipokea habari zihusuzo kanisa.
1. taarifa za masimulizi kutoka kwa watu wa nyumbani mwa Kloe, zilizopelekea Paulo kuandika sura ya 1-4
 2. taarifa ya masimulizi kutoka kwa wawakilishi wa kanisa (yaani, Stefana, Fortunato, na Akaiko), yaliyopelekea kuwepo kwa sura ya 5-6
 3. maswali yaliyoandikwa kutoka ndani ya kanisa, yaliyopelekea kuwepo kwa sura 7-16
- B. Kanisa likawa la kimigogoro, likiungwa mkono na viongozi mbalimbali: Paulo, Apolo, Petro, na huenda ni chama cha Kristo (kama vile 1:12). Si kanisa pekee lililoligawa kanisa katika aina mbalimbali za viongozi, bali pia katika mambo mbalimbali na matumizi ya karama za kiroho. Hoja kuu ya kutokuelewana ilikuwa ni kwa sababu ya mamlaka ya Kitume ya Paulo (hasa II Wakorintho)!

VII. MAWASILIANO YA PAULO PAMOJA NA KANISA LA KORINTHO—SHAURI LILILOPENDEKEZWA

- A. Je! ni barua ngapi alizoandika Paulo kwenda Korintho?
1. hizi mbili, I na II Wakorintho
 2. tatu, na nyingine zilizopotea

3. barua nne, pamoja na zile mbili zilizopotea
4. baadhi ya wanazuoni wa sasa wamezibaini sehemu za barua mbili zilizopotea katika II Wakorintho
 - a. barua za awali (I Nya. 5:9) katika II Nya. 6:14-17:1 yote)
 - b. barua iliyokuwa imekatikakatika (II Nya. 2:3-4,9; 7:8-12) katika II Nya. 10-13 yote)
5. tano, pamoja na II Nya. 10-13 na kuwa waraka wa tano, uliotumwa baada ya taarifa ya Tito iliyohusiana na habari mbaya zilizofuatia

B. Nadharia #3 inaonekana kwendana vema

1. Barua ya awali, iliyopotea (I Nya. 5:9)
2. I Wakorintho
3. Barua iliyotengana, uliyopotea (huenda sehemu ya kile kilichonukuliwa katika II Nya. 2:1-11; 7:8-12)
4. II Wakorintho

C. Matengenezo mapya yaliyopendekezwa

TAREHE	ZIARA	BARUA
<p>50-52 B.K. Ziara ya Pili ya Kimisheni ya Paulo</p> <p>52 B.K. Gallilo alikuwa gavana kuanzia 52 B.K (Matendo 18:12-17)</p> <p>56 B.K. (Majira ya Masika)</p> <p>56 B.K. (Majira ya baridi) au 57 B.K. (Majira ya baridi)</p>	<p>a. Wakati wa Ziara ya Pili ya Kimisheni ya Paulo alikaa huko Korintho kwa miezi kumi na minane (kama vile Matendo ya Mitume 18:1-11)</p> <p>b. Paulo anasikia kuhusu matatizo yaliyo ndani ya kanisa akiwa Efeso kutokana na vyanzo viwili (1) watu wa nyumbani mwa Kloe, I Kor. 1:11 na Akaya, I Kor. 16:17. Kwa uwazi wanaleta barua kutoka katika makanisa ya nyumba ya huko Korintho yenye kujumuisha maswali.</p>	<p>a. I Kor. 5:9-11 inaonekana kuurejelea barua inayohusu hali ya ukengeufu wa mwenendo nwema ndani ya kanisa. Waraka huu haujulikani isipokuwa: (1) kama wengine wanavyodhani, kwamba II Kor. 6:14-7:1 ni sehemu ya wraka wa kauli iliyopita ya wakati usio timilifu na inairejelea II Wakorintho</p> <p>b. Paulo anayajibu maswali haya (kama vile I Kor.7:1,25; 8:1; 12:1; 16:2,) kwa kuandika I Wakorintho. Timotheo (kama vile I Kor.4:17) anachukua jukumu la kutoka Efeso (kama vile I Kor. 16:8) kwenda Korintho. Timotheo hakuwa na uwezo wa kutatua matatizo yaliyokuwa ndani ya Kanisa.</p>

<p>57-58 B.K. (Majira ya baridi)</p>	<p>c. Paulo anaanua kuwa na dharura, ziara ya kimaumivu ya kwenda Korintho (hii haikunukuliwa katika Matendo, kama vile II Kor. 2:1). Hii haikuwa na mafanikio, bali aliapa kurudi.</p> <p>d. Paulo anapanga kukutanana Tito huko Troa, lakini Tito hakufika, hivyo Paulo anakwenda Makedonia (kama vile II Kor. 2:13; 7:5,13), huenda Filipi (kama vile MSS B⁶, K,L,P).</p> <p>e. Ziara ya mwisho ya Paulo ya kwenda Korintho iliyonukuliwa inaonekana kurejelewa katika Matendo 20:23. Ingawa hii haikuitaja Korintho kwa jina, inadhaaniwa. Alikaa mahali pale wakati wa majira ya baridi.</p>	<p>c. Paulo anaandika anaandika waraka wenye ukali (kama vile II Kor. 2:3-4:9; 7:8-12) kwa makanisa ya nyumbani ya huko Wakorintho yaliyofikiwa na Tito (kama vile II Kor. 2:13; 7:13-15). Waraka huu haujulikani, isipokuwa, kama wengine wanavyodhani, sehemu yake ni II Kor. 10-13.</p> <p>d. Alimkuta Tito na kusikia kwamba kanisa limehitikia juu ya kuongoza kwake na kisha kuandika II Wakorintho katika shukrani kubwa sana (kama vile 7:11-16). Hili lilifikiwa na Tito.</p> <p>e. Hali ya mabadiliko iliyonakiliwa ilijitokeza kati ya sura 1-9 na 10-13 inafafanuliwa na baadhi ya wanzuoni kama habari mbaya zaidi (huenda ulikuwa uamsho kutokana na athari za hapo nyuma na ongezeko la athari mpya) kutoka makanisa ya nyumbani ya huko Korintho baada ya sura ya 1-9 kuwa imekwisha kuandikwa. (F.F.Bruce).</p>
--------------------------------------	--	--

VIII. HITIMISHO

- A. Katika kitabu cha I Wakorintho tunamuona Paulo, mchungaji, akishughulikia matatizo ya kanisa. Katika barua hii na katika Wagalatia, tunamuona akitumia injili ya kweli ya kiulimwengu katika namna mbalimbali, huku akijikita sana katika hitaji la kanisa: uhuru wa makanisa ya Wagalatia/mipaka ya kanisa la Kikorintho.

- B. Kitabu hiki kwa vyo vyote vile ni mlolongo wa kifungu cha “dinosaria wa kitamaduni” au kweli ya kanuni ya kupata mali nyingi iliyotumika katika muktadha fulani wa kihistoria /kitamaduni. Yatupasa kujihadhari dhidi ya kuichanganya kweli na matumizi ya kiutamaduni ya kweli hiyo. Kwa mjadala ulio mzuri zaidi kuhusiana na jambo hili la ufasiri hasa wa Maandiko wenye umuhimu sana angalia Gordon D. Fee na Douglas Stuart’s *How To Read the Bible for All Its Worth*, uk. 65-76.
- C. Kitabu hiki kitakusukuma katika kujiwekea mipaka ya uwezo wako wa kiroho wa kuifasiri Biblia. Hiki kitakulazimisha kufikiri upya juu ya vipengele vya thiolojia yako. Hiki kitafungua dirisha la mapenzi ya Mungu katika siku zetu, uzungumzaji wa kiutendaji, kama yalivyo maandiko mengine machache ya kibiblia.

IX. MAELEZO YA KIMUHTASARI YA I WAKORINTHO

- A. Utangulizi 1:1-9
 - 1. Salamu, 1:1-3
 - 2. Shukrani, 1:4-9
- B. Matatizo yaliyosemekana kuwako huko Korintho, 1:10-6:20
 - 1. Matengano ndani ya kanisa kwa sababu ya kutokuelewana kwa uongozi wa Kikristo (yaani, Paulo, Apolo, Petro) nia na ujumbe, 1:10-4:12
 - 2. Mtikisiko wa mwenendo mbaya, 5:1-13
 - 3. Madai ya Kikristo, 6:1-11
 - 4. Uhuru wa Kikristo uliowekewa mipaka kupitia majukumu, 6:12-20
- C. Barua kutoka Korintho yenye kuuliza maswali yaliyoonekana kuwa ya usumbufu, 7:1-1-16:4
 - 1. Ujinsia wa mwanadamu, 7:1-40
 - 2. Uhusiano wa utamaduni wa ibada za sanamu na uhuru wa Mkristo, 8:1-11:1
 - 3. Ibada ya Kikristo na ukiroho, 11:2-14:40
 - 4. Tambuzi za kiundani za matukio ya siku za mwisho, hasa ufufuo, 15:1-58
 - 5. Mchango wa kanisa mama lililoko Yerusalemu, 16:1-4
- D. Maelezo ya kuhitimisha
 - 1. Mipango ya ziara za Paulo (na wahudumu wenzake) , 16:5-12
 - 2. Maonyo ya mwisho na salamu, 16:13-24

X. USOMAJI UNAOPENDEKEZWA JUU YA MAWAZO YA PAULO

- A. *The Mind of St. Paul*, William Barclay, kilichochapishwa na Harper & Row
- B. *Paul, Apostle of the Heart Set Free*, F. F. Bruce, kilichochapishwa na Eerdmans
- C. *The Origins of Paul’s Religion*, J. Gresham Machen, kilichochapishwa na Eerdmans
- D. *Paul, An Outline of His Theology*, Herman Ridderbos (kilichofasiriwa na John De Witt), kilichochapishwa na Eerdmans
- E. *Epochs in the Life of Paul*, A. T. Robertson, kilichochapishwa na Baker
- F. *A Man In Christ*, James S. Stewart, kilichochapishwa na Harper & Row
- G. *Dictionary of Paul and His Letters*, kilichochapishwa na IVP
- H. *Paul in the Roman World, The Conflict at Corinth*, Robert M. Grant, kilichochapishwa na Westminster, John Knox Press

I. *Philo and Paul Among the Sophists*, Bruce W. Winter, kilichochapishwa na Eerdmans

J. *After Paul Left Corinth*, Bruce W. Winter

XI. MANENO NA WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. waliotakaswa, 1:2
2. milele, 2:7,8
3. "mafumbo ya Mungu," 2:10
4. "shamba la Mungu," 3:9
5. "ninyi mmekuwa hekalu la Mungu," 3:16,17
6. "siri za Mungu," 4:1
7. "kumtolea Shetani mtu huyo," 5:5
8. "mtawahukumu malaika," 6:3
9. "Na baadhi yenu ," 6:11
10. "Kwa habari za wanawali," 7:25
11. "mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa," 9:27
12. "wavitoa kwa mashetani," 10:20
13. "kushirikiana katika meza ya Bwana," 10:21
14. "kwa ajili ya malaika," 11:10
15. "nasikia kuna faraka kwenu," 11:18
16. "Yesu amelaaniwa," 12:3
17. "kupambanua roho," 12:10
18. shaba iliayo na upatu uvumao, 13:1
19. "ijapo ile iliyo kamili," 13:10
20. "tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo," 13:12
21. kuhutubu, 14:39
22. atakapobatilisha, 15:24
23. "ile changizo kwa ajili ya watakatifu," 16:1

XII. WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. Sosthene, 1:1
2. Watu wa nyumbani mwa Kloe, 1:11
3. Apolo, 1:12
4. Kefa, 1:12
5. Krispo na Gayo, 1:14
6. "hao wanaoitawala dunia hii," 2:6,8
7. mwanadamu wa tabia ya asili, 2:14
8. watu wenye tabia ya rohoni, 3:1
9. watoto wachanga katika Kristo, 3:1
10. Kefa, 15:5
11. wale Thenashara, 15:5
12. Yakobo, 15:7

XIII. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Korintho, 1:2

2. makanisa ya Galatia, 16:1
3. Yerusalemu, 16:3
4. Makedonia, 16:5
5. Efeso, 16:8
6. Akaya, 16:15
7. Asia, 16:19

XIV. MASWALI YA MJADALA

1. Kwa nini Wayahudi walimkataa Yesu kama Masihi?
2. Kwa nini Wayunani walimkataa Yesu?
3. Kwa nini Paulo alitengeneza usemi wa namna hii kuhusu falsafa iliyo katika 1:18-25 na 2:15?
4. Eleza maana ya 1:26-31.
5. Je! 3:10-15 inamrejelea nani?
6. Kwa nini kanisa lilishutumiwa na Paulo katika 5:1-8?
7. Fafanua 6:1-11 inazuia madai ya Wakristo ya sasa?
8. Je! Paulo anamaanisha kwamba ujane ni mapenzi ya Mungu katika sura ya 7?
9. Je! 7:12-13 inamaanisha kwamba waamini wanaweza kuoana na wasio amini?
10. Ni kwa namna gani sura ya 8 ni kama Warumi 14?
11. Kwa nini Paulo asingeliweza kuchukua fedha kutoka kanisa la Korintho? (9:3-18)
12. Eleza maana ya 9:19-23.
13. Fafanua 10:1-13 katika maneno yako mwenyewe.
14. Kwa nini 10:13 ni mstari wa kushangaza sana kwa waamini?
15. Fafanua kanuni ya kiroho ya 10:23 katika maneno yako mwenyewe.
16. Ni kwa namna gani 11:5 ina mkanganyiko na 14:34?
17. Je! 11:30 inamaanisha kuwa baadhi ya waamini walikufa kwa sababu ya kuishiriki Mza ya Bwana?
18. Fafanua hali ya usemi wa Paulo ulio katika 11:34.
19. Nini maana ya kanuni ya kiroho iliyo katika 11:7?
20. Ni kwa namna gani karama za kiroho zilihusianishwa na vipaji vya asili? Ni wakati gani waamini huzipokea karama zao za kiroho?
21. Ni kwa namna gani 12:29-30 inajibu swali la, "Yawapasa waamini wote Kunena kwa lugha"? (14:5)
22. Katika 13:8 nini kitapita na nini kitabaki?
23. Ni kwa namna gani sura ya 14 inasawiri matumizi ya kunena kwa lugha katika ibada ya hadhara?
24. Ni makundi gani matatu ambayo Paulo anayawekea mipaka katika ibada ya hadhara iliyo katika sura ya 14?
25. Orodhesha hoja za injili iliyo katika 15:1-4.
26. Ni wakati gani katika maisha ya Yesu ambapo 15:6 inajitokeza?
27. Ni kwa namna gani 15:22 inafanana na Warumi 5:12-21?

UTANGULIZI WA II WAKORINTHO

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Kitabu hiki, ni zaidi ya barua yo yote ile ya Paulo, hiki kinatuonyesha moyo na fikra za Mtume wa Mataifa. Huu ndiyo ukaribu tulio nao kwa wasifu wake wa kiroho/kichungaji.
- B. Kitabu hiki kinaweza kuwa kazi ya ufasaha wa kimazungumzo iliyokamilika. Raymond E. Brown, *An Introduction to the New Testament*, anasema, “hiki kinaweza kuwa cha ufasaha wa kimazungumzo katika ubora miongoni mwa maandiko yote ya Paulo” uk. 541. Hata hivyo, hili lilifanyika kwa ajili ya kulipinga kundi la Wapotoshaji lililokuja toka Korintho na kuzishambulia mbinu za uzungumzaji wa Paulo pamoja na fahirisi yake (yaani, mashambulizi yake juu ya hekima katika I Kor. 1-4).

MADA MAALUM : WAPOTOSHAJI

Neno hili la Kiyunani *sophia* linamaanisha hekima. Neno *sophistēs* lenye kuhusiana na hili lilikuja kumaanisha “mtu mwenye ujuzi” au “aliyeelimishwa katika ufasaha wa mazungumzo.” Mara nyingi neno hili linamaanisha mzungumzaji wa mhadhara, huyu ni msafiri wa mara kwa mara, aingiaye mjini na kujaribu kuanzisha shule ya kuwafundisha watoto wa madarasa ya wasomi. Uzugumzaji wa kimhadhara ndiyo uliowasababisha wazazi

kuwatafuta kwa ajili ya masomo binafsi au kwa ajili ya shule ya watoto wao.

Kulikuwa na mashindano ya kustaajibisha kati ya hawa “watu wenye hekima” yenye kuhusiana na kujulikana kwao na uwezo wao wa kuwashawishi wanafunzi. Pia kulikuwa na mpangilio wa miongozo kwa ajili ya uzungumzaji wa awali. Moja ya hatua za mpangilio huu ulikuwa wakati wa mwanafalsafa kuzitaja sifa zake na nguvu zake.

Matatizo ya Paulo huko Korintho yalionekana kuhusiana na

1. matengano madogomadogo ndani ya Kanisa, kila mtu akidai kuwa mfuasi wa kiongozi fulani (I Kor. 1-4)
2. Waasi wa Kiyahudi waliofundishwa kuwa walimu wa uongo toka Yerusalemu (II Kor. 10-13)

Paulo kuipinga “hekima” katika I Kor. 1-4 kuliweka mazingira ya yeye kushambuliwa na wale waliokuwa wakitukuzwa katika falsafa zao, waliofundishwa katika ufasaha wa mazungumzo na kuwahukumu wale wote katika mwongozo wa sifa hizi. Inashangaza kwamba walimu wa Kiyahudi wangetukuzwa katika madaraja yao ya kifalsafa, lakini kitangulizi kinawekwa na Philo wa Iskandria ndani ya dini ya Kiyahudi na huenda hata

mafunzo na mrejeo wa Apolo wa Iskandria.

Paulo hakuwa mzungumzaji wa hadharani mwenye kung’aa. Hivyo alishambuliwa kwa sababu ya hili. Huyu alilipiza kwa kung’arishwa na uandishi, ulinganifu, uundaji bora, muundo wa ufasaha wa mazungumzo ulio katika II Kor. 10-13. Alitumia maneno yao, miundo yao na kuiweka bayana mitazamo yao isiyo sahihi na majigambo yao.

- C. Kitabu hiki ni mchanganyiko wa kigeni, kama alivyo Paulo mwenyewe, huzuni na mawazo ya kiroho, hisia huru zitokazo katika mabadiliko ya hasira hadi furaha kuu.
- D. Kitabu hiki ni barua ya kweli na kama barua inakuwa nusu ya mazungumzo. Vitangulizi vingi vya kimantiki na hali nyinginezo za undani wa miitikio ya Paulo vimepotea. Huu ni mfano mzuri wa ukweli kwamba hizi barua za Agano Jipya kiuhalisia ziliandikwa kama ushabihiano wa mahitaji mahususi, si hotuba huru za kithiolojia.

- E. Kitabu hiki kimekuwa kikipingwa na wasomi katika kuhubiri kwao. Hii si kwa kukusudia kwa sababu hiki ndicho chanzo cha hatima ya mjadala wa Paulo kuhusiana na mateso katika maisha ya Ukristo.
- F. Kwa wachugaji, kitabu hiki kinatoa miongozo ya kiundani ya namna ya kushughulikia matatizo ndani ya makanisa mama. Paulo anatupa mfano wa kufuatisha ndani ya mashambulizi binafsi na kutoelewana.

II. MWANDISHI

- A. Hata ndani ya upinzani wote wa sasa wa uandishi wa kitamaduni wa vitabu vya kibiblia, kamwe kitabu hiki hakikuweza kukataliwa kuwa ni cha Paulo.
- B. Hiki kina wasifu mzuri sana na ni vigumu sana kuvielewa baadhi ya vifungu vyenye uwezekano wa mtu kujaribu kumuiga Paulo kwa kuandika kitabu kama hiki. Ugumu na upekee wa barua hii unazungumzia uhalisia wake. Ni kweli kwamba wanazuoni wengi wa Agano Jipya wanafikiri kwamba II Wakorintho ni barua changamano wenye kuunganisha barua kadhaa tengefu za Paulo na kuwa katika barua mmoja. Naamini juu ya muungano wake kwa sababu:
 1. Hakuna maelezo ya kutokuwepo kwa umoja katika machapisho yo yote ya kale ya Kiyunani.
 - a. Hakuna tofauti za vipengele vya kifasihi
 - b. Hakuna machapisho ambayo hayakuzibeba sura zote kumi na tatu.
 2. Ingawa II Kor. 13 haikujulikana dhahiri kwa Clement wa Rumi mnamo 96 B.K, inanukuliwa na Polycarp mnamo mwaka 105 B.K.
 3. Kitabu hiki kinafahamika kama kitu kimoja. Kunaonekana kuwepo dhamira fulani zenye kuonyesha umoja wake, kama vile kifungu “mateso.”
 4. Ushahidi wa ndani umewekewa mipaka sana katika kuweka utetezi wa umuhimu wa mgawanyo wa II Wakorintho.
- C. Paulo anaelezwa kuwa mwandishi katika 1:1 na 10:1.

III. TAREHE

- A. Tarehe ya II Wakorintho kwa namna ya kutotenganishwa imeunganishwa na I Wakorintho na kitabu cha Matendo ya Mitume.
- B. Matendo ya Mitume 18:1-18 na 20:2-3 inalihusianisha tendo la Paulo kuwa huko Korintho, lakini pia inaonekana kuwa na safari moja ambayo haikunukuliwa (II Wakorintho 2:1; pamoja na ziara ya tatu inayotajwa katika 12:14; 13:1-2).
- C. Swali kuu ni uhusiano wa muda kati ya ziara za Paulo na barua yake kwa Korintho.
- D. Tatizo halisi la kuyapa tarehe matukio yenye kuhusiana na Korintho ni kwamba hatuna ushahidi wa ndani au taarifa kati ya Matendo 18:1-18 na Matendo 20:2-3, isipokuwa ushahidi wa ndani wenye utata wa baraka za Korintho wenyewe.
- E. Mawasiliano ya Paulo pamoja na Kanisa la Korintho—Matengenezo yaliyopendekezwa

TAREHE	ZIARA	BARUA
<p>50-52 B.K. Safari ya Pili ya Umisheni ya Paulo</p> <p>52 B.K. Gallio alitawala kama gavana kuanzia 52 B.K. (kama vile Matendo 18:12-17)</p> <p>56 B.K. (Majira ya Masika)</p> <p>56 B.K. (Majira ya baridi) au 57 B.K. (Majira ya baridi)</p>	<p>a. Katika ziara hii ya Pili ya Paulo alikaa Korintho kwa miezi kumi na minane (kama vile Matendo 18:1-11)</p> <p>b. Paulo anasikia kuhusu matatizo yaliyo ndani ya kanisa akiwa Efeso kutokana na vyanzo viwili (1) watu wa nyumbani mwa Kloe, I Kor. 1:11 na Akaya, I Kor. 16:17. Kwa uwazi wanaleta barua kutoka katika makanisa ya nyumba ya huko Korintho yenye kujumuisha maswali.</p> <p>c. Paulo anaamua kuwa na dharura, ziara ya kimaumivu ya kwenda Korintho (hii haikunukuliwa katika Matendo, kama vile II Kor. 2:1). Hii haikuwa na mafanikio, bali aliapa kurudi.</p> <p>d. Paulo anapanga kukutana na Tito huko Troa, lakini Tito hakufika, hivyo Paulo anakwenda</p>	<p>a. I Kor. 5:9-11 inaonekana kuirejelea barua iliyohusu hali ya mwenendo mbaya ndani ya kanisa. Barua hii haijulikani isipokuwa:(1) kama wengine wanavyodhani, kwamba II Kor. 6:14-7:1 ni sehemu ya wraka wa kauli iliyopita ya wakati usio timilifu na inairejelea II Wakorintho</p> <p>b. Paulo anayajibu maswali haya (kama vile I Kor.7:1,25; 8:1; 12:1; 16:2,) kwa kuandika I Wakorintho. Timotheo (kama vile I Kor.4:17) anachukua jukumu la kutoka Efeso (kama vile I Kor. 16:8) kwenda Korintho. Timotheo hakuwa na uwezo wa kutatua matatizo yaliyokuwa ndani ya Kanisa.</p> <p>c. Paulo anaandika waraka wenye ukali (kama vile II Kor. 2:3-4:9; 7:8-12) kwa makanisa ya nyumbani ya huko Wakorintho yaliyofikiwa na Tito (kama vile II Kor. 2:13; 7:13-15). Waraka huu hana jina, isipokuwa, kama wengine wanavyodhani, sehemu yake ni II Kor. 10-13.</p>

<p>57-58 B.K. (Majira ya baridi)</p>	<p>Makedonia (kama vile II Kor. 2:13; 7:5,13), huenda Filipi (kama vile MSS B⁶, K,L,P).</p> <p>e. Ziara ya mwisho ya Paulo ya kwenda Korintho iliyonukuliwa inaonekana kurejelewa katika Matendo 20:23. Ingawa hii haikuitaja Korintho kwa jina, inadhaaniwa. Alikaa mahali pale wakati wa majira ya baridi.</p>	<p>d. Alimkuta Tito na kusikia kwamba kanisa limeitikia juu ya kuongoza kwake na kisha kuandika II Wakorintho katika shukrani kubwa sana (kama vile 7:11-16). Hili lilifikiwa na Tito.</p> <p>e. Hali ya mabadiliko iliyonakiliwa ilijitokeza kati ya sura 1-9 na 10-13 inafafanuliwa na baadhi ya wanazuoni kama habari mbaya zaidi (huenda ulikuwa uamsho kutokana na athari za hapo nyuma na ongezeko la athari mpya) kutoka makanisa ya nyumbani ya huko Korintho baada ya sura ya 1-9 kuwa imekwisha kuandikwa. (F.F.Bruce) au (2) sura 1-9 ni ujumbe wa Paulo kwa waamini walio waaminifu katika Korintho, ambapo sura 10-13 ni ujumbe wa Paulo kwa waamini walio waasi katika Korintho (kutoka J.W.MacGorman).</p>
--------------------------------------	---	---

IV. IDADI YA BARUA ALIZOZIANDIKA PAULO HUKO KORINTHO

A. Kama mbili, I na II Wakorintho

B. Tatu, pasipo kupotea barua hata mmoja

C. Nne, pamoja na barua mbili zilizopotea

D. Baadhi ya wanazuoni wa sasa wanazipata barua zilizopotea ndani ya II Wakorintho

1. barua ya awali (I Kor. 5:9) katika II Kor. 6:14-7:1
2. barua kali (II Kor. 2:3-4,9; 7:8-12) katika II Kor. 10-13

E. Tano, pamoja na II Kor. 10-13 kuwa barua ya tano, iliyotumwa baada ya taarifa ya Tito yenye kuhusiana na taarifa mbaya zilizofuatia

F. Naamini C (pia tazama H. C. Thiessen, *Introduction to the New Testament*, uk. 209)

1. Barua ya awali—iliyopotea (I Kor. 5:9)
2. I Wakorintho
3. Barua yenye ukali—iliyopotea (II Kor. 2:1-11, 7:8-12)
4. II Wakorintho

V. MAADUI WA PAULO HUKO KORINTHO

- A. Katika II Wakorintho tatizo linaonekana kuwa la matengano madogomadogo ndani ya makanisa ya nyumbani (si matengano yasiyoepukika na yenye kufanana na yale yaliyo katika I Wakorintho, lakini huenda ndiyo haya).
1. kundi la waamini wenye kuziunga mkono tamaduni na mapokeo ya Kirumi
 2. kundi la waamini wenye kuziunga mkono tamaduni za Kiyunani na mafundisho ya ufasaha wa mazungumzo
 3. kundi la waamini wenye kuziunga mkono jadi za tamaduni na mapokeo ya Kiyahudi
 4. kundi la waamini wasiyo na nguvu pamoja wale waliotengwa na jamii
- B. Kuwasili kwa wachochezi wa Kiyahudi kutoka Palestina kulisababisha ongezeko la machafuko (kama vile II Kor. 10- 13). Hawa walikuwa tofauti na wale waliozifuata mila na desturi za Kiyahudi za wanasheria wa Kigalatia na Kiyahudi/Kiyunani na wa Kikolosai. Huenda hawa walikuwa wamefundishwa elimu ya ufasaha wa mazungumzo, walimu wa karama, sawa na Apolo.
- C. Hapa kuna baadhi ya mashtaka yaliyoibuliwa dhidi ya Paulo ambapo aliitikia.
1. Paulo mtu wa kubadilika badilika (yaani, mipango ya ziara zake ilibadilika, kama vile 1:15 na kuendelea).
 2. Paulo alikuwa mwandishi mwenye nguvu, lakini dhaifu katika kujizungumzia (kama vile 10:10).
 3. Paulo hakuwa mzungumzaji fasaha mwenye kunolewa (kama vile 10:10; 11:6).
 4. Paulo hakuikubali fedha (kama vile 11:7 na kuendelea; 12:13 na kuendelea).
 5. Paulo hakuwa Mtume wa kweli (kama vile 11:5,13; 12:4).
 6. Paulo hakuwa Myahudi mwenye msingi wa imani (kama vile 11:21na kuendelea).
 7. Paulo hakuwa na uelekeo wa mafunuo na maoni ya kiroho kama walivyokuwa (kama vile 12:1 na kuendelea).

VI. SABABU NA KUSUDI LA II WAKORINTHO

- A. Shukrani kwa ajili ya mwitikio chanya wa kanisa kwa uongozi wa Paulo (kama vile 2:12,13; 7:11-16)
- B. Maandalizi ya ziara ya tatu ya Paulo (kama vile 10:1-11). Ile ya pili hakika ilikuwa ya maumivu na isiyo na mafanikio. Mabadiliko ya mwelekeo wa hisia za sura 10-13 ni dhahiri. Wengine wamekuwa wakidai kwamba haya ni matokeo ya barua kadhaa za Paulo kwa kanisa la Korintho zilizounganishwa na II Wakorintho. Pia inawezekana kwamba Paulo aliziandika barua hizi baada ya kusikia kuhusu mlipuko wa upinzani ndani ya ushirika wa Korintho. Hii ni nyongeza ya kihisia.
- C. Kwa kuzikanusha safari za walimu wa uongo wa Kiyahudi (kama vile 10-12) hawa waliyakataa mambo kadhaa ya Paulo kama inavyoonyeshwa
1. utu
 2. nia au shauku
 3. mamlaka
 4. namna ya uwasilishaji
 5. ujumbe wa injili

VII. VIPENGELE YAKINI VYA KIFASIHI

- A. Kukifupisha kitabu hiki ni vigumu sana kwa sababu ya:

1. kubadilika badilika kwa hali
2. tofauti za masomo
3. mabano yaliyowekewa upanuzi (2:14-7:1 au 7:4)
4. maarifa yetu yaliyowekewa mipaka ya hali ya maeneo ya mahali

B. Hata hivyo, kuna migawanyo mikuu mitatu ya masomo yaliyo dhahiri:

1. Paulo anautikia ujumbe wa Tito na kuhusianisha mipango yake ya safari, sura 1-7 (kuna mabano makubwa yenye kushughulika na huduma ya kitume ya Paulo, 2:14-7:1 au 7:4)
2. Utiaji moyo wa Paulo kwa ajili ya ukamilishaji wa changizo za kanisa la Yerusalemu, sura 8-9
3. Paulo kuulinda uongozi wake, sura 10-13

C. Naukubali umoja wa II Wakorintho kwa sababu

1. Hakuna dondoo za kutokuwepo kwa umoja ndani ya machapisho yo yote ya kale ya Kiyunani
 - a. hakuna tofauti za vipengele vya kifasihi
 - b. hakuna machapisho ambayo hayakubeba sura zote kumi na tatu
2. Ingawa II Kor. 13 haikujulikana dhahiri kwa Clement wa Rumi mwaka 96 B.K, hii inanukuliwa na Polycarp mnamo mwaka 105 B.K.
3. Kitabu hiki kinafahamika kama kitu kimoja. Hiki kinaonekana kuwa dhamira fulani zenye kuonyesha umoja wake, kama vile "mateso."
4. Ushahidi wa ndani unawekewa mipaka sana kwa ajili ya kuulinda mgawanyo muhimu wa II Wakorintho.

VIII. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KI-MUHTASARI

1. Neema na amani, 1:2
2. "katika siku ile ya Bwana wetu Yesu," 1:14
3. aliyetutia muhuri, 1:22
4. "anayetushangiliza
5. "harufu ya kumjua," 2:14
6. "walighoshio neno la Mungu," 2:17
7. "barua zenye sifa," 3:1
8. "utokao kwa Bwana, aliye Roho," 3:18
9. utu wa nje, 4:16
10. utu wa ndani, 4:16
11. nyumba ya maskini, 5:1
12. "arabuni ya Roho," 5:5
13. kiumbe kipya 5:17
14. - aliyetupatanisha, 5:18
15. "silaha za vita vyetu si za mwili," 10:4
16. malaika wa nuru, 11:14
17. mbingu ya tatu, 12:2
18. Peponi, 12:4
19. busu takatifu, 13:12

IX. WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. "mungu wa dunia," 4:4
2. Beliari, 6:15
3. Tito, 7:6

X. MAENEO YALIYOONYWESHWA KATIKA RAMANI

1. Akaya, 1
2. Asia, 1:8
3. Makedonia 1:16
4. Yudea, 1:16
5. Korintho, 1:23
6. Troa, 2:12
7. Dameski, 11:32

XI. MASWALI YA MJADALA

1. Nini maana za kithiolojia za 1:20?
2. Fafanua katika maneno yako nwenyewe 3:6.
3. Ni kwa namna gani neno "utaji" limetumika katika maana mbili katika sura 3? (4:3)
4. Orodhesha mateso ya Paulo yaliyo katika 4:7-11; 6:4-10; 11:23-28
5. Je! waamini watajitokeza mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo? Ikiwa ni hivyo, kwa lipi?
6. Fafanua katika maneno yako mwenyewe kuhusu kanuni ya kiroho ya 5:14-15.
7. Je! mafundisho ya 5:21 yanaeleza nini?
8. Orodhesha kanuni za utoaji zinazopatikana katika sura 8-9.
9. Je! ni kwa namna gani maadui wa Paulo walimsawiri katika 10:10?
10. Je! Paulo anamrejelea nani katika 11:4?
11. Orodhesha njia anazozitumia Paulo kujilinganisha na wengine katika 11:21-30.
12. Je! ni mwiba gani wa Paulo katika mwili? (12:7)

UTANGULIZI WA WAGALATIA

I. UTANGULIZI

- A. Kitabu cha Wagalatia ni moja ya upanuzi wa maelezo yaliyo wazi ya msingi mpya na kweli huru ya wokovu kwa neema pekee, kupitia imani pekee. Mara nyingi kitabu hiki kinaitwa “Uhuru wa Ukristo wa Magna Carta.”
- B. Barua hii inatiwa shauku na nguvu ya Mageuzi ya Protestanti.
1. Martin Luther anasema, “kitabu kidogo cha Wagalatia ni barua yangu yangu; nimejifunga mwenyewe kwa hii; ni mke wangu.”
 2. John Wesley amepata amani ya mwishoni kutokana na mahubiri ya Wagalatia.
 3. Katika kitabu chake cha *Study Guide Commentary*, uk. 11, Curtis Vaughan anandika, “vitabu vichache vina ushawishi wa ndani kabisa katika fahamu za mwanadamu, vina muundo wa mwelekeo wa historia ya mwanadamu, au kuendelea kuongea kwa uhusiano wa mahitaji muhimu ya maisha ya kisasa.”
- C. Burua hii ya bobevu ni ya kimafundisho, inawezekana ni ya kwanza kwa Paulo, ilikuwa ni utangulizi wa Warumi na kukua kwa mafundisho uthibitisho kwa imani mbali na mkazo wa dini ya Kiyahudi juu ya kuishika Sheria :
1. Wokovu hauwezi kupatikana kwa sheria na kwa neema.
 2. Wokovu ni lazima upatikane kwa sheria au kwa neema.
 3. Kumfanana Kristo katalifuatisha badiliko la kweli.
 4. Iweni makini na Ukristo wa kushikilia sheria.
- D. Kimsingi huu ni wokovu huru, kwa neema pekee kupitia kwa imani pekee, ni hitaji kuu katika siku zetu kwa sababu ya kujirudia rudia, wewevu unavuta uzoefu wetu, uzoefu wa kazi katika ufahamu wa dini. Katika kila umri ukweli rahisi wa mwanzo wa Mungu, utoaji binafsi, upendo usio kuwa na masharti unapatishwa kupitia toba ya mwanadamu na kushindana katika imani ya unyenyekevu! sio kwamba waalimu wa uongo waliukataa msingi wa Kristo katika Uumbaji, lakini walimwongezea yeye. Sio kile tunachokiongeza, bali ile kwamba tunaongeza kitu chochote!

II. MWANDISHI

Uandishi wa Paulo wa barua hii kamwe hautiliwi mashaka, kama miundo ya nguzo muhimu ya tabia za barua za Paulo. Wagalatia ni habari za maisha ya mwandishi sana na binafsi. Bado ni mantiki kabisa ya hisia kubwa.

III. TAREHE NA WAPOKEAJI

- A. Vipengele hivi viwili vya msingi wa kiini lazima vihusike kwa pamoja kwa sababu ya nadharia mbili tofauti za kufanana wapokeaji zilizoathiri tarehe ya barua. Nadharia zote zina uzito wa mantiki na kuwekewa mipaka ya ushahidi wa kibiblia.
- B. Nadharia hizo mbili ni:
1. Nadharia simulizi ilikuwa imezoeleka hadi karne ya kumi na nane.
 - a. iliitwa “Nadharia ya Wagalatia wa kaskazini.”

- b. Inasadiki kwamba “Galatia” inarejelea utamaduni wa Wagalatia wa uwanda wa kati kaskazini mwa Uturuki (kama vile I Pet. 1:1). Utamaduni huu wa Wagalatia ulikuwa wa watu wa ulaya waliokuja kuishi uingereza ya kale kabla ya Rumi (Kiyunani *Keltoi* au kilatini *Gall*) Waliovamia sehemu hii katika karne ya tatu K.K. waliitwa “Wagalatia” ili kuwatofautisha wao na ndugu zao kutoka ulaya magharibi. Walishindwa katika mwaka wa 230 K.K. na Attalus I, mfalme wa Pergamo. Ushawishi wao kijiografia ulizuiwa katika kusini kati mwa Asia ndogo au Uturuki ya sasa.
 - c. ikiwa kundi hili la kiutamaduni ni la uhakika, hivyo tarehe inaweza kuwa katikati ya miaka ya 50's kipindi cha safari ya pili au ya tatu ya umisionari wa Paulo. Safari ya Paulo aliambatana na Sira na Timotheo.
 - d. Wengine wanahusisha ugonjwa wa Paulo katika Gal. 4:13 na malaria. Wanadai kwamba Paulo alienda kusini katika nyanda za juu ili kuwa mbali na bwawa, malaria-ilitapakaa, nyanda za chini pwani.
2. Nadharia ya pili inatetewa na Bwana Wm. M. Ramsay, *St. Paul the Traveller and Roman Citizen*, New York: G. P. Putnam's Sons, 1896.
- a. Kama nadharia ya utamaduni inavyoelezea “Galatia” kama utamaduni, nadharia hii inaelezea kama sehemu ya uendeshaji katika mamlaka. Inaonekana kwamba Paulo mara nyingi alitumia majina ya majimbo ya Rumi (kama vile I Kor. 16:19; II Kor. 1:1; 8:1, nk.) Jimbo la Rumi la “Galatia” lilihusisha sehemu kubwa zaidi ya utamaduni wa “Galatia.” Utamaduni huu wa Waceltic wan chi ya Ireland ulitegemezwa na Rumi mapema sana na walituzwa sehemu ya kutawala na kupanua mipaka ya mamlaka. Ikiwa sehemu hii kubwa ilikuwa inafahamika kama “Galatia,” hivyo inawezekana kwamba safari ya kwanza umisionari ya Paulo katika miji hii ya kusini mwa Antiokia katika Pisidia, Lистра, Derbe na Likaonia, iliyoandikwa katika Mdo 13-14, ni mahali pa makanisa haya.
 - b. Ikiwa mmoja atasadiki hili “Nadharia ya kusini,” basi tarehe inaweza kuwa mapema sana — karibu na, lakini kabla, “baraza la Yerusalemu” la Mdo. 15, ambalo lilielezea jambo lile lile kama katika kitabu cha Wagalatia. Baraza lilitokea katika mwaka wa 48-49 B.K na nyaraka inawezekana ilikuwa imeandikwa wakati wa kipindi kile kile. Ikiwa hii ni kweli, Wagalatia ni nyaraka ya kwanza ya Paulo katika Agano letu jipya.
 - c. Baadhi ya ushahidi kwa ajili ya nadharia ya Wagalatia wa kusini:
 - (1) Hawakutajwa kwa jina walioambatana na Paulo katika kusafiri lakini Barnaba ametajwa mara tatu (kama vile 2:1,9,13). Hii inafaa katika safari ya kwanza ya umisionari ya Paulo.
 - (2) Inatajwa kwamba Tito alikuwa hajatahiriwa (kama vile 2:1-5). Hii inafaa zaidi kabla ya baraza la Yerusalemu la Mdo. 15.
 - (3) Petro ametajwa (kama vile. 2:11-14) na tatizo la ushirika na mataifa linafaa zaidi kabla ya baraza la Yerusalemu.
 - (4) Pesa zilipopelekwa Yerusalemu marafiki kadhaa wa Paulo kutoka sehemu tofautitofauti (kama vile Mdo. 20:4) wameorodheshwa. Hakuna mmoja, hata hivyo, aliyeorodheshwa kutoka miji ya kaskazini mwa Galatia, ingawa tunajua utamaduni huu wa makanisa ya Galatia ulishiriki (kama vile I Kor. 16:1).
3. Kwa maelezo ya uwakilishi wa mabishano tofauti yahusuyo nadharia hizi muone mfasiri wa kiufundi. Kila mmoja ana malengo yafaalo lakini lengo hili katika muda hakuna makubaliano, lakini “nadharia ya kusini” inaonekana kufaa katika kweli.

C. Uhusiano wa Wagalatia kwa Matendo ya Mitume:

1. Paulo alifanya safari tano kwa kutembelea Yerusalemu, zilizoandikwa na Luka katika kitabu cha Matendo ya Mitume:
 - a. 9:26-30, baada ya kubadilika kwake
 - b. 11:30; 12:25, kwa kuleta matokeo ya njaa kutoka makanisa ya wamataifa
 - c. 15:1-30, kwa baraza la Yerusalemu
 - d. 18:22, safari fupi
 - e. 21:15 nakuendelea.,kazi nyingine ya maelezo ya mataifa
2. Kuna safari mbili za kwenda Yerusalemu zilizoandikwa katika Wagalatia:
 - a. 1:18, baada ya miaka mitatu
 - b. 2:1, baada ya miaka kumi na mine
3. inawezekana kuonekana zaidi kwamba Mdo 9:26 inasimuliwa katika Gal. 1:18. Mdo. 11:30 na 15:1 na kuendelea. Ni mpangilio wa mikutano isiyoandikwa ambayo imetajwa katika Gal. 2:1.
4. Kuna baadhi ya tofauti kati ya Mdo. 15 na Gal. 2 maelezo lakini hii inawezekana kwa:
 - a. taswira tofauti
 - b. makusudi tofauti ya Luka na Paulo
 - c. Ukweli kwamba Gal. 2 yumkini imejitokeza wakati mwingine kabla ya mkutano unaoelezewa katika Mdo. 15 lakini katika muungano nao.

D. Inawezekana mtiririko wa maandiko ya Paulo unafuata F. F. Bruce na Murry Harris na marekebisha kidogo.

<u>Kitabu</u>	<u>Tarehe</u>	<u>Sehemu kilipoandikwa</u>	<u>Uhusiano na Matendo ya Mitume</u>
1. Wagalatia	48	Shamu Antiokia	14:28; 15:2
2. Thesalonike	50	Korintho	18:5
3. II Thesalonike	50	Korintho	
4. I Wakorintho	55	Efeso	19:20
5. II Wakorintho	56	Masedonia	20:2
6. Warumi	57	Korintho	20:3
7.-10. Nyaraka za gerezani			
Wakolosai	miaka ya 60	Rumi	
Efeso	miaka ya 60	Rumi	
Filemoni	miaka ya 60	Rumi	
Wafilipi	miaka ya 62-63	Rumi	28:30-31
11.-13. Safari ya nne ya umisionari			
I Timotheo	63 (au mwishoni,	Makedonia	
Tito	63 lakini kabla	Efeso (?)	
II Timotheo	64 68 B.K)	Rumi	

IV. KUSUDI LA BARUA

- A. Paulo anaelezea sehemu tatu tofauti juu ya ujumbe unaohusu walimu wa uongo. Jumbe hizi zina tambulishwa kwa "Washika dini ya kiyahudi" kwa sababu wao waliamini kwamba mmoja awe myahudi kabla ya kuweza kuwa mkristo (kama vile 6:12). Kuhusika kwake kunahusisha mashataka ya Washika dini ya kiyahudi:
 1. Paulo hakuwa mtume halisi kama wale kumi na wawili (kama vile Mdo. 1:21-22); hivyo basi, alikuwa anategemea mamlaka yao au kwa kiasi fulani mamlaka ya kanisa mama katika Yerusalemu.

2. Ujumbe wa Paulo ulikuwa tofauti na wao, na hivyo, uongo. Hii inaonekana kusimulia lengo la dhana ya “haki kwa imani mbali na sheria.” Mitume katika Yerusalemu bado waliendelea kuwa wayahudi katika maisha yao binafsi.
3. Sehemu ya uhuru ilikuwa imeunganishwa katika baadhi ya njia na makanisa haya (kama vile 5:18-6:8). Ni kwa namna gani hili liliweza kutolewa maelezo kamili kwa kujadiliwa. Baadhi hata waliona malengo mawili katika nyaraka za Paulo: washika dini ya kiyahudi na wana wa mafunuo ya ungo (kama vile. 4:8-11). Hata hivyo, inaonekana ikisimulia zaidi vifungu hivi kwa utendaji wa wapagani. Wayahudi walihusika juu ya mtindo wa maisha ya mataifa. Ni kwa namna gani msingi wa neema huru wa Paulo unasimulia ibada ya sanamu ya wapagani na kutokua na kiasi?

B. Mafundisho, nyaraka hii inafanana na nyaraka ya Paulo kwa Warumi. Vitabu hivi viwili vina mafundisho makuu ya Paulo yanayojirudia na kujitokeza katika mipangilio tofauti.

V. MAELEZO YA KIMUHTASARI

- A. Utangulizi, 1:1-10
 1. Utangulizi mzima wa kitabu
 2. Muda wa kuandikwa kitabu
- B. Paulo anatetea utume wake, 1:11-2:14
- C. Paulo anatetea kweli za mafundisho ya injili yake, 2:15-4:20
- D. Paulo anatetea utendaji wa kushutumiwa kwa injili yake, 5:1-6:10
- E. Maelezo mafupi na mwisho, 6:11-18

VI. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. “dunia hii mbovu iliyopo sasa,” 1:4
2. “injili ya namna nyingine,” 1:6
3. Kiyahudi, 1:13
4. mapokeo ya baba, 1:14
5. “hasha,” 2:17
6. “enyi wagalatia msio na akili,” 3:1,3
7. aliyewaroga, 3:1
8. “ikiwa ni bure kweli,” 3:4; 4:11
9. “chini ya laana,” 3:10
10. “mzao wake,” 3:16
11. “iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mkono wa mjumbe,” 3:19
12. “tulikuwa tumewekwa chini ya sheria,” 3:23
13. “vitu vya kawaida,” 4:3,9
14. Aba, 4:6
15. “udhaifu wa mwili,” 4:13
16. “wa mjakazi. . .wa muungwana,” 4:23
17. kwa mfano, 4:24
18. “enendeni kwa Roho,” 5:16
19. “tunda la Roho,” 5:22
20. “kwa herufi gana kubwa,” 6:11
21. “chapa zake Yesu,” 6:17

VII. WATU WA KUWATAMBUA KI-MUHTASARI

1. “malaika wa mbinguni,” 1:8
2. Kefa, 1:18
3. Barnaba, 2:1
4. Tito, 2:2
5. “kwa hao walio wenye sifa,” 2:2,6

6. “ndugu za uongo,” 2:4
7. “wenye sifa kuwa nguzo,” 2:9
8. “kusanyiko la waliotahiriwa,” 2:12
9. “mawakili na watunzaji,” 4:2
10. Hajiri, 4:25

VIII. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. makanisa ya Galatia, 1:2
2. Arabuni, 1:17
3. Dameski, 1:17
4. Shamu, 1:21
5. Kilikia, 1:21
6. Antiokia, 2:11

IX. MASWALI YA MJADALA

1. Elezea kwa maneno yako mwenyewe 1:11-12.
2. Ni wakati gani Paulo alilitesa kanisa la Mungu? (1:13)
3. Ni kwa nini baadhi walitaka Tito atahiriwe? (7:3)
4. Elezea 2:6 kwa maneno yako mwenyewe.
5. Wagalatia 2:16 yumkini ikawa ni dhamira ya kitabu kizima. Kwa nini?
6. Elezea 2:20 kwa maneno yako mwenyewe.
7. Ni kwa namna gani unaweza kujibu swali la Paulo katika 3:3?
8. Elezea umuhimu wa dondoo ya Paulo katika Mwa. 15:6,8 kwa Gal. 3:6-8.
9. Ni kwa namna gani Yesu alifanyika laana? (3:13)
10. Ni nini kusudi la Agano Jipya katika nuru ya 3:19?
11. Kwa nini 3:22 ni kama muhtasari mzuri wa maelezo?
12. Kwa nini 3:28 ni ukweli wa muhimu?
13. Ni nini udhaifu wa mwili wa Paulo unaotajwa katika 4:13?
14. Ni nini lengo la Ukristo? (4:19)
15. Ni nini lengo la kithiolojia la Paulo katika 5:3?
16. Elezea mithali katika 5:9.
17. Ni nini ambacho 5:4 ilimaanisha, “mmeanguka na kutoka katika hali ya neema”?
18. Ni kwa namna gani 5:13 inasimuliwa katika Warumi 14:1-15:13?
19. Elezea 5:23 kwa maneno yako mwenyewe.
20. Kwa namna gani waaminio wanasimuliwa kwa waaminio watenda dhambi? (6:1-5)
21. Ni kanuni gani za kiroho zinazothibitishwa katika 6:7?
22. Kwa namna gani 6:10 inasimulia wale walio nje ya jamii ya waaminio?

UTANGULIZI WA WAEFESO

I. MAELEZO YA UTANGULIZI

- A. Kweli za kitabu hiki zimeathiri maisha ya watakatifu wengi
 - 1. Samuel Coleridge alikiita “tungo ya ki-Mungu iliyofanywa na mwanadamu”
 - 2. John Calvin ilikiita kitabu chake akipendacho zaidi katika Biblia
 - 3. John Knox aliomba mahubiri ya Calvin juu ya Waefeso yasomwe kwake wakati wa kufa kwake
- B. Kitabu hiki kimeitwa “taji ya thamani,” au jiwe la nakshi, la thiolojia ya Paulo. Maudhui makubwa ya Paulo yanaelezwa katika mtindo mzuri wa kimuhtasari.
- C. Kama Mungu aliwatumia Warumi kuchochea Mapinduzi, Atatumia Waefeso kuunganisha upya Ukristo uliovunjika. Umoja wa waamini na amani katika Kristo inapita mbali tofauti yao.

II. MWANDISHI

- A. Paulo
 - 1. Anaelezwa katika 1:1, 3:1
 - 2. Rejea kwa kufungwa (yaweze kana katika Rumi) katika 3:1; 4:1; 6:20
 - 3. Karibia desturi ya kanisa isiyo na jina
 - a. Clement wa Rumi, mnamo mwaka 95 B.K., aliandika barua kwa Korintho ambayo inanukuu 4:4-6
 - b. Ignatius (0-107 B.K.) ana nukuu kutoka 1:9; 2:19; 3:4-9
 - c. Polycarp (65-155 B.K.), mwanafunzi wa Yohana Mtume na askofu wa Smirna anaelezea uandishi wa Paulo
 - d. Irenaeus (130-200 B.K.) anaelezea uandishi wa Paulo
 - e. Clement wa Iskandria (150-210 B.K.) anaelezea uandishi wa Paulo
 - 4. Kimeorodheshwa katika
 - a. Orodha ya Marcion (aliyekuja Rumi mnamo miaka ya 140 B.K.) ya vitabu vinavyokubalika
 - b. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa vya Muratorian Fragment (180-200 B.K.), kutokea Rumi na kuwekwa katika maandiko ya Paulo
 - 5. Hitimisho la vyote Wakolosai na Waefeso vina maneno 29 ambayo yanakaribiana sana kwa ufanano katika Kiyunani (kuna maneno ya nyongeza mawili katika Wakolosai.).
- B. Mwandishi mwingine
 - 1. Erasmus alikuwa wa kwanza kutilia mashaka uandishi wa Paulo akijikita katika
 - a. Staili/aina - sentensi ndefu ambazo hazina tabia za uandishi wa Paulo kama ilivyo katika barua zingine
 - b. hakuna salamu za mtu mmoja mmoja
 - c. misamiati ya upekee
 - 2. Uanazuoni wa karne ya 18 ulianza kukataa uandishi wa Paulo
 - a. Mistari kadhaa inaonekana kutokea kwa mwamini wa kizazi cha pili, 2:20; 3:5
 - b. Maneno ya kithiolojia yalitumika yakiwa na maana tofauti (mfano: “siri”)
 - c. upekee wa aina ya barua au nyaraka iliyotumwa

C. Majibu kwa hoja za Erasmus

1. Aina ya uandishi wake ni tofauti kwasababu Paulo alikuwa na muda wa kufikiria wakati akiandikia Waefeso wakati akiwa gerezani.
2. Ukosefu wa salamu za binafsi inaelezwa na ukweli kwamba Waefeso ilikuwa barua iliyotumwa kwa makanisa mengi katika eneo. Njia ya kuelekea Rumi ambayo ilijumuisha Efeso na Bonde la Mto Lycus inaweza kuonekana katika Ufunuo 2-3. Paulo aliandika barua nyenza, Wakolosai kwa kundi bayana la makanisa matatu ambalo lilijumuisha salamu binafsi kadhaa.
3. Hesabu ya maneno ya upekee katika Waefeso ni sawasawa kabisa kama hesabu ya maneno ya upekee (*hapax legomena*) katika Warumi. Kusudi, mada, wapokeaji na mazingira yanaelezea matumizi ya maneno mapya.
4. Paulo anazungumzia “mitume na manabii” katika 1 Kor. 12:28, ambayo ni sawasawa 2:20 na 3:5. Hakuna anayekana uandishi wa Paulo wa 1 Wakorintho.

III. UHUSIANO WA KIFASIHI KATI YA WAKOLOSAI NA WAEFESO

A. Uhusiano wa kihistoria kati ya Wakolosai na Waefeso

1. Epafra (Kol. 1:7; 4:12; Filemoni 23) aliongoa wakati wa kampeni ya Paulo kwa Waefeso (Mdo.19)
 - a. Alichukua imani yake mpya na kuipeleka nyumbani kwao, Bonde la Mto Lycus.
 - b. Alianzisha makanisa matatu—katika Hierapoli, Laodikia na Kolosai.
 - c. Epafra alimtafuta Paulo kwa ajili ya ushauri ni namna gani ya kukabiliana na maoni yenye mpasuko wa kiulimwengu wa wavumishi. Paulo alikuwa gerezani huko Rumi (mwanzoni mwa miaka ya 60).
2. Walimu wa uongo walikuja na kuanza kuunganisha injili pamoja na elimu ya Kiyunani
 - a. roho na mada vilikuwa vitu vyanza vyenye umilele
 - b. roho (Mungu) alikuwa mzuri
 - c. mada (uumbaji) ulikuwa uovu
 - d. mfululizo wa miaka mingi (viwango vya malaika) ilikuwepo kati ya Mungu mkuu mwema na mungu mdogo aliyetengeneza mada
 - e. wokovu ulijikita katika maarifa ya siri ambayo yalisaidia watu kuendelea kwa miaka mingi (viwango vya kimalaika)

B. Uhusiano wa kifasihi kati ya barua mbili za Paulo

1. Paulo alisikia habari za uvumi katika makanisa haya ambayo alikuwa hajawahi kuyatembelea yeye binafsi kutoka kwa Epafra.
2. Paulo aliandika barua inayogusa na ngumu kwa ufupi, sentensi zilizojaa uzito, zilizokusudiwa moja kwa moja kwa walimu wa uongo. Maudhui makuu yalikuwa u-Bwana wa kiulimwengu wa Yesu. Hii inajulikana kama barua ya Paulo kwa Wakolosai.
3. Inavyoonekana, mara baada ya kuandika Wakolosai, kwa muda katika mikono yake katika gereza, alizalisha maudhui haya. Waefeso inaundwa na tabia ya kuwa na sentensi ndefu na kukuzwa kwa dhana za kithiolojia (1:3-14, 15-23; 2 :1-10, 14-18, 19-22; 3:1-12, 14-19; 4:11-16; 6:13-20). Inawachukua Wakolosai kama sehemu ya kuanzia na kutoa maana zake za kithiolojia. Maudhui yake makuu ni umoja wa vitu vyote katika Kristo ambayo inatofautishwa na dhana inayokua ya walimu wa uongo.

C. Muundo unaohusiana kifasihi na kithiolojia

1. Ufanano wa muundo wa msingi
 - a. vina ufunguzi unaofanana
 - b. vina sehemu za kimafundisho zinazohusiana kimsingi na Kristo
 - c. vina sehemu mahususi halisi zinazoonya mtindo wa maisha kwa kutumia vipengele vinavyofanana, misamiati na tungo
 - d. vina mistari ya ufungaji inayofanana kabisa kabisa katika maneno 29 yanayofuatana katika Kiyunani yakiwa na maneno mawili tofauti yanayoongezwa katika Wakolosai.

2. Ufanano wa maneno au tungo fupi

Efe. 1:1c na Kol. 1:2a	“mwaminifu”
Efe. 1:4 na Kol. 1:22	“takatifu na isiyo na mawaa”
Efe. 1:7 na Kol. 1:14	“ukombozi . . . msamaha”
Efe. 1:10 na Kol. 1:20	“vitu vyote . . . mbingu. . . nchi”
Efe 1:15 na Kol. 1:3-4	“kusikia . . . upendo kwa watakatifu wote”
Efe1:18 na Kol. 1:27	“utajiri wa utukufu”
Efe. 2:1 na Kol. 1:13	“nanyi mlikuwa mmekufa”
Efe. 2:16 na Kol. 1:20	“kupanishwa . . . msalaba”
Efe. 3:2 na Kol. 1:25	“wakili”
Efe. 3:3 na Kol. 1:26,27	“siri”
Efe. 4:3 na Kol. 3:14	“ umoja”
Efe. 4:15 na Kol. 2:19	“kichwa” na “kukua”
Efe. 4:24 na Kol. 3:10,12,14	“vaeni . . .”
Efe. 4:31 na Kol. 3:8	“hasira,” “ghadhabu,” “uongo,” “uzushi”
Efe. 5:3 na Kol. 3:5	“uchafu,” “mawazo mabaya,” “tamaa mbaya”
Efe. 5:5 na Kol. 3:5	“ibada ya sanamu” (tamaa mbaya)
Efe. 5:6 na Kol. 3:6	“ghadhabu ya Mungu”
Efe. 5:16 na Kol. 4:5	“mkiukomboa wakati”

3. Sentensi na tungo zilizo na ufanano sawa kabisa

Efe. 1:1a na Kol. 1:1a
 Efe. 1:1b na kol. 1:2a
 Efe. 1:2a na Kol. 1:2b
 Efe. 1:13 na Kol. 1:5
 Efe. 2:1 na kol. 2:13
 Efe. 2:5b naKol. 2:13c
 Efe. 4:1b na Kol. 1:10a
 Efe. 6:21-22 na Kol. 4:7-8 (maneno 29 yenye mfuatano wa kufanana hasa isipokuwa kwa “*kai syndoulos*” katika Wakolosai)

4. Ufanano wa tungo na sentensi

Efe. 1:21 na Kol. 1:16
 Efe. 2:1 na Kol. 1:13
 Efe. 2:16 na Kol. 1:20
 Efe. 3:7a na Kol. 1:23d, 25a
 Efe. 3:8 na Kol. 1:27

Efe. 4:2 na Kol. 3:12
Efe. 4:29 na Kol. 3:8; 4:6
Efe. 4:32b na Kol.3:13b
Efe. 5:15 na Kol. 4:5
Efe. 5:19-20 na Kol. 3:16

5. Dhana za kithiolojia zinazofanana:

Efe. 1:3 na Kol. 1:3	maombi ya shukrani
Efe. 2:1,12 na Kol. 1:21	kutengwa mbali na Mungu
Efe. 2:15 na Kol. 2:14	uadui wa sheria
Efe. 4:1 na Kol. 1:10	kutembea sawasawa
Efe. 4:15 na Kol. 2:19	mwili wa Kristo unaokua katika ukomavu kutoka katika Kichwa
Efe. 4:19 na Kol. 3:5	mawazo mabaya ya zinaa
Efe. 4:22,31 na Kol. 3:8	“wekeni kando” dhambi
Efe. 4:32 na Kol. 3:12-13	mkikirimiana Kikristo wenyewe kwa wenyewe
Efe. 5:4 na Kol. 3:8	kauli za mkristo
Efe. 5:18 na Kol. 3:16	kujazwa na Roho = neno la Kristo
Efe. 5:20 na Kol. 3:17	Mkimshukuru Mungu kwa mambo yote
Efe. 5:22 na Kol. 3:18	wake watiini waume zenu
Efe. 5:25 na Kol. 3:19	waume wapendeni wake zenu
Efe. 6:1 na Kol. 3:20	watoto watiini wazazi wenu
Efe. 6:4 na Kol. 3:21	baba msiwachokoze watoto
Efe. 6:5 na Kol. 3:22	watumwa watiini bwana zenu
Efe. 6:9 na Kol. 4:1	bwana na watumwa
Efe. 6:18 na Kol. 4:2-4	ombi la Paulo kwa ajili ya Maombi

6. Maneno yaliyotumika katika vyote Wakolosai na Waefeso yanapatikana katika fasihi nyingine za Paulo

a. “ukamilifu”

Efe. 1:23 “ukamilifu katika yeye atujazaye yote katika yote”

Efe. 3:19 “mjazwe kwa wote kwa ukamilifu wa Mungu”

Efe. 4:13 “mpaka ukamilifu wa Kristo”

Kol. 1:19 “kwa maana ukamilifu wote unakaa ndani Yake”

b. Kristo kama “kichwa” cha kanisa

Efe. 4:15, 5:23 na Kol. 1:18;2:19

c. “kutengwa”

Efe. 2:12; 4:18 na Kol. 1:21

d. “mkiukomboa wakati”

Efe. 5:16 na Kol. 4:5

e. “mmepandwa”

Efe. 3:17 na Kol. 2:7

f. “neni la kweli, injili”

Efe. 1:13 na Kol. 1:5

g. “mkizaa”

Efe. 4:2 na Kol. 3:13

- h. utungwaji usiokuwa wa kawaida na maneno (“kushikanishwa pamoja,” “atawajazeni”)
Efe. 4:16 na Kol. 2:19

D. Muhtasari

1. Zaidi ya moja ya tatu ya maneno katika Wakolosai yako katika Waefeso,. Imekadiriwa kwamba mistari 75 kati ya 155 katika Waefeso inafanana na Wakolosai. Vyote viwili vinadai kuandikwa na Paulo akiwa gerezani.
2. Vyote vilipelekwa na rafiki wa Paulo aitwaye Tikiko.
3. Vyote vilitumwa kwa eneo moja (Asia Ndogo).
4. Vyote vilizungumzia mada ya Kristo.
5. Vyote husisitiza Kristo kama kichwa cha kanisa.
6. Vyote husisitiza maisha ya mwenendo sahihi wa Mkristo.

E. Hoja Kubwa za Kutofanana

1. Kanisa siku zote lilikuwa la eneo la mahali huko kwa Wakolosai lakini kwa wote mpaka huko kwa Waefeso. Hii inaweza kuwa kwa sababu ya asili ya barua ya kuwa iliandikwa kwa ajili ya wote ya Waefeso.
2. Uvumi ambao ulikuwa tabia kubwa ya Wakolosai, hautajwi moja kwa moja katika Waefeso. However, hata hivyo, barua zote mbili zinatumia maneno yenye tabia ya walimu wa uongo (“hekima,” “maarifa,” “ukamilifu,” “siri,” “mamlaka na nguvu” na “wakili.”)
3. Kuja kwa mara ya pili ni kwa mara katika Wakolosai lakini kunachelewa katika Waefeso. Kanisa lilikuwa na linatakiwa kuhudumu katika ulimwengu ulioanguka. (2:7; 3:21; 4:13).
4. Maneno kadhaa yenye tabia za uandishi wa Paulo yanatumia tofauti tofauti. Moja ya mfano ni neno “siri.” Katika Wakolosai siri ni Kristo (Kol. 1:26-27; 2:2; 4:3), lakini katika Waefeso (1:9; 5:32) lilifichwa hapo mwanzo na Mungu lakini sasa linafunuliwa, mpango kwa ajili ya umoja wa Mataifa na Wayahudi.
5. Waefeso ina maelezo kadhaa ya Agano la Kale (1:22—Zab. 8; 2:17—Isa. 57:19) (2:20—Zab. 118:22) (4:8—Zab. 68:18) (4:26—Zab. 4:4) (5:15—Isa. 26:19, 51:17, 52:1, 60:1) (5:3—Mwa. 3:24) (6:2—3-Kut. 20:12) (6:14—Isa. 11:5, 59:17) (6:15—Isa. 52:7), lakini liko moja tu au mawili (2:3—Isa. 11:2) au (2:22—Isa. 29:13).

F. Ingawa ni maneno yanayofanana, tungo na mara kwa mara uainishi, barua pia inajumuisha kweli za kipekee.

1. Baraka za utatu za neema - Efe. 1:3-14
2. Kifungu cha neema - Efe. 2:1-10
3. Kuunganishwa kwa Wayahudi na Mataifa katika mwili mmoja - Efe. 2:11-3:13
4. Umoja na karama za mwili wa Kristo - Efe. 4:1-16
5. “Kristo na kanisa” ni mfano wa “mume na mke” Efe. 5:22-33
6. Kifungu cha vita vya kiroho - Efe. 6:10-18
7. Kifungu cha elimu juu ya upekee wa Kristo - Kol. 1:13-18
8. Taratibu za kidini za kibinadamu na sheria - Kol. 2:16-23
9. Mada ya umuhimu wa kiulimwengu ya Kristo katika Kolosai dhidi maudhui ya umoja wa vitu vyote katika Kristo katika Waefeso

- G. Katika hitimisho, inaonekana kuwa bora kufuata A. T. Robertson na F. F. Bruce katika kuelezea kwamba Paulo aliandika vitabu vyote kwa ukaribiano kwa kukuza fikra za Wakolosai katika muhuri uwasilishaji wa kweli.

IV. TAREHE

- A. Tarehe ya barua hii inaunganishwa na kifungo cha Paulo huko Efeso, Filipi, Kaisaria au Rumi. Kifungo cha Kirumi kinashabihiana bora zaidi na kweli za Matendo ya Mitume.
- B. Wakati Rumi inachukuliwa kuwa sehemu ya kifungo zaidi, swali linakuja, wakati gani? Paulo alikuwa jela mnamo miaka ya mwanzoni mwa miaka ya 60, ambayo inaandikwa katika Matendo ya Mitume lakini aliachiwa na kuandika nyaraka za Kichungaji (1 & 2 Timotheo na Tito) na baadaye alikamatwa tena na kuuawa kabla ya Juni 9, mnamo mwaka 68 B.K., ambayo ilikuwa ni tarehe ya kujiuwa kwa Nero.
- C. Dhanio la kisomi bora zaidi kwa kuandikwa kwa Waefeso ni kufungwa kwa mara ya kwanza kwa Paulo huko Rumi mnamo mwanzoni mwa miaka ya 60.
- D. Tikiko pamoja na Onesmo, yawezekana walichukua barua za Wakolosai, Waefeso na Filemoni mpaka Asia Ndogo.
- E. Mfuatano wa maandiko ya Paulo kwa mujibu wa F. F. Bruce na Murry Harris pamoja na marekebisha madogo.

<u>Kitabu</u>	<u>Tarehe</u>	<u>Mahali pa kuandikwa</u>	<u>Uhusiano na Mdo.</u>
1. Wagalatia	48 (nadharia ya kusini)	Antiokia ya Shamu	14:28; 15:2
2. 1 Thesalonike	50	Korintho	18:5
3. 2 Thesalonike	50	Korintho	
4. 1 Thesalonike	55	Efeso	19:20
5. 2 Thesalonike	56	Makedonia	20:2
6. Warumi	57	Korintho	20:3
7. - 10.			
Wakolosai	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	
Waefeso	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	28:30-31
Filemoni	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	
Wafilipi	mwishoni mwa 61-62 (gereza)	Rumi	
11. 1 Timotheo	63 (au baadaye, lakini	Makedonia	
12. Tito	63 kabla	Efeso (?)	
13. 2 Timotheo	64 mnamo 68)	Rumi	

V. WAPOKEAJI

- A. Maandiko mengi (Mafunjo ya Chester Beatty, P⁴⁶; Sinaiticus, X, Vaticanus, B; Andiko la Kiyunani la Origen, na andiko la Kiyunani la Tertullain) yanaondoa “huko Efeso” katika 1:1. Matoleo ya RSV na Williams yanaondoa tungo.
- B. Sarufi ya Kiyunani ya mstari wa 1 inaweza kuwa na jina la sehemu. Yawezekana barua ya jumla, eneo la jina la kanisa liliachwa wazi ili liweze kujazwa wakati wakusomwa kwa sauti kwa makanisa. Hii inaweza kuelezea Tungo katika Wakolosai 4:15-16, “barua toka kwa Wa-Laodikia,” ambayo yawezekana ni Kitabu cha Waefeso (Marcion alikiita Waefeso kwa jina la “barua kwenda kwa wa-Laodikia”).

- C. Waefeso kiliandikwa kimsingi kwa Mataifa, 2:1; 4:17, ambao Paulo alikuwa hajawahi kukutana nao yeye mwenyewe, 1:15; 3:2. Kanisa katika Bonde la Mto Lycus (Laodikia, Hierapoli, na Kolosai) lilianzishwa sio na Paulo bali na Epafra (Kol. 1:7; 4:12; Filemoni 23).

VI. KUSUDI

- A. Maudhui ya kitabu yanapatikana katika 1:10 na 4:1-10, ambayo yanasisitiza umoja wa vitu vyote katika Kristo. Kristo anarejeshwa taswira ya Mungu katika ubinadamu na katika ulimwengu (*kosmos*).
- B. Waefeso ni moja ya barua za Paulo kati ya nne alizoandika akiwa gerezeni. Ainisho la Waefeso na Kolosai lina ufanano sawa. Wakolosai kiliandikwa kukabiliana na uvumi wa nadharia za Elimu ya Wajuzi inayokua katika Bonde la Mto Lycus la Asia Ndogo. Waefeso iliandikwa kama barua ya jumla kwa eneo lile lile kuandaa makanisa mengine kwa ujio wa uvumi. Wakolosai ni fupi na tamu, ngumu, wakati Waefeso ni uwasilishaji uliopanuliwa wa kimantiki wa kweli ile ile kwa kutumia sentensi ndefu sana: (1:3-14, 15-23; 2:1-9; 3:1-7, na kuendelea.).

VII. AINISHO FUPI

- A. Kitabu kiasili kinagawanyika katika sehemu mbili (kama ilivyo kwa maandiko mengi ya Paulo)
1. Umoja katika Kristo, sura ya 1-3 (thiolojia)
 2. Umoja katika kanisa, sura ya 4-6 (utendeaji kazi)
- B. Ainisho la ki-maudhui lililopendekezwa
1. Ufunguzi wenye tabia ya kidesturi kama ya Paulo, 1:1-2
 2. Mpango wa Baba kwa umoja wa vitu vyote katika Kristo, 1:3-3:21
 - a. Sifa za Paulo kwa Baba, 1:3-14
 - (1) kwa upendo wa Baba kabla ya muda
 - (2) Kwa ajili ya upendo wa Bababa kupitia mwanawe kwa muda sahihi
 - (3) kwa ajili ya upendo wa Baba unaoendelea kupitia Roho kwa muda
 - b. maombi ya Paulo kwa Baba kwa ajili ya makanisa, 1:15-23
 - (1) kwa ajili ya ufunuo wa Baba katika Kristo unaweza kueleweka
 - (2) kwa ajili ya nguvu ya Baba kufanya kazi kwa nguvu katika waamini
 - (3) kwa ajili Kristo kutukuzwa kwa njia ya Baba kuliko kila kitu
 - c. Uelewa wa Paulo wa mpango wa Baba kwa wanadamu wote, 2:1-3:13
 - (1) hitaji la mwanadamu mwenye dhambi
 - (2) utoshelevu wa neema wa Baba
 - (3) mwitikio wa kiagano wa mwanadamu unaohitajika
 - (4) mpango wa Baba unaofunuliwa kikamilifu
 - d. Maombi ya Paulo kwa Baba kwa ajili ya Waaminio, 3:14-21
 - (1) kupokea nguvu ya ndani (kwa njia ya Roho)
 - (2) kuelewa injili kiukamilifu (sio kwa kweli pendekekezwa tu) katika uzoefu na upendo
 - (3) kujazwa na ukamilifu wa Mungu (ambao ni Kristo)
 - (4) yote haya yatoka kwa Mungu aliye na uweza
 3. Matamanio ya Baba kwa umoja wa watu wake Wapya, 4:1-6:20
 - a. Umoja wa Utatu wa Mungu unaaksiwa katika umoja wa watoto Wake, 4:1-16
 - (1) umoja sio sare sare, bali ni mtindo wa maisha

- (2) Mungu ni utatu katika umoja
- (3) karama za roho ni kwa ajili ya ustawi wa mwili, sio kwa ajili ya heshima kwa mtu
- (4) umoja unadai huduma
- (5) umoja upo chini ya mashambulizi ya kimalaika
- (6) umoja upo katika Kristo
- b. Umoja wa Mkristo unalinganishwa na ubinafsi wa kipagani, 4:17-5:14
 - (1) weka kando matendo ya maisha ya kale
 - (2) tafta kufanana na Kristo
- c. Namna ya kutimiliza na kuendeleza umoja, 5:15-6:9
 - (1) kuendelea siku zote kujazwa na Roho
 - (2) maisha ya kujazwa na Roho yanaelezewa
 - (a) kauli endelevu tano, mistari ya. 19-21
 - (b) mifano mitatu ya nyumbani
 - i. waume – wake
 - ii. wazazi – watoto
 - iii. bwana – watumwa
- d. Kutafuta umoja wa kufanana na Kristo, 6:10-20
 - (1) vita vya kiroho
 - (2) silaha za Mungu
 - (3) nguvu ya maombi
- 4. Salamu za hitimisho, 6:21-24

VIII. HISTORIA YA NYUMA YA KIFALSAFA NA KITHIOLOJIA YA WALIMU WA UONGO (NADHARIA YA WALIMU WA UONGO)

- A. Imani ya walimu wa uongo ya karne ya kwanza na ya pili:
 - 1. Elimu ya umilele (milele) u-pili kati ya roho (Mungu) na mada (vitu vya mwilini).
 - 2. Roho alikuwa mwema, wakati mada ilikuwa ni uovu.
 - 3. Mfululizo wa viwango vya kimalaika (*eons (miaka mingi)*) kati ya Mungu mkuu mtakatifu na mungu mdogo aliyetengeneza mada za uovu.
 - 4. Njia ya wokovu
 - a. maarifa ya kanuni za siri ambayo yaliruhusu mtembeo kupitia anga la kimalaika kutoka duniani mpaka mbinguni,
 - b. kichocheo cha ki-Mungu kwa wanadamu wote ingawa si wote walioelewa au kupokea maarifa yaokoayo,
 - c. maarifa yalikuja tu kwa kundi la wasomi kwa ufunuo maalumu.
 - 5. Maadili
 - a. isiyohusiana kabisa na maisha ya kiroho (wana huru , wapingaji)
 - b. muhimu kwa ajili ya wokovu (wanasheria).
- B. Mpingano na Ukristo wa kihistoria na kibiblia
 - 1. kutenganisha ubinadamu na Uungu wa Kristo (Walimu wa uongo walisema asingeweza kuwa Mungu asilimia zote na wakati huo huo mwanadamu asilimia zote)
 - 2. kuondoa kifo chake cha mbali kama njia pekee ya wokovu
 - 3. kuweka maarifa ya kibinadamu badala ya neema ya bure ya ki-Mungu.

IX. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. watakatifu, 1:1
2. Bwana, 1:2
3. Juu mbinguni, 1:3
4. “kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,” 1:4
5. Isiyo na mawaa, 1:4
6. Iliyoamriwa kwanza, 1:5
7. “ukombozi,” 1:7
8. siri, 1:9
9. “ukamilifu wa muda,” 1:10
10. muhuri, 1:13
11. nadhiri, 1:14
12. utukufu, 1:17
13. “alimketisha mkono Wake wa kuume,” 1:20
14. “ukamilifu katika Yeye atujazaye yote katika yote,” 1:23
15. “jinsi ya ulimwengu huu,” 2:2
16. “karama ya Mungu,” 2:8
17. “wenyeji wenzangu,” 2:19
18. “jiwe kuu la pembeni,” 2:20
19. “ujasiri na kujongea kwa ujasiri,” 3:12
20. “hila za wanadamu,” 4:14
21. “kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu,” 4:14
22. “kuenenda katika upendo,” 5:2
23. “harufu ya manukato,” 5:2
24. “ufalme wa Kristo na Mungu,” 5:5
25. “mkinyenyekeana,” 5:21
26. “silaha zote za Mungu,” 6:11
27. “kujifunga,” 6:14
28. “upanga wa Roho,” 6:17

X. WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

1. Walmu wa uongo
2. “mfalme wa nguvu za anga,” 2:2
3. Mataifa
4. mitume, 4:11
5. manabii, 4:11
6. wainjilisti, 4:11
7. kichwa, 4:15
8. shetani, 4:27
9. “wana wa kuasi,” 5:6
10. “wana wa Nuru,” 5:8
11. “majeshi ya mapepo wabaya,” 6:12
12. Tikiko, 6:21

XI. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI — HAKUNA

XII. MASWALI YA MJADALA

1. Ni nini maudhui ya msingi ya 1:3-14?
2. Kwanini tungo ya “kwenye sifa za Utukufu Wake” imetumika mara tatu katika 1:3-14?
3. Kwanini Paulo anazungumza mara kwa mara juu ya “hekima na maarifa” au “maarifa” katika kitabu hiki?
4. Ni kwa nani mstari wa 1:19 unarejerea?
5. Elezea dhana ya Kiyahudi ya nyakati mbili. (1:21)
6. Andika muhtasari wa mada ya 2:1-3.
7. Andika muhtasari wa 2:4-6.
8. Elezea maelezo ya kihistoria ya 2:14.
9. Ni ufunuo gani Paulo anaouzungumzia 3:3?
10. Kwanini Paulo anajiiita mwenyewe “mdogo wa watakatifu”? (3:8)
11. Kwanini neno “mmoja” linatumika mara kwa mara katika 4:4-6?
12. Nini karama ya Kristo katika 4:7?
13. Nukuu ya Paulo ya 4:8 inapatikana wapi katika Agano la Kale? Kwanini nukuu ya Paulo ni tofauti na ya Agano la Kale?
14. Kwanini 4:12 ni muhimu sana?
15. Je 5:5 inaweka vikwazo kwa wale wote watakaokolewa?
16. Kulewa kunahusiana vipi na kujazwa na Roho? (5:18)
17. Kwanini upendo wa Mungu na sadaka kwa kanisa kunahusiana na nyumba ya Mkristo? (5:25-33)
18. Ni kwa namna gani “heshima” na “utii” vinahusiana?
19. Kwa nini 6:18 inahitajika sana leo?

UTANGULIZI WA WAFILIPU

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Hii ni moja ya nyaraka za Paulo isiyo rasmi sana. Na katika kanisa hili hakujihisi kuhitaji kutetea mamlaka yake ya kitume. Upendo wake tele kwa ajili yao ulikuwa wazi. Aliwaruhusu hata wamtumie fedha (kama vile. 1:5,7; 4:15), ambapo hii haikuwa kawaida kwa ajili yake.
- B. Paulo alikuwa kifungoni, bado alitumia neno la furaha (jina na kitenzi) zaidi ya mara kumi na sita. Amani yake na tumaini havikuwa juu ya mazingira aliyonayo.
- C. Kuna sehemu ya mafundisho ya walimu wa uongo katika kanisa la sasa (kama vile. 3:2, 18-19). Walimu hawa wanaonekana kufanana na wale walioko katika kanisa la Galatia, walioitwa washika dini ya kiyahudi. Walisisitiza kwamba yeyote anayetaka kuwa myahudi ni lazima aweze kuwa Mkristo.
- D. Nyaraka hii inahusisha mfano wa nyimbo ya awali ya Kikristo, kanuni za imani, au shairi la kawaida ya ibada (kama vile. 2:6-11). Ni mojawapo ya ujumbe mzuri zaidi wa Kikristo katika Agano Jipya zima (kama vile. Yohana 1:1-14; Kol.1:13-20; Ebr. 1:2-3). Paulo alitumia mfano wa unyenyekevu wa Kristo ili kufuatishwa na kila mwamini (kama vile. 2:1-5), sio mwanzo katika maana ya mafundisho.
- E. Katika kitabu chenye vifungu 104, jina la Yesu au cheo limejitokeza mara 51. Ni wazi nani alikuwa katika kiini kwenye moyo wa Paulo, fahamu na theolojia.

II. FILIPU NA MAKEDONIA

A. Mji wa Filipi

- 1. Katika mwaka 356 B.K. ulikamatwa na kukuzwa zaidi na Filipo II wa Makedonia, baba yake Iskanda mkuu. Wenyeji wa kijiji hiki kwa asili waliitwa *Krenides* (uzao). Mji ulikuwa wa muhimu kwa sababu ulikuwa na shaba katika jimbo.
- 2. Katika vita ya Pydna mwaka wa 168 B.K., ulikuwa katika mamlaka ya Rumi na baadae robo ya mji ikawa katika Makedonia.
- 3. Katika mwaka wa 42 B.K., Brutus na Cassius (wa republicani) walimpiga Antony na Octavian (kifalme) karibu na Filipi, juu ya mabadiliko ya utawala katika Rumi. Baada ya vita, Antony aliimarisha baadhi ya majeshi yake ya ushindi hapa.
- 4. Katika mwaka wa 31 B.K., baada ya vita ya Actium ambapo Octavian alimshinda Antony, wafuasi wa Antony katika Rumi waliondolewa madarakani na kufukuzwa hapa.
- 5. Katika mwaka wa 31 B.K. mji Filipi ulikuwa chini ya utawala wa Rumi (kama vile. Mdo 16:12). Watu wa mji walitangazwa kuwa raia wa Rumi. Kilatini kilizungumzwa na mji ukawa kama Rumi ndogo. Ulikuwa katika sehemu ya njia ya Ignatian, barabara kuu ya mashariki kwenda magharibi mwa Rumi. Uhuru wa kiraia pekee walioufurahia kama raia wa Rumi ulikuwa ni:
 - a. hakuna kodi ya kichwa na kodi ya aridhi
 - b. haki ya kuuza na kununua mali
 - c. ulinzi wote na haki ya sheria za Rumi
 - d. viongozi maalumu wa mamlaka (mahakimu na magavana)

B. Injili inakuja Filipi

1. Katika safari ya pili ya umisionari ya Paulo alitaka kugeukia kaskazini ili kuingia Asia kati kaskazini (Uturuki ya sasa, kibiblia Bithinia). Badala yake, katika maono alimwona mtu (inawezekana Luka) wa Makedonia (kaskazini mwa Uyunani) na kumwambia uje utusadie (Mdo. 16:6-10). Kwa maono haya Roho alimwongoza Paulo kwenda ulaya.
2. Paulo aliambatana na wasaidizi wake
 - a. Sila (Silwano)
 - (1) Sila alikuwa kiongozi kutoka kanisa la Yerusalemu na mtume aliyewekwa mahali pa Barnaba kama mtenda kazi ya umisionari wa Paulo (kama vile Mdo. 15:15:22,32; 36-41);
 - (2) Sila na Paulo wote walifungwa gerezani huko Filipi (Mdo. 16:16-26);
 - (3) Paulo mara nyingi alipenda kumuita Silwano (kama vile. II Kor. 1:19; I Thes. 1:1; II Thes. 1:1);
 - (4) inawezekana kwamba baadae Sila alikuja kuambatana na Petro, kama alivyofanya Yohana Marko (kama vile I Pet. 5:12).
 - b. Timotheo
 - (1) aliamini katika safari ya kwanza ya umisionari ya Paulo (kama vile Mdo. 16:1-2; II Tim. 1:5; 3:15);
 - (2) bibi yake na mama yake walikuwa wayahudi, lakini baba yake alikuwa myunani (kama vile Mdo. 16:1; II Tim. 1:5);
 - (3) kwa sababu alishuhudiwa vyema na ndugu (kama vile Mdo 16:2) na Paulo akaiona karama ya huduma ndani yake (kama vile I Tim. 4:14; II Tim. 1:6), alimchagua kama msaidizi ili kuchukua nafasi ya Yohana Marko (kama vile Mdo. 13:13);
 - (4) Paulo alimtahiri Timotheo hivyo kwamba aweze kukubaliwa na wayahudi (kama vile Mdo. 16:3);
 - (5) Timotheo alikuja kuwa mwakilishi mwaminifu wa kitume wa Paulo (kama vile Fil. 2:19-22; I Kor. 4:17; 3:2,6; II Kor. 1:1,19).
 - c. Luka
 - (1) asiyefahamika, lakini inawezekana, mwandishi wa injili ya Luka na Matendo ya Mitume;
 - (2) ni dhahili alikuwa ni tabibu wa mataifa (kama vile. Kol. 4:14). Baadhi wanafikilia neno “tabibu” linamaanisha “mwenye elimu ya juu.” ni ukweli usio na mashaka kwamba alikuwa anafahamika katika maeneo kadhaa ya kiufundi vile vile na madawa, kama baharia. Hata hivyo, Yesu alitumia neno hili hili la kiyunani kwa ajili ya “tabibu” (kama vile. Mt. 9:12; Marko 2:17; 5:26; Luka 4:23; 5:31);
 - (3) Aliambatana na Paulo katika safari (kama vile Mdo. 16:10-17; 20:5-15; 21:1-18; 27:1-28:16; Kol. 4:14; II Tim. 4:11; Filemoni 24);
 - (4) inatia shauku kwamba “sisi” ni mwanzo wa sehemu za Matendo ya Mitume na kuishia katika Wafilipi. Katika *Paul, Apostle of the Heart Set Free*, (uk. 219), F. F. Bruce anashauri kwamba Luka alikaa Filipi ili kuwasaidia waaminio wapya na kukusanya misaada ya wamataifa kwa ajili ya kanisa la Yerusalemu.
 - (5) Luka yumkini alikuwa, katika maana, tabibu binafsi wa Paulo. Paulo alikuwa na matatizo kadhaa ya mwili kutokana na kuongoka kwake (kama vile Mdo. 9:3,9), huduma yake (kama vile. II Kor. 4:7-12; 6:4-10; 11:23-29) na udhaifu wake maalumu (kama vile. II Kor. 12:1-10).
3. Paulo alirudi Filipi katika safari yake ya tatu ya umisionari (kama vile Mdo. 20:1-3,6). Alikuwa amewatuma Sila na Timotheo mapema (kama vile Mdo. 19:19-24; Fil. 2:19-24).

- C. Filipi kama mji wa utawala wa Rumi (kama vile Mdo. 16:12)
1. Paulo alikutumia hali ya mji huu kama utawala wa Rumi katika istilahi yake
 - a. “askari wa praitorio,” 1:13
 - b. “wenyeji,” 3:20 (Mdo. 16:22-34, 35-40)
 - c. “nyumbani mwa Kaisaria,” 4:22
 2. Mji ulikuwa na idadi kubwa ya maaskari waliofukuzwa na waliostaafu. Kwa njia nyingi ulikuwa “Rumi ndogo.” Vivutio vingi vya Rumi viliweza kuonekana katika mitaa ya Filipi (kama vile. Mdo 26:21).
 3. Wote Paulo (Mdo. 22:25; 26:32) na Sila (Mdo. 16:37) walikuwa raia wa Rumi, ambao uliwaruhusu wao kuwa na haki halali na kusimama katika jamii.
- D. Jimbo la Makedonia
1. Wanawake walikuwa na uhuru wa kijamii na nafasi za kiuchumi katika Makedonia zaidi kuliko sehemu yeyote ile katika utawala wa Rumi.
 2. Hii inaelezewa kwa picha na
 - a. uwepo wa wanawake wengi waliokuwa wakiabudu kando ya mto nje ya mji wa Filipi (kama vile. Mdo 16:13);
 - b. Lidia mfanya biashara mwanamke (kama vile Mdo. 16:14);
 - c. wanawake watenda kazi katika injili (kama vile. 4:2-3);
 - d. wanawake kadhaa muhimu waliotajwa katika Thesalonike (pia katika Makedonia, kama vile. Mdo. 17:4).

III. MWANDISHI

- A. Hii ni nyaraka kuu binafsi ambayo mara zote ilimtambulisha Paulo. Viwakilishi vya awali vya mtu “mimi” na “yangu” vimetokea mara 51.
- B. Ni dondoo au dokezo kwa waandishi wa awali (kwa kukamilisha orodha ya maelezo tazama H.C. G. Moule, *Studies in Philippians*, krs. 20-21, iliyochapishwa na Kregel):
1. Clement wa of Rumi katika *I Clement*, iliyoandikwa kwa kanisa la Wakorintho yapata mwaka wa 95 B.K;
 2. Ignatius, katika *Letters of Ignatius*, yapata mwaka wa 110 B.K;
 3. Polycarp, aliyeambatana na mtume Yohana, katika *Letter to the Philippians*, yapata mwaka wa 110 B.K;
 4. utangulizi wa Marcionite (aliyefuata maelezo ya Marcion) kwa nyaraka za Paulo kwa Wafilipi yapata mwaka wa 170 B.K.
 5. Irenaeus, yapata mwaka wa 180 B.K;
 6. Clement wa Iskandria, yapata mwaka wa 190 B.K;
 7. Tertullian wa Carthage, yapata mwaka wa 210 B.K.
- C. Ingawa Timotheo ametajwa pamoja na Paulo katika 1:1, yeye alikuwa ni mtenda kazi, sio mwandishi mwenza (ingawa yumkini alitenda kama mwandishi kwa ajili ya Paulo nyakati kwa nyakati).

IV. TAREHE

- A. Tarehe inategemeana na mahali alipokuwa amefungwa Paulo (kama vile II Kor. 11:23)

1. Filipi, Mdo. 16:23-40;
2. Efeso, I Kor. 15:32; II Kor. 1:8;
3. Yerusalemu/Kaisaria, Mdo. 21:32-33:30;
4. Rumi, Mdo. 28:30 (imeelezwa katika utangulizi wa Marcionite kwa Wafilipi)

- B. Wanazuoni maarufu wanaamini kwamba kifungo cha Rumi kinafaa muktadha wa maisha ya Paulo na matendo bora zaidi. Ikiwa ni hivyo, tarehe inaonekana kufanana zaidi katika miaka ya mwanzoni mwa 60.
- C. Kitabu hiki kinafahamika kama moja ya “barua za kifungoni” za Paulo (Wakolosai, Waefeso, Filemoni, na Wafilipi). Kutoka katika fikra za ndani inajitokeza kwamba Wakolosai, Waefeso, na Filemoni viliandikwa mwanzoni kipindi cha kifungo cha Paulo na vikachukuliwa pamoja kwenda Asia ndogo na Tychicus (Kol. 4:7; Efe. 6:21). Kitabu cha Wafilipi kina mtazamo tofauti. Paulo anaona uhakika wa kuachiliwa kutoka gerezani (1:17-26) na anaweza kuwatembelea wao (2:24).

Muundo huu pia unatoa kipindi cha wakati wa: (1) ushawishi wa Paulo wa kuwafikia maaskari wa kifalme (kama vile. 1:13; Mdo. 28:16) na watumishi (kama vile 4:22); na (2) safari kadhaa kati ya Paulo na wajumbe kutoka kanisa la Filipi.

V. MAKUSUDI YA BARUA

- A. Kuwasilisha shukrani za Paulo kwa kanisa hili pendwa kwamba walimsaidia fedha mara kadhaa na hata kumtuma msaidizi, Epafrodito (kama vile. 1:3-11; 2:19-30; 4:10-20). Nyaraka pia yumkini iliandikwa kumwelezea Epafrodito kurudi mapema nyumbani wakati ambapo Paulo bado yuko gerezani.
- B. Kuwatia moyo Wafilipi juu ya hali zao. Injili kwa uhakika ilikuwa inasonga mbele ndani ya gereza. Paulo alikuwa kawekewa mipaka, lakini injili ilikuwa haina mipaka!
- C. Kuwatia moyo Wafilipi katikati ya mafundisho ya uongo ambayo yalifanana sana na washika dini ya kiyahudi katika Wagalatia. Mafundisho haya yalidai kwamba waaminio wapya wawe wayahudi kwanza na kisha Wakristo (kama vile. Mdo 15).

Hata hivyo kwa sababu ya orodha ya dhambi katika 3:19 zinawafaa walimu wa uongo wa kiyunani (mafunuo) zaidi sana kuliko wayahudi, mfanano wa mafundisho unatia mashaka. Inawezekana kwamba baadhi ya waaminio walirudia hali yao ya maisha ya nyuma ya upagani.

- D. Kuwatia moyo Wafilipi waaminio ili kuwa na furaha katika mateso ya ndani na ya nje. Furaha ya Paulo haikutegemea hali lakini imani yake katika Kristo.

Furaha hii katikati ya matatizo haikuwa ni uvumilivu wa kujitoa, lakini mtazamo wa mkristo katika ulimwengu na kushindana daima. Paulo alichora sitiari kutoka maeneo kadhaa ya maisha ili kuwasilisha mvuto wa maisha ya Ukristo

1. mpiga mbio (kama vile. 3:12,14; 4:3);
2. askari (kama vile. 1:7,12,15,16,17,22,28,30);
3. biashara (kama vile. 3:7,8; 4:15,17,18).

VI. MUHTASARI WA KIMUKTADHA

- A. Ni vigumu kuelezea kitabu cha Wafilipi kwa sababu ni cha binafsi na sio rasmi. Paulo alikuwa anaongelea marafiki na watenda kazi waaminifu katika Kristo. Moyo wake ulifurika kabla ya ufahamu wake kuweza kupangilia mawazo. Katika njia za wazi za kustaaajabisha kitabu hiki kinaufunua moyo mkuu wa mtume kwa mataifa. Paulo anahisi “furaha” katika Kristo, katika kila hali yeyote na katika huduma ya injili!
- B. Vipengele vya kifasihi
1. aina ya utangulizi wa aina ya Paulo, 1:1-2
 - a. salamu
 - (1) kutoka kwa Paulo (na Timotheo) 1:1
 - (2) kwa watakatifu walioko Filipi (inahusisha wasimamizi na mashemasi), 1:1
 - (3) mtindo wa maombi wa Paulo, 1:2
 - b. maombi, 1:3-11:
 - (1) watenda kazi katika injili tokea awali, 1:5
 - (2) wasaidizi wa huduma ya Paulo. 1:7
 - (3) maombi ya Paulo kwa ajili ya:
 - (a) upendo tele, 1:9
 - (b) ufahamu tele, 1:9
 - (c) hekima tele, 1:9
 - (d) utakatifu tele, 1:10
 2. Hofu ya Paulo kwa ajili yao juu ya hofu yao kwa ajili yake, katika kifungo, 1:12-26
 - a. Mungu alitumia muda wake kifungoni kueneza injili kwa
 - (1) askari wa mfalme, 1:13
 - (2) wengine katika nyumba ya Kaisari, 1:13; 4:22
 - (3) kuwatia moyo wahubiri, 1:14-18
 - b. Matumaini ya kuachiliwa Paulo ni kwa sababu ya:
 - (1) maombi yao, 1:19
 - (2) Roho mtakatifu, 1:19
 - c. Matumaini ya Paulo kama ni katika kuachiliwa au katika kifo, 1:20-26
 3. Kutiwa moyo kwa Paulo, 1:27-2:18:
 - a. wito kwa wanao mfanana Kristo kuungana katikati ya mateso, 1:27-30
 - b. Kuishi katika maisha binafsi ya kumfanana Kristo, 2:1-4
 - c. Kristo mfano wetu, 2:5-11
 - d. katika kushi katika amani na umoja wa nuru ya mfano wa Kristo, 2:12-18
 4. Mipango ya Paulo inasimuliwa katika Filipi, 2:19-30
 - a. kutumwa kwa Timotheo, 2:19-24
 - b. kurudi kwa Epafrodito, 2:25-30
 5. kusimama thabiti juu ya waalimu wa uongo, 1:27; 4:1
 - a. mbwa, waliotahiriwa waongo, washika dini ya kiyahudi (Mdo 15, Wagalatia), 3:1-4
 - b. urithi wa Paulo wa kiyahudi:
 - (1) katika nuru ya walimu wa uongo, 3:5-6

(2) katika nuru ya Kristo, 3:7-16

c. Huzuni ya Paulo kwa ajili yao, 3:17-21

6. Paulo anarudia maonyo yake:

a. umoja, 4:1-3

b. Tabia zinazomfanana Kristo, 4:4-9

7. Paulo anarudia shukrani zake kwa ajili ya msaada wa Wafilipi

a. kipawa chao kipya, 4:10-14

b. kipawa chao cha awali, 4:15-20 (1:5)

8. sifa ya ukaribu wa tabia ya Paulo, 4:21-23

VII. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "katika kufungwa kwangu," 1:7,13

2. "upendo," 1:8

3. "siku ya Kristo," 1:10

4. "tunda la haki," 1:11

5. "askari wa hakimu," 1:13

6. "kuteswa kwa ajili yake," 1:29

7. "hana utukufu," 2:7

8. "katika mfano wa mwanadamu," 2:7

9. ukiri, 2:11

10. "sikupiga mbio bure, wala sikujitaabisha bure," 2:16

11. "nikimiminwa juu kama sadaka ya kinywaji," 2:17

12. "jihadharini na mbwa," 3:2

13. "Mwebrania wa Waebrania," 3:5

14. "ni adui za msalaba wa Kristo," 3:18

15. "wenyeji wetu uko mbinguni," 3:20

16. "ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima," 4:3

VIII. WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

1. Wasimamizi, 1:1

2. mashemasi, 1:1

3. Timotheo, 2:19

4. Epafrodito, 2:25

5. "tohara ya uongo," 3:2

6. Sintike, 4:2

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Filipi, 1:1

2. Makedonia, 4:15

3. Thesalonike, 4:16

X. MASWALI YA MJADALA

1. Ni nini fundisho la 1:6 linasisitizia?
2. Elezea Paulo alimaanisha nini katika 1:16.
3. Ni nini tungo “Roho wa Yesu Kristo” inadokeza ?
4. Elezea 1:21 kwa maneno yako mwenyewe.
5. Ni kwa namna gani 2:6 inasimulia maisha ya Roho kabla ya kuzaliwa Yesu na uungu?
6. Kwa nini Yesu alikufa kwenye msalaba? (2:8)
7. Ni wakina nani wanarejelewa “walio mbinguni, katika dunia, na chini ya dunia”?
8. Inamaanisha nini “utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka”? (2:12)
9. Orodhesha sifa za kiyahudi za Paulo katika 2:4-6.
10. Ni nini umuhimu wa 3:9?
11. Wafilipi 4:4 inasema, “Bwana yu karibu.” Ikiwa hivyo, kwa nini hajarudi?

UTANGULIZI WA WAKOLOSAI

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Tumshukuru Mungu kwa ajili ya wavumishi wa Kolosai; kwasababu yao Paulo aliandika barua hii yenye uzito mkubwa. Kumbuka kwamba kuweza kukielewa kitabu, sharti tuhusianishe na mazingira yake ya kihistoria “nyaraka za kimatukio” Kwasababu alikuwa anahutubu juu ya matatizo ya mahali pamoja kwa kweli za injili za ujumla. Uvumi huko Kolosai ulikuwa uchanganyaji usiokuwa wa kawaida wa falsafa ya Kiyunani (Gnosticism/walimu wa uongo) na dini ya kiyahudi.
- B. U-Bwana wa ulimwengu wote wa Yesu ni maudhui kuu (kama vile 1:15-17). Elimu juu ya ukuu wa Kristo ya kitabu hiki hailinganishwi! Wakolosai inatengeneza ainisho la msingi kwa Waefeso. Paulo alijua uvumi ungeenea huko Asia Ndogo. Wakolosai inashambulia mafundisho ya uongo wakati Waefeso inakuza maudhui yake kuu ili kuandaa makanisa mengine katika kuja kwa uvumi wa mafundisho ya uongo. Msisitizo wa Wakolosai ni elimu juu ya Kristo wakati msisitizo katika Waefeso ni umoja wa vitu vyote katika Kristo, aliye Bwana wa vitu vyote.
- C. Paulo anakataa sheria, zote mbili ya Kiyahudi na ya Kiyunani kwa namna ya ya nguvu kabisa (2:6-23).

II. MJI

- A. Kiasili mji wa Kolosai ulikuwa sehemu ya ufalme wa Pergamo ndani ya Firigia. Mnamo mwaka 133 K.K. ulitolewa kuwa jimbo la kiutawala kwa Rumi.
- B. Kolosai ulikuwa kituo kikubwa sana cha kibiashara kabla ya siku za Paulo (kama vile Heroditus' *Histories* VII:30 na Xenophon *Anabasis* 1:2:6).
 - 1. Bonde ambalo Kolosai ilikuwa imo lilikuwa mzalishaji aliyekuwa anaongoza katika sufi wakati wa ulimwengu wa kale, hasa sufi nyeusi na sufi ya kupakwa rangi, zambarau na nyekundu. Udongo uliotokana na volkeno ulikuwa ardhi bora zaidi kwa ajili ya malisho na maji yenye rangi yeupe yakisaidiwa na mchakato wa kutengeneza rangi (Strabo, 13:4:14).
 - 2. Milipuko na mienendo ya Volkeno (Strabo, 12:8:6) ilisababisha mji kuharibiwa mara kwa mara katika historia; mara ya karibu zaidi ikiwa ni mnamo mwaka wa 60 B.K (Tacitus) au 64 B.K (Eusebius).
- C. Kolosai ulikuwa umeenea katika Mto Lycus, mfereji wa Mto ulioenda kwa kona kona ambao ulipita Efeso, maili 100 mpaka mtoni. Katika bonde hili ulikuwepo mji wa Hierapolis (maili 6 kutokea hapo) na Laodikia (maili 10 kutoka hapo) (kama vile 1:2; 2:1; 4:13, 15-16).
- D. Baada ya Warumi kujenga njia kuu yao kubwa mashariki-Magharibi, *Via Ignatia*, ambayo ilipita Kolosai na kuishiria kabisa, (Strabo). Hii ilikuwa ni sawa na kile kilichotokea kwa Petra katika eneo la kati ya Yordani ya Palestina.
- E. Mji ulikuwa umeundwa zaidi na mataifa (Filigia na wkazi Wayunani), lakini kulikuwa na Wayahudi kadhaa pia. Josephus anatwambia sisi kwamba Antiochus III (223-187 K.K.) alisafirisha Wayahudi

2,000 kutoka Babeli mpaka Kolosai. Kumbukumbu inatuonesha kwamba mnamo mwaka 76 B.K., Wanaume wa Kiyahudi 11,000 waliishi katika mji wa Kolosai uliokuwa mji mkuu.

III. MWANDISHI

- A. Kuna watumaji wawili, Paulo na Timotheo (kama vile Kol. 1:1). Hata hivyo, mwandishi mkuu ni Paulo; Timotheo alikuwa natuma salamu zake kama mtenda kazi pamja na Paulo na yawezekana kama mwandishi wake (*amanuensus*).
- B. Fasihi ya kale haina jina kwamba Paulo Mtume alikuwa mwandishi:
1. Marcion (aliyekuja Rumi mnamo mwaka 140 B.K.), wavumishi wapingao Agano la Kale, walilijumuisha katika nyaraka zake za Paulo
 2. Kiliorodheshwa pamoja na barua za Paulo katika Kanoni ya Muratorian (Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutokea Rumi mnamo mwaka 200 B.K.)
 3. Mababa kadhaa wa kale wa kanisa wananukuu kutoka ndani yake na kumtambua Paulo kama mwandishi
 - a. Irenaeus (aliandika mnamo mwaka 177-190 B.K.)
 - b. Clement wa Iskandria (aliyeishi mnamo mwaka 160-216 B.K.)

IV. UHUSIANO WA KIFASIHI KATI YA WAKOLOSAI NA WAEFESO

- A. Uhusiano wa kihistoria kati ya Wakolosai na Waefeso
1. Epafra (Kol. 1:7; 4:12; Filemoni 23) aliongoa wakati wa kampeni ya Paulo kwa Waefeso (Mdo.19)
 - a. Alichukua imani yake mpya na kuipeleka nyumbani kwao, Bonde la Mto Lycus.
 - b. Alianzisha makanisa matatu—katika Hierapoli, Laodikia na Kolosai.
 - c. Epafra alimtafuta Paulo kwa ajili ya ushauri ni namna gani ya kukabiliana na maoni yenye mpasuko wa kiulimwengu wa wavumishi. Paulo alikuwa gerezani huko Rumi (mwanzoni mwa miaka ya 60).
 2. Walimu wa uongo walikuja na kuanza kuunganisha injili pamoja na elimu ya Kiyunani
 - a. roho na mada vilikuwa vitu vyanza vyenye umilele
 - b. roho (Mungu) alikuwa mzuri
 - c. mada (uumbaji) ulikuwa uovu
 - d. mfululizo wa miaka mingi (viwango vya malaika) ilikuwepo kati ya Mungu mkuu mwema na mungu mdogo aliyetengeneza mada
 - e. wokovu ulijikita katika maarifa ya siri ambayo yalisaidia watu kuendelea kwa miaka mingi (viwango vya kimalaika)
- B. Uhusiano wa kifasihi kati ya barua mbili za Paulo
1. Paulo alisikia habari za uvumi katika makanisa haya ambayo alikuwa hajawahi kuyatembelea yeye binafsi kutoka kwa Epafra.
 2. Paulo aliandika barua inayogusa na ngumu kwa ufupi, sentensi zilizojaa uzito, zilizokusudiwa moja kwa moja kwa walimu wa uongo. Maudhui makuu yalikuwa u-Bwana wa kiulimwengu wa Yesu. Hii inajulikana kama barua ya Paulo kwa Wakolosai.
 3. Inavyoonekana, mara baada ya kuandika Wakolosai, kwa muda katika mikono yake katika gereza, alizalisha maudhui haya. Waefeso inaundwa na tabia ya kuwa na sentensi ndefu na kukuzwa kwa dhana za kithiologia (1:3-14, 15-23; 2 :1-10, 14-18, 19-22; 3:1-12, 14-19; 4:11-16;

6:13-20). Inawachukua Wakolosai kama sehemu ya kuanzia na kutoa maana zake za kithiolojia. Maudhui yake makuu ni umoja wa vitu vyote katika Kristo ambayo inatofautishwa na dhana inayokua ya walimu wa uongo.

C. Muundo unaohusiana kifasihi na kithiolojia

1. Ufanano wa muundo wa msingi

- a. vina ufunguzi unaofanana
- b. vina sehemu za kimafundisho zinazohusiana kimsingi na Kristo
- c. vina sehemu mahususi halisi zinazoonya mtindo wa maisha kwa kutumia vipengele vinavyofanana, misamiati na tungo
- d. vina mistari ya ufungaji inayofanana kabisa kabisa katika maneno 29 yanayofuatana katika Kiyunani yakiwa na maneno mawili tofauti yanayoongezwa katika Wakolosai.

2. Ufanano wa maneno au tungo fupi

Efe. 1:1c na Kol. 1:2a	“mwaminifu”
Efe. 1:4 na Kol. 1:22	“takatifu na isiyo na mawaa”
Efe. 1:7 na Kol. 1:14	“ukombozi . . . msamaha”
Efe. 1:10 na Kol. 1:20	“vitu vyote . . . mbingu. . . nchi”
Efe 1:15 na Kol. 1:3-4	“kusikia . . . upendo kwa watakatifu wote”
Efe1:18 na Kol. 1:27	“utajiri wa utukufu”
Efe. 2:1 na Kol. 1:13	“nanyi mlikuwa mmekufa”
Efe. 2:16 na Kol. 1:20	“kupatanishwa . . . msalaba”
Efe. 3:2 na Kol. 1:25	“wakili”
Efe. 3:3 na Kol. 1:26,27	“siri”
Efe. 4:3 na Kol. 3:14	“umoja”
Efe. 4:15 na Kol. 2:19	“kichwa” na “kukua”
Efe. 4:24 na Kol. 3:10,12,14	“vaeni . . .”
Efe. 4:31 na Kol. 3:8	“hasira,” “ghadhabu,” “uongo,” “uzushi”
Efe. 5:3 na Kol. 3:5	“uchafu,” “mawazo mabaya,” “tamaa mbaya”
Efe. 5:5 na Kol. 3:5	“ibada ya sanamu” (tamaa mbaya)
Efe. 5:6 na Kol. 3:6	“ghadhabu ya Mungu”
Efe. 5:16 na Kol. 4:5	“mkiukombo wa wakati”

3. Sentensi na tungo zilizo na ufanano sawa kabisa

- Efe. 1:1a na Kol. 1:1a
- Efe. 1:1b na kol. 1:2a
- Efe. 1:2a na Kol. 1:2b
- Efe. 1:13 na Kol. 1:5
- Efe. 2:1 na kol. 2:13
- Efe. 2:5b na Kol. 2:13c
- Efe. 4:1b na Kol. 1:10a
- Efe. 6:21-22 na Kol. 4:7-8 (maneno 29 yenye mfuatano wa kufanana hasa isipokuwa kwa “*kai syndoulos*” katika Wakolosai)

4. Ufanano wa tungo au sentensi

Efe. 1:21 na Kol. 1:16
Efe. 2:1 na Kol. 1:13
Efe. 2:16 na Kol. 1:20
Efe. 3:7a na Kol. 1:23d, 25a
Efe. 3:8 na Kol. 1:27
Efe. 4:2 na Kol. 3:12
Efe. 4:29 na Kol. 3:8; 4:6
Efe. 4:32b na Kol.3:13b
Efe. 5:15 na Kol. 4:5
Efe. 5:19-20 na Kol. 3:16

5. Dhana za kithiolojia zinazofanana:

Efe. 1:3 na Kol. 1:3	maombi ya shukrani
Efe. 2:1,12 na Kol. 1:21	kutengwa mbali na Mungu
Efe. 2:15 na Kol. 2:14	uadui wa sheria
Efe. 4:1 na Kol. 1:10	kutembea sawasawa
Efe. 4:15 na Kol. 2:19	mwili wa Kristo unaokua katika ukomavu kutoka katika Kichwa
Efe. 4:19 na Kol. 3:5	mawazo mabaya ya zinaa
Efe. 4:22,31 na Kol. 3:8	“wekeni kando” dhambi
Efe. 4:32 na Kol. 3:12-13	mkikirimiana Kikristo wenyewe kwa wenyewe
Efe. 5:4 na Kol. 3:8	kauli za mkristo
Efe. 5:18 na Kol. 3:16	kujazwa na Roho = neno la Kristo
Efe. 5:20 na Kol. 3:17	Mkimshukuru Mungu kwa mambo yote
Efe. 5:22 na Kol. 3:18	wake watiini waume zenu
Efe. 5:25 na Kol. 3:19	waume wapendeni wake zenu
Efe. 6:1 na Kol. 3:20	watoto watiini wazazi wenu
Efe. 6:4 na Kol. 3:21	baba msiwachokoze watoto
Efe. 6:5 na Kol. 3:22	watumwa watiini bwana zenu
Efe. 6:9 na Kol. 4:1	bwana na watumwa
Efe. 6:18 na Kol. 4:2-4	ombi la Paulo kwa ajili ya Maombi

6. Maneno yaliyotumika katika vyote Wakolosai na Waefeso yanapatikana katika fasihi nyingine za Paulo

a. “ukamilifu”

Efe. 1:23 “ukamilifu katika yeye atujazaye yote katika yote”
Efe. 3:19 “mjazwe kwa wote kwa ukamilifu wa Mungu”
Efe. 4:13 “mpaka ukamilifu wa Kristo”
Kol. 1:19 “kwa maana ukamilifu wote unakaa ndani Yake”
Kol. 2:9 “kwa maana ndani Yake ukamilifu wote wa Mungu wakaa”

b. Kristo kama “kichwa” cha kanisa

Efe. 4:15, 5:23 na Kol. 1:18;2:19

c. “kutengwa”

Efe. 2:12; 4:18 na Kol. 1:21

d. “mkiukomboa wakati”

- Efe. 5:16 na Kol. 4:5
- e. “mmepandwa”
Efe. 3:17 na Kol. 2:7
- f. “neni la kweli, injili”
Efe. 1:13 na Kol. 1:5
- g. “mkizaa”
Efe. 4:2 na Kol. 3:13
- h. utungwaji usiokuwa wa kawaida na maneno (“kushikanishwa pamoja,” “atawajazeni”)
Efe. 4:16 na Kol. 2:19

D. Muhtasari

1. Zaidi ya moja ya tatu ya maneno katika Wakolosai yako katika Waefeso,. Imekadiriwa kwamba mistari 75 kati ya 155 katika Waefeso inafanana na Wakolosai. Vyote viwili vinadai kuandikwa na Paulo akiwa gerezani.
2. Vyote vilipelekwa na rafiki wa Paulo aitwaye Tikiko.
3. Vyote vilitumwa kwa eneo moja (Asia Ndogo).
4. Vyote vilizungumzia mada ya Kristo.
5. Vyote husisitiza Kristo kama kichwa cha kanisa.
6. Vyote husisitiza maisha ya mwenendo sahihi wa Mkristo.

E. Hoja Kubwa za Kutofanana

1. Kanisa siku zote lilikuwa la eneo la mahali huko kwa Wakolosai lakini kwa wote mpaka huko kwa Waefeso. Hii inaweza kuwa kwa sababu ya asili ya barua ya kuwa iliandikwa kwa ajili ya wote ya Waefeso.
2. Uvumi ambao ulikuwa tabia kubwa ya Wakolosai, hautajwi moja kwa moja katika Waefeso. However, hata hivyo, barua zote mbili zinatumia maneno yenye tabia ya walimu wa uongo (“hekima,” “maarifa,” “ukamilifu,” “siri,” “mamlaka na nguvu” na “wakili.”)
3. Kuja kwa mara ya pili ni kwa mara katika Wakolosai lakini kunachelewa katika Waefeso. Kanisa lilikuwa na linatakiwa kuhudumu katika ulimwengu ulioanguka. (2:7; 3:21; 4:13).
4. Maneno kadhaa yenye tabia za uandishi wa Paulo yanatumia tofauti tofauti. Moja ya mfano ni neno “siri.” Katika Wakolosai siri ni Kristo (Kol. 1:26-27; 2:2; 4:3), lakini katika Waefeso (1:9; 5:32) lilifichwa hapo mwanzo na Mungu lakini sasa linafunuliwa, mpango kwa ajili ya umoja wa Mataifa na Wayahudi.
5. Waefeso ina maelezo kadhaa ya Agano la Kale (1:22—Zab. 8; 2:17—Isa. 57:19) (2:20—Zab. 118:22) (4:8—Zab. 68:18) (4:26—Zab. 4:4) (5:15—Isa. 26:19, 51:17, 52:1, 60:1) (5:3—Mwa. 3:24) (6:2—3-Kut. 20:12) (6:14—Isa. 11:5, 59:17) (6:15—Isa. 52:7), lakini liko moja tu au mawili (2:3—Isa. 11:2) au (2:22—Isa. 29:13).

F. Ingawa ni maneno yanayofanana, tungo na mara kwa mara uainishi, barua pia inajumuisha kweli za kipekee.

1. Baraka za utatu za neema - Efe. 1:3-14
2. Kifungu cha neema - Efe. 2:1-10
3. Kuunganishwa kwa Wayahudi na Mataifa katika mwili mmoja - Efe. 2:11-3:13
4. Umoja na karama za mwili wa Kristo - Efe. 4:1-16
5. “Kristo na kanisa” ni mfano wa “mume na mke” Efe. 5:22-33

6. Kifungu cha vita vya kiroho - Efe. 6:10-18
7. Kifungu cha elimu juu ya upekee wa Kristo - Kol. 1:13-18
8. Taratibu za kidini za kibinadamu na sheria - Kol. 2:16-23
9. Mada ya umuhimu wa kiulimwengu ya Kristo katika Kolosai dhidi maudhui ya umoja wa vitu vyote katika Kristo katika Waefeso

G. Katika hitimisho, inaonekana kuwa bora kufuata A. T. Robertson na F. F. Bruce katika kuelezea kwamba Paulo aliandika vitabu vyote kwa ukaribiano kwa kukuza fikra za Wakolosai katika muhuri uwasilishaji wa kweli.

V. TAREHE

- A. Tarehe ya barua hii ya Wakolosai inaunganishwa na kifungo cha Paulo huko Efeso, Filipi, Kaisaria au Rumi. Kifungo cha Kirumi kinashabihiana bora zaidi na kweli za Matendo ya Mitume.
- B. Wakati Rumi inachukuliwa kuwa sehemu ya kifungo zaidi, swali linakuja, wakati gani? Paulo alikuwa jela mnamo miaka ya mwanzoni mwa miaka ya 60, ambayo inaandikwa katika Matendo ya Mitume lakini aliachiwa na kuandika nyaraka za Kichungaji (1 & 2 Timotheo na Tito) na baadaye alikamatwa tena na kuuawa kabla ya Juni 9, mnamo mwaka 68 B.K., (tarehe ya kujiuwa kwa Nero), yawezekana mnamo mwaka 67 B.K.
- C. Dhanio la kisomi bora zaidi kwa kuandikwa kwa Wakolosai (Waefeso na Filemoni) ni kufungwa kwa mara ya kwanza kwa Paulo huko Rumi mnamo mwanzoni mwa miaka ya 60 (Wafilipi ilikuwa barua ya mwisho kuandikwa akiwa gerezeni, yawezekana iliandikwa kuelekea kati kati ya miaka ya 60).
- D. Tikiko pamoja na Onesmo, yawezekana walichukua barua za Wakolosai, Waefeso na Filemoni mpaka Asia Ndogo. Baadae yawezekana miaka kadhaa, Epafrodito, alipona ugonjwa wake na kuichukua barua ya Wafilipi kwenda kwenye kanisa lake la nyumbani)
- E. Mfuatano wa maandiko ya Paulo kwa mujibu wa F. F. Bruce na Murry Harris pamoja na marekebisho madogo.

<u>Kitabu</u>	<u>Tarehe</u>	<u>Mahali pa kuandikwa</u>	<u>Uhusiano na Mdo.</u>
8. Wagalatia	48 (nadharia ya kusini)	Antiokia ya Shamu	14:28; 15:2
9. 1 Thesalonike	50	Korintho	18:5
10. 2 Thesalonike	50	Korintho	
11. 1 Thesalonike	55	Efeso	19:20
12. 2 Thesalonike	56	Makedonia	20:2
13. Warumi	57	Korintho	20:3
14. - 10.			
Wakolosai	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	
Waefeso	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	28:30-31
Filemoni	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	
Wafilipi	mwishoni mwa 61-62 (gereza)	Rumi	
14. 1 Timotheo	63 (au baadaye, lakini	Makedonia	
15. Tito	63 kabla	Efeso (?)	

VI. WAPOKEAJI NA TUKIO

- A. Inavyoonekana kanisa lilianzishwa na Epafra (kama vile 1:7,8; 2:1; 4:12-13), ambaye inawezekana aliongoka huko Efeso kwa mahubiri ya Paulo (kama vile Kol. 1:7-8 na linganisha 2:1). Ilikuwa linaundwa kwa sehemu kubwa zaidi na Mataifa (kama vile 1:21; 3:7). Epafra alimuijia Paulo akiwa gerezani kutoa taarifa ya tatizo la walimu wa uongo waliofundisha mchanganyiko wa Ukristo na Falsafa ya Kiyunani iitwayo gnosticism (2:8) na sheria za kiyahudi (kama vile vipengele vya kiyahudi, 2:11, 16, 17: 3:11; kuabudu malaika, 1:16; 2:15, 18 ushikaji wa sheria ya matendo ya mwili uliopitiliza 2:20-23). Kulikuwa na jamii pana na kubwa ya Wayahudi huko Kolosai ambayo ilikuwa tayari imekwisha kuwa wafuasi wa desturi za Kiyunani. Uzuri tatizo lilijikita kwa mtu na kazi ya Kristo. Walimu wa uongo hawa walikataa kwamba Yesu alikuwa mwanadamu kamili lakini walikiri kwamba alikuwa Mungu kamili kwasababu ya uadui wao wa upinzani wa umilele wa nadharia ya u-pili ya maada na roho. Walikiri Uungu wake lakini walikana ubinadamu wake. Pia walikataa kazi yake ya upatanishi wa milele. Kwao, kulikuwa na viwango vingi vya kimalaika (*eons*) kati ya mungu mkuu mwema na mwanadamu; Yesu, japo ndiye mkuu kuliko wote, alikuwa mmojawapo wa miungu. Pia walikuwa wenye kufuata mantiki za kiakili pekee wakibagua (kama vile 3:11, 14, 16, 17) na kusisitiza maarifa ya siri maalumu (kama vile 2:15, 18, 19) kama njia ya kumfikia Mungu badala ya upatanisho wa Yesu na sadaka yake aliyoitoa badala ya wengine na mwikio wa toba wa imani ya mwanadamu.
- B. Kwasababu ya hali hii ya kithiolojia na kifalsafa, kitabu cha Wakolosai kinasisitiza
1. Upekee wa nafsi ya Kristo na kazi Yake iliyokwisha malizika ya wokovu.
 2. Umiliki wa ki-ulimwengu, utawala na umuhimu wa Yesu wa Nazareti - Kuzaliwa kwake, mafundisho yake, ufufuo wake na kupaa kwake! Yeye ni Bwana wa Yote!

VII. KUSUDI

Kusudi la Paulo lilikuwa kukanusha uvumishi wa mafundisho ya Wakolosai. Kufanikisha hili lengo, alimuinua Kristo kama sura halisi ya Mungu (1:15), Muumbaji (1:16), aliyekuwepo toka mwanzo wa vyote na mtoshelezaji wa vitu vyote (1:17), kichwa cha kanisa (1:18), aliyekuwa wa kwanza kufufuka (1:18), ukamilifu wa Mungu katika namna ya mwili (1:19, 2:9) na mpatanishi (1:20-22). Hivyo Kristo alikamilishwa kwa utoshelevu wote. Waamini “wamekamilishwa katika Kristo” (2:10). Uvumi wa Wakolosai haukuwa kamili kithiolojia kuwezesha upatikanaji wa wokovu wa kiroho. Ilikuwa ni falsafa ya uongo na tupu (2:8), ikosayo uwezo wowote wa kujizuia na asili ya zamani ya dhambi (2:23).

Maudhui yanayojirudia rudia katika Wakolosai ni utoshelevu kamili wa Kristo kama inavyotofautishwa na falsafa tupu ya kibinadamu tu. Utoshelevu huu unaelezwa katika U-Bwana wa ulimwengu wote wa Yesu. Yeye ndiye mmiliki, muumbaji na mtawala juu ya vitu vyote, vinavyoonekana na visivyonekana (kama vile 1:15-18).

VIII. UANISHO

- A. Ufunguzi wa kijadi wa aina ya Paulo
1. utambulisho pamoja na mtumaji, 1:1
 2. Utambulisho pamoja na wapokeaji, 1:2a
 3. Salamu, 1:2b
- B. Ukuu wa Kristo (Mada 1-10 ikichukuliwa kutoka uainisho wa aya ya toleo la NKJV)

1. Imani katika Kristo, 1:3-8
2. Ukuu na kudumu kwa Kristo, 1:9-18
3. Upatanishi katika Kristo, 1:19-23
4. huduma ya sadaka kwa Kristo, 1:24-29
5. Sio Falsafa, bali Kristo, 2:1-10
6. Sio sheria, bali katika Kristo, 2:11-23
7. Sio mwili bali katika Kristo, 3:1-11
8. Mvaeni Kristo, 3:12-17
9. Mwacheni Kristo atawale nyumba zenu, 3:19-4:1
10. Mwacheni Kristo kuathiri maisha yako ya kila siku, 4:2-6

C. wajumbe wa Paulo 4:7-9

D. marafiki wa Paulo wanatuma salamu, 4:10-14

E. Paulo anatuma salamu, 4:15-17

F. Ufungaji wa Paulo kwa mkono wake mwenyewe, 4:18

IX. NADHARIA YA WALIMU WA UONGO

A. Maarifa mengi zaidi yetu ya uvumi huu yanatoka kwa maandiko ya walimu wa uongo wa karne ya pili. Hata hivyo mawazo yanayokua yalikuwepo katika karne ya kwanza, (Magombo ya Bahari ya Chumvi).

B. Tatizo la Kolosai lilikuwa ni ucho tara wa Ukristo, nadharia ya walimu wa uongo inayokua na Dini ya Kiyahudi ya kisheria.

C. Baadhi walitaja nguzo za nadharia za walimu wa uongo za ki-Valentini na ki-Cerinthi wa karne ya pili

1. Maada na roho vilikuwa vya milele vilivyokuwepo kwa pamoja (nadharia ya upili katika elimu juu ya vitu vya asili). Maada ni ovu, roho ni njema. Mungu ambaye ni roho hawezi kuhusika moja kwa moja katika kutengeneza maada ovu.
2. Kuna mazalia (kwa miaka mingi au viwango vya malaika) kati ya Mungu na maada. Ya mwisho au ya chini zaidi ilikuwa YHWH wa Agano la Kale aliyeumba ulimwengu (*kosmos*).
3. Yesu alikuwa ni mazalia kama YHWH lakini mkubwa katika vipimo, karibia na Mungu wa kweli. Baadhi wanamweka kama mkuu kuliko wote japo ni mdogo kwa Mungu na hakika si Mungu mwenye mwili, (kama vile Yohana 1:14).
Kwa kuwa maada ni ovu, Yesu asingeweza kuchukua mwili wa binadamu na bado akahesabika kuwa Mungu. Alionekana tu mwanadamu, japo alikuwa kweli roho (kama vile I Yohana 1:1-3; 4:1-6).
4. Wokovu ulipatikana kwa imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu ambayo yanajulikana tu na watu maalumu. Maarifa (siri) yalihatijika kupita katika anga la kimbangu. Nadharia ya sheria ya Kiyahudi ilikuwa pia inahitajika kumfikia Mungu.

D. Walimu wa uongo wenye ujuzi walishikilia mifumo miwili inayokinzana kimaadili:

1. Kwa baadhi, mtindo wa maisha ulikuwa hauhusiani kabisa na wokovu. Kwao, wokovu na hali ya kiroho vilikuwa ndani ya maarifa ya siri (siri zisizojulikana kirahisi) kupita anga la kimalaika (*eons*).
2. Kwa wengine, mtindo wa maisha ulikuwa muhimu kwa ajili ya wokovu. Katika kitabu hiki walimu wa uongo walisisitiza mtindo wa maisha ya kushika matendo ya mwili kama ushahidi wa kuwa rohoni (kama vile 2:16-23).

E. Kitabu kizuri cha rejea ni *The Gnostic Religion* cha Hans Jonas, kilichochapishwa na Beacon Press.

X. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "tumaini mlilowekewa kwa ajili yenu mbinguni," 1:5
2. injili, 1:5
3. "anga la giza," 1:13
4. ukombozi, 1:14
5. "Mungu asiyeonekana," 1:15
6. "ukamilifu wote wakaa ndani yake," 1:19
7. "akiishafanya amani kwa kupitia damu ya msalaba wake," 1:20
8. "katika kujazwa kile kinachopungua katika mateso ya mkristo," 1:24
9. "desturi za wanadamu," 2:8
10. "mafundisho ya mwanzo ya ulimwengu," 2:8,20
11. "kuzikwa pamoja naye katika ubatizo," 2:12
12. "nanyi mlikuwa mmekufa katika makosa yenu," 2:13
13. "akiifuta ile hati ya mashitaka," 2:14
14. "uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu," 3:3
15. mshenzi, 3:11
16. "barua yangu ambayo inakuja kutokea Laodikia," 4:16

XI. WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. Epafra, 1:7; 4:12
2. "mzaliwa wa kwanza wa uumbaji wote" 1:15
3. "enzi au mamlaka au watawala au nguvu," 1:16
4. mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, 1:18
5. Muungwana, 3:11
6. Tikiko, 4:7
7. Onesmo, 4:9
8. Marko, 4:10
9. Luka, 4:14
10. Dema, 4:14

XII. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Kolosai, 1:2
2. Laodikia, 2:1
3. Hierapoli, 4:13

XIII. MASWALI YA MJADALA

1. Kwanini Paulo anazungumzia sana kuhusu maarifa na hekima? (1:9)
2. Nini onyo la 1:23 linamaanisha?
3. Ni nini siri ya Mungu iliyofichwa mbali na vizazi vilivyopita? (1:27)
4. Je Paulo hakujua watu wa kanisa hili? (2:1)
5. Namna gani mtu anawachukua mateka kwa Falsafa? (2:8)
6. Mafundisho gani mstari wa 2:9 unasisitiza?
7. Elezea historia ya nyuma ya Kirumi 2:15.
8. Ni kwa nani mstari wa 2:16-17 unarejerea?
9. Ni kwa namna gani mstari wa 2:14-23 unazungumzia sheria?
10. Kwanini dhambi ya 3:5 ni sawasawa na ibada ya sanamu?
11. Ni kwa namna gani Kol. 3:11 inahusiana na Gal. 3:28?
12. Ni kwa namna gani 3:16 inahusiana na Efe. 5:18?
13. Nini kanuni ya kiroho ya 3:23?
14. Elezea kwa maneno yako mwenyewe maneno ya mstari wa 4:6.
15. Kwanini Paulo aliandika hitimisho la barua zake zote? (4:18)

UTANGULIZI WA BARUA ZA WATHESALONIKE

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Maelezo ya Kimuhtasari

1. Barua za Thesalonike zinatupa undani wa kushangaza juu ya Paulo kama mwenye pande zote mbili yaani mmisionari na mchungaji. Tunamuona huyu akiliimarisha kanisa kwa muda mfupi na kuendelea kuomba na kushughulika na ukuaji wake, maendeleo yake, na huduma yake.
2. Tunamuona akihubiri injili kwa uaminifu, akishughulika na waamini wapya, anawakaripia, anawasifu, anawaongoza, anawasihi, anawafundisha, anawapenda, hata kujitolea kwa ajili yao. Aliwasisimua kwa wakati huu, lakini alikatishwa tamaa kadri walivyoendelea kukua.
3. Katika nyaraka hizi tunakutana na ushawishi, mtumishi wa Kristo mwenye upendo, mwenye shauku, lakini mwenye kulikuza kanisa jipya. Wote walikuwa waaminifu, wote walitumiwa na Mungu, na wote walihudumiana katika tabia ya Mungu jambo ambalo lilikuwa nadra sana miongoni mwa watu wa Mungu.

B. Mji wa Thesalonike

1. Historia fupi ya Thesalonike

- a. Mji wa Thesalonike ulikuwa juu ya Ghuba ya Thermai. Thesalonike ulikuwa mji wa pwani katika barabara kuu ya Rumi, Kupitia Ignatia (njia ya kuyaelekea mataifa), kuelekea upande wa kusini kutoka Rumi. Bandari, pia ulikuwa karibu sana na eneo la watu matajiri, eneo lililozungukwa na maji safi, uwanda wa pwani. Faida hizi tatu ziliufanya mji wa Thesalonike kuwa mkubwa sana, eneo muhimu sana kibiashara na kisiasa ndani ya Makedonia.
- b. Mji wa Thesalonike kiuhalisia uliitwa Therma, kutokana na majira ya joto ndani ya eneo hilo. Mwanahistoria wa kale, Pliny aliyemzee, anairejelea mji ya Therma na Thesalonike iliyo karibu karibu. Ikiwa hii ndiyo sababu, basi Thesalonike ilikuwa imezunguka mji wa Therma na iliuteka (Leon Morris, *The First and Second Epistles to the Thessalonians*, Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1991, uk. 11). Bado wanahistoria wanamwamini Cassander, mmoja wa jenerali wa Iskanda Mkuu, aliyeuita jina tena mji wa Therma mnamo mwaka 315 B.K. baada ya Filipi binti wa Makedonia na dada wa kambo na mke wake Iskanda, Thesalonike (Strabo VII Fragment 21). Wakati mwingine zamani za karne za kuueneza Ukristo, Thesalonika ilikuja kuitwa jina la utani "mji wa msingi wa imani" kwa sababu ya tabia yake ya Kikristo (Dean Farrar, *The Life and Work of St. Paul*, New York: Cassell and Company, Limited, 1904, uk. 364). Kwa sasa wa mji wa Thesalonike unajulikana kama Salonike bado ni mji muhimu sana katika Uyunani.
- c. Mji wa Thesalonike ulikuwa wa makutano ya kiulimwengu sawa na mji wa Korintho, uliokaliwa na watu kutoka ulimwenguni kote.
 - (1) Watu wa Kijerumani waliokuwa wakatili kutoka kaskazini walikuwa wakiishi hapa, wakiendesha dini za kipagani pamoja na tamaduni zao.
 - (2) Wayunani nao walikuwa wakiishi hapa, kutoka Akaya hadi kusini na kutoka visiwa vya Bahari ya Aegean, katika kuurudisha uhalisia wao na falsafa yao.
 - (3) Warumi kutoka magharibi pia waliishi hapa. Hasa hawa walikuwa askari waliostaafu na waliziimarisha nguvu zao, mali pamoja na nguvu za kisiasa.

(4) Mwisho, Wayahudi walikuja eneo hili kwa idadi kubwa sana kutoka mashariki; hatimaye robo tatu ya idadi kubwa ya watu ilikuwa ya Kiyahudi. Hawa walifundishwa imani ya mwenendo wa imani ya Mungu mmoja na taratibu za kitaifa.

- d. Mji wa Thesalonike, wenye idadi ya watu wapatao 200,000, kiukweli ulikuwa mji wa makutano ya kiulimwengu. Hiki kilikuwa kituo cha makimbilio na cha kiafya kwa sababu ya majira yake ya joto. Hiki kilikuwa kituo cha kibiashara kwa sababu ya bandari yake, uoto wenye rutuba na ukaribu wa Njia ya kuelekea Ignatia.
- e. Kama makazi na mji mkubwa sana, Thesalonike pia ilikuwa kituo kikuu cha makao makuu ya kisiasa ya Makedonia. Kuwa jimbo la makazi ya Kirumi na mahali pa kuishi raia wengi wa Kirumi (wanajeshi wengi waliostaafu), mji huu ulikuwa huru. Thesalonike ililipa ushuru na ilikuwa ikitawaliwa na sheria ya Kirumi, kwa kuwa Wathesalonike wengi walikuwa raia wa Kirumi. Ndiyo maana watawala wa Kithesalonike waliitwa “kamati kuu ya chama.” Jina hili halijitokezi mahali po pote katika fasihi bali limetunzwa kwa maandiko yenye kuhusiana na maadhimisho ya ukuu huko Thesalonike kama Lango la Vardar (Farrar, uk. 371n.).

2. Matukio Yaliyompelekea Paulo kwenda huko Thesalonike

- a. Matukio mengi yaliyompelekea Paulo kwenda Thesalonike, pamoja na mambo mengine yote yanayoonekana kuwa ya moja kwa moja, wito wa Mungu ulio wazi. Hapo awali Paulo hakupanga kuingia barani Ulaya. Bali shauku yake juu ya ziara yake ya kimisheni ilikuwa ni kuyatembelea makanisa kwa mara nyingine tena na kisha kuyatembelea tena makanisa yaliyoko Asia Ndogo ambayo aliyaimarisha katika safari yake ya kwanza na kisha kurudi upande wa kaskazini. Bado, wakati ulipotimia kurudi upande wa kaskazini, Mungu alianza kufunga milango. Hatima ya hili yalikuwa maono ya Paulo huko Makedonia (kama vile Matendo 16:6-10). Hili lilisababisha mambo mawili kutokea: la kwanza, bara la Ulaya liliinjilishwa na la pili, Paulo, kwa sababu ya hali iliyokuwa humo Makedonia, alianza kuziandika nyaraka Zake (Thomas Carter, *Life and Letters of Paul*, Nashville: Cokesbury Press, 1921, uk. 112)
- b. Baada ya kuutazama uelekeo wa kiroho, hali za kiroho zilizompelekea Paulo kwenda Thesalonike zilikuwa:
 - (1) Paulo alikwenda Filipi, mji mdogo pamoja na sinagogi. Kazi yake iliyofanyika mahali pale ilipingwa na wamiliki wa kinabii, msichana mtumwa aliyemilikiwa na pepo na halmashauri ya mji. Paulo alipigwa na kuteswa na bado kanisa liliendelea kukua hata ndani ya haya yote. Kwa sababu ya upinzani na adhabu ya kimwili, Paulo alilazimishwa kuondoka, huenda haraka kuliko alivyohitaji.
 - (2) Je! angekwenda wapi baada ya kutoka mahali pale? Huyu angepitia Amphipolis na Apolonia mahali ambapo pia hapakuwa na sinagogi,
 - (3) Huyu alikuja katika mji huu mkuu sana ulio ndani ya eneo hili, Thesalonike, ambayo pia haikuwa na sinagogi. Kwa mara ya kwanza Paulo alijipanga tayari kwenda kwa Wayahudi wenyeji. Huyu alilifanya hili kwa sababu
 - (a) ya maarifa ya Agano la Kale;
 - (b) ya fursa ya kufundisha na kuhubiri katika sinagogi hilo lililowakilishwa;
 - (c) nafasi yao kama watu waliochaguliwa, Watu wa agano (kama vile Mt. 10:6; 15:24; Rum. 1:16-17; 9-11);

(d) Yesu alijitoka kwa ajili yao kwanza, kisha ulimwengu—hivyo hivyo, Paulo angefuatisha mfano wa Kristo.

3. Marafiki wa Paulo

a. Paulo aliambatana na Sila na Timotheo humo Thesalonike. Luka alikuwa pamoja na Paulo huko Filipi na alibaki pale pale. Tunajifunza kuhusu hili kupitia vifungu “sisi” na “wale” vya Matendo 16 na 17. Luka anazungumzia “sisi” huko Filipi, lakini kuhusu “wao” kadri alivyosafiri kwenda Thesalonike.

b. Sila, au Silvano, ni mtu aliyechaguliwa na Paulo kutembea pamoja naye katika ziara yake ya pili ya kimisheni baada ya Barnaba na Yohana Marko kurudi Kipro:

(1) Huyu anatajwa kwa mara ya kwanza ndani ya Biblia katika Matendo 15:22 ambapo anaitwa mtu mkubwa miongoni mwa ndugu wa Kanisa la Yerusalemu.

(2) Huyu pia alikuwa nabii (kama vile Matendo 15:32).

(3) Huyu alikuwa raia wa Kirumi kama Paulo (kama vile Matendo 16:37).

(4) Huyu na Yuda Barsaba walitumwa na Kanisa la Yerusalemu kwenda Antiokia kwa ajili kuikagua hali ya pale (kama vile Matendo 15:22,30-35).

(5) Paulo anamsifu katika II Kor. 1:19 na anamtaja katika barua kadhaa.

(6) Baadaye alitambulishwa na Petro katika maandiko ya I Petro (katika I Pet. 5:12).

(7) Wote Paulo na Petro walimwita Silvano ambapo Luka anamuita Sila.

c. Timotheo pia alikuwa rafiki na mtendakazi mwenza wa Paulo:

(1) Paulo alikutana naye huko Listra mahali ambapo aliongoa katika safari yake ya kwanza ya umisheni.

(2) Timotheo alikuwa nusu Myunani (baba) na nusu Myahudi (mama). Paulo alitaka kumtumia kwa ajili ya kutenda kazi pamoja na Mataifa.

(3) Paulo alimtahiri ili aweze kutenda kazi pamoja na watu wa Kiyahudi.

(4) Timotheo anatajwa katika salamu katika: II Wakorintho, Wakolosai, I na II Wathesalonike na Filimoni.

(5) Paulo anamzungumzia kama “mwanangu hasa katika imani” (kama vile I Tim. 1:2; II Tim. 1:2; Tit. 1:4). Mtazamo wa jumla wa Paulo katika barua zake zilizo nyingi ulimaanisha kuwa Timotheo alikuwa kijana na mwenye haya.

(6) Paulo alikuwa na ujasiri na tumaini kubwa katika yeye (kama vile Matendo 19:27; I Kor. 4:17; Flp. 2:19).

d. Ni mapigano pekee katika kipengele hiki kuhusu marafiki wa Paulo wanaotajwa hawa wanaundwa na watu waliokuja kutoka Thesalonike na kutembea na Paulo kuhusiana na barua yake ya umisheni. Hawa ni Aristariko (Matendo 19:29; 20:4; 27:2) na Sekundo (Matendo 20:4). Pia, Dema angekuwa ametoka Thesalonike (Filimoni. 24; II Tim. 4:10).

4. Huduma ya Paulo ndani ya Mji

a. Huduma ya Paulo humo Thesalonike ilifuatisha uelekeo wake wa kawaida ya kiroho kwenda kwa Wayahudi kwanza na kisha kurudi kwa Mataifa. Paulo alihubiri majuma matatu ya Sabato ndani ya sinagogi. Ujumbe wake ulikuwa “Yesu ndiye Masihi.” Huyu aliyatumia Maandiko ya Agano la Kale ili kuonyesha kwamba Masihi ilimpasa kuwa Masihi ateswaye (kama vile Mwa. 3:15; Isa. 53), na si Masihi wa mlolongo wa kisiasa. Pia Paulo alisisitiza juu ya ufufuo na wokovu wa kujitolea kwa

- wote. Kwa uwazi kabisa Yesu aliwasilishwa kama Masihi aliyehaidiwa nyakati za kale ambaye angewaokoa watu wote.
- b. Mwitikio wa ujumbe huu ulikuwa kwamba baadhi ya Wayahudi, wengi waliwanyenyekea watu wa Mataifa, na wanawake wengi walimkubali Yesu kama Mwokozi na Bwana. Uchanganuzi wa makundi haya yaliyoongoka ulikuwa wa maana sana katika kuielewa barua ya Paulo kwa kanisa hili.
 - c. Watu wa mataifa waliokuwa ndani ya kanisa, walioonekana kutoyagusia madokezo ya Agano la Kale aidha katika nyaraka hizi mbili. Watu wa Mataifa walikuwa wamekwisha kumkubali Yesu kama Mwokozi na Bwana kwa sababu kadhaa:
 - (1) Dini zao za jadi zilikuwa na nguvu ndogo ya ushirikina. Thesalonike ilikuwa hatua chache toka Mt. Olympus na wote walijua kuwa vipimo vyake havikuwa sawa.
 - (2) Injili ilikuwa huru kwa wote.
 - (3) Ukristo ulihusisha kujitenga kwa utaifa wa Kiyahudi. Dini ya Kiyahudi iliwavutia wengi kwa sababu ya imani ya kumwabudu Mungu mmoja na mwenendo katika kiwango cha juu, lakini pia ilifukuza wengi kwa sababu ya sherehe zake haramu (kama tohara), na urithi wake wa kibaguzi na taratibu za kitaifa.
 - d. Idadi ya “wanawake wakuu” iliukubali Ukristo, kwa sababu ya uwezo wa wanawake hawa kufanya chaguzi za kuingia dini zao wenyewe. Wanawake walikuwa huru sana humo Makedonia na Asia Ndogo kuliko katika ulimwengu wa Uyunani ya Kirumi (Sir Wm. M. Ramsay, *St. Paul the Traveller and Roman Citizen*, New York: G. P. Putnam’s Sons, 1896, uk. 227). Daraja la wanawake wahitaji, japo walikuwa huru, bado walikuwa chini ya mamlaka ya ushirikina na miungu (Ramsay, uk. 229).
 - e. Wengi wamegundua matatizo katika urefu wa wakati ambao Paulo aliutumia kukaa huko Thesalonike:
 - (1) Matendo 17:2 inazungumzia umakini na uchanganuzi wa Paulo ndani ya sinagogi kwa maandiko ya Sabato tatu wakati alipokuwa Thesalonike.
 - (2) I The. 2:7-11 inazungumzia Paulo kwendelea na kazi zake. Hii ilikuwa kazi ya kutengeneza mahema au kama wengine walivyopendelea kutengeneza ngozi.
 - (3) Flp. 4:16 inayaunga mkono makazi ya muda mrefu, wakati Paulo alipopokea fedha mara mbili kutoka kanisa la Wafilipi wakati alipokuwa Thesalonike. Umbali uliopo kati ya hii miji miwili ni maili zipatazo 100. Wengine wanapendekeza kwamba Paulo alikaa miezi miwili au mitatu na ya kwamba Sabato tatu zinairejelea huduma kwa Wayahudi (Shepard, uk. 165).
 - (4) Kutofautiana na kwa maelezo ya wale walioongoka walio katika Matendo 17:4 na I Thes. 1:9 na 2:4 kunauunga mkono mtazamo huu, kiini cha tofauti hii iliyo katika maelezo haya ni kukataliwa kwa ibada za sanamu katika Mataifa. Mataifa yaliyo katika Matendo walikuwa Wayahudi waliobadili dini na waliokuwa tayari kugeuka kutoka katika ibada za sanamu. Muktaadha huu unamaanisha kuwa Paulo alikuwa na huduma kubwa sana katikati ya Mataifa ya kipagani kuliko Wayahudi.
 - (5) Kipindi cha lini huduma ingekuwa imetokea hakijulikani kwa sababu mara nyingi Paulo alikwenda kwa Wayahudi kwanza. Baada ya wao kuukataa ujumbe wake, aliyageukia Mataifa. Hawa walipoiitikia injili kwa wingi, Wayahudi waliona wivu (ambapo ilikuwa moja ya mbinu ya huduma ya Paulo, kama vile Rum. 9-11) na kuanzisha machafuko katikati ya umati wa mji.
 - f. Kwa sababu ya machafuko Paulo aliondoka nyumbani mwa Yasoni na kujificha pamoja na Timotheo na Sila au kwa namna fulani hawakuwepo wakati umati ulipomkamata akiwa nyumbani mwa Yasoni alipokuwa akiwaangalia. Baraza la watunga sheria lilimfanya Yasoni kuweka ulinzi ili kuhakikisha usalama. Hili lilimsababisha Paulo kuondoka ndani ya mji usiku wa manane na kwenda

huko Beroya. Bado, kanisa liliendelea kushuhudia juu ya Kristo katika kukabiliana na upinzani mrefu.

II. MWANDISHI

A. I Wathesalonike. Ni wakosoaji wa sasa pekee waliochangaa uandishi na upekee wa Paulo katika kuiandika I The, lakini hitimisho zao hazikuwashawishi wanazuoni wengi. I The. Inahitimishwa katika sheria ya Marcion (140 B.K) na katika Muratorian Fragment (200 B.K). Wote waliviorodhesha vitabu vya Agano Jipya vilivyoenea humo Rumi. Irenaeus anainukuu I Thess. Kwa jina—aliandika mnamo mwaka 180 B.K.

B. II Wathesalonike.

1. Kitabu cha II The. Mara nyingi kimekuwa hakikubaliki kama chenye tabia za Paulo ambavyo amekuwa akishambulia katika maeneo kadhaa:
 - a. Msamiati ulituliza tatizo moja. Ndani ya barua kulikuwa na maneno mengi ambayo hayapatikani ndani ya barua zingine.
 - b. “Mtindo huu umechangamana na wakati mwingine ni wa kiuchunguzi” (Heard, uk. 186).
 - c. Matukio ya siku za mwisho yanayohusiana na barua hizi kwa namna ya kudhani hayatabiriki.
 - d. II The. Imebeba mtazamo wa upekee wa mpinga-Kristo ulio katika Agano Jipya, hivyo, wengine walihitimisha kwamba Paulo asingekuwa mwandishi.
2. Uhalisia wa II The. Unajikuta katika vigezo kadhaa:
 - a. Polycarp, Ignatius, na Justin waliutambua huu;
 - b. Sheria ya Marcionite iliuhusisha huu;
 - c. Muratorian Fragment ilihusisha huu;
 - d. Irenaeus aliunukuu kwa jina;
 - e. Msamiati, mtindo na theolojia kama Pauline kama I Wathesalonike

C. Hizi Mbili Zinalinganishwa

1. Barua hizi zinafanana sana, si katika mawazo tu, bali pia uteuzi sahihi wa maneno. Ikiwa kanuni ya lugha ya ufunguzi na uhitimishaji haikuhusishwa, bado ufanano unajitokeza yapata theruthi ya nyaraka hizi.
2. Sifa jumuisi ya II Wathesalonike ni tofauti na barua ya kwanza, yenye kupooza sana na ya kikanuni zaidi. Bado hili linaweza kueleweka pindi mtu aonapo mambo ya kihisia yaliyohusishwa katika maandiko ya barua ya kwanza na kuyakuza matatizo ya barua ya pili.

D. Mpangilio wa Barua hizi

1. Nadharia nyingine zenye kuvutia zinawasilishwa na F. W. Manson kwa kutumia nukuu za Johannes Weiss'. Hawa walidai kwamba mpangilio wa kitabu hiki umeongezwa. Sababu ya hili ni:
 - a. Majaribu na mateso yaliyopo katika kipimo chao kilicho katika II Thes, lakini haya yako katika wakati uliopita ulio katika I The.;
 - b. Katika II Wathesalonike magumu ya ndani yanazungumzwa kama maendeleo mapya ambayo mwandishi wa barua hii amejifunza, ambapo katika I The. mambo haya yalijulikana kwa wale wote waliokuwa wakikumbwa na hofu;
 - c. huu usemi kwamba kitabu cha Wathesalonike hakikuwa na hitaji la kuwekewa mwongozo kuhusu nyakati na sababu (I The. 5:1) una uhusiano sana ikiwa huu utawekewa ulinganifu II The. 2;
 - d. hii fasili ya “Katika habari ya . . .” kilicho katika I The. 4:9, 13; 5:1, ni kama ile iliyo katika I Kor. 7:1,25; 8:1; 12:1; 16:1,12, ambapo mwandishi huyu anazijibu hoja zilizoibuka katika ile barua

iliyotumwa kwake. Manson anafikiri kwamba hili ni jibu kuhusiana na maswali fulani yaliyoibuka kutokana na semi zilizo katika II The.

2. Kauli mantiki kadhaa zinaweza kuikinza hoja hii:
 - a. matatizo yaliyoutawala umakini wa Paulo yanachochea na kwenda kwa kina kutoka I The. na II The.;
 - b. vifungu vilivyo katika II The. vinairejelea barua kutoka kwa Paulo (2:2, 15; 3:17) na ikiwa tunadhani barua hii si I The., basi tunalo tatizo la barua kupotea;
 - c. kumbukumbu binafsi zenye kuunda umaarufu wa sehemu ya kwanza ya barua zinakosekana katika barua ya pili, ambayo inaonekana kuwa ya asili ikiwa barua hii ni matokeo ya barua ya kwanza;
 - d. sifa ya barua inaonekana kutokuwa asili kamili katika hali hii ikiwa mpangilio huu umeongezwa upya.

III. TAREHE YA BARUA HIZI

- A. Hii tarehe ya uandishi wa Barua za Wathesalonike ni moja ya tarehe fulani zilizo nyingi tulizozijumuisha katika barua za Paulo. Imenukuliwa kwamba wakati Paulo alipokuwa katika “Korintho alikamatwa na kuletwa mbele ya Gallio, gavana wa Akaya.” Maandiko yaliyogunduliwa huko Delphi yanalijibu swali lililomrejelea Mfalme Claudio ni sawa na lile la Gallio. Hii iliwekwa tarehe mnamo mwaka wa kumi na mbili wa nguvu ya kodi ya Mfalme na baada ya kutangazwa kwake mwaka wa ishirini na sita kama Mfalme. Mwaka huu wa kumi na mbili ilikuwa kuanzia 25 Januari 52 B.K hadi 24 Januari 53 B.K. ambapo tarehe ya kutangazwa kwake mwaka wa ishirini na sita haijulikani wazi, wa ishiri na saba ilikuwa kabla ya maamuzi ya Klaudio mnamo 1 Augusti 52 B.K. ambayo yangetolewa kwa Gallio wakati wa nusu ya kwanza ya mwaka 52. Na sasa magavana waliuchukua utawala upesi katika kipindi cha joto na kutawala kwa mwaka mmoja. Hii ingeonekana hivyo, hivyo, Galio alilingiza neno lake la utawala upesi katika kipindi cha joto mnamo mwaka 51” (Morris, uk. 15).
- B. Tendo hili la kuliwekea tarehe neno utawala wa gavana halisuruishi tatizo la tarehe bayana ya Barua za Wathesalonike kwa ukamilifu. Paulo alikuwa huko Korintho kwa miezi 18 (Matendo 18:11) lakini ni kwa wakati gani alijitokeza mbele ya Galio haijulikani. Watoa maoni wengi wanaipa I na II Wathesalonike katika 50-51 B.K.
- C. Mtiririko yakini wa maandiko yenye kuwafuatisha F. F. Bruce na Murry Harris ni pamoja na nyongeza ndogondogo

<u>Kitabu</u>	<u>Tarehe</u>	<u>Maeneo ya Maandiko</u>	<u>Uhusiano na Matendo ya Mitume</u>
1. Wagalatia	48	Ashuru Antiokia	14:28; 15:2
2. I Wathesalonike	50	Korintho	18:5
3. II Wathesalonike	50	Korintho	
4. I Wakorintho	55	Efeso	19:20
5. II Wakorintho	56	Makedonia	20:2
6. Warumi	57	Korintho	20:3
7.-10. Barua za ndani ya Gereza			
Wakolosa	mnamo miaka ya 60	Rumi	
Waefeso	mnamo miaka ya 60	Rumi	
Filemoni	mnamo miaka ya 60	Rumi	
Wafilipi	miaka ya 62-63	Rumi	28:30-31
11.-13. Safari ya Nne ya Kimisheni			

I Timotheo	63 (au baadaye,	Makedonia
Tito	63 lakini kabla	Efeso (?)
II Timotheo	64 68 B.K.)	Rumi

IV. MATUKIO YANAYOZIZUNGUKA BARUA ZA WATHESALONIKE

- A. Matukio haya yaliyompelekea Paulo kuziandika barua kwa Wathesalonike ni changamano na yana msokoto. Tofauti fulani zilizojitokeza lazima zieleweke, hasa kuhusiana na mapangilio wa kimwili na mpangilio wa kihisia. Paulo alilazimika kuwaacha waamini wapya wa Kithesalonike kwa sababu Wayahudi walihimiza sana ushirikina, umati mkubwa wa watu waabuduo miungu ya mji kuanzisha ghasia ndani ya nyumba ya Yasoni katika kumtafuta Paulo na wenzake. Baada ya kusikilizwa mbele ya Baraza la watunga sheria, Yasoni na viongozi wengine wa Kikristo walilazimika kula kiapo cha ulinzi ili kuhakikisha uwepo wa amani. Paulo alipopata taarifa juu ya hili alifahamu kwamba yampasa kuondoka na kumwacha kijana huyu, kanisa changa. Huyu, hivyo, alikwenda Beroya pamoja na Timotheo na Sila. Kwa uwazi Timotheo alibaki kwanza (kama vile Matendo 17:10) baadaye aliungana na Sila kwa ajili ya kwenda Athene (kama vile Matendo 17:15). Hapo awali mapokezi ya kiuaminifu ya Wayahudi huko Beroya yalikuwa ya baraka kwa Paulo katika sura ya upinzani wa Kiyahudi wenye nguvu hapo awali. Bado hili halikuchukua muda mrefu. Wayahudi kutoka Thesalonike waliingia Beroya na kuanzisha ghasia. Hivyo, ilimpasa Paulo kuondoka tena.
- B. Kwa wakati huu Paulo alikwenda Athene ambapo alipokea makaribisho hafifu na yasiyo na mwitikio. Huyu alikuwa mpya kwa wasomi wa falsafa. Uzoefu wake ndani ya Makedonia ulibainishwa kupitia mateso na upinzani. Huyu alipigwa, alivuliwa nguo hadharani, na kufukuzwa nje ya mji usiku wa manane. Wasomi walimdhiki, na wapagani na watu wa nchi yake walimchukia (kama vile II Kor. 4:7-11; 6:4-10; 11:23-29).
- C. Paulo alilazimika kuliacha kanisa hili la Thesalonike lenye matumaini kwa wakati muhimu. Hawa walikuwa wachanga katika imani na walikuwa wakikumbana na adha na mateso. Paulo asingeliweza kusimama imara. Alikuwa na hofu juu ya waamini wapya, maeneo fulani kati ya Beroya na Athene, Paulo aliwaagiza Timotheo na Sila kurudi katika makanisa mapya ya Makedonia. Timotheo alikwenda Thesalonike. Wengi walifikiri kuwa alikaa na kuhudumu pale kwa miezi sita hadi mwaka mmoja. Kanisa lilikuwa na uhitaji sana wa mtu wa kuwafundisha, kuwafaraji na kuwatia moyo. Timotheo mwenyewe alikuwa muumini mpya aliye mwaminifu. Huyu aliongoa wakati wa safari ya kwanza ya kimisheni ya Paulo, lakini alikuwa na Paulo tangu Paulo alipokwenda Listra katika safari yake ya pili ya kimisheni. Huyu ndivyo alivyokuwa, hivyo, alikuwa mpya katika huduma lakini Paulo alimuimarisha kwa namna kubwa. Hii ilikuwa kazi ya kwanza ya Timotheo kama mwakilishi wa Paulo aliye mbobezi.
- D. Paulo alihudumu ndani ya Athene akiwa peke yake na kuvunjika moyo sana kukandamizwa sana kwa sababu ya mwitikio hafifu wa injili ndani ya Makedonia na wasiwasi wake endelevu kwa waamini wapya wa eneo hili. Kwa namna fulani huyu alikuwa na wasiwasi juu ya kanisa la Thesalonike. Je! kanisa lingekuwepo kwa muda huu mfupi na katika hali hizi ngumu na lingeendelea kuvumilia? (Carter, uk. 115) Kwa kuliongeza hili huyu hakupokea neno lo lote toka kwa Timotheo na Sila kwa wakati fulani (miezi sita hadi mwaka mmoja, ingawa wengine wanasema kuwa ulikuwa mwaka mmoja au miezi miwili (Farrar, uk. 369). Hii ilikuwa hali ya kihisia ambapo tunamuona Paulo akiwa na hali aliyoingia nayo ndani ya Korintho.
- E. Katika Korintho mambo mawili yalitokea ambayo yalimtia moyo sana Paulo.
1. Yale maono kwamba Mungu alikuwa na wengi ndani ya Korintho ambao wangeitikia injili (Matendo 18:9-10).
 2. Timotheo na Sila waliwasili na kuleta habari njema (Matendo 18:5). Huu ulikuwa ujumbe wa Timotheo kutoka Thesalonike ambao ungempelekea Paulo kuandika akiwa Korintho. Paulo aliyaitikia maswali na mambo ya kiutendaji kutoka kanisani na kuyakabili kimafundisho.

F. Mandiko ya II The. hayakuendelea baada ya I The. kwa sababu haikufanikisha yale yote ambayo Paulo angeyatmainia kutokea. Pia, alikuwa makini na matatizo mengine. Wanazuoni wengi waliamini kuwa II The. Iliandikwa miezi ipatayo sita baada ya I The.

V. KUSUDI LA BARUA

A. Barua za Wathesalonike zina makusudi matatu fungamano:

1. kuishiriki furaha na shukrani ya Paulo kwa Mungu kwa ajili ya uaminifu na Ufanano wa Kristo kwa Wathesalonike, hata ndani ya mateso.
2. kuzijibu hoja za shauku yake na sifa zilizokuwa zikiibuka dhidi yake.
3. Kujadili juu ya kurudi kwa Bwana. Dokezo la awali la mahubiri ya Paulo kuhusu matukio ya siku za mwisho lilisababisha maswali ndani ya Wakristo wa Thesalonike:
 - a. Ni jambo gani litatokea kwa waamini ambao walikufa kabla ya kurudi kwa Bwana?
 - b. Nini kingetokea kwa waamini waliokuwa katika kusanyiko kwa kuchukua maamuzi ya kuacha kuenenda Kikristo na waliokuwa tayari kukusubiri kurudi kwa Bwana (Barclay, kr. 21-22).

B. Mengi yaliyoelezwa hapo juu yanaweza kuelezwa kwa ukweli kwamba hili lilikuwa kanisa changa na lenye shauku kubwa. Kwa sababu ya hali mbalimbali, watu wa kanisa hili walikuwa hawajafundishwa na kuadibishwa kwa ukamilifu. Matatizo haya yaliwakilisha kile ambacho kingetarajiwa kwa kanisa la asili hii: waamini wapya, wanyonge, wenye hofu, wasiojishughulisha, wenye maono, na wenye mkanganyiko.

C. Kuwepo kwa II Wathesalonike kulikuwa, "Hii inamaanisha agizo la pili kwa hali ile ile, agizo lililowekwa baada ya kuzigundua dalili za ukaidi ambao haukuondolewa kwa tiba ya kwanza" (Walker, uk. 2968).

VI. BIBLIOGRAFIA YA VYANZO VILIVYODOKEZWA

Barclay, William. *The Letters and the Revelation. The New Testament. Juzuu 2.* New York: Collins, 1969.

Carter, Thomas. *Life and Letters of Paul.* Nashville: Cokesbury Press, 1921.

Farrar, Dean. *The Life and Work of St. Paul.* New York: Cassell na Company, Limited, 1904.

Heard, Richard. *An Introduction to the New Testament.* New York: Harper na Row Publishers, 1950.

Metzger, Bruce Manning. *The New Testament: Its Background, Growth and Content.* Nashville:

Abingdon Press, 1965. Manson, T. W. *Studies in the Gospels and Epistles.* Philadelphia: Westminster, 1962.

Morris, Leon. *The First and Second Epistles to the Thessalonians.* Grand Rapids: Eerdmans, 1991.

Ramsay, W. M. *St. Paul the Traveller and Roman Citizen.* New York: G. P. Putnam's Sons, 1896.

Shepard, J. W. *The Life and Letters of Paul.* Grand Rapids: Wm. B. Eerdmans Publishing Company, 1950.

Walker, R. H. *The International Standard Bible Encyclopedia.* Juzuu. V. N. D.

VII. MUHTASARI WA YALIYOMO *

A. Salamu, 1:1

B. Maombi ya Shukrani, 1:2-4

- C. Kumbukumbu ya yaliyopita, 1:5-2:16
 - 1. Mwitikio wa Wathesalonike juu ya mafundisho asilia, 1:5-10
 - 2. Mahubiri ya Injili huko Thesalonike, 2:1-16
 - a. Utakatifu wa shauku ya kundi hili, 2:1-6a
 - b. Kundi kukataa msaada, 2:6b-9
 - c. Tabia ya kundi ilikuwa ya ukamilifu, 2:10-12
 - d. Ujumbe wa kundi hili kuhusiana na Neno la Mungu, 2:13
 - e. Mateso, 2:14-16

- D. Uhusiano wa Paulo na Wathesalonike, 2:17-3:13
 - 1. Shauku yake ya kurudi, 2:17,18
 - 2. Furaha ya Paulo kwa Wathesalonike, 2:19, 20
 - 3. Jukumu la Timotheo, 3:1-5
 - 4. taarifa, 3:6-8
 - 5. Utoshelevu wa Paulo, 3:9, 10
 - 6. Maombi ya Paulo, 3:11-13

- E. Nasaha kwa wale wanaoyaishi maisha ya Kikristo, 4:1-12
 - 1. Kwa ujumla, 4:1, 2
 - 2. Utakatifu wa ujinsia, 4:3-8
 - 3. Upendo wa kidugu, 4:9, 10
 - 4. Maisha ya mtu yastahiliyo, 4:11, 12

- F. Matatizo Yahusianayo na Kuja Mara ya Pili, 4:13-5:11
 - 1. Waamini waliokufa mbele ya Parousia (kurudi kwa Yesu Mara ya Pili), 4:13-18
 - 2. Kipindi cha Parousia (Kuja kwa Yesu Mara ya Pili), 5:1-3
 - 3. Watoto wa siku zile, 5:4-11

- G. Nasaha za Jumla, 5:12-22

- H. Hitimisho, 5:23-28

*KITABU HIKI HAKIELEZI KWA MUHTASARI KWA UKARIBU KATIKA KIPENGELE CHA MAFUNDISHO NA KIPENGELE CHA KIUTENDAJI KAMA ZILIVYO BARUA NYINGINE NYINGI ZA PAULO. IKIWA UELEKEO WA JUMLA UNAFUATIWA NA MJADALA WA PAULO JUU YA KUJA MARA YA PILI KATIKA 4:17-18 NI KIPENGELE CHA KIUTENDAJI, SI CHA KIMAFUNDISHO! KUJA MARA YA PILI SI MAFUNDISHO YANAYOTAKIWA KUKUBALIWA TU, BALI NDIYO MAISHA YAMPASAYO MTU KUYAISHI KATIKA MATARAJIO YA KURUDI KWAKE KWA WAKATI WO WOTE

VIII. MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KI-MUHTASARI

- 1. "Nanyi mkawa wafuasi wetu," 1:6
- 2. "Mungu aliye hai, wa kweli", 1:6
- 3. "ghadhabu itakayokuja," 1:9
- 4. "kama vile mlezi awatunzavyo," 2:7
- 5. "hawapatani na watu wo wote," 2:15
- 6. "shetani akatuzuia," 2:18
- 7. "kuyatengeneza mapungufu ya imani yenu," 3:10
- 8. Kutakaswa, 4:3
- 9. Waliolala, 4:13
- 10. "hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti," 4:6
- 11. "parapanda ya mungu," 4:16

12. "mawingu,"4:17
13. "hivyo tutakuwa pamoja na bwana,"4:17
14. Tusilale,5:6,7
15. Kiasi, 5:8
16. "tukijivika kifuani imani na upendo" 5:8
17. "chapeo yetu iwe tumaini la wokovu,"
18. Busu takatifu 5:26
19. Ustahimilivu, II The. 1:4
20. Maangamizi ya milele, II The.
21. Ukengeufu, II The. 2:3
22. "bwana yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, II The. 2:8

IX. WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. Silvano, II The. 1:1
2. malaika mkuu, I The. 4:16
3. "wakati wasemapo. . .," I The. 5:3
4. "mtu wa kuasi," II The. 2:3
5. "azuiaye sasa," II The. 2:7
6. "ndugu aendaye bila utaratibu," II The. 3:6

X. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Thesalonike, 1:1
2. Makedonia, 1:8
3. Akaya, 1:8
4. Filipi, 2:2
5. Yudea, 2:14
6. Athene, 3:1

XI. MASWALI YA MJADALA

1. Paulo anayafafanua mahubiri yake katika namna tano katika 2:3 na 5. Ziorodheshe.
2. Kwanini Paulo asingeikubali fedha kutoka ndani ya makanisa aliyoyahubiri? (2:9)
3. Ni kwa namna gani 4:11 inahusiana na hali ya kihistoria ambayo ilimsababisha Paulo kuiandika barua hii? (Pia II The.3:6-12)
4. Ni kwa namna gani 4:17 inahusiana na shangwe?
5. Sura ya 5:1 ina mrejelea nani?
6. Kwa nini Paulo anawafafanua waamini kama askari" (5:8)
7. Ni kwa namna gani 5:12-13 inahusiana na huduma za sasa?
8. Orodhesha mambo ambayo waamini wanapewa wito wa kuyafanya katika 5:14-22.
9. Kubadilika kwa mwanadamu kunajikita katika 5:23?
10. Nini wazo kuu la II The. 1? Je! Inatofautianaje na I The. 1?
11. Je! II The. 2:4 inadai kujenga upya Hekalu la Kiyahudi?
12. Ni kwa namna gani II The. 2:11 inahusiana na mapenzi huru ya mwanadamu na majukumu yake?
13. Ni kwa namna gani II The. 2:13-15 inaweka usawa wa maamuzi ya kabla na mapenzi huru?

UTANGULIZI WA BARUA ZA KICHUNGAJI 1 & 2 TIMOTHEO na TITO

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Eneo la kijiografia limetajwa katika 1 Timotheo, Tito, na 2 Timotheo halishabihiani na mpangilio wa matukio wa aidha Matendo ya Mitume au nyaraka zingine za Paulo.
1. safari ya Efeso (kama vile I Tim. 1:3)
 2. safari ya Troa (kama vile II Tim. 4:13)
 3. safari ya Mileto (kama vile II Tim. 4:20)
 4. Umisheni wa Krete (kama vile Tito 1:5)
 5. Umisheni Uhispania (kutoka kwa Clement wa Rumi, 95 B.K. na utangulizi wa Uidhinishwaji wa Muratorian, 180-200 B.K.)
- Hivyo ninafikiri kwamba Paulo aliachiwa kutoka gerezani (mwanzoni mwa miaka ya kati ya 60, ambayo imeandikwa katika I Clement 5, iliyoandikwa mnamo mwaka wa 95 B.K.) na kuchukua safari ya nne ya umishenari, na baadaye aliachiwa na kuuawa kabla ya mwaka 68 B.K. (kujiuwa kwa Nero).
- B. Kusudi la barua hizi kiujumla ilifikiriwa lilikuwa ni uongozi (mpangilio wa kanisa). Hata hivyo katika *New International Biblical Commentary, Vol. 13*, juu ya I na II Timotheo na Tito, Gordon Fee ananishawishi kwamba kutukia kwa nyaraka hizi kulikuwa mafundisho ya uongo yaliyoibuka ndani ya makanisa ya nyumbani ya Efeso (I Timotheo) na katika kisiwa cha Krete (Tito).
- C. Kwa njia fulani Barua za Kichungaji zinajenga utaratibu wa kiuongozi sawasawa na *Manual of Discipline* (Mwongozo wa nidhamu) wa Waesene. Miongozo hii ilikuwa muhimu sana kwa ufahamu wa mwanzo na upotoaji wa muundo na mafundisho ya kitume.
- D. Ufanano wa nyaraka za kichungaji na misamiati katika kitabu cha Luka na Matendo ya Mitume inawezekana ikawa kutokana na ukweli kwamba Paulo alimtumia kama mwandishi (kama vile C. F. C. Moule, *Tatizo la Nyaraka za Kichungaji: A Reappraisal*). S. G. Wilson hata ameelezea katika *Luka na nyaraka za Kichungaji* kwamba vitabu hivi vitatu inaweza kuwa lilikuwa jaribio la Luka kuandika juzuu ya tatu kuainisha namna ya upelekaji wa Injili zaidi ya Rumi.
- E. Kwanini vitabu hivi vitatu vilifungwa kwa pamoja? Je yawezekana kwamba vinashughulikia nyakati tofauti/sehemu/mambo? Ni katika 1 Timotheo na Tito ambavyo vinaongelea mpangilio wa kanisa. Hii ni (1) ni misamiati yao; (2) walimu wa uongo wanaonekana kuunganisha vitabu hivi; na (3) ukweli kwamba kiuwepesi havishabihiani katika mtiririko wa Matendo ya Mitume (ikiwa vinawekwa pamoja).

II. MWANDISHI

- A. Barua zenyewe zinadaiwa kutoka kwa Paulo mwenyewe (kama vile I Tim. 1:1; II Tim. 1:1; na Tito 1:1) kwenda kwa wawakilishi wake wawili wa kitume, Timotheo na Tito
- B. Swala la uandishi wa Barua za kichungaji lilianza kufanyiwa hoja mnamo karne ya 19 na 20. Kukataliwa kwa uandishi wa Paulo siku zote umejikita katika
1. mpangilio wa uongozi wa kanisa uliokuwa (sifa za viongozi)
 2. mafundisho ya uongo ya kiasi kikubwa (kulikoandikwa karne ya pili)
 3. thiolojia iliyokua (matamko ya imani)

4. utokaji kando/utofautiano wa misamiati na muundo (robo ya maneno hayatumika katika maandiko mengine ya Paulo)

C. Tofauti hizi zinaelezewa

1. haya ni maandiko ya mwisho ya Paulo, yawezekana akimtumia Luka kama mwandishi
2. misamiati na muundo vinategemeana na mahali pa tukio
3. mawazo ya walimu wajuzi yalikuawa ni maendeleo ya mawazo ya karne ya kwanza ya Kiyahudi (kama vile Magombo ya Bahari ya Chumvi)
4. Paulo alikuwa mwanathiolojia mwenye uwezo mkubwa sana na mwandishi mbunifu mwenye misamiati mingi

D. Kuna ukuaji mkubwa wa mfano wa kihistoria

1. Paulo kumtumia mwandishi wa Kikristo mwenye taaluma ya uandishi (kwa maana hii yawezekana akawa ni Luka)
2. Paulo kumtumia mwandishi mwenza (yaani mmoja ya watu waliounda kundi lake la umisheni, kama vile II Tim. 4:11)
3. Matumizi ya Paulo ya liturujia au nukuu za tenzi (muhtasari mzuri unapatikana katika *Dictionary of Paul and His Letters*, kilichohaririwa na Hawthorne na Martin, kilichochapishwa na IVP, ukur. 664). Mapendekezo kwamba sehemu za Barua za kichungaji ni nukuu kutoka vyanzo vingine kunasaidia kuelezea hesabu ya *hapax legomena* (maneno yaliyotumika mara moja tu katika Agano Jipya), nahau zizizo andikwa na Paulo na matumizi yamaalumu ya maneno ya Paulo.
 - a. maneno ya kithiolojia kumuelezea Mungu (kama vile I Tim. 1:17; 6:15-17)
 - b. orodha ya uovu (kama vile I Tim. 1:9-10)
 - c. mienendo sahihi ya wake (kama vile I Tim. 2:9-3:1a)
 - d. sifa za wahudumu (kama vile I Tim. 3:1b-13)
 - e. ukiri wa ki tenzi (kama vile I Tim. 2:5-6; 3:16; II Tim. 1:9-10; Tito 3:3-7)
4. tenzi (kama vile I Tim. 6:11-12,15-16; II Tim. 2:11-13; Tito 2:11-14)
 - a. midrash ya Agano la Kale (kama vile I Tim. 1:9-10; 2:9-3:1a; 5:17-18; II Tim. 2:19-21; Tito 3:3-7)
 - b. Kanuni
 - (1) “neni la uaminifu” (kama vile I Tim. 1:15; 2:9-3:1a; II Tim. 2:11-13; Tito 3:3-8)
 - (2) “kujua hili kwamba” (kama vile I Tim. 1:9-10; II Tim. 3:1-5)
 - (3) “vitu hivi” (kama vile I Tim. 4:6,11; II Tim. 2:14; Tito 1:15-16; 2:1)
5. nukuu kutoka kwa mshairi wa Kiyunani (kama vile Tito 1:12 [Epimenides na/au Euripides])

E. Inashangaza kwamba “wafuasi wa Paulo” wa karne ya pili wangetaja maelezo ya kibayana kwa kutumia majina ya watu (yaani Himenayo, I Tim. 1:20; II Tim. 2:17; Iskanda, I Tim. 1:20; Zena, Tito 3:13) na matukio (ugonjwa wa Trofimo huko mileto, II Tim. 4:20; au majukumu ya wajane, I Tim. 5:9) ambayo hayatajwi mahali pengine popote katika maandiko ya Paulo. Mambo haya hayashabihianai na madhanio ya waandishi wa kupika uongo. Kwa makala nzuri juu ya uandishi wa uongo kuhusiana na barua za Agano Jipya, agalia *An Introduction to the New Testament*, cha Carson, Moo, na Morris, kur. 367-371.

III. TAREHE

- A. ikiwa hii ni kweli kwamba Paulo aliachiwa kutoka gerezeni (baada ya kufungwa kwa kitabu cha Matendo ya Mitume, yawezekana mwaka 59-61 B.K.), basi kuna desturi za mwanzoni za shughuli zake mara baada ya kutoka gerezeni (yaani mahubiri huko Uhispania, kama vile Rum. 15:24,28)?
1. Barua za Kichungaji (kama vile II Tim. 4:10)
 2. I Clement 5
 - a. Paulo alihubiri katika mashariki na Magharibi (yaani Uhispania)

- b. Paulo aliwawa chini “vibaraka” (yaani Tigellinus na Sabinus, aliyefanya kazi katika mwaka wa mwisho wa utawala wa Nero, 68 B.K.)
3. Utangulizi wa Muratorian Fragment (orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutoka Rumi mnamo mwaka 180-200 B.K.)
4. Toleo la Eusebius la *Historical Ecclesiastical History* 2:22:1-8 inasema kwamba Paulo aliachiwa kutoka katika kufungwa na Warumi
- B. Inaonekana kwamba 1 Timotheo na Tito vilikuwa karibu sana kwa kuandikwa kabla ya Paulo kukamatwa tena. 2 Timotheo ni maandiko ya mwisho ya Paulo na salamu ya kwaheri akiwa gerezani.
- C. Mtiririko unaowezekeka kuwa wa maandiko ya Paulo kufuatia F. F. Bruce na Murry Harris pamoja na kuasili kwa sehemu kidogo.

<u>Kitabu</u>	<u>Tarehe</u>	<u>Mahali pa kuandikwa</u>	<u>Uhusiano na Mdo.</u>
15. Wagalatia	48	Antiokia ya Shamu	14:28; 15:2
16. 1 Thesalonike	50	Korintho	18:5
17. 2 Thesalonike	50	Korintho	
18. 1 Thesalonike	55	Efeso	19:20
19. 2 Thesalonike	56	Makedonia	20:2
20. Warumi	57	Korintho	20:3
21. - 10.			
Wakolosai	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	
Waefeso	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	28:30-31
Filemoni	mwanzoni mwa 60 (gereza)	Rumi	
Wafilipi	mwishoni mwa 61-62 (gereza)	Rumi	
17. 1 Timotheo	63 (au baadaye, lakini	Makedonia	
18. Tito	63 kabla	Efeso (?)	
19. 2 Timotheo	64 mnamo 68)	Rumi	

IV. WAPOKEAJI

- A. Jina la Nyaraka za Kichungaji linatoka kwa fasiri ya D. N. Berdot ya mnamo mwaka 1703. Kinazungumzia tabia yao ya pekee na maudhui. Timotheo na Tito hata hivyo sio wachungaji bali wawakilishi wa kitume.
- B. Barua hizi hazikuandikwa kwa makanisa bali kwa muundo wa kifasihi wa barua kwenda kwa watenda kazi wenza wa Paulo. Paulo anawahutubia makutano kama anavyoandikia kundi lake la viongozi. Dokezo juu ya upana wa hadhira wa Paulo ni
1. utangulizi rasmi unaotaja mitume wake
 2. the pluralwingi “ninyi” katika ufungaji wa mwisho wa barua zote tatu
 3. utetezi wa Paulo wa utume wake (kama vile I Tim. 2:7)
 4. Maandiko ya Paulo kwa Timotheo kuhusu vitu ambavyo alitakiwa awe amekwisha kuvijua kutokea muda ule wa Paulo (cf. kama vile I Tim. 3:15)

V. MAZINGIRA/KUSUDI

- A. Kusudi kubwa lilikuwa ni kuzuia/kukabili na mafundisho ya uongo (kama vile I Tim. 1:3-7). Mafundisho hasa yanaweza kuwa hali ya kiyahudi na walimu wa uongo (kama sawasawa na walimu wa uongo wa Efeso na Kolosai). Yawezekana vilikuwa vikundi tofauti.

- B. Agano la Kale linatoa miongozo ya kibayana kwa ajili ya mpangilio wa jamii inayoamini. Agano Jipya halina maeleko ya kibayana juu ya mpangilio au taasisi za kanisa. Barua za Kichungaji (I Timotheo, II Timotheo, na Tito) vinakaribiana inapokuja suala la miongozo ya Agano Jipya.
- C. I Timotheo kiliandikwa:
1. kumuomba Timotheo akae Efeso (kama vile I Tim. 1:3)
 2. kushugulikia walimu wa uongo (kama vile I Tim. 1:19-20; 4:1-5; 6:4-5,20-21)
 3. kusaidia kupangilia uongozi (kama vile I Tim. 3)
- D. Tito alikuwa na kazi hiyo hiyo kukabiliana na walimu wa mafundisho ya uongo (kama vile 1:5)
- E. II Timotheo anamkuta Paulo gerezani kukiwa na tumaini dogo sana la kuachiliwa huru (kama vile 4:6-8, 16-18)
- F. Kuna mkazo mkubwa wa “mafundisho yenye maana” (yaani mafundisho sahihi) unaoonekana katika barua zote hizi (kama vile I Tim. 1:10; 4:6; 6:3; II Tim. 1:13; 4:3; Tito 1:9; 2:1) au “imara katika imani” (kama vile Tito 1:13; 2:2). Mungu alimwamini Paulo kwa hili “mafundisho yaliyo sahihi” (kama vile I Tim. 1:11); Paulo akamkabidhi jukumu hili Timotheo (kama vile I Tim. 6:20) na Timotheo alitakiwa kuyakabidhi kwa watu wote waaminifu (kama vile II Tim. 2:2).

VI. WALIMU WA UONGO

- A. Ni ngumu kujadili walimu wa uongo kwasababu ya kukosekana kwetu kwa taarifa za karne ya kwanza. Paulo anaandika kwa wale wote waliowajua walimu hawa wa uongo kwanza. Hivyo hajadili kwa ukamilifu thiolojia yao lakini siku zote akishutumua mitindo yao ya maisha na nia zao (kama anavyofanya Yuda).
- B. Jambo kubwa la ufasiri linahusiana na iwapo walikuwa
1. Wayahudi
 2. Wayunani
 3. au vyote viwili
- C. Walimu wa uongo wanaonekana kuwa mchanganyiko wa tabia za Kiyahudi na walimu wenye ujuzi. Lakini ni kwa namna gani uamsho wa dini hizi mbili ambazo ni tofauti kabisa ziwe kama kitu kimoja kwa kuunganika?
1. Dini ya Kiyahudi siku zote ilijumuisha viashiria vya u-pili (kama vile Magombo ya Bahari ya Chumvi)
 2. Walimu wajuzi wa karne ya pili walikuza maudhui hizi za kifalsafa na kithiolojia za Mashariki ya karibu ya kale kuwa za kawaida
 3. dini ya kiyahudi ya ugenini ilikuwa a hamasa zaidi kuliko uanazuoni wa kisasa kuliko ilivyokuwa imekusudiwa
 4. Kuna mfano wa karne ya kwanza kwa mafundisho ya uongo ya kiyahudi yenye asili ya walimu wajuzi katika kitabu cha Wakolosai
- D. Baadhi ya viashiria vya walimu wa uongo
1. kipengele cha Kiyahudi
 - a. walimu wa uongo
 - (1) walimu wa sheria (kama vile I Tim. 1:7)
 - (2) sherehe za tohara (kama vile Tito 1:10)
 - b. walimu wa uongo walionya juu ya hadisthi za kusadikika za Kiyahudi (kama vile I Tim. 3:9; Tito 1:14)
 - c. walimu wa uongo walijali sana sheria za vyakula (kama vile I Tim. 4:1-5)

- d. walimu wa uongo walijali sana uzao (kama vile I Tim. 1:4; 4:7; II Tim. 4:4; Tito 1:14-15; 3:9)
2. vipengele vya Walimu Wajuzi (Angalia Mada Maalum katika Tito 1)
 - a. walikataza kujizuia na kuacha vitu fulani
 - (1) walikataza ndoa (kama vile I Tim. 2:15; 4:3)
 - (2) kuachwa kwa vyakula fulani (kama vile I Tim. 4:4)
 - b. unyonyaji wa kingono (kama vile I Tim. 4:3; II Tim. 3:6-7; Tito 1:11,15)
 - c. msisitizo katika maarifa (kama vile I Tim. 4:1-3; 6:20)

VII. UIDHINISHWAJI

- A. Nyaraka a Paulo zilikusanywa pamoja katika juzuu moja iliyoitwa “Mtume” na baadaye kupitishwa katika makanisa yote. Maandiko ya Kiyunani pekee ya barua za Paulo ambayo yanakosa 1 na 2 Timotheo na Tito (pia II Wathesalonike na Filemoni) ni maandiko ya Mafunjo kutokea miaka ya 200, yaitwayo P⁴⁶ (kutoka mafunjo ya Chester Beatty). Hata haya ni makisio kwasababu maandiko yanakosa kurasa kadhaa za kuhitimisha. Maandiko mengine yote ya Kiyunani yanajumuisha kile kilichokuja kuitwa “nyaraka za Kichungaji.”
- B. Vyanzo vya kale ambavyo vinanukuu au kutaja Barua za Kichungaji
 1. viongozi wa kanisa la kwanza
 - a. Pseudo-Barnabas (70-130 B.K.) ananukuu II Timotheo na Tito
 - b. Clement wa Rumi (95-97B.K.) anaelezea I Timotheo na II Timotheo na nukuu ya Tito 3:1
 - c. Polycarp (110-150 B.K.) anataja I Timotheo, II Timotheo, na Tito
 - d. Hermas (115-140 B.K.) ananukuu I Timotheo na II Timotheo
 - e. Irenaeus (130-202 B.K.) ananukuu mara kwa mara kutoka I Timotheo, II Timotheo, na Tito
 - f. Diognetus (150 B.K.) anamnukuu Tito
 - g. Tertullian (150-220 B.K.) ananukuu I Timotheo, II Timotheo, na Tito
 - h. Origen (185-254 B.K.) ananukuu I Timotheo, II Timotheo, na Tito
 2. orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa ambavyo inajumuisha Barua za Kichungaji
 - a. Muratorian Fragment (kutokea Rumi mnamo mwaka wa 200 B.K.)
 - b. Barococcio (206 B.K.)
 - c. Apostolic List (300 B.K.)
 - d. Cheltenham List (360 B.K.)
 - e. Athanasius’ Letter (367 B.K.)
 3. matoleo ya mwanzoni ambayo yanajumuisha Barua za Kichungaji
 - a. Kilatini cha kale (150-170 B.K.)
 - b. Kishamu cha kale (200 B.K.)
 - c. mabaraza ya kanisa ya kale ambayo yaliki hadhi ya kuvuviwa ya Barua za kichungaji
 - d. Nicea (325-340 B.K.)
 - e. Hippo (393 B.K.)
 - f. Carthage (397 na 419 B.K.)
- C. Mchakato wa maafikiano kati ya makundi ya Kikristo uya ufalme wa Kirumi yalikuza uidhinishwaji. Maafikiano haya hakika yaliathiriwa na mgandamizo wa nje na ndani. Mahitaji ya msingi kwa ujumuishwaji katika kuidhinishwa kunaonekana kuwa
 1. mahusiano na Mtume
 2. ujumbe wenye mwendelezo pamoja na maandiko mengine ya Kitume
 3. maisha yenye mabadiliko ya wale wote waliokutana na maandiko haya
 4. kukubaliana kunakokua katika orodha ya maandiko yaliyokubaliwa kati ya makanisa haya ya kale
- D. Hitaji la idhini lilikua kwasababu
 1. kuchelewa kwa Kurudi kwa mara ya Pili
 2. umbali wa kijiografia kati ya makanisa na Mitume

3. vifo vya Mitume
4. kuinuka kwa mapema kwa walimu wa uongo
 - a. dini ya Kiyahudi
 - b. Falsafa ya Kiyunani
 - c. mchanganyiko wa viashiria vya Kiyahudi na walimu wajuzi (Wakolosai)
 - d. Dini zingine za siri za Kiyunani-Kirumi (mfano Mithra)
Hii ilitokea kadiri injili ilivyosambaa katika desturi zingine tofauti tofauti.

E. Suala la uidhinishwaji kihistoria inahusiana na uandishi. Makanisa ya kale yalikubali Nyaraka za Kichungaji kama maandiko ya Paulo. Madhania yangu mwenyewe juu ya uidhinishwaji kunajumuisha kuhusishwa kwa Roho, sio tu katika maandiko bali pia katika mikuanyiko na utunzaji. Swali la uandishi wa Paulo (ambalo ninalidhania) haliathiri uvuvio na uishinishwaji.

VIII. I TIMOTHEO - MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "mwanangu wa kweli wa imani," 1:2
2. anayekufuru, 1:13
3. Amina, 1:17
4. mpatanishi, 2:5
5. fidia, 2:6
6. "inua mikono mitakatifu," 2:8
7. "asiyeonywa, 3:2
8. "apendaye mvinyo," 3:8
9. "siri ya imani," 3:9
10. "mafundisho ya mapepo," 4:1
11. "wamepotea katika dhamiri zao wenyewe," 4:2
12. "mavazi ya kidunia," 4:7
13. "kuwekewa mikono," 4:14; 5:22
14. wazee, 4:14
15. "waheshimu wajane walio wajane kweli kweli," 5:3
16. "nadhiri ya kwanza," 5:12
17. "heshima maradufu," 5:17
18. kuridhika, 6:6
19. nuru isiyoweka kukaribiwa, 6:16

IX. I TIMOTHEO- WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. Baba, 1:2
2. "walimu wa sheria," 1:7
3. "mfalme wa milele," 1:17
4. Hymenayo na Iskanda, 1:20
5. mwangalizi, 3:2
6. shemasi, 3:8
7. wanawake, 3:11
8. wazee, 5:17
9. Pontio Pilato, 6:13

X. I TIMOTHEO – MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Makedonia, 1:3
2. Efeso, 1:3

XI. I TIMOTHEO – MASWALI YA MJADALA

1. elezea kwa maneno yako mwenyewe walimu wa uongo wanaotajwa katika 1:3-4.

2. Je 1:9-11 inaaksi Amri Kumi? Ikiwa ndio, nini tofauti?
3. Kwanini Paulo alijiona mwenyewe kama mwenye dhambi kuliko wote? (1:15)
4. Tukio gani linarejerewa katika maisha ya Timotheo katika 1:18 refer?
5. Inamaanisha nini kwamba Paulo anamaanisha kumkabidhi Shetani? (1:20)
6. Kwanini 2:4 ni mstari muhimu hivyo?
7. Elezea 2:9 kwa ufahamu wa desturi za karne ya kwanza.
8. Ni kwa namna gani 2:12 inafanya kazi leo?
9. Elezea 2:15 kwa maneno yako mwenyewe.
10. orodhesha sifa za mwangalizi (3:1-7)
11. Kwanini 3:16 inasemekana kuwa nukuu kutoka katika tenzi ya kale?
12. Kwanini walimu wa uongo walikataza kuoana? (4:3)
13. Ni kwa namna gani 4:4 inahusiana na Warumi 14?
14. Elezea 4:10 kwa maneno yako mwenyewe.
15. Ni tukio gani 4:14 inaelezea?
16. Ni kwa namna gani 5:19 inaaksi Agano la Kale?
17. Tatizo gani la kidesturi linaelezewa katika 5:23?
18. Elezea 6:10 kwa maneno yako mwenyewe.
19. Wapi vyeo/majina ya Yesu katika 6:15 yanatokea?

XII. II TIMOTHEO - MANENO NA TUNGO ZA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "ichochee karama ya Mungu," 1:6
2. "hazina uliyokabidhiwa wewe," 1:14
3. Donda-ndugu, 2:17
4. "muhuri hii," 2:19
5. vyombo, 2:20
6. Bwana, 2:21
7. "kwa wakati ukufaa na usiofaa," 4:2
8. hadithi za uongo, 4:4
9. "vitabu. . .vile vya ngozi," 4:13
10. "vinywa vya simba," 4:17

XIII. II TIMOTHEO – WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. tangu zamani za wazee, 1:3
2. Loisi, 1:5
3. Eunike, 1:5
4. Onesiforo, 1:16
5. Hymenayo, 2:17
6. Fileto, 2:17
7. Yanesi na Yambre, 3:8,9
8. mwinjiisti, 4:5
9. Dema, 4:10
10. Luka, 4:11
11. Marko, 4:11
12. Tikiko, 4:12
13. Iskanda, 4:14

XIV. II TIMOTHEO – MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Asia, 1:15
2. Rumi, 1:17
3. Efeso, 1:18; 4:12
4. Antiokia, 3:11

5. Ikonja, 3:11
6. Listra, 3:11
7. Thesalonika, 4:10
8. Galatia, 4:10
9. Dalmatia, 4:10
10. Troa, 4:13
11. Korintho, 4:20
12. Mileto, 4:20

XV. II TIMOTHEO - MASWALI YA MJADALA

1. Paulo alifungwa wapi?
2. Elezea 1:12 kwa maneno yako mwenyewe.
3. Ni kwa namna gani 1:9 kama Tito 3:5a?
4. Onesiforo alifanya nini kwa ajili ya Paulo aliyeko gereza? (1:16-18)
5. II Timotheo 2:2 ni mstari muhimu sana. Kwanini?
6. Kwanini 2:11 inasadikika kuwa nukuu kutoka tenzi za hapo mwanzo?
7. Ni nini kinachomaanishwa katika 2:15?
8. Je 2:25 inamaanisha kwamba Mungu anatoa toba? Ikiwa ndiyo, ni nini maana yake?
9. Orodhesha vitui ambavyo waaminio wanatakiwa wafanye kuwasaidia "waliopotoka." (2:24-25)
10. Nani na nini 3:6-7 inakabiliana nacho?
11. Kwanini 3:16 ni mstari muhimu sana?
12. Kwanini Paulo hakuweza kumponya Trofimo?

UTANGULIZI WA TITO

I. MREJEO WA KIMUHTASARI

- A. Kitabu cha Tito ni sehemu ya mkusanyiko wa barua za Paulo zijulikanazo kama “Barua za Kichungaji.” Hii ni kwa sababu ya I Timotheo, Tito, na II Timotheo zinazoshughulika na maonyo ya Paulo kwa watendakazi pamoja naye juu ya (1) namna ya kushughulika na waalimu wa uongo, (2) namna ya kushughulika na uongozi ulio katika makanisa mama, na (3) namna ya kusisitiza wema. Mpangilio thabiti ulio wazi wa vitabu hivi ni: I Timotheo na/au Tito na baadaye, II Timotheo. Tito inashughulikia mambo yale yale yaliyo katika I Timotheo. Kitabu cha Tito kinaweza kuwa kimeandikwa kwanza kwa sababu utangulizi wake ulio mrefu sana kithiolojia umehusishwa sana, sana kama kitabu cha Warumi.
- B. Mijongeo ya Paulo kijiografia na panao na hawa watenda kazi pamoja naye haikidhi mijongeo hii ya Paulo katika kitabu cha Matendo. Hivyo, wengi wanadhani kwamba Paulo aliachiliwa toka gerezani na aliendelea na safari ya nne ya umisheni.
- C. Tarehe ya safari hii ya nne ya umisheni kwa wakati mwingine ingeweza kuwa kati ya miaka ya 60 B.K hadi 68 B.K. kwa sababu Paulo alikatwa kichwa chini ya utawala wa Nero na Nero alijiua mnamo mwaka 68 B.K. (wengi wanadhani ni katika kipindi cha mateso ya mwaka 65 B.K.).

II. MTU, AITWAYE TITO

- A. Tito alikuwa mmoja wa watenda kazi wa Paulo waloaminiwa. Hili linadhihirishwa kwa ukweli kwamba Paulo alimsimika kwa ajili ya dosari za ghasia za Korintho na Krete.
- B. Huyu alikuwa mtu kamili wa Mataifa (Timotheo pekee ndiye aliyekuwa nusu-Myunani), aliyebadili dini chini ya mahubiri ya Paulo. Paulo alikataa kumtahiri (kama vile Gal. 2:3).
- C. Huyu anatajwa mara kwa mara katika barua za Paulo (kama vile II Kor. 2:13; 7:6-15; 8:6-24; 12:18; Gal. 2:1-3; II Tim. 4:10) na inashangaza sana kwamba Luka hamtaji katika kitabu cha Matendo. Baadhi ya watoa maoni wanatoa nadharia kwamba:
 - 1. huyu anaweza kuwa jamaa ya Luka (huenda nduguye) na tendo la kulitaja jina lake lingeweza kuonekana kama tendo la ukiukaji wa kitamaduni kwa upande wa Luka.
 - 2. Tito ndiyo chanzo kikuu cha habari za Luka kuhusu maisha na huduma ya Paulo na, hivyo, kama alivyo Luka, naye asingepewa jina.
- D. Huyu alitembea pamoja na Paulo na Barnaba katika Mabaraza yote muhimu ya Yerusalemu, kama ilivyoandikwa katika Matendo 15, ambapo suala la uhusiano wa waamini wapya wa Mataifa kwa Sheria ya Musa lilijadiliwa na kutatuliwa.
- E. Kitabu hiki kinajikita katika ushauri ambao Paulo alimpa Tito kuhusu huduma yake juu ya Krete. Tito anatenda kazi kama msaidizi maalumu/mwakilishi.
- F. Taarifa za mwisho zilizo katika Agano Jipya kuhusu Tito ni kwamba huyu alitumwa kuhudumu huko Dalmatia (kama vile II Tim.4:10).

III. WAALIMU WA UONGO

- A. Kwa uwazi kuna kundi la walimu wa uongo juu ya Krete walioipinga injili ya Paulo.
 - 1. Mafundisho yao ya kithiolojia yalikuwa na mwelekeo wa mgogoro kati ya maisha ya ki-Mungu yaliyotegemewa kwa waamini wote.

2. marejeleo ya maisha ya ki-Ungu: 1:1,16; 2:7,14; 3:1,8,14
3. ufupisho wa sifa: 2:11-14; 3:4-7

B. Kuna vikolezo dhahiri vya Kiyahudi katika ufundishaji huu wa uongo (kama vile 1:10,14; 3:8-9). Waasi hawa ni muungano wa sheria za Kiyahudi na madhaanio ya Kiyunani yaliyofikiriwa (mapotoe, angalia Mada Maalumu katika 1:1). Hawa ni sawa na waalimu wa uongo wanaoelezwa katika I Timotheo, Wakolosai, na Waefeso. Tazamio la Barua za Kichungaji ni uasi, si kuutenga umoja wa kanisa.

IV. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. utauwa, 1:1
2. “katika tumaini la uzima wa milele,” 1:2
3. “ambao Mungu asiyeweza kusema uongo,” 1:2
4. mkaribishaji, 1:8
5. hadithi za Kiyahudi, 1:14
6. mafundisho yenye uzima, 2:1
7. wastahivu, 2:2
8. “katika ulimwengu huu wa sasa,” 2:12
9. “tumaini lenye baraka,” 2:13
10. atukomboe, 2:14
11. “kuoshwa kwa kuzaliwa,” 3:5

V. WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. wazee, 1:5
2. askofu, 1:7
3. “wale wa tohara,” 1:10
4. “nabii wao,” 1:12
5. “kwa wenye uwezo na mamlaka,” 3:1
6. Tikiko, 3:12
7. Apolo, 3:13

VI. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Krete, 1:5
2. Nikopoli, 3:12

VII. MASWALI YA MJADALA

1. Kwa nini ni muhimu sana kwamba wote Mungu Baba na Yesu Mwana wanaitwa “Mwokozi” (3 mara tatu kila mtu) katika Tito?
2. Ni kwa namna gani 1:16 inahusiana na walimu wa uongo?
3. Je! 2:1-5 inawarejelea sana viongozi wa kanisa au washirika wa kanisa?
4. Kwa nini 2:11 ni mstari wa muhimu sana?
5. Je! 2:13 inamwita Yesu Mungu?
6. Kwa nini 3:5a ndiyo dhamira kuu ya Paulo?
7. Je! 3:5b inafundisha nini juu ya ubatizo wa kuzaliwa upya?

UTANGULIZI WA FILEMONI

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Kitabu hiki ni mfano wa barua binafsi, hivyo katika karne ya kwanza lilizoeleka katika dunia Uyunani-Rumi. Inawezekana kufaa katika moja ya karatasi za mafujo (kama vile. III Yohana). Inatia mashaka kwa nani alielezewa awali: (1) Filemoni; (2) Afia na Arkipo (kama vile Kol. 4:17) au (3) au katika maana nyingine, kwa kanisa zima.
- B. Barua hii inatoa mwanga kwa
 - 1. mbinu za kichungaji za mtume Paulo
 - 2. makanisa ya nyumbani ya karne ya kwanza (kama vile. Rum. 16:5; I Kor. 10:19; Kol. 4:15)
- C. Ukristo tayari ulikuwa na msingi wa kubadili jamii inayoizunguka ulimwengu wa kimediterania. Vizuizi vya kijamii vya kuizuia injili vilikuwa vimeshindwa (kama vile. I Kor. 12:13; Gal. 3:28; Kol. 3:11).

II. MWANDISHI

- A. Asili binafsi ya nyaraka inathibitisha kwa wasomaji wengi (isipokuwa mmoja, F. C. Baur) kwamba mwandishi alikuwa Paulo, mtume.
- B. Kitabu cha Filemoni na Wakolosai vinasimuliana kwa ukaribu
 - 1. Asili ile ile
 - 2. baadhi ya watu wakitoa salamu
 - 3. Ukaribu ule ule
 - 4. Tikiko alipeleka barua ya Wakolosai na kusafiri na Onesimo (kama vile. Kol. 4:7,9). Ikiwa Filemoni ni nyaraka yenye tabia za kuandikwa na Paulo, hivyo na Wakolosai (ambacho kilitiliwa mashaka na wanazuoni kadhaa wa kisasa).
- C. inaorodhesha kati ya barua za Paulo na maelezo ya awali ya Marcion (aliyekuja Rumi katika mwaka wa 140 B.K) na orodha ya vitabu vilivyowakfishwa, kipande cha Muratorian (kilichoandikwa Rumi kati ya mwaka 180-200 B.K).

III. TAREHE

- A. Tarehe ya barua hii inahusiana na moja ya vifungo vya Paulo (Efeso, Filipi, Kaisaria, au Rumi). Kifungo cha Rumi kinafaa ukweli wa matendo bora zaidi.
- B. Tangu Rumi ilipo thibitishwa kuwa sehemu ya kifungo, swali linaibuka —ni wakati upi? Paulo alikuwa gerezani mwanzoni mwa miaka ya 60's na hili limweandikwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Hata hivyo, aliachiliwa na aliandika nyaraka za kichungaji (I na II Timotheo na Tito) na alikamatwa tena na kuuwawa kabla ya tarehe 9 mwezi wa sita, 68 B.K.(kujiua kwa Nero). Wasomi wabobevu wanakisia maandiko ya Wakolosai, Waefeso, na Filemoni yalikuwa ya kifungo cha awali cha Paulo, mwanzoni mwa miaka ya 60. Wafilipi inawezekana kiliandikwa katikati ya miaka ya 60.
- C. Tikiko, pamoja na Onesimo, inawezekana walichukua barua za Wakolosai, Waefeso, na Filemoni kwenda Asia ndogo. Baadae (inawezekana miaka kadhaa baadae) Epafrodito, alipona kutokana na ugonjwa wa kimwili, alichukua barua ya Wafilipi na kuirudisha katika kanisa lake la nyumbani.
- D. Inawezekana mtiririko wa maandiko ya Paulo unafuata F .F. Bruce na Murray Harris (na marekebisho kidogo).

Kitabu

Tarehe

Sehemu ya Kuandikwa

Uhusiano na Matendo ya mitume

1. Wagalatia	48	Shamu Antiokia	14:28; 15:2
2. I Wathesalonike	50	Korintho	18:5
3. II Wathesalonike	50	Korintho	
4. I Wakorintho	55	Efeso	19:20
5. II Wakorintho	56	Makedonia	20:2
6. Warumi	57	Korintho	20:3
7.- 10. Nyaraka za kifungoni			
Wakolosa	mwanzoni 60	Rumi	
Waefeso	mwanzoni 60	Rumi	
Filemoni	mwanzoni 60	Rumi	
Wafilipi	mwishoni 62-63	Rumi	28:30-31
11. -13. Safari ya nne ya umisionari			
I Timotheo	63 (au baadae,	Makedonia	
Tito	63 lakini kabla	Efeso (?)	
II Timotheo	64/68 B.K.)	Rumi	

IV. MUDA KWA AJILI YA BARUA (watu waliotajwa katika Filemoni)

- A. Filemoni alikuwa mtumwa katika Kolosai. Yeye alimwamini Paulo, inawezekana wakati Paulo akihudumu katika Efeso.
- B. Onesimo alikuwa mtumwa aliyetoroka. Yeye pia alimwamini Paulo, alipokuwa katika kifungo huko Rumi (61-63 B.K). inatia shaka ni kwa namna gani walikutana. Labda (1) wote walikuwa kifungoni, (2) Onesimo alikuwa ametumwa katika jukumu kwa Paulo au (3) Onesimo alimtafuta Paulo kwa ajili ya ushauri baada ya kubadili fikra yake juu ya kukimbilia mbali.
- C. Epafra alikuwa mwamini wa kutoka Asia ndogo na mwanzilishi wa makanisa katika bonde la mto Lycus,(Kolosai, Laodikia na Hierapoli). Alileta neno kwa Paulo kifungoni juu ya maoni katika Wakolosai na juu ya uaminifu wa Filemoni.
- D. Tikiko alikuwa mbebaji wa barua tatu za Paulo hadi katika eneo hili: Wakolosai, Waefeso, na Filemoni (kama vile. Kol. 4:7-9; Efe. 6:21-22). Onesimo pia alirudi nae ili kukutana na bwana wake (kama vile mstr. 11). Filemoni ni mojawapo ya barua mbili binafsi zilizohifadhiwa katika Agano Jipya (kama vile III Yohana). Yapata miaka hamsini baadae (110 B.K.) Ignatius, akiwa njiani kwenda Rumi ili awe shahidi, aliandika barua (“kwa Waefeso” 1:3) kwa Askofu wa Efeso aliyemitwa Onesimo! Hii inaweza kuwa mtumwa aliyeamini!

V. KUSUDI LA BARUA

- A. Ni kuonyesha ni namna gani Paulo alitumia mamlaka yake ya kitume na utiaji moyo wa kichungaji.
- B. Ni kuonyesha namna gani Ukristo umewafanya kaka na dada kuwa nje ya utumwa na wamiliki wa watumwa, matajiri na maskini! Ukweli huu unaweza, katika muda, kubadilisha kabla ya utawala wa Rumi.
- C. Ni kuonyesha imani ya Paulo kwamba ataachiliwa kutoka kifungoni Rumi na kurudi Asia ndogo.

VI. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. “kanisa lililo katika nyumba yako,” mstr. 2
2. mtoto wangu, Onesimo, mstr. 10
3. hakufai. . .akufaa, mstr. 11
4. “sikuambii kwamba nakuwia hata nafsi yako,” mstr. 19

VII. WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. Afia, mstr. 2
2. Onesimo, mstr. 10
3. Epafra, mstr. 23
4. Marko, mstr. 24

VIII. MAENEO YALIYOONYESHA KATIKA RAMANI — HAKUNA

IX. MASWALI YA MJADALA

1. Ni kwa namna gani Paulo alitetea mamlaka yake ya kitume katika 1:8?
2. Ni kwa namna gani kitabu hiki kidogo kinalivunja jambo la utumwa?
3. Je mstari wa 18 unadokeza kwamba Onesimo aliiba kutoka kwa bwana wake?
4. Je mstari wa 19 unadokeza kwamba Paulo kwa ujumla alitumia mwandishi?

UTANGULIZI WA WAEBRANIA

I. MAELEZO MUHIMU YA UFUNGUZI

Kadiri nilivyokisoma kitabu hiki kimekuwa dhahiri zaidi na zaidi kwamba thiolojia yangu imechongwa na Paulo. Ni ngumu sana kwangu kuruhusu uwingi wa waandishi wengine wa Agano Jipya kuwasilisha mawazo yao yaliyovuviwa kwasababu napenda kuwaweka katika vipengele vya ufanano wa Paulo. Hii hasa iko wazi katika makazo wa Waebrania katika kuendelea katika imani. Katika kitabu cha Waebrania imani nio nafasi ya kisheria (kuhesabiwa haki kwa imani), bali maisha ya uaminifumapaka mwisho (sura za 11-12).

Nasita kwamba maswali mengi ninayokabiliana nayo ndani ya Waebrania yangewezwa kuwa yameulizwa na mwandishi wake (sio Petro wala Yakobo). Waebrania ni nyaraka ya kimazingira, kama vitabu vingine katika Agano Jipya. Natakiwa nimruhusu mwandishi azungumze ahata kama hatanipa raha; hata pale hatumii vipengele vyangu au hata ahapiliza na kuharibu vipengele vyangu. Nathubutu kuweka mbadala wa thiolojia yangu ya kimfumo kwa ajili ya ujumbe uliovuviwa wa mwandishi wa Agano Jipya.

Napendelea kutubia mifano yangu ya kithiolojia na kuishi ndani ya mvutano wa Agano Jipya ambao siuelewi kikamilifu au kuupenda! Nasita kutazama Agano Jipya kupitia chujio la vipimo vya injili ya kisasa yenye uongofu. Nataka kukiri ahadi za kibiblia; ahadi za upendo wa Mungu, utoshelevu na nguvu itunzayo; japo nashawishika na maonyo yenye nguvu na mamlaka ya waandishi wa Agano Jipya. Natamani kwa nguvu sana kusikia Waebrania, lakini ina maumivu sana! Nataka kuelezea na kuondoa mivutano. Nadhani kiuhalisia nataka kukiri wokovu kuwa bure na maisha ya Mkristo yenye kugarimu kila kitu. Lakini wapi ninapopigia mstari wakati kigezo hakikutimizwa? Je kuna ushirika wa milele wa Mungu katika imani ya kuanza au mwitikio wa imani inayoendelea? Waebrania kidhahiri inataja mamlaka ya mwitikio wa imani inayoendelea. Maisha ya Kikristo yanaangaliwa kwa namna ya kumaliza sio mwanzo!

Hii haikusudiwi kuthibitisha kumaanisha wokovu unaotegemea matendo. Imani ni ushahidi na sio mpango (ambao ni neema). Waaminio hawaokolewi kwa matendo bali ndani ya matendo. Matendo sio namna ya kufikia wokovu bali matokeo ya wokovu. Kule kufanana na Kristo kwa kimungu kwa kila siku kunakofanywa kwa uaminifu sio jambo fulani tunalofanya bali ni namna tulivyo sisi ndani yake. Kama hakuna mabadiliko na kubadilika na maisha ya imani, hakuna ushahidi, wala usalama. Ni Mungu tu anayejua moyo na mazingira. Dhamana haimaanishi kuwa kisindikizi cha maisha ya imani bali ushahidi wa kuanzia wa kithiolojia wa mtindo wa maisha yenye uhitaji.

Maombi yangu ni kwamba tutaruhusu mwandishi huyu aliyevuviwa kuzungumza kidhahiri na sio kupunguza Waebrania kuwa tanbihi ya kithiolojia kwa vipimo vya mfumo wa kithiolojia, ikiwa ni wafuasi wa Calvin au wa-Arminian.

II. TAMBUZI ZA UFUNGUZI

A. Kitabu hiki kinatumia maandiko ya Agano la Kale kwa wafasiri wa kiyahudi kuzungumza ujumbe wake. Ili kuweza kuelewa kusudio la asili la mwandishi, kitabu hiki lazima kifasiriwe kwa ufahamu wa Dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza, sio wazo la kisasa la kimagharibi.

B. Kitabu hiki kinaanza kama Mahubiri (hakina salamuwala ufunguzi uliozoeleka wa salamu) na kinaishia kama barua (kwa kufuata ufungaji kama wa Paulo wa sura ya 13). Inawezekana mahubiri ya kisinagogi yalibadilishwa kuwa katika barua. Mwandishi anaita kitabu chake “neni la maonyo” katika 13:22. Tungo hii pia inatumika katika Matendo ya Mitume 13:15 katika mahubiri.

C. Fasiri hii ni yenye maarifa ya Agano Jipya juu ya agano la Musa:

1. mtazamo wa kimamlaka wa Agano la Kale
2. ulinganifu wa maagano ya kale na jipya
3. Kitabu pekee cha Agano Jipya ambacho kinamuita Yesu kuhani wetu mkuu

- D. Kitabu hiki kimejaa maonyo ya kuwa waangalifu kutoanguka (“kurudi nyuma” kama vile 10:38), au kurudi katika Dini ya Kiyahudi (yaani sura za 2,4,5,6,10,12; kama vile *No Easy Salvation* cha R. C. Glaze, Jr., kilichochapishwa na Insight Press).
- E. Ingawa ni ujumuishwaji uliopitiliza, kinasaidia kumuona Paulo na msisitizo wake juu ya wokovu kama kazi iliyokwisha kumalizika na Mungu mwenye mamlaka yote (yaani kuhesabiwa haki kwa imani) kuelezea usalama kama kweli ya kwanza. Petro, Yakobo na Barua ya 1 na 2 Yohana inasisitiza majukumu yanayoendelea ya Agano Jipya na kuelezea kwamba usalama ni wa kila siku ukithibitishwa na maisha yaliyobadilika na yanayobadilika. Mwandishi wa Waebrania, akisisitiza maisha ya uaminifu (kama vile sura ya 11), anaelezea usalama kutoka katika mtazamo wa maisha yaliyokwisha kukamilika. Mawazo ya kawaida ya kisasa ya kimagharibi yanajaribu kudhoofisha mitazamo hii wakati waandishi wa Agano Jipya kwa mwandishi mmoja wa kimungu (yaani Roho), anataka awashikilie na kuthibitisha yote matatu. Dhamana haijawahi kuwa lengo bali matokeo ya imani itendayo kazi katika ahadi za Mungu.

III. UANDISHI

- A. Ingawa uandishi wa Waebrania uko katika mabishano, kazi za mwanzoni kabisa za Walimu wenye ujuzi (yaani Injili ya Kweli, Injili ya Philipo na Injili ya Yohana) zinawanukuu mara kadhaa ambacho kinaonesha kuwa ilichukuliwa kuwa upande wa maandiko ya Kikristo yenye mamlaka na karne ya pili (kama vile kazi ya Andrea Helmbold iitwayo *The Nag Hammadi Gnostic Texts and the Bible*, kur. 91).
- B. Kanisa la Mashariki (Iskandria na Misri) lilikubali uandishi wa Paulo kama inavyoonekana kwa kutajwa katika orodha yake ya Waebrania katika maandiko ya Paulo mwanzoni mwa maandiko ya mwanzo ya kimafunjo ya P⁴⁶. Maandiko haya yanaitwa Chester Beatty na yalinukuliwa mwishoni mwa karne ya pili. Yanakiweka Waebrania baada ya Warumi. Baadhi ya viongozi wa kiiskaria walitambua matatizo ya kifasihi yanayohusiana na uandishi wa Paulo.
1. Clement wa Iskandria (150-215 B.K., akinukuliwa na Eusebius) anasema kwamba Paulo alikiandika katika Kiebrania na Luka akakitafsiri katika Kiyunani.
 2. Origen (185-253 B.K.) alisema kwamba mawazo ni ya Paulo lakini kiliandikwa baadaye na mfuasi kama Luka au Clement wa Rumi.
- C. Kitabu hiki kimeondolewa katika orodha ya nyaraka za Paulo zilizoasilishwa na Kanisa la Magharibi iitwayo Muratorian Fragment (orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutokea Rumi mnamo mwaka 180-200 B.K.).
- D. Tunafanyaje kuhusu mwandishi
1. Alikuwa anavyoonekana Mkristo Myaahudi wa karne ya pili (2:3).
 2. Ananukuu kutoka fasiri ya Kiyunani ya Agano la Kale iitwalo Septuagint (Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani kutoka Kiebrania).
 3. Anatomia taratibu za hema la kukutania na sio taratibu za kisasa za hekalu.
 4. Anaandika kwa kutumia sarufi ya Kiyunani na sintaksia (kitabu hiki si cha kirafiki. Mlalo wake ni wa Agano la Kale, sio wa kifalsafa).
- E. Kitabu hiki hakina jina lakini mwandishi wake alikuwa akijulikana sana kwa wapokeaji wake (kama vile 6:9-10; 10:34; 13:7,9).

- F. Kwanini kuna mashaka kuhusu uandishi wa Paulo
1. staili yake ni tofauti sana (isipokuwa sura ya 13) kutoka katika maandiko mengine ya Paulo.
 2. misamiati ni tofauti sana.
 3. Kuna tofauti za wazi katika maneno na matumizi ya vifungu na msisitizo.
 4. Wakati Paulo anawaita rafiki zake na watenda kazi wenzake “ndugu” jina la mtu linakuja kwanza (kama vile Rum. 16:23; I Kor. 1:1; 16:12; II Kor. 1:1; 2:13; Flp. 2:25) lakini 13:23 ina “ndugu yetu Timotheo.”
- G. Nadharia za uandishi
1. Clement wa Iskandria katika kitabu chake *Hypotyposes* (kilichonukuliwa na Eusebius) aliamini kwamba Luka kilifasiriwa katika Kiyunani kutoka katika tafsiri ya Paulo ya asili ya Kiebrania (Luka alitumia bora ya Kiyunani).
 2. Origen alisema aidha Luka au Clement wa Rumi alikiandika lakini kikifuatiwa na mafundisho ya Paulo.
 3. Jerome na Augustine walikubali uandishi wa Pulo tu kusaidia kukubaliwa kwa kitabu katika uidhinishwaji kulikokuwa kunafanywa na kanisa la Magharibi.
 4. Tertullian (De Pudic. 20) aliamini Barnaba (Mlawi aliyekuwa mshirika mwenza wa Paulo) wote itkuwa ndiye aliyekiandika.
 5. Martin Luther alisema Apollo, msomi mwenye akili na mafunzo atokaye Iskandria aliyekuwa na ukaribu na Paulo (kama vile Mdo. 18:24), ndiye aliyekiandika.
 6. Calvin alisema Clement wa Rumi (cha kwanza kunukuliwa mnamo mwaka 96 B.K.) au Luka ndiye aliyekuwa mwandishi.
 7. Adolph von Harnack alisema Akila na Priscilla (walimfundisha Apolo injili kamili na walikuwa na mahusiano na Paulo na Timotheo, kama vile Mdo. 18:26) kuwa ndiye aliyekiandika.
 8. Sir William Ramsey alisema kwamba Philipo (mwinjilisti) alikiandika kwa ajili ya Paulo wakati akiwa gerezani.
 9. Wengine wameeleza Filipo na Sila (Silvano)

IV. WAPOKEAJI

- A. Jina “kwa Waebrania” inaweka wazi kuwa kimeandikwa kwa ajili ya watu Waebrania, hivyo kitabu kiliandikwa kwa Wayahudi wote (kama vile Clement wa Iskandria, akinukuliwa na Eusebius, Eccl. Hist.VI, 14).
- B. Ushahidi wa ndani ukifuatiwa na R. C. Glaze, Jr.’s *No Easy Salvation* nasema kwamba kundi Fulani la Wayahudi wanaoamini au sinagogi wanazungumzwa (kama vile 6:10; 10:32-34; 12:4; 13:7,19,23).
1. Wanaonekana kuwa waaminio wa Kiyahudi kwasababu ya nukuu kadhaa za Agano la Kale na Mada (kama vile 3:1; 4:14-16; 6:9; 10:34; 13:1-25).
 2. Walikuwa wamepitia mateso kadhaa (kama vile 10:32; 12:4). Dini ya Kiyahudi ilichukuliwa kama dini ya kisheria inayotambuliwa na mamlaka za Kirumi wakati baadaye Ukristo ulichukuliwa kama kinyume na sheria wakati ilipotengana na kuabudu katika sinagogi.
 3. Walikuwa wameshakuwa waaminio wa muda mrefu lakini walikuwa bado wachanga (kama vile 5:11-14). Walikuwa na hofu kubwa kujitenga na Dini ya Kiyahudi (kama vile 6:1-2).
- C. Maandiko tata ya 13:24 yangemaanisha kwamba kiliandikwa (1) kutokea Italia au (2) kwenda Italia, yawezekana Rumi.
- D. Mahali pa wapokeaji kunaunganishwa na nadharia tofauti juu ya waandishi.
1. Iskandria - Apollo
 2. Antiokia - Barnaba

3. Kaisaria - Luka au Philipo
4. Rumi - Clement wa Rumi na kutajwa kwa Italia katika 13:24.
5. Uhispania - Hii ilikuwa nadharia ya Nicolas wa Lyra (1270-1340 B.K.)

V. TAREHE

- A. Kabla tu ya uharibifu wa Yerusalemu uliofanywa na kamanda wa Kirumil (baadaye Mfalme) Tito, mnamo mwaka 70 B.K.
 1. mwandishi anamtaja mwenza wa Paulo, Timotheo kwa Jina (kama vile 13:23)
 2. maandishi anarejerea sadaka zinazoendelea (kama vile 8:13; 10:1-2) katika Hekalu
 3. mwandishi anataja mateso ambayo yanaweza kuendana na siku za Nero (54-68 B.K.)
 4. mwandishi anatia moyo wasomaji kutorudi katika dini ya Kiyahudi na ibada zake
- B. Baada ya mnamo mwaka 70 B.K.
 1. mwandishi anaonekana kutumia taratibu za hema la kukutanikia, na wala sio hekalu la Herode
 2. mwandishi anataja mateso
 - a. yawezekana chini ya Nero (kama vile 10:32-34)
 - b. baadaye yawezekana chini ya Domitian (kama vile 12:4-13)
 3. kitabu kinaweza kuhusiana na uamsho wa Dini ya Kiyahudi ya walimu (maandiko kutoka Jamnia) baadaye katika karne ya kwanza
- C. Kabla ya mnamo mwaka 95 B.K. kwasababu kitabu kinanukuliwa na Clement wa Rumi

VI. MAKUSUDI

- A. Wayahudi Wakristo wanahamasishwa kuacha sinagogi mna kujichanganya na watu wa jumla (kikamilifu) pamoja na kanisa (kama vile 13:13).
- B. Wakristo Wayahudi wanahamasishwa kuchukua jukumu la kimisheni la kiinjili (kama vile Mt. 28:19-20; Mdo. 1:8).
- C. Wayahudi wasioamini katika ushirika na wakristo hawa Wayahudi ni shabaha ya sura ya 6 na 10. Tazama uwepo wa makundi matatu, “ninyi,” “sisi,” na “wao.” Wanaonywa kibinafsi kuitikia kwenye utele na ushahidi ulio wazi katika maisha ya Wakristo wenzao marafiki na wanaoabudu nao.
- D. Matengenezo haya ya kihistoria yanachukuliwa *kutoka No Easy Salvation* cha R. C. Glaze, Jr. “Tatizo halikuwa kwamba mvutano kati ya Wakristo walio wengi na wasio wakristo walio wachache. Kinyume chake kabisa ni kweli. Wakristo Wakiyahudi wa kusanyiko hili walikuwa wamechakachua imani yao sana na na namna ya uwakili kwamba makundi mawili yangeabudu kwa pamoja kama kusanyiko moja. Hakuna kundi ambalo kwa sana liliweza kusumbua linguine kidhamiri. Hakukuwa tena na malumbano na mahubiri ya kundi moja la Kikristo kusababisha ushawishi na maamuzi upande wa washirika wasiookolewa wa Sinagogi. Wakristo walikuwa katika hali ya kimkwamo kwasababu ya kukosa kwao utayari kukubali mahitaji kamili ya kuishi kwa ujasiri maisha ya ukristo. Wasioamini walikuwa wamefanywa wagumu wa mioyo kwa mwendelezo mpaka kufikia hatua ya utofauti wa asilimia zote. Makundi haya yalikuwa yamekuwa yana ushirikiano na waliorudi nyuma wasiosali. Kutokuwa tayari kwa kundi la Kikristo ‘kwenda katika ukamilifu’ (6:1) kulisababishwa na mambo mawili: kushikilia sana desturi za Dini ya Kiyahudi na kukosekana kwa utayari wa kulipa gharama ya utambulisho kamili pamoja na Ukristo” (ukur. 23).

VII. AINISHO FUPI LA WAEBRANIA

- | | |
|----------|------------------------------|
| 1:1-3 | Ukuu wa Mwana juu ya manabii |
| 1:4-2:18 | Ukuu wa Mwana juu ya malaika |

3:1-4:13	Ukuu wa Mwana juu ya Sheria ya Musa
4:14-5:10; 6:13-7:28	Ukuu wa Mwana juu ya Ukuhani wa Haruni
5:11-6:12	Ukuu wa Wayahudi waaminio juu ya Wayahudi wasioamini
8:1-10:18	Ukuu wa Mwana juu ya taratibu za Agano la Musa
10:19-13:25	Ukuu wa Mwana unaochagizwa na kufunuliwa katika waamini

VIII. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "katika siku hizi za mwisho," 1:2
2. "mg'ao wa utukufu Wake," 1:3
3. "uwakilishi hasa wa asili yake," 1:3
4. Mfalme, 1:3
5. "ili kwamba tusitoke mbali nayo," 2:1
6. "neni linalozungumzwa kupitia malaika," 2:2
7. "aonje kifo kwa ajili ya kila mmoja," 2:9
8. "mwandishi mkamilifu wa wokovu," 2:10
9. "kuhani mkuu," 2:17; 4:15
10. upatanishi, 2:17
11. Mtume, 3:1
12. Kuhani Mkuu, 3:1
13. ukiri, 3:1; 4:14
14. leo, 3:13
15. "siku ya saba," 4:4
16. "pumziko la Sabato," 4:9
17. "akipita katika mbingu," 4:14
18. "bado bila dhambi," 4:15
19. "tujongee karibu," 4:16
20. "mafundisho ya kwanza," 5:12
21. kuoshwa, 6:2
22. "ahadi," 6:15
23. "pazia," 6:19
24. "Yesu amekuwa dhamana ya agano lililo bora," 7:22
25. upatanishi, 7:25
26. hema, 8:2
27. "nakala na kivuli cha vitu vya mbinguni," 8:5
28. "agano jipya bora," 8:8,13
29. "Patakatifu pa patakatifu," 9:3
30. fimbo ya Haruni, 9:4
31. kiti cha rehema, 9:5
32. "kundi kubwa la mashuhuda," 12:1
33. "shina la uchungu," 12:15
34. "Yerusalemu wa mbinguni," 12:22

IX. WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHTASARI

1. "mzaliwa wa kwanza," 1:6
2. "yeye aliyekuwa na nguvu juu ya mauti," 2:14
3. "aliyepambana nae," 3:16
4. Melkizedeki, 5:6
5. Kuna makundi matatu yanayotajwa katika 5:11-6:8: "ninyi," "wale," na "sisi." Je kila moja inamrejerea nani?
6. Kerubi, 9:5
7. Henoko, 11:5

8. Rahabu, 11:31
 9. "Mchungaji mkuu," 13:20
 10. Timotheo, 13:23
- X. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI
1. Salemu, 7:1
 2. Yeriko, 11:30
 3. Mlima Sayuni, 12:22
 4. Italia, 13:24
- XI. MASWALI YA MJADALA
1. Orodhesha vipengele vya "mwana" vinavyotajwa katika 1:2-4
 2. Kwanini malaika wanatajwa sana mwanzoni mwa sura za Waebrania?
 3. Ni kwa namna gani malaika wanahusiana na waaminio? (1:14)
 4. Ni kwa namna gani Yesu alifanywa chini kidogo kuliko malaika? (2:9)
 5. Ni kweli kuu gani ya 2:18; 4:15?
 6. Musa na Yesu wanalinganishwaje katika 3:1-6?
 7. Nini kinamaanishwa katika 3:7 kuhusu Roho?
 8. Ni nini 3:12 inazungumzia?
 9. Ni nini kinamaanishwa katika 3:11, "hawataingia rahani mwangu"?
 10. Ni nini kinasemwa katika 3:14 kuhusu dhamana ya Mkristo?
 11. Elezea 4:12 kwa maneno yako mwenyewe.
 12. Kwanini mwandishi wetu analeta habari ya kuhani wa Kikanaani wa kale? (5:6-10)
 13. Elezea umuhimu wa 5:8-9.
 14. Orodhesha mafundisho katika 6:1-2. Je ni Wayahudi au Wakristo? Kwanini?
 15. Kwanini neno "lisilowezekana" katika 6:6 linapinga wale wote wanaoamini unaweza kuokolewa, ukapotea na ukaokolewa?
 16. Kwanini Melkizedeki anasadikiwa kutokuwa na baba na mama? (7:3)
 17. Kwanini Ibrahimu kulipia Zaka kwa Melkizedeki muhimu sana? (7:4-10)
 18. Je 8:13 na 10:4 inamaanisha nini kuhusu Agano la Kale?
 19. Ni kwa namna gani 9:22 inapinga dini ya Hindu?
 20. Ni kwa namna gani 10:25 na 39 inahusiana na mazingira ya kihistoria?
 21. Ni kwa namna gani sura ya 6 inahusiana na sura 10?
 22. Weka kwa kifupi sura ya 11 kwa maneno yako mwenyewe.
 23. Ni kwa nani 12:2 inarejerea?
 24. Kwanini 13:8 ni muhimu sana?

UTANGULIZI WA YAKOBO

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Hiki kilikuwa kitabu pendwa zaidi cha Soren Kierkegaard katika Agano Jipya kwasababu kilisitiza Ukristo wa matendo wa kila siku.
- B. Hiki kilikuwa kitabu kisicho na mashiko zaidi kwa Martin Luther katika Agano Jipya kwasababu inaonekana kukinzana na kauli ya msisitizo ya Paulo ya “kuhesabiwa haki kwa imani” katika Warumi na Wagalatia.
- C. Hiki ni kitabu cha aina yake tofauti na vitabu vingine vya Agano Jipya
 1. ni kama zaidi ya kitabu kipya cha agano cha Mithali (yaani, fasihi ya hekima) ikizungumzwa na nabii mkali
 2. kiliandikwa mapema baada ya kifo cha Yesu na bado cha Kiyahudi na chenye mwongozo wa kuweka katika matendo

II. MWANDISHI

- A. Mwandishi wa kidesturi ni Yakobo (Kiebrania, “Yakobo”), ndugu asiye wa kuzaliwa tumbo moja wa Yesu (moja kati ya wanne, kama vile Mt.13:55; Marko 6:3; Mdo. 1:14; 12:17; Gal. 1:19). Alikuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu (48-62 B.K, kama vile Mdo. 15:13-21; Gal. 2:9).
 1. Alikuwa akiitwa “Yakobo mwenye haki na baadaye alipewa jina la utani la “magoti ya ngamia” kwasababu kwa mwendelezo aliomba kwa kupiga magoti (kutoka Hegesippus, akinukuliwa na Eusebius)
 2. Yakobo hakuwa mwamini (kama vile Marko 3:21; Yohana 7:5). Yesu alimtokea yeye mwenyewe mara baada ya Ufufuko (kama vile 1 Kor. 15:7).
 3. Alikuwepo katika chumba cha juu PAMOJA NA WANAFUNZI (kama vile Mdo. 1:14) pamoja na wanafunzi (kama vile Mdo. 1:14) na yumkini pia wakati Roho alipokuja katika siku ya Pentekoste.
 4. Alikuwa ameo (kama vile I Kor. 9:5).
 5. Anatajwa na Paulo kama nguzo (yaweze kana mtume, kama vile Mdo. Gal. 1:19) lakini hakuwa mmoja wa Kumi na mbili (kama vile Gal. 2:9; Mdo. 12:17; 15:13ff).
 6. katika *Antiquities of the Jews*, 20:9:1, Josephus anasema kwamba alipigwa mawe mnamo mwaka 62 B.K. kwa amri kutoka kwa Masadukayo wa Baraza la Sinagogi wakati desturi zingine (waandishi wa karne ya pili, Clement wa Iskandria au Hegesippus) anasema kwamba alisukumwa juu ya ukuta wa Hekalu.
 7. Kwa vizazi vingi baada ya kifo cha Yesu ndugu wa Yesu aliteuliwa kama kiongozi wa kanisa huko Yerusalemu.
- B. Katika *Studies in the Epistle of James*, A. T. Robertson anakiri uandishi wa Yakobo: “Kuna uthibitisho mwingi kwamba nyaraka iliandikwa na mwandishi wa kauli katika Mdo. 15:13-21—Ufanano wa kiumbali wa mawazo na aina ya uandishi inapishana kidogo kwa uigilizaji tu au unakili. Ufanano huo huo unatokea kati ya Nyaraka ya Yakobo na barua kwa Antiokia (Mdo. 15:23-29). Kuna pia udhahiri wa kumbu kumbu katika Mlima ambao Yakobo anaweza kuwa alisikia yeye mwenyewe au angalau kusikia juu yake. Kuna udhahiri huo huo wa taswira katika nyaraka ambayo ina ukuu wa tabia ya mafundisho ya Yesu” (ukur. 2).
A.T. Robertson hapa anafuatishia J. B. Mayor’s *The Epistle of St. James*, kur.. iii-iv.
- C. Kuna watu wengine wawili wanaoitwa kwa majina ya Yakobo katika mafungu ya kitume katika Agano Jipya. Hata hivyo Yakobo, ndugu wa Yohana aliuwawa mapema sana mnamo mwaka 44 B.K. na Herode Agrippa I (kama vile Mdo.12:1-2). Yakobo wengine, “the less (wadogo)” au “the

younger (wenye umri mdogo)” (kama vile Marko 15:40), hawatajwi nje ya orodha ya mitume. Mwandishi wa Nyaraka yetu alikuwa kidhahiri akijjulikana sana.

- D. Kumekuwepo na nadharia tatu juu ya mahusiano ya Yakobo na Yesu:
1. Jerome anasema kwamba alikuwa ni mpwa wa Yesu (na Alphaeus na Maria wa Klopas). Alipata hili kwa kulinganisha Mt. 27:56 na Yohana 19:25.
 2. Desturi za kanisa Katoliki zinaelezea kwamba alikuwa ndugu asiye wa damu kwa ndoa ya kwanza ya Yusufu (kama vile fasiri ya Origen Mt. 13:55 na Epiphanius katika Heresies, 78).
 3. Tertullian (160-220 B.K.), Helvidius (366-384 B.K) na Waprotestanti wengi zaidi wanaelezea kwamba alikuwa ndugu kabisa wa Yesu kwa uzao wa Yusufu (kama vile Marko 6:3; I Kor. 9:5).
 4. Mbadala #1 na #2 zilikuwa kulinda mafundisho ya Kanisa la kikatoliki juu ya ubikra wa Mariamu.

III. TAREHE

- A. ikiwa uandishi huo hapo juu utakubaliwa:
1. Mwanzoni kabla ya baraza la Yerusalemu (Mdo. 15) mnamo mwaka 49 B.K. (ikiwa tarehe hii ni ya kweli basi Yakobo ni kitabu cha mwanzoni kabisa kuzalishwa).
 2. Baadaye, mara kabla ya kifo cha Yakobo mnamo mwaka 62 B.K.
- B. Tarehe ya mwanzoni kabisa inaweza kutumika:
1. matumizi ya “Sinagogi” katika 2:2
 2. kukosekana kwa mpangilio wa kikanisa
 3. matumizi ya neno “mzee” katika namna ya Kiyahudi katika 5:14
 4. Hakuna kutajwa kwa mkanganyiko juu ya umisheni kwa Mataifa (kama vile Mdo. 15)
 5. Yakobo anaonekana kuandika kwa jamii za waaminio wa mwanzoni wa Kiyahudi mbali na Yerusalemu na yawezekana nje ya Palestina (kama vile 1:1)
- C. tarehe ya baadaye inapewa upendeleo:
1. mrejesho ule wa Yakobo (kama vile 2:14-20) kwa baru a ya Paulo kwa Warumi (kama vile 4:1ff), kuchukua mjongeo wa kinyume ili kusahihisha matumizi yasiyokuwa sawa yanayofanywa na walimu wa uongo (kama vile II Pet. 3:15-16). Ikiwa hii ni kweli, jina zuri la Yakobo ingekuwa “Usahihishaji wa mpito wa kati.”
 2. Kitabu kidhahiri klinadhania mafundiaho ya msingi ya Mkristo kwasababu ya kutokuwepo kwake kabisa kutoka katika kitabu.

IV. WAPOKEAJI

- A. Rejea kwa “makabila kumi na mbili yaliyotawanyika kote duniani” (1:1) ni dokezo letu kuu. Pia ujumuishi wa barua katika “nyaraka za katoliki” (yaani, barua zinazohutubia makanisa kadhaa) inaaksi asili yake ya ujumla. Kidhahiri moja ya kanisa si linalopewa uzito kama makundi kadhaa ya watu waliotawanyika na hawa wanaonekana kuwa Wakristo wa Kiyahudi nje ya Palestina.
- B. Kuna tafsiri tatu za tungo katika 1:1:
1. Wayahudi—Hii inaonekana kuwa na mashaka kwasababu ya kujiruadia rudia kwa matumizi ya “wapendwa,” kukosekana kwa kweli kuu za kiinjili juu ya Yesu pamoja na kutajwa kwa bayana kwa imani katika Kristo katika 2:1. Pia baada ya Uhamisho wa Babeli, makabila ya asili kumi na mbili hayakuwahi kurudi. Stiari hiyo hiyo inatumika kiuwakilishi wa waaminio katika Ufunuo 7:4-8.
 2. Wakristo wa kiyahudi—Hii inaonekana kuwezekana zaidi kwasababu ya ladha ya Kiyahudi ya kitabu na nafasi ya uongozi wa Yakobo katika kanisa la Yerusalemu.

3. Kanisa kama Israeli ya kiroho—Hii inawezekana kwasababu ya matumizi ya “ugeni” katika 1 Pet. 1:1 kama maelezo ya Paulo ya kanisa (Wayahudi waaminio na Mataifa) kama Israeli ya kiroho (kama vile Rum. 2:28-29; 4:16ff; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9).

V. KUTUKIA (MUDA) - kuna nadharia mbili:

- A. Jaribio la kutumia kibayana Agano Jipya kwa maisha ya Wakristo wa Kiyahudi wa karne ya kwanza.
- B. Baadhi wanaamini kwamba ilikuwa Wayahudi wenye fedha waliokuwa wakiwatesa Wayahudi wa Kikristo. Inawezekana kwamba Wakristo wa mwanzoni walikuwa chini yakutumiwa vibaya na kundi la kipagani. Ilikuwa ni dhahiri muda wa mahitaji ya kimwili na mateso (kama vile 1:2-4,12;2:6-7; 5:4-11,13-14).

VI. AINA YA UWASILISHAJI WA KIFASIHI

- A. Barua hii/mahubiri yanaaksi maarifa ya fasihi ya hekima, kote katika uidhinishwaji (Ayubu-Wimbo Uliobora) na kipindi cha Ukimya kati ya Agano Jipya na Agano la Kale (Ecclesiasticus mnamo mwaka 180 K.K.). Msisitizo wake ni mtindo wa kimaisha—imani katika matendo (kama vile 1:3-4).
- B. Kwa njia Fulani, mtindo nunafanana na vyote walimu wa hekima za Kiyahudi (kama wastoiki). Mifano baadhi ni:
1. mtindo wa wazi (kuruka kutoka mada moja na kwenda nyingine)
 2. kauli shurutishi nyingi (ziko 54)
 3. Ukosoaji (mpingaji ni kama mwenye kuuliza maswali, kama vile 2:18; 4:13). Hii pia inaonekana katika Malaki, Warumi na 1 Yohana.
- C. Ingawa kuna nukuu za moja kwa moja chache kutoka Agano la Kale (kama vile 1:11; 2:8,11,23; 4:6), kama kitabu cha Ufunuo, kuna maelezo mengi ya Agano la Kale.
- D. Muainisho wa Yakobo ni karibia mrefu kuliko kitabu chanyewe. Hii inaaksi mbini ya walimu wa Kiyahudi ya kuruka kutoka mada kwenda mada nyingine kwa ajili ya kutunza umakini wa hadhira. Walimu wa kiyahudi wanaita “lulu katika uzi/kamba.”
- E. Yakobo kinaonekana kuwa muunganiko wa aiana ya uwasilishaji wa kifasihi wa Aganao la Kale: (1) wazee (walimu wa hekima) na (2) manabii (kama kabisa Amosi au Yereimia). Anatumia kweli za Agano la Kale lakini anazosha katika mafundisho ya Yesu akiwa mlimani. (Angalia Sehemu B. chini ya maudhui hapa chini).

VII. MAUDHUI

- A. Yakobo anatumia maelezo ya maneno ya Yesu yanayopatikana katika Vitabu vya Injili zaidi kuliko kitabu chochote (yaani, 1:5,6,22; 2:5,8,13; 3:12,18; 4:10,12; 5:12). Hata inawezekana kwamba Yakobo inajumuisha nukuu kutoka kwa Yesu (kama vile 1:27; 2:13; 3:18; 4:11-12,17).

- B. Yakobo ni kiashiria na aksi ya Mahubiri ya Mlimani.

YAKOBO	MAHUBIRI YA MLIMANI
1:2	Mt. 5:1-2
1:4	Mt. 5:48
1:5	Mt. 7:7 (21:26)
1:12	Mt. 5:3-11
1:20	Mt. 5:22
1:22-25	Mt. 7:24-27
2:5	Mt. 5:3 (25:34)
2:8	Mt. 5:43; 7:12

2:13	Mt. 5:7 (6:14-15; 18:32-35)
3:6	Mt. 5:22,29,30
3:12	Mt. 7:16
3:18	Mt. 5:9; 7:16-17
4:4	Mt. 6:24
4:11-12	Mt. 7:1
4:13	Mt. 6:34
5:2	Mt. 6:19-20
5:10-11	Mt. 5:12
5:12	Mt. 5:34-37

C. Kinatumika katika Thiolojia (imani bila matendo imekufa). Kati ya mistari 108, 54 ni kauli shurutishi.

VIII. UIDHINISHWAJI

A. Ujumuiishi wa Yakobo ulikuja kwa kuchelewa na mgumu.

1. Yakobo hakikuwa katika orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutokea Rumi mpaka mnamo mwaka 200 B.K. ikiwa katika "Muratorian Fragment."
2. Hakikuwa katika orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutoka Afrika kaskazini, mnamo mwaka 360, iitwayo "Cheltenham List" (pia ikiitwa Karl Mommsen's catalog).
3. Hakijumuishwa katika toleo la zamani la Kilatini katika Agano Jipya.
4. Orodha ya Eusebius ni moja ya vitabu vipingwavyo (Waebrania, Yakobo, 2 Pet, 2 na 3 Yohana, Yuda na Ufunuo), Hist. Eccl.II:23:24-24; III:25:3.
5. Hakikupokelewa katika kanisa la Magharibi mpaka karne ya 4 na hakikunukuliwa katika kanisa la Mashariki mapaka mapitio ya fasiri za kishamu ya karne ya 5 iitwayo Peshitta.
6. Kilikataliwa na Theodore wa Mopsuetia (392-428 B.K.), kiongozi wa shule ya Antiokia ya ufasiri wa Biblia (Alikataa nyaraka zote za kikatoliki).
7. Erasmus alikuwa na mashaka juu yake, kama ilivyokuwa kwa Martin Luther, aliyekiita "waraka mwepesi" kwasababu lihisi kilipingana na msisitizo wa Warumi na Wagalatia juu ya "uhesabiwaji haki kwa Imani."

B. Ushahidi wa upekee wa Yakobo:

1. Kilielezwa katika maandiko ya Clement wa Rumi (95 B.K.) na baadaye katika karne ya pili na Ignatius, Polycarp, Justin Martyr, na Irenaeus.
2. Kimetolewa maelezo katika maandiko ya Kikristo yasiyoidhinishwa lakini yenye umaarufu mkubwa yaitwayo *Shepherd of Hermas (Mchungaji wa Hermas)*, yaliyoandikwa mnamo mwaka 130 B.K..
3. Kilinukuliwa moja kwa moja na Origen (185-245 B.K.) katika fasiri yake juu ya Yohana, XIX:23.
4. Katika toleo lake liitwalo Hist. Eccl. 2:23, Eusebius alikiweka katika orodha katika "vitabu vipingwavyo," lakini akaongeza kwamba kilikuwa kikikubalika na makanisa mengi zaidi.
5. Kilijumuishwa katika fasiri ya Kishamu iliyopitiwa manamo mwaka 412 B.K. (iitwayo Peshitta).
6. Origen na John wa Dameski huko Mashariki na Jerome na Augustine katika Magharibi walichagiza ujumuishwaji wa kitabu hiki katika uidhinishwaji. Kilipokea hadhi ya uidhinishwaji katika Baraza la Hippo, mnamo mwaka 393 B.K., na Carthage, 397 B.K. na tena mnamo mwaka 419 B.K.
7. Kilikubaliwa na Chrysostom (345-407 B.K.) na Theodoret (393-457 B.K.), wote wakiwa viongozi wa shule ya ufasiri wa Biblia ya Antiokia.

IX. MAANA ZA MANENO NA TUNGO KWA MUHTASARI

1. "makabila kumi na mbili," 1:1
2. kutawanyika, 1:1

3. “kuizingatia,” 1:2
4. kuthibitisha, 1:12
5. taji la uzima, 1:12
6. “hakuna kubadilika badilika wala kivuli,” 1:17
7. “watendaji wa neno,” 1:22
8. sheria kamilifu, 1:25
9. “mapepo nayo huamini,” 2:19
10. “hukumu ya dhati,” 3:1
11. kuzimu, 3:6
12. “kuapa kwa mbingu au kwa nchi,” 5:12
13. upako, 5:14
14. “ungamanieni ninyi kwa ninyi,” 5:16

X. WATU WA KUWATAMBUA KWA MUHATASARI

1. “mtu wa kusitasita,” 1:8
2. “Baba wa mianga,” 1:17
3. Rahabu, 2:25
4. “Bwana wa Sabato,” 5:4
5. Ayubu, 5:11
6. wazee, 5:14
7. Eliya, 5:17

XI. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI — HAKUNA

XII. MASWALI YA MJADALA

1. Inawezekanaje 1:2 kuwa kweli?
2. Maombi yanawezaje kuzuliwa? (1:5-8; 4:1-5)
3. Ni kwa namna gani 1:9-11 inarudisha nyuma matazamio ya kikazi ya kimila?
4. Ni kwa nama gani 1:13 inalinganishwa na Mt. 6:13?
5. Ni kwa namna gani 1:22 ni maudhui ya kitabu?
6. Je 2:1-7 inazungumzia mazingira ya kuabudu au mazingira ya suluhu za upatanishaji za kanisani? Kwanini?
7. Ni tukio gani la maisha ya Mkristo 2:7 inarejea?
8. Kwanini 2:10 ni kweli ya muhimu?
9. Kwanini 2:17 imesabisha mgogoro mkubwa sana katika kanisa? (kama vile 2:20)
10. Ni kwa namna gani Paulo na Yakobo wanamtumia Ibrahimu kama mfano lakini katika namana tofauti? (2:18-26)
11. Elezea hoja ya 3:1-5 kwa maneno yako mwenyewe.
12. Elezea tofauti kati ya hekima ya ulimwengu na hekima ya Mungu (3:15-17)
13. Kwanini 4:5 ni ngumu kufasiri?
14. Kwanini 5:1-6 ishangaze waaminio wa Kiyahudi?

UTANGULIZI WA 1 PETRO

I. UANDISHI

A. Ushahidi wa ndani juu ya uandishi wa Mtume Petro

1. kwa upekee huu ulianza 1:1
2. madokezo ya maneno na uzoefu wa maisha ya Yesu na wale Kumi na Wawili
 - a. mifano iliyochukuliwa kutoka kwa E. G. Selwyn's *The First Epistle of St. Peter*, 1946
 - (1) 1:3 - Yohana 21:27
 - (2) 1:7-9 - Luka 22:31; Marko 8:29
 - (3) 1:10-12 - Luka 24:25 na kuendelea; Matendo 15:14 na kuendelea
 - (4) 3:15 - Marko 14:29,71
 - (5) 5:2 - Yohana 21:15 na kuendelea
 - b. mifano iliyochukuliwa kutoka kwa Alan Stibbs' *The First Epistle General of Peter*, 1971
 - (1) 1:16 - Mt. 5:48
 - (2) 1:17 - Mt. 22:16
 - (3) 1:18 - Marko 10:45
 - (4) 1:22 - Yohana 15:12
 - (5) 2:4 - Mt. 21:42 na kuendelea
 - (6) 2:19 - Luka 6:32; Mt. 5:39
 - (7) 3:9 - Mt. 5:39
 - (8) 3:14 - Mt. 5:10
 - (9) 3:16 - Mt. 5:44; Luka 6:28;3:20 - Mt. 24:37-38
 - (10) 4:11 - Mt. 5:16
 - (11)4:13 - Mt. 5:10 na kuendelea
 - (12)4:18 - Mt. 24:22
 - (13)5:3 - Mt. 20:25
 - (14)5:7 - Mt. 6:25 na kuendelea
3. Maneno na vifungu vyenye kufanana na mahubiri ya Petro yaliyo katika Matendo
 - a. 1:20 - Matendo 2:23
 - b. 2:7-8 - Matendo 4:10-11
 - c. 2:24 - Matendo 5:30; 10:39 (hasa, Matumizi ya neno la Kiyunani *xylon* na neno mti)
 - d. 4:5 - Matendo 10:45
4. ulinganifu wa sasa wa umisheni wa karne ya kwanza
 - a. Silwano (Sila) - 5:12
 - b. Marko (Yohana Marko) - 5:13

B. Ushahidi wa ndani juu ya uandishi wa Mtume Petro

1. ulikubaliwa na kanisa la mwanzo hapo awali na kwa mapana sana
 - a. uwekaji wa vifungu wenye kufanana, huenda nukuu, na Clement wa Rumi katika barua yake ya *Letter to Corinthians* (95 B.K.)
 - b. uwekaji wa vifungu wenye kufanana, huenda nukuu, katika *Epistle of Barnabas* (130 B.K.)
 - c. uliodokezwa na Papias, Askofu wa Hieropoli (140 B.K.) katika nukuu ya Eusebius' *His. Eccl.*
 - d. ulionukuliwa na Polycarp katika *Epistle to the Philippians* 8:1, lakini huu hautaji kitabu cha I Petro kwa jina (Polycarp alikufa mnamo mwaka 155 B.K.)
 - e. ulionukuliwa na Irenaeus (140-203 B.K.)
 - f. ulionukuliwa na (185-253 B.K.). Origen aliiamini hiyo I Pet. 5:13, ambapo Petro anamwita Marko "mwanangu" akimaanisha kwamba huyu aliiandika Injili ya Petro.
 - g. ulionukuliwa na Tertullian (150-222 B.K.)

C. Sababu za kijiuliza juu ya uandishi wa Mtume Petro

1. Hii haikuorodheshwa katika Muratorian Fragment, orodha ya vitabu vya kisheria vilivyounyanishwa huko Rumi kati ya mwaka 180 na 200 B.K.
2. Kiyunani ni kizuri, ni ki-Koine cha Kiyunani kilichong'aa, jambo linaloshangaza kutokana na mvuvi wa Kigalilaya ambaye "hakuwa na elimu" (*a grammatos*, kama vile Matendo 4:13)
3. hii inaleta maana sana kama yale maandishi ya Paulo humo Rumi na kwa Waefeso
4. fasili yake ya mateso inayofafanuliwa katika I Petro inaendana vema na tarehe inayofuatia
 - a. Domitian (81-96 B.K.)
 - b. Trajan (98-117 B.K.)

D. Majibu yakini kwa wanazuoni wa sasa

1. Kipande cha Muratorian kimeharibika na mstari upatao mmoja wa maandiko yake unakosekana (kama vile B. F. Westcott's *A General Survey of the History of the Canon of the New Testament*, toleo la 6. uk. 289).
2. Petro hakuwa na elimu (kama vile Matendo 4:13), bali alipewa mafunzo katika shule mojawapo ya Kiyahudi. Kwa uwazi kabisa Wayahudi wengi ndani ya Galilaya walizifahamu lugha mbilimbili tangu kuzaliwa. Suala kuu lingine katika mjadala huu ni Petro kumtumia mwandishi. Uwekaji wa maneno katika I Pet. 5:12 ni kudhani kwamba huyu alimtumia Silwano (Sila).
3. Wote Petro na Paulo waliinukuu liturjia au mambo ya kimafunzo mara kwa mara (nyaraka za katekisimu) ambayo yalikuwa ya kawaida katika kanisa la kale. Pia kila mmoja alikuwa na mawasiliano na mwingine mwaka mzima (yaani, Matendo, Gal. na II Pet. 3:15-16).
Kwangu mimi sababu dhahiri ya ufanano kati ya maandiko ya Petro na Paulo inaweza kuelezwa na Petro na matumizi ya wenza wa Paulo wa kimisheni Sila (Silwano) kama mwandishi.
4. I Petro si lazima iakisi mateso ya Dola nzima. Ukiri wa Petro kwa waamini kuhitaji kuitii serikali (kama vile 2:13-17) usingekuwa wa kawaida katika siku zile za mateso ya Dola nzima.
Kuongezaka kwa ugonjwa wa kiakili (54-68 B.K.) wa Nero (mf. Madai ya grandiose) kulihamasisha kuwepo kwa madhehebu ya jadi, hasa katika Asia Ndogo, kwa ajili ya kuanzisha mateso. I Petro inaendana na siku za Nero zaidi kuliko zile za Domitian (81-96 B.K.) au siku zile za Trajan (98-117 B.K.). Pia inawezekana kwamba sehemu ya mateso inatokana na makundi ya Kiyahudi pamoja na watawala wa serikali za jadi au madhehebu ya kifalme.

E. Hakuna lo lote katika I Petro yenyewe yenye kudai kipindi kinachofuatia au mwandishi.

II. TAREHE

- A. Kwa uwazi tarehe inahusiana na uandishi.
- B. Tamaduni zinaunganisha kifo cha Petro na Paulo humo Rumi chini ya Nero, huenda 65 B. K. Ikiwa ni hivyo, basi I Petro itakuwa iliandikwa mnamo mwaka 63-64 B.K.
- C. Katikati ya karne ya kwanza tarehe inawezekana ikiwa 1 Petro inadokezwa na Clement wa Rumi (95 B.K).
- D. A. T. Robertson anaamini kwamba Petro alikufa mnamo mwaka 67-68 B.K. na kuandika 1 Petro mwaka 65-66 B.K. Nafikiri huyu alikufa mnamo mwaka 64-65 B.K na aliandika kabla ya hili.

III. WAPOKEAJI

- A. Tabia ya barua za karne ya kwanza, wapokeaji wanaelezwa katika 1:1 kama "wale walioishi kama wageni waliojitenga katika Pontus, Galatia, Cappadocia, Asia, na Bithynia zima." Haya majimbo ya Kirumi (ikifikiriwa kuwa Galatia ni tamaduni za Galatia kaskazini) yako katika Uturuki ya sasa ya kaskazini. Kwa uwazi maeneo haya yanatambua kuwa Paulo hakuinjilisha (kama vile Matendo 16:6) ama Petro (kama vile 1:12). Huenda haya makanisa yalitokana na Wayahudi walioongoka waliorudi nyumbani baada ya siku ya Pentekoste (kama vile Matendo 2:9-11).

- B. Ingawa makanisa haya yameanzishwa na waamini wa Kiyahudi kwa asili yake wakati wa uandishi wa Petro, mengi yalikuwa ya watu wa Mataifa
1. watoto wa kutii (1:14)
 2. mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu (1:18)
 3. sasa ni taifa la Mungu (2:9-10, ombi kwa Hosea 1:9-10; 2:23)
 4. kati ya Mataifa (2:12)
 5. kutenda mapenzi ya Mataifa (4:3-4)
- C. Kitabu hiki hakikuhusisha misingi ya Kiyahudi
1. matumizi ya maneno “wageni” na “waliojitenga” yanauakisi mpangilio wa Kiyahudi (kama vile Yohana 7:35; Matendo 7:6)
 2. matumizi ya Maandiko ya Agano la Kale
 - a. Kutoka 19 (kama vile 2:5,9)
 - b. Isaya 53 (kama vile 1:19; 2:22,24,25)
Hata hivyo, mifano hii si lazima iliakisi kanisa la Kiyahudi, bali
 3. Uamishaji wa majina ya Agano la Kale toka Israeli hadi kwa kanisa (yaani, “ufalme wa makuhani”)
 - a. 2:5
 - b. 2:9
 4. Hati ya kanisa (yaani, nyenzo za katekismus kwa waamini wapya), iliyotenda kazi kwa nafasi ya maandiko ya Agano la Kale la Kimasihi
 - a. 1:19 - Isaya 53:7 (yaani, mwana-Kondoo)
 - b. 2:22 - Isaya 53:5
 - c. 2:24 - Isaya 53:4,5,11,12
 - d. 2:25 - Isaya 53:6
- D. Ingawa Petro alitwa kwa upekee kwa ajili ya kumtumikia Yesu (kama vile Gal. 2:8), huyu, kama alivyo Paulo, alitembea na wote Wayahudi na watu wa Mataifa (kama vile Matendo 10). Kuongoka kwa Kornelio kulionyesha umuhimu wa Petro kuijumuisha injili! I Petro inauakisi utambuzi huu mpya.

IV. KUSUDI

- A. I Petro alikuwa na vipengele vyote vya kimafundisho na vya kiutendaji. Hata hivyo, kama Paulo alivyozigawa barua zake katika kipengele cha mwanzo kihusucho mafundisho na kipengele cha hitimisho la maombi, Petro anaviungansa vyote. Kitabu hiki ni kigumu sana kukiweka katika muhtasari. Katika namna nyingi hiki kinaakisi mahubiri zaidi kuliko barua.
- B. Suala kuu linalojadiliwa ni taabu na mateso. Hili linafanyika katika namna mbili.
1. Yesu anawasilishwa kama hitimisho la mfano wa mateso na kukataliwa (kamavile 1:11; 2:21,23; 3:18; 4:1,13; 5:1).
 2. Wafuasi wa Yesu wanapewa wito wa kuufuatisha muundo na mtazamo wake (kama vile 1:6-7; 2:19; 3:13-17; 4:1,12-19; 5:9-10).
- C. Kwa upande wa taabu na mateso lilikuwa jambo la kawaida sana katika miaka ya kale ya Ukristo, si jambo la kushangaza kuona ni kwa mara ngapi tendo la Kuja kwa mara ya Pili linatajwa. Kitabu hiki, kama yalivyo maandiko mengi ya Agano Jipya, chote kinahusiana na matukio ya siku za mwisho.

V. AINA YA UWASILISHAJI

- A. Kitabu hiki kina sifa za ufunguzi na ufungaji wa karne ya kwanza ya Kiyunani cha Kirumi
1. 1:1-2
 - a. Mwandishi
 - b. Wapokeaji

- c. Maombi
- 2. 5:12-14
 - a. salamu za maagano
 - (2) kutoka kwa yule
 - (2) kwenda kwa yule
 - b. maombi

- B. Kiini cha barua hii kinalandana sana na mahubiri kuliko barua. Wengi wamekuwa wakidhani kuwa hiki kilikuwa
 - 1. Mahubiri ya kwanza
 - 2. liturjia ya ubatizo wa kwanza
 - 3. vipande vya kwanza vya nyenzo za katekisimu ya kanisa la mwanzo vilivyounganishwa
- C. Barua hii inaonekana kuigusia 4:11 kwa wimbo wa kumshukuru Mungu, lakini si machapisho ya Kiyunani yaliyokuwa yamestishwa kwa wakati huu. Inawezekana kwamba 4:12-5:11 ni ufupisho wa makusudi wa barua nzima.
- D. Mimi binafsi naamini kwamba I Petro anatenda kazi kama barua ya mzunguko kwa makanisa pamoja na Petro ambaye kwa upekee alikuwa hajaanza, ni sawa na Kolosai ya Paulo (iliyotumwa kwa Wakolosai, Laodikia, na Hierapoli, kama vile Kol. 4:13), lakini pia tumaini la jumla kwa waamini kuwa makini na matatizo yajayo, sawa na barua za Paulo kwa Wagalatia na Waefeso.
- E. Aina hii ya mzunguko inaeleza juu ya upungufu wa barua kipekee ya ufunguzi na uhitimishaji. Pia inaeleza upungufu binafsi wa mifano ya mateso.

VI. UIDHINISHAJI

- A. Naihusisha aina ya urasimishaji katika I Petro kwa sababu ya jambo hili linakanganya sana na II Petro.
- B. I Petro inaorodhesha Eusebius' *Eccl. His.* 3:3:25, kama sehemu ya "vitabu vyenye ukinzani." Katika kanisa la kale haikushukiwa kamwe kama barua ya kweli ya Mtume Petro.
- C. Suala la urasimishaji limezidishwa kwa sababu ya idadi ya ubandia wa maandiko yaliyoandikwa na Petro. Kanisa la kale halikuweza kukubaliana na haya kamwe, lilitambua I Petro tu na kuitilia mashaka II Petro kama maandiko ya kweli toka kwa Mtume huyu.
 - 1. Matendo ya Petro
 - 2. Matendo ya Petro na Andrea
 - 3. Matendo ya Petro na Paulo
 - 4. Shauku ya Petro na Paulo
 - 5. Matendo ya Petro na wale Kumi na Wawili
 - 6. Waraka wa Petro kuhusu matukio ya siku za mwisho
 - 7. Injili ya Petro
 - 8. Shauku ya Petro
 - 9. Kuhubiri kwa Petro
 - 10. Matendo ya Petro yahusuyo wokovu

(Kwa mjadala mzuri wa matukio ya kila maandiko haya angalia *Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible* Juzuu 4; kr. 721-723, 732-733, 740.) Hakuna hata moja ya maandiko haya ambayo kwa uwazi yamesemekana kuwa ya Petro na ambayo kwa undani yalifikiriwa kuwa sehemu ya sheria ya Agano Jipya. Hili, ndani yake na kwalo, linasema kuhusu kujumuishwa kwa I na II Petro.

MTU, AITWAYE PETRO

I. FAMILIA YAKE

- A. Familia ya Petro iliishi katika Galilaya ya Mataifa yaliyo katika mji wa Bethsaida kaskazini mwa ufukwe wa Bahari ya Galilaya (au Bahari ya Tiberia kama vile Yohana 1:44), lakini kwa namna iliyo dhahiri hii ilikwenda Kapernaumu kwa wakati fulani (kama vile Marko 1:21,29).
- B. Jina la baba yake Petro lilikuwa Yona (kama vile Mt. 16:17) au Yohana (kama vile Yohana 1:42; 21:15-17).
- C. Jina lake alilopewa lilikuwa Simoni (kama vile Marko 1:16,29,30,36), jina ambalo lilikuwa la kawaida katika Palestina ya karne ya kwanza. Huu ulikuwa muundo wa Kiyahudi wa jina Simeoni (kama vile Matendo 15:14; II Pet. 1:1), ambalo lilikuwa jina la Makabila kumi na Mawili ya Israeli (kama vile Mwa. 29:33; Kut. 1:1).
- D. Yesu alimpa upya mtu huyu jina la Petro (*Petros*, lenye kumaanisha “mwamba,” ambapo ilimaanisha kuieleza nguvu yake ya mwisho na uwezo wake) katika Mt. 16:18; Marko 3:16; Luka 6:14; na Yohana 1:42. Muundo wa Kiaramu ni *Cephas* (kama vile Yohana 1:42; I Kor. 1:12; 3:22; 9:5; 15:5; Gal. 1:18; 2:9,11,14). Mara nyingi katika Agano Jipya majina haya mawili yanawekwa pamoja (kama vile Mt. 16:16; Luka 5:8; Yohana 1:40; 6:8,68; 13:6,9,24,36; 18:10,15,25; 20:2,6; 21:2-3,7,11,15).
- E. Jina la ndugu yake Petro lilikuwa Andrea (kama vile Marko 1:16). Huyu alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mbatizaji (kama vile Yohana 1:35,40) na baadaye muumini na mfuasi wa Yesu (kama vile Yohana 1:36-37). Huyu ndiye aliyemleta Simoni kwa Yesu (kamavile Yohana 1:41). Miezi mingi baadaye Yesu alikumbana nao huko Bahari ya Galilaya na kuwaita kuwa wanafunzi wake kwa muda wote (kama vile Mt. 4:18-20; Marko 1:16-18; na Luka 5:1-11).
- F. Huyu alikuwa na mke (kama vile Marko 1:30; I Kor. 9:5), lakini watoto hawakutajwa.

II. KAZI YAKE

- A. Familia ya Petro ilikuwa ikimiliki mashua kadhaa za uvuvi na hata kukodi watenda kazi.
- B. Familia ya Petro inaweza kuwa na ukaribu na Yakobo, Yohana, na baba yao, Zebedayo (kama vile Luka 5:10).
- C. Petro alirudi upesi katika uvuvi baada ya kifo cha Yesu (kama vile Yohana 21)

II. HAIBA YAKE

- A. Nguvu ya Petro
 - 1. Huyu alikuwa mfuasi aliyejitolea kwa dhati, lakini mwenye msukumo usio wa kawaida (kama vile Marko 9:5; Yohana 13:4-11).
 - 2. Huyu alitenda matendo ya imani, lakini mara nyingi alishindwa (mf. kutembea juu ya maji, kama vile Mt. 14:28-31).
 - 3. Huyu alikuwa shujaa na alikuwa tayari kufa (kama vile Mt. 26:51-52; Marko 14:47; Luka 22:49-51; Yohana 18:10-11).
 - 4. Baada ya kufufuka kwake, Yesu alimweleza kama kiongozi binafsi wa wale Kumi na Wawili asiye na sifa katika Yohana 21 na kumpa nafasi ya toba na kumrejesha katika uongozi.
- B. Udhaifu wa Petro
 - 1. Huyu alikuwa na mwelekeo wa awali juu ya sheria za Kiyahudi
 - a. kula pamoja na watu wa Mataifa (Gal. 2:11-21)
 - b. sheria/miiko ya vyakula (Matendo 10:9-16)
 - 2. Huyu, kama Mitume wengine wote, hakuelewa kwa ukamilifu mafundisho mapya ya Yesu na maana yake
 - a. Marko 9:5-6

- b. Yohana 13:6-11; 18:10-11
- 3. Kwa namna ya kipekee huyu alikuwa akikaripiwa vikali na Yesu (Marko 8:33; Mt. 16:23)
- 4. Huyu alikutwa akiwa amelala badala ya kuomba katika saa kuu ya Yesu maombi yaliyohitajika katika bustani ya Gethsemane (Marko. 14:32-42; Mt. 26:36-46; Luka 22:40-60)
- 5. Huyu alirudiarudia tendo la kumkana Yesu (Marko 14:66-72; Mt. 26:69-75; Luka 22:56-62; Yohana 18:16-18,25-27)

IV. UONGOZI WAKE WA KUNDI LA KITUME

- A. Kuna orodha nne za Mitume (kama vile Mt. 10:2-4; Marko 3:16-19; Luka 6:14-16; Matendo 1:13). Mara nyingi Petro anaorodheshwa kwanza. Wale kumi na Wawili waligawanyika katika makundi matatu kati ya manne. Naamini hili liliwapa mwanya wa kuzungukazunguka makwao kwa ajili ya kuziangalia familia zao.
- B. Mara nyingi Petro alitumika kama mzungumzaji wa kundi la Kitume (kama vile Mt. 16:13-20; Marko 8:27-30; Luka 9:18-21). Vifungu hivi pia vimekuwa vikitumika kueleza juu ya mamlaka ya Petro ndani ya kundi (kama vile Mt. 16:18). Hata hivyo, ndani ya muktadha huu anakaripiwa na Yesu kama chombo cha Shetani (kama vile Mt. 16:23; Marko 8:33). Pia, wakati wanafunzi walipokuwa wanabishana juu ya nani aliye mkubwa, Petro hakudhaaniwa kuichukua nafasi hiyo (kama vile Mt. 20:20-28, hasa mst. 24; Marko 9:33-37; 10:35-45).
- C. Petro hakuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu. Hili lilimwangukia Yakobo, ndugu wa kambo wa Yesu (kama vile Matendo 12:17; 15:13; 21:18; I Kor. 15:7; Gal. 1:19; 2:9,12).

V. HUDUMA YAKE BAADA YA KUFUFUKA KWA YESU

- A. Kazi ya uongozi wa Petro inaonyeshwa dhahiri katika sura za hapo awali za Matendo
 - 1. Huyu aliongoza katika uchaguzi baada ya kuondoka kwa Yuda (kama vile Matendo 1:15-26).
 - 2. Huyu alihubiri mara ya kwanza siku ya Pentekoste (kama vile Matendo 2).
 - 3. Huyu alimponya kiwete na kuhubiri mahubiri yaliyonukuliwa (kama vile Matendo 3:1-10; 3:11-26).
 - 4. Kwa ujasiri huyu alizungumza na Wakuu wa Sinagogi katika Matendo 4.
 - 5. Huyu aliitawala nidhamu ya kanisa a Anania na Safira katika Matendo 5.
 - 6. Huyu alizungumza katika Baraza la Yerusalemu katika Matendo 15:7-11.
 - 7. Matukio mengine kadhaa na miujiza vinawekwa kwake katika Matendo.
- B. Petro, hata hivyo, mara nyingi hakuashiria maana ya injili
 - 1. Huyu aliichukulia dhana ya Agano la Kale (kama vile Gal. 2:11-14).
 - 2. Ilimpasa kuwa na mageuzi ya kipekee kwa ajili ya wokovu wa Kornelio (kama vile Matendo 10) na Mataifa mengine.

VI. MIAKA YA UKIMYA

- A. Kuna habari chache au hakuna kabisa kuhusu Petro baada ya Baraza la Yerusalemu la Matendo 15
 - 1. Wagalatia 1:18
 - 2. Wagalatia 2:7-21
 - 3. I Wakorintho 1:12; 3:22; 9:5; 15:5
- B. Desturi za Kanisa la Kale
 - 1. Tendo la Petro kuwa mfiadini katika Rumi linatajwa ndani ya barua ya Clement wa Rumi kwa kanisa la huko Korintho mnamo mwaka 95 B.K.
 - 2. Tertullian (150-222 B.K.) pia maelezo yahasuyo ufiadini wa Petro katika Rumi chini ya Nero (54-68 B.K.).

3. Clement wa Iskandria (200 B.K.) anasema kuwa Petro aliuawa akiwa huko Rumi.
4. Origen (252 B.K.) anasema kuwa Petro alifiadini kwa kusulibishwa, kichwa chini, katika Rumi.

VII. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. alivyotangulia kuwajua, 1:2
2. "kununyiziwa damu," 1:2
3. "alituzaa mara ya pili," 1:3
4. majaribu ya namna mbalimbali, 1:6
5. "kujaribiwa kwa imani yenu," 1:7
6. "kufunuliwa kwake Yesu Kristo," 1:7,13
7. roho, 1:9
8. "mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa," 1:19
9. "Naye amejulikana kweli tangu zamani, kabla haijawekwa misingi ya dunia," 1:20
10. "kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu," 1:23
11. "yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa," 2:2
12. "jiwe lililo hai," 2:4
13. "ukuhani mtakatifu," 2:5
14. jiwe kuu la pembeni, 2:6
15. "Jiwe la kujikwaza," 2:8
16. Tiini, 2:13
17. "alizichukua dhambi zetu katika mwili wake," 2:24
18. "kwa kupigwa kwake mliponywa," 2:24
19. kuhurumiana, 3:8
20. tayari, 3:15
21. "ubatizo, unaowaokoa ninyi," 3:21
22. kuwajaribu, 4:12
23. "mpingeni huyo," 5:9

VIII. WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. "alivyo mtakatifu," 1:15
2. "Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu," 2:25
3. wazee, 5:1
4. Mchungaji mkuu, 5:4
5. Silwano, 5:12
6. Marko, 5:13

IX. MAENEO YALIYOONYESHA KATIKA RAMANI

1. Ponto, 1:1
2. Galatia, 1:1
3. Capadokia, 1:1
4. Asia, 1:1
5. Bithania, 1:1
6. Sayuni, 2:6
7. Babeli, 5:13

X. MASWALI YA MJADALA

1. Fasili juu ya urithi wa muumini. (1:4-5)
2. Eleza 1:11 kwa maneno yako mwenyewe.

3. Je! malaika huyo anataka kujua nini? (1:12)
4. Je! ni kwa namna gani yawapasa Wakristo kutii 1:16?
5. Ni kwa namna gani mtu huukulia wokovu? (2:2)
6. Kwa nini 2:5 na 9 ni za muhimu sana?
7. Ni kwa namna gani 2:16 inahusiana na Warumi 14?
8. Ni kwa namna gani 3:3 ina uhusiano na siku za leo?
9. Je! uhusiano wetu na wenzetu unawezaje kuyaathiri maombi yetu? (3:7)
10. Je! Yakobo alikwenda kuhubiri wapi ambapo aliwaendea kwa roho waliokuwa kifungoni?
(3:19)
11. Elezea 3:22 katika mwangaza wa theolojia ya mafunuo ya uongo.
12. Ni dhamira gani iliyo kuu ya 1 Petro?

UTANGULIZI WA II PETRO

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Sababu au nafasi ya utangulizi huu si kwa ajili ya kujadili kwa undani kuhusiana na matatizo yanayohusiana na uandishi wa II Petro. Mimi binafsi nimehitimisha kwamba hakuna sababu yenye kulazimisha kuukataa uandishi wa Petro. Vyanzo vitatu vimekuwa msaada katika kufikiri juu ya suala hili.
1. Makala ya Bruce M. Metzger "Literary Forgeries and Canonical Pseudepigrapha" katika kitabu chake cha *The Journal of the Society of Biblical Literature*, 1972, kr. 3-24.
 2. Makala ya Michael J. Kruger "The Authenticity of 2 Peter" katika *The Journal of the Evangelical Theological Society*, Juzuu. 42, Na. 4, kr. 645-671.
 3. Kitabu cha E. M. B. Green *2 Peter Reconsidered*, Tyndale Press, 1961.
- B. Kama nifikiriavyo kuhusu uwezekano wa kwamba II Petro haikuandikwa na Petro, mambo mengi yanatokana na fikra zangu.
1. Nani aliyeandika II Petro suala hili haliubadilishi mtazamo wangu kwamba hii imevuviwa na ni ya kiuaminifu. Uandishi ndiyo huyaathiriyo maarifa ya ufasiri wa biblia, si uvuvio, ambao ni imani ya madhaanio ya awali na tendo la kumbukumbu za kihistoria.
 2. Kwa nini natiwa hofu juu ya ubandia huu? Kwa uwazi kabisa karne ya kwanza ya ulimwengu wa Uyunani ya Kirumi ilikuwa imelizoea hili (makala ya Metzger).
 3. Siko tayari kuliruhusu hili kwa sababu ya upendeleo wangu binafsi au uwezo nilionao wa kuuthamini kwa uaminifu ushahidi wa kihistoria na wa kimuktadha? Je! utamaduni unanielekeza katika hitimisho fulani?
 4. Kalinisa la kale lilijiuliza juu ya uandishi wa Petro, lakini si juu ya ujumbe wa vitabu hivi (isipokuwa kanisa la Shamu). Huu ni ujumbe wenye kuegemea imani fulani iliyo katika umoja wa kithiolojia pamoja na vitabu vingine vya Agano Jipya kwa uhusiano na mahubiri ya Petro yaliyo katika kitabu cha Matendo ya Mitume.
- C. Eusebius anatumia aina tatu katika kuyachanganua maandiko ya Kikristo:
1. Yaliyotambuliwa
 2. Yaliyojadiliwa
 3. ya uigaji
- Huyu aliiweka II Petro karibia na Yakobo, Yuda, II Yohana, na III Yohana katika aina 2 (yaani, zilizoigwa). Eusebius anaikubali I Petro; ana mashaka juu ya II Petro, na kuipinga hii kama ya uigaji kama maandiko mengine ya Petro yalivyo (1) Matendo ya Petro; (2) Injili ya Petro; (3) kuhubiri kwa Petro; na (4) ujumbe wa Petro kuhusu matukio ya siku za mwisho.

II. UANDISHI

- A. Hiki ni kitabu cha Agano Jipya kilicho cha uigaji zaidi kama chenye kujikita katika uandishi wa kiutamaduni.
- B. Sababu za mashaka haya yote ni za ndani (muundo wake na maudhui yake) na za nje (ukubalifu wake wa awali).
1. Za nje
 - a. hizi hazikuorodheshwa na Marcion (145 B.K.) au Muratorial Fragment (170 B.K.).

- b. hii inapatikana katika Mafunjo ya Bodamer⁷² ya karne tatu ya mwanzo
 - c. haikunukuliwa moja kwa moja na waandishi wa Kanisa la Kale (Origen na Methodius)
 - d. haikukubalika katika Sheria kwa urasmi hadi lilipofanyika Baraza la Carthage 397 B.K, ambalo kwa uwazi lilifuatisha barua ya Athanasius 367 B.K. Hii ilipingwa katika Kanisa la Mashariki hadi karne ya tano
 - e. si katika tafsiri ya Kiashuru (Peshita) ya karne ya tano
 - f. maandishi ya Eusebius, ya mwaka 325 B.K. (*Ecclesiastical History* 3:25:3) yanakiiondoa hiki miongoni mwa vitabu vilivyoigwa (II Petro, Yuda, Yakobo, II Yohana, na III Yohana)
2. Za ndani
- a. muundo wake ni wa tofauti sana na 1 Petro (1 Petro sarufi ya Kiyunani, ambapo II Petro sivyo ilivyo; Jerome aliweka tofauti hii ili kuwatenganisha waandishi)
 - b. II Petro inaonekana kuifuatisha aina ya kifasihi ijulikanayo kama “Asianism,” ambayo ilikuwa sifa bainifu ya baadhi ya fasihi za Asia Ndogo
 - c. dokezo la vyanzo vya ziada vya kisheria limesababisha matatizo makubwa, lakini I Petro inaonekana kutengeneza dokezo juu ya I Enoch
 - d. II Petro na Yuda zina baadhi ya uhusiano wa kifasihi (II Pet. 2:1-18 na Yuda 4-13 na II Pet. 3:1-3 na Yuda 17-18); nani iliinukuu hii haijulikani
 - e. kitabu hiki kinadai kuandikwa na Mtume Petro; 1:1,14,16-18; 3:1,15

C. Aina ya uwasilishaji

1. Je! hii ndiyo barua halisi ya karne ya kwanza?
- a. ina ufunguzi na uhitimishaji halisi
 - b. hii, hata hivyo, inaonekana kuwa barua ya msingi kwa makanisa kadhaa, kama Wagalatia, Waefeso, Yakobo, na I Yohana
 - c. Hii inaweza kurasimisha aina ya uwasilishaji wa Kiyahudi uitwao “ushahidi,” ambao unabainishwa kwa
 - (1) mahubiri ya maagano
 - a) Kumbukumbu 31-33
 - b) Yoshua 24
 - c) Ushahidi wa Mababa wa Imani kumi na Wawili
 - d) Yohana 13-17
 - e) Matendo 20:17-28
 - (2) utabiri wa mauti yajayo (kama vile II Timotheo)
 - (3) marudi ya wasikilizaji wake kwa ajili ya kuzitunza tamaduni zake
2. Uhusiano kati ya II Petro 2 na Yuda
- a. Kwa namna iliyo dhahiri hii imeonekana kunukuliwa kifasihi.
 - b. Hili dokezo la vyanzo visivyo vya kisheria limesababisha wengi kuvikataa vitabu vyote Yuda na II Petro, hata I Petro inadokeza juu ya I Enoch na Paulo hata nukuu za mashairi ya Kiyunani.
3. Kitabu chenyewe kinadai kutokana na Mtume Petro
- a. Huyu anatamkwa katika 1:1. Huyu anaitwa Simeoni Petro. Petro ni jina alilopewa na Yesu (kama vile Mt. 16). Simeoni (si Simoni) ni adimu na si la kawaida. Ikiwa mtu alikuwa akijaribu kuliandika jina la Petro uchaguzi wa herufi za Kisemiti unashangaza sana na unaleta ubandia.
 - b. Dai lake la kuwa shahidi wa macho wa kubadilika sura kwa Yesu (kama vile Mt. 17:1-8; Marko 9:2-8; Luka 9:28-36) katika 1:16-18.

- c. Dai lake la kuiandika barua ya kwanza (kama vile 3:1), yenye kumaanisha I Petro.
4. Msingi wa Imani
- a. Hakuna jambo lo lote katika barua hii lenye kuyakanganya mafundisho ya Kitume ya Agano Jipya.
 - b. Kuna mambo machache yaliyo ya kipekee (yaani, ulimwengu kuangamizwa kwa moto na maandishi ya Paulo yanaonekana kama Maandiko), lakini hakuna jambo lo lote lililo la mafunuo ya uongo au la ukubalifu au la uasi ulio dhahiri.

MASHAKA YA NJE

1. Eusebius anayaorodhesha maandiko ya Kikristo ya karne za kwanza na za pili katika aina tatu
 - a. Yaliyokubaliwa
 - b. Yenye kutiliwa mashaka
 - c. Yaliyoigwa
 - II Petro, karibia na Waebrania, Yakobo, II na III Yohana vitabu vyote hivi vinaorodheshwa katika aina ya kuigwaji.
2. II Petro haionekani katika sheria ya Marcion (154 B.K.), bali Marcion pia alivikataa vitabu vingi vya Agano Jipya.
3. II Petro haijitokezi katika Muratorian Fragment (180-200 B.K.), bali orodha hii inaonekana kuhathiriwa na pia haikiorodheshi kitabu cha Waebrania, Yakobo, au I Petro.
4. Hii ilipingwa na kanisa la (ki-Shamu) Mashariki
 - a. si katika Peshitta (nusu ya karne ya kwanza)
 - b. hii iliwekwa katika Philoxeniana (507 B.K.) toka Iraq na lile toleo la Harclea (616 B.K.) toka Afrika
 - c. Chrysostom na Theodore wa Mopsuestia (yaani, viongozi wa shule ya ufasiri ya Antiochian) walizikataa nyaraka zote za kikatholiki.
5. II Petro inaonekana kunukuliwa katika “Injili ya Kweli” na “Wasiwasi wa Yohana” vipengele vinavyopatikana katika maandiko ya mafunuo ya uongo ya Nag Hammadi (kama vile *The Nag Hammadi Gnostic Texts and the Bible* na Andrew K. Helmbold, uk. 91). Maandiko haya yaliyo katika asili ya Kimisri ni tafsiri za maandiko ya kale ya Kiyunani. Endapo II Petro inadokezwa na hakuna uwezekano wa hii kuwa imeandikwa katika karne ya pili.
6. Hii imewekwa katika P⁷², iliyowekewa tarehe na UBS⁴ (uk. 8) kama ya karne ya tatu au ya nne.
7. Hii inadokezwa au kunukuliwa na Clement wa Rumi (95 B.K.)
 - a. I Clement (9:2 - II Petro 1:17)
 - b. I Clement (23:3 - II Petro 3:4)
 - c. I Clement (35:5 - II Petro 2:2)
8. Hii pia inaweza kuwa imedokezwa katika kitabu cha Justin Martyr (115-165 B K.) *Dialogue with Trypho* 82:1 - II Pet. 2:1. Haya ndiyo maeneo pekee katika maandiko ya kale ya Kikristo ambapo neno la Kiyunani *pseudopphetai* linatumika.
9. Irenaeus (130-200 B.K.) huenda anadokeza juu ya II Petro (huyu ananukuliwa na Eusebius’ *His. Eccl.* 5:32:2 - II Pet. 3:8 na 3:1:1 - II Pet. 1:15).
10. Clement wa Iskandria (150-215 B.K.) aliandika maoni ya kwanza (ingawa sasa yamepotea) kuhusu II Petro.
11. Hii inajitokeza katika barua ya Athanasius (367 B.K.), ambayo ilikuwa orodha ya kisasa vitabu vya kisheria kwa wakati huo.

12. Hii ilikubalika kama ya kisheria na kanisa la kale la mabaraza ya Laodikia (372 B.K.) na Carthage (397B.K.)
13. Inafurahisha kwamba maandiko mengine Petro yadhaaniwayo (yaani, Matendo ya Petro, na Matendo ya Andrea na Petro, na Matendo ya Petro na Paulo, Shauku ya Petro na Paulo, Matendo ya Petro na wale Mitume Kumi na Wawili, mazungumzo ya Petro kuhusu matukio ya Siku za mwisho, na Mahubiri ya Petro) yote haya yalipingwa na makanisa ya kale kama uigaji (yaani, yasiyovuviwa).

III. TAREHE

- A. Hii inategemeana na uandishi.
- B. Ikiwa mtu anavutiwa na uandishi wa Petro kwa wakati mwingine kabla ya kifo chake (kama vile 1:14).
- C. Desturi za kanisa zinadaia kwamba Mtume Petro alifia Rumi wakati Nero akiwa Kaizari. Nero ndiye alianzisha mateso kwa Wakristo mnamo mwaka 64 B.K. Huyu alijiua mnamo mwaka 68 B.K.
- D. Ikiwa mfuasi wa Petro aliandika kwa kutumia jina lake, basi tarehe hii ya mwaka 130-150 B.K. huenda ni kwa sababu II Petro ilinanukuliwa katika *pocalypse of Peter* pamoja na *The Gospel of Truth and Apocryphon of John*.
- E. Mtaalamu wa utafiti wa mambo ya kale Mmarekani W. F. Albright anadai kwamba hii iliandikwa kabla ya 80 B.K. kwa sababu ya ufanano wake na Magonbo ya Bahari ya Chumvi.

IV. WAPOKEAJI

- A. Kama I Petro inarejelewa katika II Petro 3:1 basi wapokeaji wangeweza kuwa wale wale (yaani, Uturuki ya kaskazini).
- B. II Petro inaweza kuwa ya kiushuhuda kwa ajili ya kuwatia moyo waamini wote ili wayastahimili majaribu, kuwapinga waalimu wa uongo, kuishi kwa uaminifu ndani ya desturi za injili katika matarajio ya Kuja mara ya Pili.

V. MKAZO

- A. Kupambana na uasi, huenda ni kutokana na kushamiri kwa mafunuo ya uongo ya wapinga dini (2:1-22; 3:15-18)
- B. Kujadili juu ya kuchelewa kwa Kristo kuja mara ya pili (3:3-4). Kwa wakati huu walimu wa Uongo na watenda dhambi wengine watahukumiwa na watoto wa Mungu watatukuzwa.

VI. KUTUKIA

- A. Kama I Petro inavyoeleza kuhusiana na mateso na taabu, II Petro inaeleza juu ya waAlimu wa uongo.

- B. Chimbuko halisi la mafundisho ya uongo halijulikani, lakini linaweza kuhusiana na Mapotoe ya wapinga dini (kama vile 2:1-22; 3:15-18). Kitabu hiki kinatumia msamiati wa kiufundi uliotumiwa wakati wa kushamiri kwa Mapotoe na dini za siri. Hii inaweza kuwa mbinu ya msamaha wa makusudi kwa ajili ya kuishambulia theolojia yao.
- C. Kitabu hiki, kama ilivyo II Wathesalonike, kinaeleza juu ya suala la kukawia, lakini pasipo mashaka, Kuja mara ya Pili, ambapo katika Mungu watoto watatukuzwa na wasioamini watahukumiwa (kama vile 3:3-4). Inafurahisha kwamba I Petro kwa ubainifu wake inatumia neno *apocalupsis* kulirejelea tendo la kurudi kwa Yesu, ambapo II Petro inatumia neno *parousia*. Labda hili lianaakisi matumizi ya maandishi mbalimbali (yaani, Jerome).

VII. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. mtumwa, 1:1
2. uweza wake wa Uungu, 1:3
3. utauwa, 1:3
4. “washirika wa asili ya kiungu,” 1:4
5. “washirika wa tabia ya Uungu,” 1:11
6. “kuwekea mbali maskani yangu kwaja upesi,” 1:14
7. “Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake,” 1:16
8. “tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake,” 1:16
9. “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu 1:17
10. “nyota ya asubuhi kuzuka,” 1:19
11. manabii wa uongo, 2:1
12. waalimu wa uongo, 2:1
13. “malaika waliokosa,” 2:4
14. shimoni (yaani, Tartarus), 2:4
15. “na kudharau mamlaka,” 2:10
16. “tamaa ya mambo machafu,” 2:10
17. “ile amri takatifu,” 2:21
18. “mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu,” 3:12
19. “mbingu mpya na nchi mpya,” 3:13
20. “mawaa wala aibu,” 3:14

VIII. WATU WA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. Nuhu, 2:5
2. Lutu, 2:7
3. Balaamu, 2:15

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI — HAKUNA

X. MASWALI YA MJADALA

1. Je! 1:1 ni wito wa Yesu Mungu?
2. Je! ni kwa namna gani 1:10 inahusiana na ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu?
3. Ni wakati gani Yesu aliponena na Petro kuhusu kifo chake? (1:14)
4. Orodhesha ni kwa namna gani sura ya 1 inaakisi siku za Petro na siku za Yesu.

5. Ni kweli gani iliyo kuu ambayo 1:20-21 inaikiri?
6. Orodhesha sifa za waalimu wa uongo walio katika sura ya 2.
7. Kwa nini 2:1, “wakimkana hata Bwana aliyewanunua,” ni ya mkazo sana?
8. Kwa nini 2:8 inashangaza? (2:20)
9. Ifafanue 2:20 katika maneno yako mwenyewe.
10. Ni kitu gani halisi wanachokieleza waalimu wa uongo katika 3:4?
11. Kwa nini inasemekana kuwa dunia iliumbwa nje ya maji? (3:5)
12. Nini maana ya 3:8?
13. Ni kwa namna gani 3:9b inahusiana na I Tim. 2:4?
14. Ni sehemu gani katika Biblia ambapo kweli ya 3:10 inasemekana kuwa?
15. Kwa nini ni muhimu sana Petro kumtaja Paulo?
16. Nini wazo kuu la II Petro?

UTANGULIZI WA 1 YOHANA

I. UPEKEE WA KITABU HIKI

- A. Kitabu cha 1 Yohana sio barua ya binafsi wala barua iliyoandikwa kwa kanisa moja kama “Ujumbe Mtulivu wa sehemu ya kazi kutoka makao Makuu” (barua ya ushirika).
1. Hiki hakina utamaduni wa utangulizi (kutoka kwa nani, kwenda kwa nani).
 2. Hiki hakina salamu binafsi au ujumbe wa mwisho.
- B. Hakuna majina binafsi yaliyotajwa. Huu ni upekee wa hali ya juu ambao si wa kawaida katika vitabu vilivyoandikwa kwa makanisa mengi, kama vile Waefeso na Yakobo. Barua pekee katika Agano Jipya ambayo haina jina la mwandishi ni Waebrania. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba hii iliandikwa kwa waamini wa sasa wa kanisa la nyumbani wanaokumbana na tatizo la waalimu wa uongo.
- C. Barua hii ni kitheolojia maandiko ya yenye nguvu
1. Ukuu wa Yesu
 - a. Mungu kamili na mwanadamu kamili
 - b. wokovu huja kwa imani katika Yesu Kristo, si uzoefu wa kiroho au maarifa ya siri (waalimu wa uongo)
 2. Hitaji kwa ajili ya maisha ya ki-Kristo (majaribu matatu ya Ukristo halisi)
 - a. upendo wa kindugu
 - b. utii
 - c. kukataliwa kwa mfumo wa ulimwengu ulioanguka
 3. Uhakika wa wokovu wa milele kupitia imani katika Yesu wa Nazarethi (neni “sasa” limetumika mara 27)
 4. Namna ya kuwatambua waalimu wa uongo
- D. Maandiko ya Yohana (hasa I Yohana) kwa kiasi fulani ni ki-Koine cha Kiyunani kilicho kigumu kwa mwandishi ye yote yule wa Agano Jipya, bado kitabu hiki, kama ambapo hakuna kitabu kingine, kinachimbua undani wa maana hii na kweli za milele za Mungu katika Yesu Kristo (yaani, Mungu ni Nuru, 1:5; Mungu ni Pendo, 4:8,16; Mungu ni roho, Yohana 4:24).
- E. Inawezekana kwamba I Yohana ilimaanisha kuwa barua ya kiliitoshereza Injili ya Yohana. Mapotoe ya uasi wa karne ya kwanza yanaunda mrejesho wa vitabu vyote. Injili hii ina kweli ya kiunjilisti, ambapo I Yohana inaandikwa kwa ajili ya waamini.
Mfasiri maarufu Westcott anadai kwamba Injili inaukiri Uungu wa Yesu, ambapo I Yohana inaukiri ubinadamu wake. Vitabu hivi vinaendana!
- F. Yohana anaandika katika maneno meupe na meusi (uwili). Hii ni sifa bainifu ya Magombo ya Bahari ya Chumvi na mapotoe ya waalimu wa uongo. Muundo wa fasiri mbili za I Yohana ni wa vitenzi vyote (nuru dhidi ya giza) na mtindo (maelezo hasi hufuatiwa na chanya). Hii ni tofauti kutoka katika injili ya Yohana, ambayo inatumia uwili sambamba (kutoka juu dhidi ya kutoka chini).
- G. Ni vigumu kutoa muhtasari wa I Yohana kwa sababu ya Yohana kutumia dhamira zilizojiurududia. Kitabu kinafanana na pambo la sufi za ukweli zilizofumwa pamoja katika mipangilio inayojiurududia (kama vile Bill Hendricks, *Tapestries of Truth, The Letters of John*).

II. MWANDISHI

- A. Uandishi wa kitabu cha 1 Yohana ni sehemu ya mjadala juu ya uandishi wa Johannine Corpus —Injili, I Yohana, II Yohana, III Yohana na Ufunuo.
- B. Kuna misingi miwili ya misimamo

1. Utamaduni
 - a. Utamaduni ulikubaliwa kati ya makasisi wa awali wa kanisa kwamba Yohana, mtume aliyependwa, alikuwa mwandishi wa I Yohana
 - b. Maelezo ya ushahidi wa kanisa la awali
 - (1) Clement wa Rumi (90 B.K.) alifanya vidokezo kwa I Yohana
 - (2) Polycarp wa Smirna, *Philippians* 7 (110-140 B.K) akidondoo 1 Yohana
 - (3) Justin Martyr's, *Dialogue* 123:9 (150-160 B.K.) akidondoo 1 Yohana
 - (4) Dokezo la I Yohana limefanywa katika maandiko ya
 - a) Ignatius wa Antiokia (tarehe ya kuandikwa inatia mashaka lakini katika mwanzo wa miaka ya 100 B.K.)
 - b) Papias wa Hierapolis (aliyezaliwa kati ya 50-60 B.K. na shahidi yapata mwaka 155 B.K.)
 - (5) Irenaeus wa Lyons (130-202 B.K.) aliiona I Yohana kuwa ya Mtume Yohana. Tertullian, mtetezi wa awali aliyandika vitabu 50 dhidi ya waasi, mara nyingi aliinukuu I Yohana
 - (6) Maandiko mengine ya kale ambayo yaona uandishi wa Mtume Yohana ni Clement, Origen na Dionysius wote watatu wa Alexandria, sehemu ya Muratorian (180-200 B.K.) na Eusebius (karne ya tatu).
 - (7) Jerome (nusu ya pili ya karne ya nne) anathibitisha uandishi wa Yohana lakini anakubali kwamba ulikataliwa na baadhi katika siku zake.
 - (8) Theodore wa Mopsuestia, Askofu wa Antiokia kutoka mwaka 392-428 B.K. aliukataa uandishi Yohana.
 - c. Ikiwa Yohana, tunafahamu nini juu ya mtume Yohana?
 - (1) Alikuwa mwana wa Zebedayo na Salome
 - (2) Alikuwa ni mvuvi katika bahari ya Galilaya na ndugu yake, Yakobo (inawezekana walimiliki mitumbwi kadhaa)
 - (3) Baadhi wanaamini mama yake alikuwa dada yake Mariamu, mama yake Yesu (kama vile Yohana 19:25; Marko 15:20)
 - (4) Ni dhahiri alikuwa tajiri kwa sababu:
 - a) Aliajiri wafanyakazi (kama vile Marko 1:20)
 - a) Alikuwa na Mitumbwi kadhaa
 - b) Alikuwa na nyumba katika Yerusalemu (kama vile Mt. 20:20)
 - (5) Yohana alikuwa na haki ya kuingia katika nyumba ya kuhani mkuu katika Yerusalemu, hii inaonyesha alikuwa baadhi ya mtu mashuhuri (kama vile Yohana 18:15-16)
 - (6) Alikuwa ni Yohana aliyemtunza Mariamu, mama yake Yesu, alikuwa mwaminifu
 - d. Utamaduni wa kanisa la awali kwa kauli moja unathibitisha kwamba Yohana aliishi zaidi kuliko mitume wote na baada ya kifo cha Mariamu katika Yerusalemu alihamia Asia ndogo na kuishi Efeso, mji mkubwa katika eneo hilo. Kutoka mji huu alichukuliwa uhamishoni hadi kisiwa cha Patmo (pwani ya bahari) na baadae akaachiliwa na kurudi Efeso (Eusebius anawanukuu Polycarp, Papias na Irenaeus).
2. Elimu ya sasa
 - a. Kundi kubwa la wanazuoni wa sasa wanatambua mfanano kati maandiko yote ya Johannine, hasa katika tungo, maneno, miundo ya kisarufi. Mfano wake mzuri ni nafasi iliyoachwa ambayo inaelezea maandiko haya: uzima dhidi ya kifo, kweli dhidi ya uongo. Mgawanyo huu wa sehemu mbili zilizo wazi unaweza kuonekana kama maandiko ya siku; magombo ya Bahari ya Chumvi na mwanzo wa maandiko ya mafunuo.
 - b. Kuna nadharia kadhaa juu ya uhusiano kati ya vitabu vitano vya desturi vinavyodhaniwa kuwa vya Yohana. Baadhi ya makundi yanadai uandishi kwa mtu mmoja, watu wawili, watu watatu, na kadhalika. Inaonekana sehemu ya kukubalika zaidi ni kwamba maandiko yote ya Johannine ni matokeo ya fikra za mtu mmoja, hata kama ilifanywa dhaifu na wanafunzi wake kadhaa.
 - c. Maelezo yangu mafupi ni kwamba Yohana, miaka ya mtume, aliandika vitabu vitano vyote hadi mwisho wa huduma yake katika Efeso.
3. Hoja ya uandishi ni hoja ya wafasiri wa fasihi, sio uvuvio. Mwisho mwandishi wa maandiko ni Mungu!

III. TAREHE — Kwa uwazi kabisa hii inahusianishwa na uandishi

- A. Ikiwa Mtume Yohana aliziandika barua hizi, na hasa I Yohana, tunayoizungumzia wakati mwingine ni kipindi cha kuhitimisha karne ya kwanza. Hii ingetoa mwanya wa kushamiri kwa mifumo ya mapotoe ya waalimu wa uongo/kifalsafa na pia ingeshabihiana na istirahi ya I Yohana (“watoto wadogo”), ambayo inaonekana kumaanisha mzee kuzungumza na kundi la waamini walio wachanga. Jerome Anasema kuwa Yohana aliishi miaka 68 baada ya kusulibiwa kwa Yesu. Hii inaonekana kushabihiana na utamaduni huu.
- B. A.T. Robertson anafikiri kuwa I Yohana aliiandika barua hii kati ya mwaka 85-95 B.K, ambapo Injili iliandikwa mnamo mwaka 95 B.K.
- C. Kitabu cha *The New International Commentary Series on I John* na I. Howard Marshall mwandishi wa kitabu hiki anadai kwamba tarehe kati ya mwaka 60-100 B.K. i karibu kama wanazuoni wa sasa wangependa kuikadiria tarehe ya maandiko ya Yohana.

IV. WAPOKEAJI

- A. Utamaduni unaeleza kwamba kitabu hiki kiliandikwa kwa ajili ya Jimbo la Kirumi la Asia Ndogo (Uturuki magaharibi, pamoja na Efeso kuwa eneo lake la kimakazi.
- B. Barua hii inaonekana kuwa imetumwa kwa kudi maalumla makanisa ya Asia Ndogo ambayo yalikuwa yakikumbwa na matatizo ya kukabiliwa na waalimu wa uongo (kama Wakolosai na Waefeso), kwa upekee (1) unyeyekevu wa kimapotoe ambao uliukanusha ubinadamu wa Kristo, lakini huu uliukiri uungu wake na (2) mapotoe ya wenye kuiruhusu anasa waliotenga theolojia toka mwenendo/maadili.
- C. Augustine (karne ya nne B.K.) anasema kuwa hiki kiliandikwa kwa ajili ya Parthians (Babeli). Huyu anafuatishwa na Cassiodrus (karne ya sita ya kale B.K.). Huenda hili lilitokana na mkanganyiko wa kifungu “mteule”, na kifungu, “mteule hapa Babeli,” ambacho kinatumika katika I Petro 5:13 na II Yohana 1.
- D. The Muratorian Fragment, orodha ya kale ya kisheria ya vitabu vya Agano Jipya vilivyoandikwa kati ya mwaka 180-200 B.K. katika Rumi, vinaeleza kwamba bara hii iliandikwa “baada ya nasaha za wanafunzi wenzake na maaskofu” (katika Asia Ndogo).

V. UASI

- A. Barua yenyewe kwa uwazi ni mapambano dhidi ya aina ya mafundisho ya uongo (kama vile “Kama tunasema. . .” 1:6 na kuendelea na “asemaye . . .” 2:9; 4:20 [karipio]).
- B. Tunaweza kujifunza baadhi ya kanuni mafundisho ya uasi kwa kutumia ushaidi wa ndani kutoka I Yohana.
 - 1. kulipinga umbo mwili la Yesu Kristo
 - 2. kuupinga upekee wa Yesu Kristo katika wokovu
 - 3. kutoyaishi maisha ya Kikristo kwa usahihi
 - 4. mkazo juu ya maarifa (mara nyingi ni ya siri)
 - 5. mwelekeo wa kujienga
- C. Mpangilio wa karne hii ya kwanza
Ulimwengu wa Kirumi wa karne ya kwanza ulikuwa wa wakati wa kiuchaguzi kati ya pande za Mashariki na Magharibi. Ile miungu ya Kiyunani na mahekalu ya miungu ya Kirumi vyote hivi vilikuwa na sifa mbaya. Dini za siri zilikuwa maarufu sana kwa sababu ya mkazo wa uhusiano binafsi pamoja na Uungu na maarifa ya siri. Falsafa ya Kiyunani ya kiulimwengu ilikuwa maarufu na kushamiri pamoja na

mitazamo mingine ya kiulimwengu. Katika ulimwengu huu wa uchaguzi baadaye dini ilikuja kuwa mbali na imani ya Kikristo (Yesu ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu, kama vile Yohana 14:6). Kwa vyo vyote ilivyo historia halisi ya uasi, hii ilikuwa juhudi ya kuufanya Ukristo kuwa katika ufino na ukubalifu wa maarifa kwa hadhira Kiyunani Kirumi.

D. Chaguzi yakini za kundi wanamapotoe linalo linaloelezwa na Yohana

1. Mapotoe ya awali

a. Mafundisho ya msingi ya mapotoe ya karne ya kwanza yanaonekana kuwa na mkazo juu ya uwili wa (milele) kithiolojia kati ya roho na jambo husika. Roho (Mungu Mkuu) alikuwa akifikiliwa kuwa mwema, ambapo suala lilikuwa ouvu wa kiurithi. Ukinyume huu unashahabiana na wazo la Plato dhidi ya mambo yanayoonekana, ya kimbingu dhidi ya kidunia, yasiyoonekana dhidi ya yaonekanayo.

Pia kulikuwa na mkazo mkali juu ya umuhimu wa maarifa ya siri (neni la siri au mfumo wa sheria uliowekwa ambao uliiruhusu nafsi kupenya katika ulimwengu wa kimalaika [*aeons*] hadi kwa mungu mkuu) ulio muhimu kwa ajili ya wokovu.

b. Kuna mifumo miwili ya mapotoe ya awali ambayo kwa uwazi ingekuwa katika historia ya I Yohana

(1) Mapotoe ya kiutiifu, yenye kuukana utu wa Yesu kwa sababu ya suala la uovu

(2) Mapotoe ya Cerinthian, yenye kumtambua Kristo kama mmoja wa *aeons* wengi au viwango vya kimalaika kati ya mungu mwema mkuu na suala la uovu. Huyu ni “Roho wa Kristo” aliyemshukia Yesu wakati wa ubatizo na kumwacha kabla ya kusulibiwa kwake.

(3) wa makundi haya mawili ambayo baadhi yao yalikuwa na uzoefu wa kujinyima anasa (ikiwa mwili unataka, huo ni uovu), wangine ni wale wenye kuruhusu anasa (ikiwa mwili unataka, utimizie). Hakuna ushahidi ulioandikwa kuhusu uendelezaji wa mfumo wa mapotoe katika karne ya kwanza. Hii si hadi katikati mwa karne ya pili ambapo ushahidi ulioandikwa ulionekana. Kwa habari zaidi kuhusu “mapotoe” angalia

(a) *The Gnostic Religion* na Hans Jonas, kilichochoapishwa na Beacon Press

(b) *The Gnostic Gospels* na Elaine Pagels, kilichochoapishwa na Random House

(c) *The Nag Hammadi Gnostic Texts* na Biblia na Andrew Helmbold

2. Ignatius anapendekeza chanzo kingine yakini cha uasi katika maandishi yake kwa *the Smyrnaeans* iv-v.

Hawa uliupinga utu wa Yesu na maisha ya anasa.

3. Bado pamoja na hayo uwezekanao wa chanzo cha uasi ni Meander wa Antiokia, anayejulikana kutokana na maandishi ya Irenaeus, *Against Heresies* XXIII. Huyu alikuwa mfuasi wa Simon Msamaria na mtetezi wa maarifa ya siri.

E. Uasi Siku za leo

1. Hii roho ya uasi ipo katika siku hizi zetu pale watu wanapojaribu kuichanganya kweli ya Kikristo na mifumo mingine ya mawazo.

2. Hii roho ya uasi l pamoja nasi katika siku hizi zetu pale watu wanapoweka mkazo “sahihi” wa mafundisho katika kuutenga mbali uhusiano binafsi na maisha ya imani.

3. Hii roho ya uasi ipo katika siku hizi zetu pale watu wanapougeuza Ukristo kuwa katika maarifa ya wasomi waliojitenga.

4. Hii roho ya uasi ipo katika siku zetu pale watu wanapolibadilisha tendo la kujinyima anasa au kuruhusu anasa.

VI. KUSUDI

A. Huu ulitazamia waamini kuwapa furaha (kama vile 1:4)

1. kuwatia maoyo ili waishi maisha ya ki-Mungu (kama vile 1:7; 2:1)

2. kuwaamrisha (na kuwakumbusha)

3. kupendana (kama vile 4:7-21) na si ulimwengu (kama vile 2:15-17).

4. Kuwahakikishia juu ya wokovu wao katika Kristo (kama vile 5:13)

B. Huu ulikuwa na mafundisho yaliyowaelekea waamini

1. kuupinga upotofu wa kuutenga Uungu wa Yesu na ubinadamu wake
2. kuupinga upotofu wa kujitenga kiroho katika usomi pasipo kuyaishi maisha ya ki-Mugu
3. kuupinga upotofu kwamba mtu aweza kuokolewa kwa kuwatenga wengine

VII. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. tangu mwanzo, 1:1
2. Neno la uzima, 1:1
3. uzima wa milele, 1:2
4. ushirika (*koinōnia*), 1:3
5. Mungu ni nuru, 1:5
6. tukienenda, 1:6, 7
7. damu yake Yesu , 1:7
8. Watoto wangu wadogo, 2:1
9. kipatanisho, 2:2; 4:10
10. twajua, 2:3, 4, 18, 20, 21, n.k.
11. anakaa, 2:6, 17, 24, 25, 27, n.k.
12. amri mpya, 2:7
13. kwa ajili ya jina lake, 2:12
14. duniani, 2:15
15. wakati wa mwisho, 2:18
16. mmepakwa mafuta, 2:20, 27
17. amkiriye, 2:23; 4:2, 3, 15, n.k.
18. ziharibuni hizo roho, 4:1
19. siku ya hukumu, 4:17
20. "Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni umoja," 5:8
21. dhambi isiyo ya mauti, 5:16
22. aliyezaliwa na Mungu, 5:18
23. jilindeni nafsi zenu na sanamu, 5:21

VIII. WATU WA KUWATAMBUA KIMUHTASARI

1. Mwombezi, 2:1
2. mwongo, 2:4, 22
3. wapinga Kristo, 2:18; 4:3
4. wapinga Kristo, 2:18
5. wale wanaotaka kuwapoteza, 2:26
6. Ibilisi, 3:8, 10
7. Kaini, 3:12
8. yule mwovu, 5:18

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI – Hakuna

X. MASWALI YA MJADALA

1. Kwa nini 1 Yohana 1:1-4 inatumia vitenzi vingi sana vyenye kuziakisi maana (yaani, sikiliza, onekana, tazama, hamgusi, onekana, sikiliza)?
2. Kwa nini wengine wanasema kuwa hawana dhambi? (1:8)
3. Kwa nini 1:9 ni mstari muhimu sana? Je! huu unamwongelea nani?
4. Ni kwa namna gani unahusianisha 1:10 pamoja na 3:6 na 9?
5. Ni kwa namna gani 2:2 inahusiana na Yohana 3:16?

6. Kwa nini neno “twajua” linatumika mara nyingi sana katika I Yohana? Toa ufafanuzi wa maana nyingine ya Kiebrania.
7. Je! kifungu cha sasa cha, “Ikiwa tunasema . . .,” kinamaanisha au kudokeza nini?
8. Hawa waalimu wa uongo wanaozungumziwa na Yohana ni akina nani? Eleza juu ya imani zao ambazo ziko kinyume na Ukristo wa Kibiblia!
9. Je! mafundisho ya 3:2 yanahusiana na nini?
10. Kwa nini 3:6 na 9 ni vigumu sana kuzifasiri?
11. Ni kwa namna gani 4:8 inahusiana na kuupigana na Wakristo?
12. Hii dhana ya Utatu inajitokeza katika 4:13-14. Toa fasili ya dhana hii katika maneno yako mwenyewe.
13. Toa ufafanuzi wa 4:19 katika maneno yako mwenyewe.
14. Kuna majaribu matatu katika I Yohana yenye kuwahakikishia waamini kuwa wao ni Wakristo. Yaorodheshe majaribu hayo.
15. Kwa nini 5:13 ni mstari muhimu sana?
16. Je! 5:14-15 inawaahidi waamini kuwa maombi yao yatajibiwa kwa ukamilifu mara zote?
17. Ni dhambi gani ipelekeo mauti? (5:16)
18. Je! 5:18 inawaahidi waamini kuwa kamwe hawatajaribiwa au hawataguswa na Shetani? Kwa nini au kwa nini si hivyo?
19. Je! kifungu, “ulimwengu wote utaangukia katika nguvu ya yule mwovu,” kinamaanisha?

UTANGULIZI WA II na III YOHANA

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Barua hii imeitwa kwa nija la III Yohana tu kwa sababu kwa kiasi fulani nia fupi sana kuliko II Yohana. Hakika nafikiri zote II Yohana na III Yohana zinaunda ujumbe wenye usawa kwa kanisa mama, huenda ni mahali fulani katika Jimbo la Kirumi la Asia Ndogo, hadi mwishoni mwa karne ya kwanza.
- B. II Yohana inashughulika na tatizo la uasi, waalimu wasio na makao maalumu, ambapo III Yohana inashughulika na makalipio kwa ajili ya kuwasaidia wahubiri wa Kikristo wenye kuzungu sehemu mbalimbali.
- C. Kuna aina tatu za watu wa naotajwa kwa upekee katika III Yohana:
1. Gayo (mcha-Mungu katika kanisa lililompokea)
 - a. Garo ametajwa mara tatu katika sehemu zingine za Biblia: Gayo wa Makedonia, Matendo 19:29; Gayo wa Derbe, Matendo 20:4; na Gayo wa Korintho, Rum. 16:23; I Kor. 1:14.
 - b. Maandiko yajulikanayo kama “Vyama vya Kitume” yanamwrodhesha Gayo wa III Yohana kama Askofu wa Pergamo, aliyeteuliwa na Yohana.
 2. Diotrefe (mvurugaji ndani kanisa lililompokea)
 - a. Mtu huyu anatajwa hapa tu katika Agano Jipya. Jina lake ni adimu sana na linamaanisha “mwangalizi wa Zeus.” Ni kejeli ya namna gani ambayo mtu huyu alipewa baada ya “Zeus” ambayo ingekuwa kinyume na wasafiri wakati “Zeus” alipokuwa “mlinzi wa wasafiri.”
 - b. Mtazamo wake unawekwa bayana katika mstari wa 9-10.
 3. Demetrio (mleta barua za Yohana kwa kanisa hili mama)
 - a. Kwa uwazi kabisa huyu ni mmoja wa wamisionari waliokuwa wakizunguka sehemu mbalimbali na mleta barua toka kwa Mtume katika Efeso.
 - b. Desturi iitwayo “Vyama vya Kitume” inamwrodhesha Demetrio kama Askofu wa Fildefia, aliyeteuliwa na Mtume Yohana.
- D. Kanisa la kale lilipambana na namna ya kutathmini na kuwaunga mkono wahubiri wanaozunguka sehemu mbalimbali, waalimu, na wainjilisti. Moja ya maandishi ya Kikristo yasiyofungamana na sheria kutoka karne ya pili ya zamani iitwayo *The Didache* au *The Teaching of the Twelve Apostles* ina mwongozo hii:

SURA YA XI—KUHUSU WAALIMU, MITUME, NA MANABII

“Mtu awaye yote, hivyo, ajapo na kuwafundisha mambo haya yote kama yalivyokwisha kunenwa kabla, mpokeeni. Bali ikiwa atawafundisha na kuurudia uharibifu wa mambo haya, msimsikilize; bali *ikiwa atafundisha ili* kuzidisha haki na maarifa ya kumjua Bwana, mpokeeni kama Bwana. Lakini kuhusu mitume na manabii, kwa mujibu wa Injili, fanyeni hivyo: Kila mtume ajaye kwenu na apokelewe kama Bwana.

Lakini hatakaa *isipokuwa* siku moja; bali ikiwa kuna ulazima, pia kwa wakati ujao; lakini ikiwa atakaa siku tatu, huyu ni nabii wa uongo. Na mtume atakapokwenda zake, asichukue cho chote bali mkate hadi atakapopata makao; lakini akiomba fedha, huyu ni nabii wa uongo”(uk.380).

SURA YA XII—MAPOKEZI YA WAKRISTO

“Bali azungumzapo katika Roho, Nipeni fedha, au kitu cho chote, huyu msimsikilize; bali awaambiapo wapeni wenye uhitaji, asiwepo mtu wa kumhukumu.

Bali kila ajeye kwa jina la Bwana na apokelewe, na baadaye mtamthibitisha na kumjua; kwa hili mtaelewa jema na baya. Ikiwa ajaje kwenu ni mpitaji, msaidieni kama mwezavyo; lakini hatakaa nanyi, isipokuwa kwa siku tatu au mbili, ikiwa kuna ulazima. Lakini ajitoleapo kukaa nanyi, kuwa fundi pamoja nanyi, na afanye kazi na kula; bali ikiwa hana biashara, kulingana na ufahamu wenu lione hili, kama mtu

wa Kikristo, huyu hatawaacha bila kazi. Bali ikiwa hatakuwa na hiari ya kufanya hivyo, huyu ni kutumia Jina la Kristo vibaya. Angalieni jitengeni na mtu huyu”(uk. 381).

II. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. “tangu mwanzo,” 1:1
2. “Mungu ni nuru,” 1:5
3. Tukiziungama, 1:9
4. “Watoto wangu wadogo,” 2:1
5. Mwombezi, 2:1
6. kipatanisho, 2:2
7. twajua, 2:3
8. “anaka ndani yake,” 2:6
9. “Msiipende dunia,” 2:15
10. “ni wakati wa mwisho,” 2:18
11. mafuta yake, 2:27
12. “Roho na maji na damu,” 5:8
13. “Iko dhambi iliyo ya mauti,” 5:16
14. “jilindeni nafsi zenu na sanamu,” 5:21

III. WATU WA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. Neno la uzima, 1:2
2. mpinga Kristo, 2:18 (II Yohana mst. 7)
3. mpinga Kristo, 2:18
4. kwa mama mteule, II Yohana mst. 1
5. na watoto wake, II Yohana mst. 1
6. “Watoto wa ndugu yako aliye mteule,” II Yohana mst. 13
7. Gayo, III Yohana mst. 1
8. Diotrefe, mst. 9
9. Demetrio, mst. 12

IV. MAENEO YALIYOONYESHWA KWA RAMANI —HAKUNA

V. MASWALI YA MJADALA

1. Kwa nini 1:1-5 ina vitenzi vingi vyenye kuhusiana na milango mitano ya fahamu?
2. Kwa nini mtu aseme kuwa hawana dhambi? (1:8)
3. Ni kwa namna gani 2:2 inahusiana na Yohana 3:16?
4. Toa fasili ya 2:7-8 katika maneno yako mwenyewe.
5. Je! 2:12-14 inahusiana na makundi ya umri mbalimbali ndani ya kanisa au Wakristo wote?
6. Toa maelezo ya 2:22-23 katika mwangaza wa theolojia ya mapotoe.
7. Ni kweli kuu ya aya hii, 2:28-3:3?
8. Kwa nini 3:6 na 9 ni vigumu sana kuifasiri?
9. Ni kwa namna gani 3:15 inahusianana Mahubiri ya Mlimani?
10. Toa fasili ya 3:20 katika maneno yako mwenyewe.
11. Ni kwa namna gani mtu huzijaribu roho? (4:1-6)
12. Je! ni kwa namna gani 4:2 inahusiana na theolojia ya mapotoe? (II Yohana mst.)
13. Nini kweli kuu ya 4:7-24?
14. Ni kwa namna gani 5:13 inatenda kazi kama moja ya dhamira za kitabu kizima?
15. Je! Mungu hujibu maombi yote? (5:14-15)
16. Je! II Yohana 10 inairejelea mambo ya mtu au kanisa na mtu? Kwa nini?
17. Je! III Yohana mst. 2 ni andiko lenye kuahidi afya na ustawi?

UTANGULIZI WA YUDA

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Yuda ni kitabu cha kuogopesha juu ya hatari ya kosa linalojirudia, uasi, na hukumu. Waaminio mara zote wanatakiwa wawe macho. Ulinzi wao ni katika
1. wito wa Baba, upendo, na kuwa na nguvu
 2. ufahamu wa maandiko, maisha ya ucha Mungu, na rehema kuwaelekea waaminio washirika walioumizwa.
- B. Bado, hata katikati ya maonyo, hitimisho la Yuda ni mojawapo ya maombi imara ya uthibitisho wa kuwa na nguvu ya Mungu.
- C. Uhusiano kati ya kitabu cha Yuda na II Petro una mashaka kama ya:
1. ni kipi kimojawapo kiliandikwa kwanza
 2. kwa nini vinafanana na bado ni tofauti
 3. ni kwa namna gani kimoja kinaelezea ukengeufu ujao na kingine ukengeufu uliopo
 4. kama kulikuwa na maelezo ya kanisa la awali kutoka upande gani waandishi walichora
 5. kama mifano yoyote ya waasi inayohusisha waaminio
- D. Kitabu hiki kinatoa picha ya uwiano wa kitheolojia kati ya
1. kuwa na nguvu za Mungu (mistr. 1,24)
 2. waaminio kujilinda wenyewe (mstr. 21)

II. MWANDISHI

- A. Yuda (Kiebrania, Yuda, au Kiyunani, Yudas) anajielezea mwenyewe kwa vyeo viwili
1. “mtumwa mwaminifu wa Yesu Kristo” – hii sio hali halisi ile ile kama cheo cha kawaida cha Paulo, Ingawa inaonekana ni ile ile katika Kiingereza. Paulo mara zote aliweka jina “mtumwa” kwanza, ikifuatiwa na tungo MILIKISHI elezi. Hii pia ni kweli ya II Petro.
Hata hivyo, mpangilio wa neno katika Yuda ni sawa sawa kama mpangilio wa neno katika Yakobo (tungo ya awali MILIKISHI elezi).
 2. “ndugu yake Yakobo” – kuna watu wengi katika Agano Jipya wanaoitwa Yakobo (Yakobo), lakini kwa jina pekee, pasipo cheo, inakumbusha mmoja wa Yakobo 1:1. Yakobo, ndugu yake Yesu, alikuwa ni kiongozi wa kanisa la Yerusalemu wakati wa safari za umisionari za Paulo (kama vile. Mdo 15). Inakisiwa kwamba walichaguliwa ndugu wote, nje ya unyenyekevu, sio kufanana wao kama uzao wa kimwili unaohusika kwa Yesu.
- B. Kisio rahisi la wazi kwa mtu ambaye anafahamika zaidi na mtendaji (kama vile I Kor. 9:3) katika kanisa la awali, lakini ni nani aliyeokolewa hakuna tarifa. Ikiwa mtu Fulani aliandika baadae mwishoni kipindi anataka kuandika kwa jina la mtu maarufu aliyepita (uongo), Yuda anaweza kuwa sio mteuliwa mwema.
- C. Mapokeo ya kale yanadai kwamba Yuda alikuwa mwebrania mkristo na ndugu yake Yesu (kama vile. Mt. 13:55; Marko 6:3) inaegemea katika mawazo kadhaa
1. familia yenye uhusiano kwa Yakobo (kama vile. Yakobo 1:1)

2. kutumika kwa upana zaidi katika Agano la kale
3. fasihi ya kiebrania imetumia sifa mara tatu
 - a. matukio matatu ya ukanaji wa imani katika Agano la kale
 - b. tabia tatu katika Agano la kale
 - c. salamu ya wazi
 - 1) vitenzi vitatu: “itwa,” “mpendwa,” “lindwa”
 - 2) maombi matatu: “neema,” “amani,” “upendo”

D. Mbinu ya kiyunani na muundo wa Yuda umeandikwa vizuri zaidi katika Koine ya Kiyunani. Yuda lazima ana mwelekeo wa mtazamo wa kiulimwengu (kama vile. I Kor. 9:5). Kwa umbali kama tabia, anafanana sana na Yakobo; ametumia hakuna maana, kutazamia ujio wa mamlaka kwa ajili ya maisha ya ucha Mungu katika dunia hii yenye dhambi na uasi.

III. TAREHE

A. hakuna uthibitisho, ni kisio pekee.

B. ngoja tutaje baadhi ya vigezo

1. wakati wa uhai wa Yuda kama alikuwa ndugu mdogo wa Yakobo na ndugu wa Yesu
2. kitabu cha fasihi ya Yuda kinahusiana na II Petro. Kwa vifungu ishirini na tano katika Yuda, kumi na sita (mistr. 3-18) ina baadhi ya uhusiano na II Pet. 2:1-18. Kama Petro ndiye mwandishi wa II Petro, hivyo tarehe inakabiliana sana na wakati wa uhai wake (alifariki mwaka wa 64 B.K.). Ni, ijapokuwa, inatia mashaka ni nani alimdososa nani:
 - a. II Petro anamdososa Yuda
 - b. Yuda alimdososa II Petro
 - c. wote walitumia kumbukumbu za awali au tamaduni za kanisa

C. Yaliyomo katika kitabu yanadokeza tarehe ya katikati ya karne ya kwanza. Muda wa kutosha umepita kwa ajili ya machukizo kuendelea. Uwepo wa kimwili wa mitume sasa umepita (mistr. 18-19). Hata hivyo, mfano mmoja wa mafundisho hujafanikiwa. Yuda anataja matatizo ya maadili ya walimu wa uongo, lakini hajadili makosa ya mafundisho. Alitumia mifano ya Agano la kale, sio mafundisho ya Yesu (dondoo au hadithi).

D. Katika *Historical Ecclesiasticus* III:19:1-20:6, Eusebius anataja tamaduni.

1. kwamba wana wa wana wa Yuda walichukuliwa hadi Rumi kukutana na Domitian katika kesi ya uhaini
 2. kwamba walikuwa uzao wa kifalme wa kiyahudi
 3. kwamba walikuwa jamaa za Yesu wa Nazareti
- Domitian alitawala kutoka mwaka 81-96 B.K.

E. Tarehe kutoka miaka ya 60 hadi miaka ya 80 inawezekana.

IV. WAPOKEAJI NA KUTUKIA

A. Kanisa la awali halikuwa kubwa sana kitheolojia; hata mitume walisisitiza madai tofauti ya injili. Kama mitume walivyoanza kufa (au angalau walikuwa wachache na pia kuwa mbali kushaurika) na ujio wa pili uliendelea kuchelewa, kanisa la awali lilikutana na changamoto “ya kuwa aina moja” ya kigezo cha

kukubaliwa kwa ajili ya mafundisho ya injili. Agano la kale, maneno na hadithi za Yesu, na mafundisho ya mitume yalikuwa kanuni.

B. Yuda aliandika katika siku za mabadiliko na matatizo ya mamlaka wazi. Waaminio (kama kanisa la mahali au eneo la kijiografia linatia mashaka) walikutana na uvamizi mkubwa wa makosa kupitia theolojia/filosofia ya kubahatisha. Ni nini kilifahamika kama machukizo:

1. waasi walikuwa sehemu ya kusanyiko la kanisa (“karamu zenu za upendo” kama vile mstr. 12)
2. waasi walikuwa waovu, waliwatawala walimu ambao walisababisha mgawanyiko katikati ya watu wa Mungu (kama vile. mstr. 19)
3. waasi wanaonekana wakitumia au kujadili “malaika” katika theolojia yao
4. waasi wanaonekana wakisisitizia “maarifa” (*ufunuo*)

Kama mmojawapo anafanana na ulimwengu wa Uyunani-Rumi wa karne ya kwanza na ya pili, tabia hizi zinadokeza vuguvugu la kifilosofia/kitheolojia linalofahamika kama “mafunuo.” Ni ukweli wa uhakika kwamba asili ya waasi hawa wa karne ya pili walikuwa wameenea zaidi sehemu za mashariki ya karibu. Misingi miwili ya tabia za mafunuo ipo hadi leo katika magombo ya bahari ya chumvi.

Vitabu vingi vya Agano jipya (Efe. - Kol, vya kichungaji, I, II Yohana) viliandikwa ili kupambana sambamba na aina ya mafundisho ya uongo/walimu.

V. KUSUDI

A. Mwandishi alitamani kuandika juu ya wokovu wao uliozoeleka (kama vile mstr. 3).

B. Uvamizi wa mafundisho ya uongo na walimu ndani ya ushirika katika nyakati za kanisa (kama vile. mstr.12) kulisababisha mwandishi aeleze jambo kali sana la “imani mliyokabidhiwa na kwa ajili kanisa lote” (kama vile. mistr. 3,20). Lengo lake lilikuwa imani halisi, lakini alikaribia dhamira kupitia maisha ya ucha Mungu (orthopraxy), sio mafundisho (yanafanana sana na Yakobo 2:14-24). Kwa namna gani watu waliishi kwa kujionyesha vizuri katika theolojia yao.

C. mwandishi alitaka kuwatia moyo waaminio kwa ajili ya

1. ukuaji wa kiroho (kama vile. mstr. 20)
2. kuwa na uhakika wa wokovu (kama vile mistr. 21,24-25)
3. kuwasidia walio na mashaka (kama vile Mistr. 22-23)

VI. UIDHINISHAJI

A. Hiki kilikuwa ni kitabu cha kwanza kukubaliwa (kama vile Dondoo na Clement wa Rumi yapata mwaka wa 94 B.K), kisha baadaye kuzua mjadala na mwishowe kukubaliwa kabisa (baraza la Nikea, 325 B.K na Carthage, 397 B.K).

B. Tatizo lake kuu ni katika kupata kulasimishwa hadhi yake ilikuwa ya vitabu visivyo lasimishwa (I Henoko na lisilohakikishwa na Musa). Vitabu hivi, hasa I Henoko, kimesambaa sana katikati ya waaminio wa karne ya kwanza na ulikuwa ni ushawishi wa kitheolojia.

1. Kwa nini hili tatizo? Je linadokeza kwamba vitabu visivyo lasimishwa vina mamlaka?
 - a. Agano la kale linadodosa maandiko yasiyo-vuviwa (kama vile Hes. 21:14-15,26-30 [unabii wa Balaamu katika Hes. 22-23]; Yoshua. 10:13; II Sam. 1:18 nakuendelea; I Fal. 11:41; 14:19,29; 15:7,23,31)

- b. Yesu alitumia vyanzo visivyolasimishwa kama jambo la kutolea ufafanuzi (kama vile Mt. 23:35)
 - c. Stefano alitumia vyanzo visivyo lasimishwa (kama vile. Mdo 7:4,14-16)
 - d. Paulo mara nyingi alitumia vyanzo visivyo lasimishwa
 - 1) Wataalamu wa sheria za kiyahudi Midrash wanamhusisha Kristo kama mwamba kwamba uliwafuata wana wa Israeli jangwani kipindi cha kutangatanga (kama vile. I Kor. 10:4)
 - 2) majina ya waganga wa Farao kutoka kitabu cha Kut. 7:11,22; 8:7 (kama vile. II Tim. 3:8) yalichukuliwa kutoka baadhi maandiko ya kiyahudi
 - 3) Waandishi wa kiyunani
 - a) mshairi Aratus (Mdo 17:28)
 - b) mshairi Menander (I Kor. 15:33)
 - c) mshairi Epimenides au Euripes (Tito 1:12)
 - e. Yakobo alitumia utamaduni wa wataalamu wa sheria za kiyahudi katika Yakobo 5:17
 - f. Yohana alitumia matukio ya sayansi kuhusu ulimwengu wa mashariki ya karibu katika Ufu. 12:3
2. Kwa nini Yesu alitumia hivi vyanzo visivyo lasimishwa?
- a. inawezekana vilikuwa huru kutumiwa na walimu wa uongo
 - b. inawezekana viliheshimiwa na kusomwa na wapokeaji
- C. kuhimili ulasimisho wa Yuda ni kusaidiwa na
1. dondoa au dokezwa na
 - a. Clement wa Rumi (94-97 B.K.)
 - b. Polycarp (110-50 B.K.)
 - c. Irenaeus (130-202 B.K.)
 - d. Tertullian (150-220 B.K.)
 - e. Athenagoras (177 B.K.)
 - f. Origen (185-254 B.K.)
 (Haya yametolewa kutoka fasiri ya kimataifa ya kihakiki, kr. 305-308)
 2. majina yaliyomo ni
 - a. Clement wa Alexandria (150-215 B.K.)
 - b. Cyril wa Yerusalemu (315-386 B.K.)
 - c. Jerome (340-420 B.K.)
 - d. Augustine (400 B.K.)
 3. waliotajwa katika orodha za ulasimishwaji wa
 - a. kipande cha Muratorian (200 B.K.)
 - b. Baroccio (206 B.K.)
 - c. Athanasius (367 B.K.)
 4. yaliyo thibitishwa na mabaraza
 - a. Nikea (325 B.K.)
 - b. Hippo (393 B.K.)
 - c. Carthage (397 na 419 B.K.)
 5. tafsiri za sasa ni
 - a. Latini ya kale (150-170 B.K.)
 - b. Toleo la Shamu, Peshitta (karne ya 5 B.K.)

- D. Kanisa la baadae lilikuwa na mashaka na hadhi ya ulasimishaji wa Yuda (kuvuviwa). Eusebius anakiorodhesha kati ya vitabu vyenye mashaka (*Hist. Eccl.* III:25). Wote Chrysostom na Jerome wanataja dondoo kutoka vyanzo visivyo lasimishwa kama sababu ya mashaka yao na baadhi kama vilivyo lasimishwa. Kilikataliwa na kanisa la awali la Shamu pamoja na II Petro, II na III Yohana. Hii inawezekana kwa sababu sehemu hii ilikuwa ya utawala ambao uliathiriwa na mafunuo ya kiyahudi ya malaika. Hata hivyo, kitabu cha Yuda na I Petro vinaongeza moto wa ushawishi wa walimu wa uongo.
- E. sasa neno juu ya I Henoko. Kiliandikwa asili katika kiebrania (lakini sasa kimepotea kwa sehemu katika Kiaramu katikati ya magombo ya bahari ya chumvi), kinatafsiriwa katika Kiyunani (sehemu pekee zilizopo) na kwa mwaka wa 600 B.K. zilinakiriwa huko Ethiopia (nakala moja imebakia). Kitabu kiliandikwa kipindi cha ukimya, lakini kilihaririwa mara nyingi, kama nakala ya Ethiopia inavyoonyesha. Kilikuwa na ushawishi sana katika kanisa la awali; Tertullian anakidodosa kama maandiko. Kinadondoa katika nyaraka ya Barnaba (kama maandiko) na Irenaeus na Clement wa Iskandria. Kilipoteza upendeleo katika kanisa la awali kwa karne ya nne.

VII. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "wokovu wetu," mstr. 3
2. "imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja," mstr. 3
3. ufisadi, mstr. 4
4. "makao yao," mstr. 6
5. "vifungo vya milele chini ya giza," mstr. 6
6. "mambo ya mwili," mstr. 7
7. "moto wa milele," mstr. 7
8. karamu za upendo, mstr. 12
9. mtakatifu, mstr. 14
10. "kuomba katika Roho Mtakatifu," mstr. 20
11. "Mungu pekee," mstr. 25

VIII. WATU WA KUTAMBUA KIMUHTASARI

1. "watu waliojiingiza," mstr. 4
2. "malaika wasioilinda enzi yao wenyewe," mstr. 6
3. Mikaeli, mstr. 9
4. Balaamu, mstr. 11
5. Kora, mstr. 11
6. Henoko, mstr. 14
7. "yeye awezaye," mstr. 24

IX. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Misri, mstr. 5
2. Sodoma na Gomora, mstr. 7

X. MASWALI YA MJADALA

1. Ni aina gani ya walimu wa uongo ambao Yuda anawarejelea? (kama vile. 8-13)
2. Kwa nini Yuda anadondoa vitabu vilivyo lasimishwa? (mistr. 9, 14-15)
3. Ni kwa namna gani mtu anaweza kujilinda katika upendo wa Mungu? (mstr. 21)

4. Ni nini kiini cha dhamira ya Yuda?
5. Ni kwa namna gani Yuda anasimuliwa katika II Petro?

UTANGULIZI WA UNABII WA AGANO LA KALE

I. UTANGULIZI

A. Maelezo ya Ufunguzi

1. Jamii ya waaminio haiamini namna ya ya kutafsiri unabii. Kweli zingine zimekwisha weka wekwa bayana kama ilivyo kwa nafasi ya Waorthodox katika karne nyingi, lakini si katika karne hii.
2. Zipo hatua kadhaa za unabii wa Agano la Kale
 - a. Premornarchial (Kabla ya utawala wa Kifalme)
 - (1) Watu binafsi walioitwa manabii
 - (a) Ibrahimu – Mwanzo 20:7
 - (b) Musa – Hesabu 12:6-8; Kumbukumbu la Torati 18:15; 34:10
 - (c) Haruni – Kutoka 7:1 (Msemaji wa Musa)
 - (d) Miriam – Kutoka 15:20
 - (e) Medad na Eldad – Hesabu 11:24-30
 - (f) Debora – Waamuzi 4:4
 - (g) Wasiokuwa na majina – Waamuzi 6:7-10
 - (h) Samweli - 1 Samweli 3:20
 - (2) Rejea ya manabii kama kundi – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
 - (3) Kundi la Kinabii au ushirika – 1 Samweli 10:5-13; 19:20; 1 Wafalme 20:35, 41; 22:6, 10-13; 2 Wafalme 2:3,7; 4:1, 38; 5:22; 6:1, nakadhalika.
 - (4) Masihi aitwaye nabii – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
 - b. utawala wa kifalme usioandikwa (wakimlenga mfalme);
 - (1) Gadi – 1 Samweli 22:5; 2 Samweli 24:11; 1 Mambo ya Nyakati 29:29
 - (2) Nathan – 2 Samweli 7:2; 1 Wafalme 1:22
 - (3) Ahijah – 1 Wafalme 11:29
 - (4) Yehu – 1 Wafalme 16:1, 7, 12
 - (5) Wasiotajwa – 1 Wafalme 18:4, 13, 22
 - (6) Eliya – 1 Wafalme 18- 2 Wafalme 2
 - (7) Mikaya – 1 Wafalme 22
 - (8) Elisha 2 Wafalme 2:9, 12-13
 - c. Maandiko ya kale ya manabii (yanayo lenga taifa pamoja na mfalme); Isaya – Malaki (isipokuwa Danieli)

B. Istilahi za Kibiblia

1. *ro'eh* = "muonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Samweli 9:9. Rejea hii yenyewe inatuonesha mpito kutoka katika neno nabi. Ro'eh inatokana na istilahi ya jumla "kuona." Mtu huyu alizielewa njia za Mungu na mipango yake na aliulizwa kutambua mapenzi ya Mungu katika jambo lolote.
2. *Hozeh* = "muonaji" (BDB 302, KB 3011), 2 Samweli 24:11. Ni jamii ya neon lenye maana sawa na Ro'eh. Inatokana na neno "kuona." Njeo ya wakati uliopita ya neno hili ni "tazama" ambalo limetumika mara nyingi ikimaanisha manabii.
3. Nabi' = "nabii" (BDB 611, KB 661), inayohusiana na lugha ya Akkadia ya kitenzi *Nabu* = "kuita" na kiarabu *Naba'a* = "kutangaza". Hili ni neon limetajwa mara nyingi katika Agano la kale kumaanisha nabii. Limetumika zaidi ya mara 300. Asili kabisa haijulikana kwa hakika japo "kuita" kwa wakati huu inaonekana kama mbadala mzuri zaidi. Yawezekana uelewa mzuri zaidi unatoka YHWH yanayoeleza mahusiano ya Musa kwa Farao kupitia Haruni (rejea kutoka 4:10-16; 7:1; Kumbukumbu la torati 5:5). Nabii ni mtu anayezungumza kwa niaba ya Mungu kwa watu wake. (Amosi 3:8; Jeremia 1:7,17; Ezeieli 3:4).
4. Istilahi zote tatu zinatumiwa katika huduma ya Nabii katika 1 Mambo ya Nyakati 29:29; Samueli – Ro'eh; Nathani – Nabi' na Gadi – Hozeh.
5. Kifungu cha maneno, *'ish ha – 'elohim*, "Mtu wa Mungu" pia ni namna pana ya kumaanisha msemaji wa Mungu. Inatumika mara 76 katika Agano la Kale kwa kumaanisha "nabii"

6. Neno "Nabii" kwa asili ni la Kigiriki. Inatokana na neno (1) *pro* = "kabla" au "kwa niaba ya" na (2) *phemi* = "kuzungumza."

II. MAANA YA UNABII

- A. Neno unabii lilikuwa pana kimaana katika lugha ya kiebrania kuliko Kingereza. Vitabu vya historia vya Yoshua, Wafalme (isipokuwa Ruthu) vinatajwa na Wayahudi kama "Manabii waliopita". Wote Ibrahimu (Mwanzo 20:7; Zaburi. 105:15) and Moses (Kumbukumbu la Torati 18:18) wanatajwa kama Manabii (pia Miriam, Kutoka 15:20). Kwahiyo kuwa makini unapokuwa unatazama maana kutoka katika lugha ya Kingereza!
- B. "Unabii kisheria kabisa waweza kusema ni ule uelewa wa historia unaokubali maana zile tu zinazohusiana na uungu, kusudi la kiungu, ushirika wa kiungu," *Interpreter's Dictionary of the Bible*, toleo la. 3, ukurasa wa. 896.
- C. "Nabii si mwanafalsafa au mwana taaluma ya Theolojia, bali msaidizi wa agano aletaye neno la Mungu kwa watu wake ili kutengeneza hatima zao kwa kufanya mageuzi ya siku zao za sasa," Prophets and Prophecy, *Encyclopedia Judaica* toleo la. 13 ukurasa wa. 1152.

III. KUSUDI LA UNABII

- A. Unabii ni njia ya Mungu kuzungumza na watu wake, kuwapa miongozo katika mazingira yao ya sasa na tumaini katika kuyaendesha maisha yao na matukio ya duniani. Ujumbe wao ulikuwa wa jumla. Ilikusudiwa kuonya, kutia moyo, kuhamasisha imani na toba, na kuwafahamisha watu wa Mungu kuhusu Mungu mwenyewe na mipango yake. Iliwashikilia watu wa Mungu katika maagano na Mungu. Katika hili inatakiwa iongezwe kuwa mara nyingi imekuwa ikitumika kufunua uchaguzi wa Mungu wa wasemaji (Kumbukumbu la Torati 13:1-3; 18:20-22). Hii ukiipa umaanani kabisa utagundua ilimaanisha Masihi.
- B. Mara nyingi nabii aliichukua historia na migongano ya kithiolojia ya siku zake na kuangazia hayo katika mazingira ya matukio ya siku za mwisho. Namna ya muono huu wa siku za mwisho kihistoria katika Israeli ni wa kipekee na katika hali yakeya uchaguzi wa kiungu na ahadi za kiagano.
- C. Ofisi ya nabii inaonekana kutengeneza usawa (Yeremia 18:18) na kuchukua ofisi ya Kuhani Mkuu kama njia ya kufahamu mapenzi ya Mungu. Urimm na Thummim inabadilika katika ujumbe wa mdomo kutoka kwa msemaji wa Mungu. Ofisi ya nabii inaonekana pia kupita mbali katika Israeli baada ya Malaki. Haitokei mpaka baada ya miaka 400 baadae kwa Yohana Mbatizaji. Haeleweki namna ambavyo kipawa cha "unabii" kwa Agano Jipya kinavyoshabihiana na Agano la Kale. Manabii wa Agano Jipya (Matendo ya Mitume 11:27-28; 13:1; 15:32; 1 Wakorintho. 12:10,28-29; 14:29,32,37; Waefeso. 4:11) sio vifunuo vya ufunuo mpya au maandiko, bali wasimulizi wa yajayo na wazungumzaji wa mambo ya mbele ya mapenzi ya Mungu katika hali za agano.
- D. Unabii hauna msingi sana au hausisitizi katika utabiri kwa asili. Utabiri ni njia mojawapo ya kutthibitisha ofisi yake na ujumbe wake, ila lazima izingatiwe "chini ya asilimia 2% ya unabii wa Agano la Kale ni kuhusu wa kimasiya". Chini ya asilimia 5% kiuhalisia inafunua nyakati za Agano Jipya. Chini ya asilimia 1% inahusu matukio yajayo. "fee na Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa wa 166).
- E. Manabii wanamwakilisha Mungu kwa watu, wakati Makuhani wanawawakilisha watu kwa Mungu. Haya ni maelezo ya jumla. Kuna utofauti kwa kama Habakkuki, ambaye anauliza maswali kwa Mungu.
- F. Sababu moja inayoleta ugumu kuwaelewa manabii ni kwasababu hatujui muundo wa vitabu vyao. Havina mfuatano unaoeleweka. Vinaonekana ni vyenye hoja na mada kweli lakini si kama vile mtu

angetegemea. Mara nyingi hakuna mazingira ya wazi ya kihistoria wala muda maalumu, au mgawanyiko wa wazi wa mambo ya kiungu. Vitabu hivi ni vigumu

1. Kuvisoma kwa mara moja
2. Kufafanua kwa mada
3. Kug'amua kweli kuu au kusudio la mwandishi katika kila uungu.

IV. TABIA ZA UNABII

- A. Katika Agano la Kale inaonekana kukua kwa dhana ya “nabii” na “unabii”. Hapo mwanzo katika Israeli kulitokea ushirika wa manabii, ukiongozwa na viongozi shupavu wenye uvuvio wa Mungu kama Eliya na Elisha. Kuna wakati neno “wana wa manabii,” ilitumika kuzungumzia kundi hili (II Wafalme 2). Manabii walikuwa na tabia ya kujawa na furaha ya kupiliza (1 Samweli 10:10-13; 19:18-24)
- B. Hata hivyo kipindi hiki kilipita mara kwa mara kwa manabii mmoja mmoja. Kulikuwa manabii (wa kweli na waongo) waliojitambulisha pamoja na mfalme, na waliishi katika Kasri la Kifalme (Gad, Nathan). Pia, kulikuwa na wale waliojitegemea, wakati mwingine wasiokuwa na hadhi kabisa za jamii ya ki-Israeli (Amosi) walijumuisha wote wanawake na wanaume (2 Wafalme 22:14)
- C. Nabii mara nyingi alikuwa mfunuaji ya hatima, anayefanya katika mazingira ya mwanadamu yanavyoenda. Mara nyingi jukumu la nabii ilikuwa ni kufunua mpango wa Mungu kwa uumbaji wake ambao hauathiriwi na mwikio wa kibinadamu. Huu mpango wa wa ulimwengu wa matukio ya mwisho wa nchi ni wa kipekee katika manabii wa Mashariki ya Karibu ya Kale. Utabiri na Agano ni mapacha waendao pamoja katika ujumbe wa kinabii (rejea Fee na Stuart, ukurasa wa 150). Hii inamaanisha manabii husisitiza ujumuishwaji katika lengo. Siku zote, japo si kila eneo, hujelekeza katika kuambia taifa.
- D. Mambo mengi ya kinabii yakitolewa kwa njia ya kinywa. Baadae iliunganishwa kwa njia ya mada, mfululizo, au namna nyingine ya uandishi wa Mashariki ya Karibu ambao imepotea huku kwetu. Kwakuwa ilikuwa kwa njia ya kinywa, haikuwa na muundo kama unaokuwa katika kazi iliyo andikwa. Hii inafanya vitabu kuwa vigumu kusoma na ngumu kuelewa bila kuwa na historia ya mazingira halisi.
- E. Manabii walitumia namna kadhaa kuwasilisha jumbe zao
1. Matukio ya kimahakama – Mungu anawapeleka watu wake mahakamani, mara nyingi ni kesi ya kutalikiana ambapo YHWH anamkataa mke wake (Israeli) kwasababu ya kukosa uaminifu wake (Hosea 4; Mika 6).
 2. Mazingira ya msiba – mzani haswa kwa ajili ya ujumbe wa namna hii na tabia zake “ole” inajitenga kama aina yake kivyake vyake (Isaiah 5; Habakuki 2)
 3. Matamko ya Agano la Baraka - asili ya masharti ya Baraka imesisitizwa na madhara yake, yote ya wema na ubaya, yanatajwa kwa ajili ya baadae (Kumbukumbu la Torati 27-28).

V. SIFA ZA KIBIBLIA KWA AJILI YA KUMTHIBITISHA NABII WA KWELI

- A. Kumbu kumbu la Torati 13:1-5 (utabiri/ishara)
- B. Kumbu kumbu la Torati 18:9-22 (nabii wa uongo/nabii wa kweli)
- C. Wote wawili wanawake na wanaume wanaitwa na kupewa jina kama nabii wa kike au wa kiume
1. Miriamu – Kutoka 15
 2. Debora – Waamuzi 4:4-6
 3. Hulda – 2 Wafalme 22:14-20; 2 Nyakati 34:22-28

Katika desturi zinazotuzunguka manabii wanathibitishwa na kupimwa kwa namna ya miujiza. Katika Israeli walipimwa na kuthibitishwa kwa

1. Jaribu la kithiolojia – kwa kutumia Jina la YHWH

2. Jaribu la kihistoria – utabiri wa kweli ulio sahihi

VI. MIONGOZO YA KUKUSAIDIA KATIKA KUTAFSIRI UNABII

- A. Tafta kujua lengo la kwanza la nabii (mwandishi) kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria na muktadha wa maandishi ya kiungu.
 - B. Soma na tafsiri mambo yote, sio sehemu tu; fafania na yaliyomo. Angalia inavyoshabihiana na mazingira ya unabii. Jaribu kufafania kitabu kizima.
 - C. Endelea na kufanya makisio ya utafsiri wa kawaida wa hadithi mpaka vitu katika habari vikuelekeze katika matumizi yaliyofichwa kimaana; hivyo badili lugha iliyofichwa katika maandishi.
 - D. Fafania matendo ya kiishara katika ufahamu wa mazingira ya kihistoria na usambamba wa hadithi. Kuwa na uhakika wa kukumbuka maanadishi ya kale ya Mashariki ya Karibu si kama yale ya kisasa ya kimagharibi.
 - E. kuwa mwangalifu wa utabiri
 - 1. Je unahusisha siku za mwandishi?
 - 2. Je uliwahi kutimia katika historia ya Israeli?
 - 3. Je ni kweli yamekwisha kuwa matukio yajayo?
 - 4. Je yana kutimizwa kwa sasa nab ado yanasubiri kutimizwa siku zijazo?
 - 5. Waruhusu maandishi wa Biblia wakuongoze katika majibu na sio maandishi wa kisasa.
- Vitu vya kuzingatia
- 1. Je utabiri umekidhi kigezo cha sharti la mwikio
 - 2. Kuna uhakika kwa Yule ambaye unabii umemlenga? (Na kwa nini)?
 - 3. Je kuna uwezekano, wa kibiblia na/au kihistoria, wa kutimia mara mbili?
 - 4. Waandishi wa Agano Jipya, chini ya uvuvio waliweza kumuona mesiya katika sehemu nyingi katika Agano la Kale kiasi ambacho hakipo kwetu. Wanaonekana kutumia aina hii ya mchezo. Kwakuwa hatujavuviwa basi ni bora tukawaachia utaratibu huu wao.

VII. VITABU VYA KIMSAADA

- A. *A Guide to Biblical Prophecy* cha Carl E. Amending na W. Ward Basque
- B. *How to Read the Bible for All Its Worth* cha Gordon Fee na Douglas Stuart
- C. *My Servants the Prophets* cha Edward J. Young
- D. *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic* cha D. Brent Sandy
- E. *Cracking the Old Testament Code*, D. Brent Sandy and Ronald L. Giese, Jr.

MAKALA YA UTANGULIZI WA MUHIMU – UFUNUO

(Kwanini Wakristo wana Fasiri Nyingi Zisizobadilika Juu Ya Ufunuo)

Katika miaka ya masomo yangu ya elimu juu ya siku za mwisho wa nchi nimegundua kwamba Wakristo wengi hawana au hawapendi mtiririko, ulioboreshwa, ulioendelea unaoonesha nyakati za mwisho. Kuna Wakristo wenye mlengo mkubwa wa eneo hili la Ukristo kwa ajili ya theolojia, saikolojia, au sababu ya kidhehebu. Wakristo hawa wanaonekana kusumbuliwa sana na namna gani jambo hili litaisha, na kwa namna fulani kukosa ule umaana wa Injili! Waamini hawawezi kuathiri ajenda ya Mungu juu ya mwisho wa nchi, lakini wanaweza kushiriki katika mamlaka ya Injili (rejea Mathayo. 28:19-20; Luka 24:46-47; Matendo ya Mitume 1:8). Waamini wengi wanakiri kuja kwa mara ya Pili kwa Kristo na kule kutimilizwa kwa mwisho kwa ahadi za Mungu. Tatizo la kiutafsiri linainuka kutoka katika namna ya kuelewa kutimilizwa huku kutoka katika utata kadhaa wa kibiblia.

1. Mvutano kati ya mifano ya kinabii ya Agano la Kale na mifano Mipya ya Kitume ya Agano jipya.
2. Mvutano kati ya Uungu mmoja wa Biblia (Mungu mmoja kwa ajili ya wote) na kuchaguliwa kwa Israeli (watu maalumu)
3. Mvutano baina ya kipengele cha sharti cha agano na ahadi za kibiblia (“ikiwa...basi”) na uaminifu usio na masharti wa Mungu kwa ukombozi wa binadamu aliyeanguka
4. Mvutano kati ya aina ya uandishi wa Mashariki ya Karibu na mifano ya uandishi wa kimagharibi
5. Mvutano kati ya Ufalme wa Mungu wa sasa na ujao.
6. Mvutano kati ya imani katika kurudi kwa Kristo na imani kwamba matukio kadhaa lazima yatokee kwanza.

Naomba tujadili mivutano hii moja baada ya nyingine.

MVUTANO WA KWANZA (Agano la Kale, kabila, utaifa na kipengele cha jiografia dhidi ya waamini wote dunia nzima). Manabii wa Agano la Kale walitabiri juu ya urejesho wa Ufalme wa Kiyahudi katika Palestina iliyo katikati ya Yerusalemu ambapo mataifa yote ya dunia yatakusanyika kumsifu na kuutumikia utawala wa Daudi, lakini si Yesu wala Mtume yoyote wa Agano jipya aliwahi kuweka msisitizo katika ajenda hii. Si uvuvio wa Agano la Kale (rejea Mathayo 5:17-19)? Je maandishi wa agano jipya wameondoa sehemu matukio muhimu yanyakati za mwisho?

Kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu.

1. Manabii wa Agano la Kale (Isaya, Mika, Malaki)
2. Waandishi wa mambo ya mwisho wa nchi wa Agano la Kale (rejea Ezekieli 37-39; Daniel 7-12; Zakaria)
3. Waandishi wa kati ya maagano, maandishi wayahudi wa siku za mwisho wasio wakanoni (kama I Enoch kinachosemekana kilitakiwa kifuata baada ya Yuda)
4. Yesu mwenyewe (rejea Mathayo 24; Marko 13; luka 21)
5. Nyaraka za Paulo (rejea 1 Wakorintho 15; 2 Wakorintho 5; 1 Wathesalonike 4-5; 2 Wathesalonike 2)
6. Nyaraka za Yohana (1 Yohana na Ufunuo)

Je haya yote yanatufundisha kwa hakika ajenda ya mwisho wa nchi (matukio, mfululizo, watu)? Kama sio kwanini? Je si yote kuwa yamevuviwa (isipokuwa maandishi ya kati ya maagano ya Kiyahudi).

Roho alifunua ukweli kwa maandishi wa Agano la Kale kwa namna na sehemu ambayo wangeelewa. Hata hivyo, kupitia ufunuo endelevu Roho alipanua dhana hii ya Agano la Kale juu ya siku za mwisho wan chi katika namna pana (“maajabu ya Kristo,” rejea Waefeso 2: 11-3:13). Ifuatayo ni baadhi ya mifano inayoendana:

1. Jiji la Yerusalemu katika Agano la Kale imetumika kama ulinganifu kwa watu wa Mungu (Sayuni), lakini inatajwa katika Agano Jipya kama neno linaloelezea kupokelewa na Mungu kwa watubuo wote, wanadamu waaminio (“Yerusalemu Mpya” ya Ufunuo 21-22). Maana kubwa zaidi ya kithiolojia iliyokuzwa ya jiji linavyoonekana kuwa watu wapya wa Mungu (Wayahudi waaminio na Mataifa) inatajwa kwa mbele katika ahadi za Mungu kukomboa binadamu aliyeanguka katika Mwanzo 3:15, kabla hata hapajawa na Muyahudi yoyote au Mji mkuu wa Kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (rejea 12:1-3) ilihusisha mataifa (rejea Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5) angalia Mada Maalumu: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH.

2. Katika Agano la Kale, maadui wa watu wa Mungu ni mataifa yaliyozunguka Near East ya Kale, lakini katika Agano Jipya wamekuza kwa wasioamini wote, wampingao Mungu, watu wenye uvuvio wa kishetani. Vita imehamishwa kutoka kijiografia, migogoro ya kikanda kwenda ulimwenguni kote, mgogoro wa kiulimwengu (rejea Wakolosai).
3. Ahadi ya ardhi ambayo ni sehemu ya Agano la Kale (ahadi ya Mwanzo, rejea 12:7 13:15; 15:7,15, 16; 7:8) sasa imekuwa dunia nzima. Yerusalemu mpya inashuka chini kwa nchi iliyombwa tena, sio Mashariki ya Karibu tu au kinginecho (rejea Ufunuo 21-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ya dhana za kinabii ya Agano la Kale inayokuzwa. Mbegu ya Ibrahimu sasa imetahiriwa kiroho (Warumi 2:28-29) (rejea Hosea 1:10; 2:23, ikinukuliwa kutoka Warumi 9:24-26; pia Walawi. 26:12; Kutoka 29:45, imenukuliwa kutoka 2 Wakorintho 6:16-18 and Kutoka 19:5; Kumbukumbu la torati 14:2, imenukuliwa katika Tito 2:14). Hekalu sasa ni Yesu (rejea Mathayo 26:61; 27:40; Yohana 2:19-21) na kupitia yeye kanisa la nyumbani (rejea 1 Wakorintho 3:16) au kwa mwamini mmoja mmoja (rejea 1 Wakorintho 6:19). Hata Israel na tabia za zinazofunua maneno ya Agano la Kale sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu (kama vile "Israeli," rejea Warumi 9:6 Wagalatia 6:16, kama "Ufalme wa Makuhani," rejea 1 Petro 2:5, 9-10; Ufunuo 1:6)

Mifano ya kinabii imekuwa ikitimizwa, ikikuzwa, na sasa ikujumuisha. Yesu na waandishi wa Kitume hawawasilishi nyakati za mwisho kama ile ya manabii wa Agano la Kale (rejea Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecy and Fulfillment*). Watafsiri wa kisasa wanaojaribu kutengeneza mifano ya Agano la Kale au kugeuza kimaarifa ya kitabu cha Ufunuo kwenda katika kitabu cha Kiyahudi na kulazimisha maana isiyoeleweka, yenye utata kauli za Yesu na Paulo! Waandishi wa Agano Jipya hawawakatai manabii wa Agano la Kale, lakini huonesha kilele cha walichomaanisha kwa ujumla. Hakuna mfumo uliopangwa katika mwisho wan chi kunakozungumzwa na Yesu au Paulo. Kusudi lao kimsingi kabisa ni kiukombozi au kichungaji.

Hata hivyo ndani ya Agano Jipya kuna mvutano. Hakuna mfumo rasmi wa wazi wa matukio ya siku za mwisho. Katika namna nyingi kwa mshangao mkubwa Ufunuo unatumia dhana za Agano la Kale katika kuelezea mwisho badala ya mafundisho ya Yesu (rejea Mathayo 24; Marko 13)! Inafuata namna ya uandishi ulioanzishwa na Ezekieli, Danieli, na Zakaria, lakini ilikua wakati wa katia ya Agano la Kwanza na Jipya (fasihi ya Kiyahudi ya nyakati za mwisho wa nchi). Hii ilikuwa najia ya Yohana ya kuunganisha Agano la Kale na Jipya. Inatazama taratibu za nyakati za kale ya uasi wa mwanadamu na kujithatiti kwa Mungu katika ukombozi! Lakini hata hivyo lazima izingatiwe kwamba ingawa Ufunuo unatumia lugha ya Agano la Kale, watu na matukio, inayatafsiri katika ufahamu wa karne ya kwanza ya Rumi.

MVUTANO WA PILI (Hali ya uwepo wa Mungu mmoja dhidi ya watu wateule)

Msisitizo wa Kibiblia upo kwa mmoja, roho, muunbaji-mkombozi, Mungu (rejea Kutoka 8:10; Isaya 44:24; 45:5-7, 14,18, 21-22; 46:9; Yereimia 10:6-7). Upekee wa Agano la Kale katika siku zake lenyewe ilikuwa ni hali ya Mungu mmoja. Mataifa yote yazungukayo yalikuwa yakiabudu miungu mingi. Umoja wa Mungu ndio moyo wa Ufunuo wa Agano la Kale (rejea Kumbukumbu la Torati 6:4) uumbaji ni eneo kwa ajili ya kusudi la ushirika kati ya Mungu na mwanadamu, aliyeumbwa kwa sura na mfano wake (rejea Mwanzo 1:26-27). Hata hivyo, mwanadamu aliasi, atatenda dhambi dhidi ya upendo wa Mungu, uongozi, na kusudi (rejea Mwanzo 3). Upendo wa Mungu na kusudi lilikuwa kubwa sana na hakika kuwa alihaidi kukomboza uanadamu ulioanguka (rejea Mwanzo 3:15)!

Mvutano unaanza pale Mungu anapochagua kumtumia mtu mmoja, familia moja, taifa moja kufikia wanadamu wengineo. Uchaguzi wa Mungu wa Ibrahimu (Mwanzo 12; 15; 17; 18) na Wayahudi kama ufalme wa Makuhani (rejea Kutoka 19:4-6) ulisababisha kiburi badala ya huduma, kubaguana badala ya kujumuika kwa pamoja. Wito wa Mungu kwa Ibrahimu ulijumuisha kusudio la kubariki wanadamu wote (Mwanzo 12:3). Lazima ikukmbukwe na isisitizwe kwamba kuchaguliwa kwa Agano la Kale ilikuwa ni huduma, sio wokovu. Waisraeli wote hawakuwa sawa machoni pa Mungu, kamwe si kuokolewa kwa msingi wa haki ya uzaliwa (rejea Yohana 8:31-59; Mathayo 3:9), lakini kwa imani binafsi na utii (Mwanzo. 15:6, imenukuliwa kutoka Warumi. 4:3,9,22; Wagalatia 3:6). Israeli ilipoteza kusudi lake (kanisa kwa sasa ndio ufalme wa makuhani, rejea Ufunuo 1:6; 1 Petro 2:5,9) na kugeuza mamlaka katika neema, huduma katika msimamo maalumu! Mungu alichagua mmoja kuchagua wote!

MVUTANO WA TATU (maagano yenye masharti dhidi ya maagano yasiyo na masharti)

Kuna mvutano wa kithiolojia au kugawanyika kati ya maagano yasiyo na masharti na yenye masharti. Ni kweli ya hakika kabisa kuwa kusudi/mpango wa ukombozi wa Mungu si wa masharti (rejea Mwanzo 15:12-21). Hata hivyo, mwikio wa kimamlaka wa mwanadamu siku zote huwa ni wa masharti!

Ule utaratibu wa “iwapo...ndipo” inaonekana katika vitabu vyote Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu ni mwaminifu; mwanadamu si mwaminifu. Mvutano huu umesababisha hali ya kutoelewana isiyo ya kawaida. Watafsiri wamejifanya kugemea upande mmoja tu “pembe ya kutoelewa vizuri,” uaminifu wa Mungu au juhudi za mwanadamu, Ukuu wa Mungu au utashi huru wa mwanadamu. Zote ni za Kibliblia na muhimu.

Hii ina husiana na siku za mwisho wa nchi, kwenda kwenye ahadi za Mungu za Agano la Kale kwa Waisraeli. Iwapo Mungu alihaidi, basi hiyo inatosha! Mungu anafanya kazi kwa ahadi zake; heshima yake huusika (rejea Ezekieli 36:22-38). Maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti hukutana na Kristo (rejea Isaya 53), sio Israeli! Kilele cha uaminifu wa Mungu kiko katika wa ukombozi wa wote watakao tubu na kuamini, si kwa kigezo cha nani alikuwa baba yako au mama yako! Kristo, sio Israeli ndio msingi wa Maagano yote ya Mungu na ahadi. Kama kuna sehemu ya mabano katika thiolojia katika Biblia, sio Kanisa, bali Israeli (Matendo ya Mitume 7 na Wagalatia 3).

Kusudi la ulimwengu la kutangaza Injili limekabidhiwa kwa Kanisa (rejea. Mathayo 28:19-20; Luka 24:47; Matendo ya Mitume 1:8). Hili ni sharti na kiagano! Hii haimaanishi Mungu amewakataa kabisa Wayahudi (rejea Warumi 9-11). Kunawezekana kukawa na sehemu na kusudi kwa ajili ya siku za Mwisho, kuamini kwa Israeli (rejea Zakaria 12:10)

MVUTANO WA NNE (mifano ya kiuandishi ya Mashariki ya karibu dhidi ya ile ya Kimagharibi)

Aina ya uandishi ni kipengele muhimu sana katika kuitafsiri Biblia kwa usahihi (angalia Fee and Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth*). Kanisa lilikua katika mazingira ya kiutamaduni wa kimagharibi (Kigiriki). Fasihi ya Mashariki ina mafumbo mengi sana zaidi, inatumia ulinganifu wa vitu visivyofanana, na yenye ishara kuliko ya kisasa, mifano ya utamaduni wa Kimagharibi. Inaweka mkazo kwa watu, makabiliano, na matukio zaidi ya ukweli kamili unaopendekezwa. Wakristo wamekuwa katika hukumu ya kutumia historia yao wenyewe na mifano ya kiunadishi kutafsiri unabii wa Kibiblia (yote Agano la Kale na Agano Jipya). Kila kizazi na ujumla ya kijiografia umetumia desturi, historian a ukawaida kutafsiri Ufunuo. Kila mmoja wao alikosea! Ni majivuno kufikiria kuwa desturi ya kimagharibi ndio mahali pa kuanzia pa unabii wa kibiblia.

Aina ya uandishi ambayo kwa asili, imevuviwa mwandishi kuchagua kuitumia kuandika ni mkataba na msomaji (Bruce Corley). Kitabu cha Ufunuo sio hadithi ya Kihistoria. Ni mkusanyiko wa barua (Sura ya 1-3), unabii, na zaidi sana maandishi yanayozungumza juu ya mwisho wa nchi. Ni makosa kuifanya Biblia iseme zaidi ya kilichokusudiwa na mwandishi wa asili ambayo ni sawa na kuifanya iseme chini ya yale yaliyokuwa yamekusudiwa! Majivuno wa Watafsiri na misingi yao ya kiimani si ya kuweka kabisa katika kitabu kama cha Ufunuo.

Kanisa halijawahi kukubaliana kuhusu tafsiri sahihi ya Ufunuo. Ninachotamani ni kusikia na kujishughulisha na biblia nzima, si vijisehemu tu. Ufahamu wa Biblia wa Kimashariki unawasilisha ukweli katika namna za safu za mvutano. Hali yetu ya Kimagharibi kuelekea ukweli unaopendekezwa sio kwamba haufai, bali hauna ulali wa usawa! Nafikiri inawezekana saa nyingine kuondoa angalau baadhi ya vifuniko katika kutafsiri Ufunuo kwa kuzingatia kusudi la kubadilika kwake kwenda kwa vizazi vinavyofuata vya waaminio. Ni wazi kwamba watafsiri wengi kuwa Ufunuo lazima utafsiriwe katika ufahamu wa siku zake na aina ya uandishi wake. Namna ya kihistoria ya kuelezea Ufunuo lazima izingatie nini wasomaji wa kwanza wangukuwa nacho, na wangeelewa. Kwa namna nyingi watafsiri wa kisasa wamepoteza maana ya ishara nyingi za kitabu. Lengo la kwanza la Ufunuo ilikuwa ni kuwatia moyo waamini wanaopitia dhiki. Inaonesha namna Mungu anavyoshughulikia Historia (kama alivyofanya kwa manabii wa Agano la Kale); ilikubali kuwa historia inaelekea kwenye muda ulioteuliwa, hukumu au Baraka (kama ilivyokuwa kwa Manabii wa Agano la Kale). Ilikubalika katika namna ya karne ya kwanza ya kiyahudi ya siku za mwisho za upendo wa Mungu, uwepo, nguvu na ukuu!

Inafanya kazi kwa namna hiyohiyo kithiolojia kwa kila kizazi cha waaminio. Inaelezea mapambano ya kiulimwengu ya wema na uovu. Maelezo ya karne ya kwanza yanaweza yakawa yalitupoteza, lakini si kweli zenye nguvu na zifarijizo. Pale watafsiri wa kisasa wa kimagharibi wanapojaribu kulazimisha maelezo ya Ufunuo kwenda kwenye historia yao ya sasa, utaratibu wa tafsiri za uongo huendelea!

Inawezekana kwamba maelezo ya kitabu yanaweza yakarudi kwa kasi kuwa kawaida (kama ilivyokuwa Agano la Kale ikilinganisha kuzaliwa, maisha na kifo cha Kristo) kwa kizazi cha mwisho cha waaminio wanapokabiliana na kutishiwa kifo na kiongozi mpinga Mungu (rejea 2 Wathesalonike 2) na desturi. Hakuna anayefahamu kutimilizwa kwa kawaida kwa Ufunuo mpaka maneno ya Yesu (rejea. Mathayo 24; Marko 13; and Luka 21) na Paulo (rejea. 1 Wakorintho 15; 1 Wathesalonike 4-5; na 2 Wathesalonike 2) pia yatapokuwa halisi kihistoria. Kubashiri, kubuni buni na kukaa katika imani za kidhebehu si sawa. Fasihi ya mwisho wa nchi inaruhusu huku kubadilika. Mshukuru Mungu kwa ajili ya taswira na ishara zinazopita hadithi za kihistoria! Mungu yupo kazini; Yeye anatalawa; Anakuja!

Watoa maoni wengi wa kisasa wanakosa sehemu muhimu ya aina hii ya uandishi! Watafsiri wa kimagharibi wa Kisasa mara nyingi hutafuta mtiririko mzuri wa kueleweka wa kithiolojia badala ya kuwa sawa na utata, ishara na aina ya uandishi ya kitamthiliya ya Kiyahudi ya fasihi ya siku za mwisho. Kweli hii inaelezwa vizuri na Ralph P. Martin katika makala yake, "Approaches to New Testament Exegesis," katika kitabu *New Testament Interpretation*, kilichohaririwa na I. Howard Marshall:

"Mpaka tutakapotambua ubora wa kitamthiliya wa maandiko haya na kurejea katika namna ambayo lugha inavyotumika kama njia ya kuelezea ukweli wa kidini, tutakosea sana katika kufahamu mambo ya siku za mwisho, na kimakosa tunajaribu kutafsiri maono yake kama vile sasa noo kitabu cha mabo ya kawaida tu na chenye lengo la kufunua matukio yanayojulikana na historia yenye taarifa. Kujaribu kufanya jambo hili la mwisho ni kuingia katika kila namna ya matatizo ya kiutafsiri. Na zaidi sana inapelekea upotevu wa maana muhimu ya siku za mwisho na hivyo kupotea thamani kubwa ya ukuu wa Mungu katika sehemu ya Agano jipya kama tamko la Kitamthiliya katika lugha ya kishairi ya uungu ya Uungu wa Mungu na Kristo na mgongano wa utawala wake unaochanganya ukuu na upendo (Ufunuo 5:5,6; the Lion is the Lamb)" (ukurasa wa 235).

W. Randolph Tate katika kitabu chake cha *Biblical Interpretations* (Tafsiri za Kibiblia):

"Hakuna aina ya uandishi mwingine wa Biblia iliyosomwa kwa dhati sana kwa matokeo yanatokatisha tama kama vitabu vinavyoongelea mwisho wan chi kama vitabu vya Danieli na Ufunuo. Aina hii ya uandishi ilidhoofika kutokana na historia mbovu ya tafsiri zisizo sahihi kutokana na kukosa uelewa wa msingi wa aina yake ya kifasihi, muundo na kusudi. Kwasababu ya tamko hilo kufunua kile kinachotakiwa kutokea kwa muda mfupi, siku za mwisho zimekuwa zikichukuliwa kama ramani ya njia na mpango wa siku zijazo. Kosa baya ya kuchukuliwa huku ni ile dhana kwamba namna ya rejea ya vitabu iko katika nyakati anazoishi msomaji wa wakati huo badala ya wakati anaoishi mwandishi. Kwenda kwa namna hii kwa bila muongozo kwa siku za mwisho (haswa Ufunuo) inazifanya kazi kana kwamba ni lugha ya siri au fumbo ambalo matukio ya sasa yanaweza kutumiak kutafsiri ishara za maandiko. Kwanza, mtafsiri lazima atambue kwamba vitabu vya siku za mwisho vinawasilisha ujumbe wake kupitia viwakilishi vya kiishara. Kutafsiri viwakilishi kikawaida wakati inalinganisha vitu ni kukosea katika kutafsiri. Jambo kubwa sio kama matukio katika siku za mwisho ni ya kihistoria. Matukio yanaweza yakawa ya kihistoria; yanaweza yakawa kuwa yalitokea, au yatatokea lakini mwandishi anawasilisha matukio na anazungumza maana kupitia taswira na namna hizo" (ukurasa wa 137).

Kutoka katika *Dictionary of Biblical Imagery*, edited by Ryken, Wilhost and Longman III:

"Wasomaji wa leo mara nyingi wamefumbwa na wanachanganyikiwa na aina hiii ya uandishi. Taswira isiyotarajiwa na mambo yaliyo nje ya ulimwengu huu yanaleta giza na kutoka nje katika maandiko mengi. Ukichukulia maandiko haya kwa thamani ya usoni inawaacha wasomaji wengi wakihangaika kutafuta kujua 'itatokea nini iwapo,' kwahiyo kupoteza lengo la ujumbe wa siku za mwisho" (ukurasa wa 35)

MVUTANO WA TANO (ufalme wa Mungu kwa sasa na baadaye)

Ufalme wa Mungu ni sasa, na baadaye. Hali hii ya mtafaruku wa kithiolojia inalengwa katika siku za mwisho wa nchi. Kama hakuna anayetegemea kutimilizwa kwa nabii zote za Agano la Kale kwa Waisraeli hivyo Ufalme unakuwa haswa kurejeshwa kwa Israeli katika eneo lao la Kijiografia na kuheshimiwa kabla kwa thiolojia! Hii ingesababisha kuwa kanisa lingekuwa limetwaliwa katika Sura ya 5 na Sura zinazobaki zihusiane na Israeli.

Hata hivyo kama lengo ilikuwa katika ufalme kuanzishwa na Mesiya aliyahaidiwa na Agano la Kale, halafu ipo na kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza, na alafu lengo linakuwa kuwa hai tena, maisha, mafundisho, mauti, na ufufuo wa Kristo. Mkazo wa kithiolojia upo katika wokovu wa sasa. Ufalme umekuja, Agano la Kale linatimilizwa kwa Kristo kujitoa kwa jili ya wokovu kwa wote, siyo Yeye kutawala milele juu ya wengine!

Ni kweli ya uhakika kuwa Biblia inazungungumzia kuja kote kuwili kwa Kristo, lakini msisitizo unawekwa wapi zaidi? Inaonekana kwangu kwamba unabii mwingi wa Agano la Kale linalenga kwenya kuja kwa mara ya kwanza, kuanzishwa kwa ufalme wa kimasiya (rejea Danieli 2). Katika Agano la Kale mkazo upo kwenye kutawala milele kwa Mungu, na namna ya kushihirishwa huko kwa utawala ni huduma ya Masiya (rejea 1 Wakorintho 15:25-27). Sio swali la kipi ni kweli; yote ni kweli, lakini mkazo upo wapi? Lazima isemwe kwamba baadhi ya Watafsiri wanajikita sana kwenye kutawala milele kwa Masiya (rejea ufahamu wa kumuktadha kwenye Ufunuo 20) kwamba wamepoteza shabaha ya kibiblia kwenye kutawala milele kwa Baba. Kutawala kwa Kristo ni tukio la utangulizi. Kuja kwa Kristo kote hakukuwa wazi katika Agano la Kale, wala kutawala kwa muda kwa Masihi!

Msingi wa kuhubiri kwa Yesu na kufundisha ni ufalme wa Mungu. Ni vyote (wokovu na huduma), na baadae (katika kuendelea na nguvu). Ufunuo kama shabaha yake ni utawala wa kimelenia wa Masiya (rejea Ufunuo 20), ni utangulizi, sio kilele (Ufunuo 21-22). Haiku wazi katika Agano la Kale kwamba utawala wa Muda ni muhimu; kwa kusema kweli, kutawala kwa Masiya kwa Danieli 7 ni milele, si kwa kwa millennia.

MVUTANO WA SITA (kurudi kwa Kristo kunakotarajiwa dhidi ya kuchelewa kurudi mara ya pili (*parousia*))

Waaminio wengi wamefundishwa kwamba Yesu anakuja hivi karibuni, punde na bila kutegemea (rejea. Mathayo 10:23; 24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30; Ufunuo 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; Lakini kila kizazi kilichotegemea kilikuwa kimekosea! Uharaka (mapema) wa kuja kwa Yesu ahadi yenye nguvu ya tumaini la kila kizazi, lakini uhalisia ni kwa mmoja (na huyo ni Yule apitiaye dhiki). Waaminio laziima waishi kama vile Anakuja kesho, lakini waweke mipango na kufanyia kazi Agizo Kuu (rejea Mathayo 28:19-20) kama akikawia.

Baadhi ya vifungu katika Injili na Wathesalonike wa 1 na 2 yamejikita kwenye kukawia kwa Kuja kwa Mara ya Pili (*Parousia*). Kuna matukio ya kihistoria ambayo lazima yatimie kwanza;

1. Kuhubiriwa kwa ulimwengu wote (rejea Mathayo 24:14; Marko 13:10)
2. Kufunuliwa kwa “mwanadamu mwenye dhambi” (rejea Mathayo 24:15; 2 Wathesalonike 2; Ufunuo 13)
3. Dhiki kuu (Mathayo 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata wa kimakusudi (rejea Mathayo 24:42-51; Marko 13:32-36)! Ishi kila siku kama vile ndiyo siku yako ya mwisho ila panga na pata mafunzo kwa ajili ya huduma ya baadaye!

UTHABITI NA USAWA

Lazima isemwe kwamba shule mbalimbali za utafsiri wa matukio ya siku za mwisho yote yana ukweli nusu. Wanaelezea na kutafsiri vyema baadhi ya vifungu. Tatizo linakuja katika kuendelea na kutafuta ulali wa usawa. Mara nyingi kuna mapendekezo yanayotumia vifungu vya Biblia kujazilizia katika mifupa ya kithiolojia zilizoandaliwa. Biblia haifunui mfuatano mzuri, mpangilio wa siku za mwisho. Ni kama albamu ya picha ya familia. Picha zile ni za kweli ila haziko katika mpangilio, mazingira na katika mfuatano. Baadhi ya picha zimeanguka kutoka nje ya albamu na kizazi kingine cha wanafamilia hawajui namna ya kuzirudisha tena. Msingi wa kupata tafsiri sahihi ya Ufunuo ni lengo na mwandishi wa awali kama ilivyofunuliwa katika aina ya uandishi wake. Watafsiri wengi sana wanajaribu kubeba vifaa vyao na taratibu zao kutoka katika aina ya uandishi wa Agano Jipya kwenda katika Tafsiri zao za Ufunuo. Wanaweka shabaha zao katika Agano la Kale badala ya kuruhusu mafundisho ya Yesu na Paulo kutengeneza muundo wao wa kithiolojia na kuacha Ufunuo uwe kama kielelezo.

Lazima ni kubali kuwa nakabili maoni haya ya Ufunuo kwa hofu na uoga, si kwasababu ya laana ya Ufunuo 22:18-19, lakini kwasababu ya kiwango cha mgongano na kutofautiana kwa tafsiri ya kitabu hiki uliosababishwa na kuendelea kusababisha katika ya watu wa Mungu. Napenda Ufunuo wa Mungu. Ni kweli pale ambapo wanadamu wote ni waongo (rejea Warumi 3:4)! Tafadhali tumia Maoni haya kama jaribio la kuamsha mawazo na sio kutoa maana, kama kibao cha kukuonesha uendapo na sio ramani ya barabara, kama “vipi ingekuwa,” nana sio “hilo ndilo neno la Bwana.” Nimekutana uso kwa uso na mapungufu yangu mimi mwenyewe, upendeleo na ajenda za kithiolojia. Nimeona pia zile za Watafsiri wengine. Inakuwa inaonekana watu wanatafuta katika Ufunuo wanachokitegemea kikipata. Aina yenyewe ya uandishi inapelekea matumizi mabaya! Hata hivyo, ipo katika Biblia kwa makusudi. Kimewekwa kama “neni” la hitimisho na sio kwa ajali au bahati mabaya. Kina ujumbe wa Mungu

kwa watoto Wake wa kila kizazi. Mungu anataka tuelewe! Hebu tuungane, sio kutengeneza vijiwe; tukubali yale yaliyo ya kweli, wazi na yenye dhamira kuu, sio yale yanayoweza kuwa au kufanyika kuwa ya kweli. Mungu atusaidie sisi sote!

Tumia nafsi hii kuorodhesha madhanio yako mwenyewe kutafsiri Ufunuo. Sisi sote tulete upendeleo wetu katika kutafsiri kitabu hiki. Kubainisha kunatusaidia kukabiliana nayo na kushinda nguvu yake na kuweka mipaka katika misimamo yetu ya kidini.

- 1.
- 2.
- 3.
- 4.

UTANGULIZI WA UFUNUO

I. MAELEZO YA UFUNGUZI

- A. Wakati mwingi wa maisha yangu ya utu uzima ya taaluma/thiolojia nilikuwa na dhana kuwa wale wanaoamini Biblia huichukulia “kawaida” (na huo ndo ukweli wa masimulizi ya kihistoria). Ingawa imekuwa wazi zaidi kwamba kwangu kuufanya unabii, ushairi, maandiko yanayotabiri mwisho wa dunia kawaida ni kukosa uvuvio uliokusudiwa wa andiko hilo. Kusudio la Mwandishi na sio ukawaida wa maandiko ndio ufunguo wa kuelewa Biblia katika usahihi wake. Kuifanya Biblia iseme zaidi (kubainisha mafundisho ya kidhehebu) ni hatari sana na ni upotoshaji kuitafsiri katika namna ambayo itafanya iseme kidogo kuliko ilivyokusudiwa mwanzoni na mwandishi aliyevuviwa. Lengo linatakiwa kuwa na muktadha mpana, mazingira ya kihistoria na lile kusudio lililoainishwa na mwandishi katika andiko na katika uchaguzi wake wa mbinu ya uwasilishaji. Namna ya uwasilishaji ni makubaliano ya kifasihi kati ya mwandishi na msomaji. Kutolielewa jambo hili hakika hupelekea katika upotoshaji wa tafsiri sahihi.

Kitabu cha ufunuo sio masimulizi ya kihistoria bali ukweli wa uhakika ambao hautakiwi kuchukuliwa kawaida kawaida. Namna ya uwasilishaji wenyewe kinapaza sauti kutwambia jambo hili iwapo tutakuwa tayari kusikia tu. Hii haina maana kuwa hakina uvuvio au kuwa si kweli bali ni vile tu kiko kitamathali, kimefumbwa kimaana, kimetumia lugha ya ishara, chenye ulinganifu na taswira. Wayahudi na wakristo wa karne ya kwanza walielewa sana aina hii ya maandiko kuliko sisi! Ishara za ukristo katika *“The Lord of the Rings”* au *“The Chronicles of Narnia”* zinaweza zikawa sambamba na zile za kisasa.

- B. Ufunuo kipekee kabisa ni fasihi yenye uwasilishaji wa maandishi ya Kiyahudi juu ya mambo yajayo. Namna hii ilikuwa ikitumika mara nyingi nyakati zilizojaa mivutano (kama vile Israeli ilipokuwa ikitawaliwa na mataifa) kuelezea imani kuwa Mungu anashughulika na mambo yao na historia yao na kuwa angeleta ukombozi kwa watu wake. Aina hii ya uandishi ina tabia zifuatazo;
1. Hisia kali ya kutambua kwa dhati ukuu wa Mungu (Imani kwa Mungu mmoja na udhabiti)
 2. Mashindano kati ya wema na uovu, zama hizi za uovu na zama za haki zitakazokuja (kuwepo kwa pande mbili)
 3. Matumizi ya alama katika maneno ya siri (mara nyingi kutoka katika agano la kale au, kutoka miongoni mwa maandiko ya Kiyahudi ya nyakati zijazo kati ya agano la kale na agano jipya.
 4. Matumizi ya rangi, wanyama, na wakati mwingine binadamu.
 5. Matumizi ya upatanisho wa kimalaika kwa njia za maono na ndoto lakini mara nyingi kupitia tafsiri za malaika
 6. Kuweka msisitizo na mkazo katika matukio ya hali ya hewa ya siku za mwisho au nyakati mpya zijazo punde.
 7. Matumizi ya seti za alama za kudumu pasipo uhalisia kuzungumza ujumbe wa Mungu juu ya siku/nyakati za mwisho.
 8. Baadhi ya mifano ya aina hii ya uwasilishaji ni kama
 - (a) Agano la Kale
 - (1) Isaya 13-14, 24-27, 56-66
 - (2) Ezeieli 1:26-28, 33-48
 - (3) Danieli 7-12
 - (4) Joeli 2:28 – 3:21
 - (5) Zakaria 1-6, 12-14
 - (b) Agano jipya
 1. Mathayo 24, Marko 13, Luka 21 na I Wakorintho 15 (katika baadhi ya maeneo)
 2. II Wathesalonike 2 (katika namna nyingi zaidi)
 3. Ufunuo (Sura 4-22)
 - (c) Danieli 7-12 na ufunuo 4-22 ni mfano halisi wa aina hii ya uandishi katika Biblia
 9. Vitabu visivyopitishwa visivyohusu sheria za kanisa (imechukuliwa kutoka kwa D.S. Russel, *The Method and Message of Jewish Apocalyptic*, ukurasa wa 37 – 38
 - a. I Enoch, II Enoch (The Secrets of Enoch)

- b. The Book of Jubilees
 - c. The Sibylline Oracles III, IV, V
 - d. The Testament of The Twelve Patriarchs
 - e. The Assumptions of Moses
 - f. The Psalm of Solomon
 - g. The Martyrdom of Isaiah
 - h. The Apocalypse of Moses (Life of Adam and Eve)
 - i. The Apocalypse of Abraham
 - j. The Testament of Abraham
 - k. II Esdras (IV Esdras)
 - l. II & III Baruch
10. Kuna hali ya kuwepo kwa pande mbili katika namna ya uandishi huu. Inauangalia ukweli katika mfuatano wa pande mbili, kwa kuonyesha utofauti kwa kulinganisha, au kuvutana (hii imeonekana sana katika maandiko ya Yohana) kati ya;-
- a. Mbingu na nchi
 - b. Zama za uovu (binadamu waovu na malaika waovu) – zama mpya za haki (wanadamu wacha Mungu na malaika wenye hofu ya Mungu)
 - c. Ulimwengu wa sasa - ulimwengu ujao
- Haya yote yanaelekea katika kilele na ukamilisho unaoletwa na Mungu. Hii si nchi ambayo Mungu alikusudia iwe bali yeye anapanga na kufanya kazi kukamilisha mapenzi yake ya uhusiano wake wa karibu aliouasisi katika bustani ya ya Edeni. Tukio la Kristo ni alama na kiashiria muhimu cha mpango wa Mungu lakini vitu hivyo viwili vinaletwa na hali ya kuwepo kwa pande mbili.

C. Kazi hizi za utabiri juu ya mwisho wa nchi hazijawahi kuwasilisha kwa njia ya mdomo; bali siku zote ziliandikwa. Ni kazi za fasihi zenye muundo madhubuti sana. Muundo wake ni muhimu sana ili kupata tafsiri sahihi. Sehemu kubwa ya mpango uliopangwa wa kitabu cha ufunuo ni vipengele saba vya fasihi ambavyo vina uelekeo unaofanana katika baadhi ya maeneo (kama vile mihuri saba, baragumu saba, na vitasa saba). Katika kila mzunguko hukumu inaongezeka; mihuri, $\frac{1}{2}$ uharibifu; baragumu, $\frac{1}{3}$ uharibifu, vitasa, uharibifu kamili; katika kila kipengele cha kuja kwa mara ya pili kwa Kristo au matukio ya vifo, kuzimu, hukumu na mbingu vinatokea; (1) mihuri wa 6, ufunuo 6:12-17; (2) baragumu saba, ufunuo 11:15-18, hukumu ya malaika ya mwisho katika ufunuo 14:14-20; (3) vitasa saba, ufunuo 16:17-21 na tena katika ufunuo 19:11-21, na pia katika ufunuo 22:6-16 (pia chunguza sehemu tatu katika cheo cha Mungu) katika ufunuo 1:4, 8 na Kristo katika ufunuo 1:17, 18, “Yeye aliyeko, “Yeye aliyekuwako” na utagundua sehemu ya ajaye imeachwa katika ufunuo 11:17 na ufunuo 16:5 jambo hili likimaanisha kuwa milele imekwisha kuja (kuja kwa mara ya pili) hii ina maanisha kitabu hakifuati utaratibu wa kupanga miaka na matukio kwa mfuatano au mfululizo bali ni tamthiliya katika vipengele kadhaa vinavyoonesha nyakati zijazo kwa wakati mmoja kwa kuendelea kwa nguvu na kwa namna ya hukumu ya Agano la kale la kurudiarudia (kutoka kwa James Blems, *Revelation as Drama and “The Genre of Revelation” in Review and Expositor*, Septemba. 1980, ukurasa 393-408)

Kuna sehemu saba za fasihi ukijumlisha sehemu ya utangulizi na hitimisho

1. Utangulizi ufunuo 1:1-84
2. Ufunuo 1:9-3 (Kristo na Mekanisa saba)
3. Ufunuo 4-8:1 (Mbingu na mihuri saba [Ufunuo 2:1-17 baada ya muda kati ya mihuri wa 6 na 7])
4. Ufunuo 8:2-11 (Malaika saba wenye baragumu [Ufunuo 10:1-11:13 baada ya muda kupita kati ya baragumu cha 6 na saba])
5. Ufunuo 12-14 (Jamii mbili na viongozi wake)
6. Ufunuo 15-16 (Malaika saba na vitasa)
7. Ufunuo 17_19 (Babeli na hukumu yake)
8. Ufunuo 20-22:5 (Hukumu na mbingu mpya na nchi)
9. Hitimisho, ufunuo 22:6-21

Mwandishi mwingine aliyeamini katika dhana ya kurudiarudia kwa muhtasari na ufupisho ni William Hendriksen. Katika kitabu chake, *More Than Conquerors*, anafafanua kitabu ifuatavyo;

1. Ufunuo 1-3 (Kristo katikati ya vinara vya taa)
2. Ufunuo 4-7 (kitabu chenye mihuri saba)
3. Ufunuo 8-11 (baragumu saba za hukumu)
4. Ufunuo 12-14 (Mwanamke na mwana wa binadamu ateswavyo na joka na wasaidizi wake[mnyama na kahaba])
5. Ufunuo 15-16 (vitasa saba za ghadhabu)
6. Ufunuo 17-19 (anguko la kahaba na mnyama)
7. Ufunuo 20-22 (hukumu juu ya joka ikifuatiwa na mbingu mpya na nchi, Yerusalemu mpya, ukurasa wa 28)

Katika *More Than Conquerors*, William Hendriksen anasema kuwa Ufunuo una sehemu saba: Ufunuo 1-3;4-7;8-11; 12-14; 15-16; 20-22 na kila sehemu hii inaenda sambamba na kuchukua kipindi kati ya kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza na kuja kwa Kristo kwa mara ya pili. Kila kimoja kinaisha na sehemu inayohusiana na hukumu na kuja kwa mara ya pili (ukurasa wa 22-31).

Ingawa naamini kwa hakika katika usambamba wa tamthiliya ya mihuri, baragumu, na vitasa na pia navutiwa sana na 17-19 vile ilivyo sambamba na 20-22 (kuna kuja kwa mara ya pili katika ufunuo 19:11-21 na kuja kwa mara ya pili tena katika Ufunuo 22:6-15; angalia kwa umakini mstari wa 15; uovu haujaondolewa bado, kama vile katika Ufunuo 19:14-15), sioni mahali vipengele hivi vinapoishia katika kurudi kwake mara ya pili (*Parousia*), hasa katika sura 1-3, labda kuwepo na kipengele cha hukumu kinachoonekana kama tukio la mwisho wa nchi (linganisha Ufunuo 2:5, 7, 11, 16-17, 25-26; 3:5, 10, 12, 18-21). Hata hivyo, kwangu mimi, kurudia rudia kwa namna ya sehemu saba inatengeneza zaidi na zaidi uwezekano wa uelewa sambamba na muundo wa kitabu chote.

D. Ni wazi kuwa namba “saba” inachangia sehemu kubwa katika muundo wa kitabu kama ambayo inaweza kuonekana kutoka katika makanisa saba, mihuri saba, baragumu saba, na vitasa saba. Mifano mingine yenye “saba” ni:

1. Baraka saba, Ufunuo 1:3; 14;13 16:15; 19:9; 20:6; 22:7, 14
2. Vinara vya taa saba, Ufunuo 1:12
3. Roho saba za Mungu, Ufunuo 1:4; 3:1 4:5; 5:6
4. Nyota saba, Ufunuo 1:16, 20; 2:1
5. Taa saba za moto, Ufunuo 4:5
6. Mihuri saba katika kitabu, Ufunuo 5:1
7. Pembe saba, macho saba ya mwana kondoo, Ufunuo 5:6
8. Sifa saba ya Yesu kusifiwa, Ufunuo 5:12
9. Ishara saba za kiasili, Ufunuo 6:12-14
10. Aina saba za watu, Ufunuo 6:15
11. Sifa saba za Mungu anayesifiwa, Ufunuo 7:12
12. Malaika saba wakaa mbele za Mungu, Ufunuo 8:2, 6
13. Baragumu saba zibebwazo na malaika saba, Ufunuo 8:6 (Ufunuo 15:1, 6, 7, 8; 17:1; 21:9)
14. Ishara saba, Ufunuo 12: 1, 3; 13: 13, 14, 15:1; 16:14; 19:20
15. Vichwa saba, vilemba saba vya joka mwekundu, Ufunuo 12:3
16. Vichwa saba vya mnyama wa majini, Ufunuo 13:1; 17:3, 7
17. Malaika saba, Ufunuo 14:6-20
18. Mapigo saba, Ufunuo15:1; 21:9
19. Milima saba, Ufunuo 17:9
20. Wafalme saba, Ufunuo 17:10
21. Vitu saba visivyokuwepo tena katika sura ya 21-22 (Ufunuo 21:1, 4 [mara nne]; Ufunuo 21:25; 22:3)

- E. Tafsiri ya kitabu hiki inaweza changiwa sana na elimu ya thiolojia. Dhana za mtu zinaweza kupelekea maelezo yaliyo na maana zaidi ya moja. Dhana hizi za kithiolojia zinafanya kazi katika viwango Fulani
1. Asili ya ishara
 - a. Dokezo za Agano la kale
 - (1) Mada za agano la Kale kama uumbaji, anguko,, gharika, kutoka, urejesho wa Israeli
 - (2) Mamia ya madokezo (yasiyonukuliwa moja kwa moja) kutoka katika Agano la kale la Manabii
 - b. Maandiko ya Kiyahudi ya kati ya maagano (I Enoch, II Baruch, Sibylline Oracles, II Esdras)
 - c. Karne ya kwanza ya kipindi cha Wagiriki-Waroma
 - d. Hesabu ya kuumbwa kwa ulimwengu ya Near Eastern ya kale (haswa Ufunuo 12)
 2. Muda wa kuanza na kumalizika kwa kitabu
 - a. Karne ya kwanza
 - b. Kila karne
 - c. Kizazi cha mwisho
 3. Utaratibu wa vipimo vya ki-thiolojia (angalia maana katika ukurasa wa 14, "Historical Theories of Interpretation" C; a good summary, *Four Views on the Book of Revelation*, Ed. C. Marvin Pate)
 - a. Wenye mlengo wa kuwa matukio haya yalishatimia (Preterist)
 - b. Wanye mlengo kuwa matukio yanayotokea yako juu ya uwezo wa binadamu. (Historicist)
 - c. Wenye mlengo wa mambo yajayo (Futurist)
 - d. Wenye mlengo wa nadharia (idealist)
 4. Nafasi ya Theolojia katika sura ya 20 (angalia jedwali katika ukurasa wa 193; good summaries: (1) *The Meaning of the Millennium: Four Views*, ed. Robert G Clouse and *Three Views of the Millennium and Beyond*, ed. Darrell L. Bock)
 - a. Milenia
 - b. Baada ya Millenia
 - c. Kabla ya Millenia
 - d. Mgawanyo wa kabla ya millennia

Katika mwanga wa kugawanyika kwa katika elimu ya kutafsiri maandiko (mbinu tofauti za kutafsiri) na imani zisizo sahihi (mtazamo wa kujua kila kitu), mtafsiri anawezaje kuendelea?

 1. Tukubaliane kuwa wakristo wa kisasa hawana uelewa wa namna ya kutambua dhana za kihistoria kama waliyokuwa nayo wakristo wa kwanza namna ambavyo wangeelewa.
 2. Tukubaliane kuwa kila kizazi cha Wakristo kimelazimisha Ufunuo katika mazingira yao wenyewe ya kihistoria na wote wamekosea mpaka hapo.
 3. Tujitahidi kusoma Biblia zetu kabla ya kusoma mifumo na utaratibu wa ki-thiolojia. Angalia muktadha ama mazingira ya maandiko ya kila maono na hali ya ukweli mkuu katika tamko moja la andiko. Ukweli utabaki na kusimama kwa kila kizazi wakati umaalumu wa maelezo yanaweza kuwa ya kwa jili ya kizazi cha kwanza tu na au kizazi cha mwisho cha waamini. Maelezo yanaweza kuwa na mahusiano, lakini historia, itafunua utimilifu wake.
 4. Tukumbuke kwamba kitabu hiki kimekusudiwa hasa kuwa neno la faraja na kutia moyo katika uaminifu katikati ya dhiki wanazofanywa na wasioamini kwa waaamini. Kitabu hiki hakijakusudiwa kutoa majibu ya shauku ya kila kizazi cha waaminio, hakikusudiwa kutoa ufafanuzi wa kina wa matukio ya siku za mwisho.
 5. Ni salama kukiri kuwa jamii iliyoanguka ya binadamu ipo katika mgongano na ufalme wa Mungu. Mwanzoni yaweza kuonekana kama uli wengu umeshinda (kama Kalvari), lakini subiri; Mungu ni mwenye uwezo wote, yeye ndiye anaye endesha historia, ya maisha na mauti. Watu wake ni washindi ndani yake!
- F. Licha ya ugumu na utata wa tafsiri, kitabu hiki kina ujumbe na ni neno la Mungu lililovuviwa kwa ajili ya watu wake katika kila kizazi. Kitabu hiki cha kipekee kinastahili kuwekewa nguvu ya ziada ya makusudi kukisoma. Nafasi yake katika azimio la kikanoni la Agano Jipya ni alama ya ujumbe wake. Alan Johnson, *The Expositor's Bible Commentary*, Vol. 12, kinasema "Hakika, inawezekana kabisa kuwa ukiacha vitabu vya Injili, vitabu vinavyoonyesha mwisho wa nchi vimejaa mafunzo mengi ya msingi katika mafundisho ya

Ukristo na uanafunzi kuwahi kuwepo katika Maandiko Matakatifu. Haitakiwi hata ulokole wa baadhi ya watu walioweka mkazo wao mkubwa katika unabii zaidi ya Kristo, bila hata kuzingatia mgawanyiko uliopo wa namna ya kinavyotafsiriwa unatakiwa utukatishe tamaa sisi ya kuutafuta ukweli wa ukristo wetu katika kitabu hiki kizuri sana kwa namna yake” (ukurasa wa 399).

Kumbuka, hakika haya ndiyo maneno ya Yesu kwa kanisa lake! Kanisa la leo halitakiwi kujaribu kuyapuuza au kuyapunguza! Yamekusudiwa kuwaandaa waaminio kwa ajili ya dhiki na mgogoro katika ufahamu wa uweza wa Mungu (imani kwa Mungu mmoja), uhalisia wa Yule muovu (upili wenye kikomo), hali inayoendelea ya anguko (uasi wa binadamu), na ahadi za Mungu kumkomboa mwanadamu (agano lisilo na masharti, angalia Mwanzo 3:15; 12:1-3; Kutoka 19:5-6; Yohana 3:16; 2 Wakorintho 5:21).

II. MWANDISHI

A. Ushahidi wa ndani wa uandishi wa Mtume Yohana

1. Mwandishi mwenyewe amejitaja mwenyewe mara nne kama Yohana (rejea Ufunuo 1:1, 4, 9; 22:8)
2. Pia alijiita mwenyewe
 - a. Mtumwa mwaminifu (rejea Ufunuo 1:1; 22:6)
 - b. Ndugu yenu na mwenye kushiriki dhiki (rejea Ufunuo 1:9)
 - c. Nabii (angalia Ufunuo 22:9), na akakiita kitabu chake unabii (rejea Ufunuo 1:3; 22:7, 10, 18, 19)
3. Analijua Agano la kale (hatumii LXX, bali Targums) na nyikani kama kipindi cha upotevu, Sanduku la agano na taratibu za ibada za kisinagogi za wakati huu.

B. Ushahidi wa nje wa uandishi wa Mtume Yohana kutoka kwa waandishi wa kwanza wa Kikristo

1. Mtume Yohana, mwana wa Zebedayo
 - a. Justin Martyr (Rumi, baada ya Kristo mwaka 110-165) katika *Dialogue with Trypho* 81.4)
 - b. Ireneus (Lyons, baada ya Kristo mwaka 120-202) katika *Against Heresies* IV.14.;17.6; 21.3; V.16.1; 28.2; 30.3; 34.6;35.2
 - c. Tertullian (Afrika Kaskazini, kabla ya Kristo mwaka 145-220) katika *Against Prexeas* 27
 - d. Origen (Iskandria, baada ya Kristo mwaka 181-252) katika
 - (1) *On the Soul*, L:8:1
 - (2) *Against Marcion*, II:5
 - (3) *Against Heretics*, III:14, 25
 - (4) *Against Celsus*, IV:6, 32; VIII:17
 - e. Orodha ya kale ya vitabu vya kanuni za kikanisa vya karne ya pili (Muratorian Canon) (Rumi , baada ya Kristo 180-200)
2. Wengineo
 - a. Yohana Marko – Hii ilitajwa kwanza na Dionysius, Askofu wa Mji wa Alexandria (baada ya Kristo mwaka 247-264), yeye alikataa uandishi wa Mtume Yohana lakini akaendelea kuiweka kazi yake katika azimio la Kanoni. Sababu kuu aliyoitoe kwa nini akatae ilijikita katika misamiati na staili yake pamoja na maandiko mengine ya Yohana yasiyoeleweka asili yake. Alimshawishi pia Eusebius wa Kaisaria.
 - b. Yohana mzee – Hii inatokana na nukuu za Eusebius kutoka kwa Papias (*Eccl. Hist.* 3.39. 1-7). Ingawa nukuu ya Papias yumkini ilitumia cheo hiki badala ya Mtume Yohana ili isije ikamaanisha mwandishi mwingine.
 - c. Yohana Mbatizaji – (ikiwa na maboresho ya kiuandishi mengine) imependekezwa na J. Massyngberde Ford katika Anchor Bible Commentary, ikiweka msisitizo wa Yohana Mbatizaji kumuita Yesu “mwanakondoo”. Sehemu nyingine ambapo neon hili linaitwa ni katika kitabu cha Ufunuo.

C. Dionysius, Askofu wa Alexandria (baada ya Kristo mwaka 247-264) na mwanafunzi wa Origen, alikuwa wa kwanza kuonesha mashaka (kitabu chake kilipotea lakini ananukuliwa na Eusebius wa Kaisaria anayekubaliana nae) kwamba uandishi wa Mtu Yohana umejikita katika

1. Mtume Yohana hajitaji kuwa yeye ndiye Yohana Yule wa Injili wala barua zake hazioneshi hivyo lakini Ufunuo unatoka kwa “Yohana”
 2. Muundo wa Ufunuo ni tofauti na Injili na barua zingine
 3. Misamiati ya Ufunuo ni tofauti na Injili na barua zake.
 4. Staili ya kisarufi ya Ufunuo ni ya kinyonge na isiyo na ubora ukilinganisha na ile ya Injili na barua zake
- D. Yawezekana changamoto kubwa kabisa ya kisasa inayokabili uandishi wa Mtume Yohana inatoka kwa R.H.Charles katika Saint John, Vol I p. xxxixff.
- E. Waandishi wengi wa kisasa wamekataa uandishi wa kienyeji wa vitabu vingi vya Agano Jipya. Mfano mzuri wa jambo hili unaohusiana na Ufunuo anaweza akawa Raymond E. Brown, Mtaaluma maarufu wa Kikatoliki wa Johannine. Mfululizo wa toleo la utangulizi la Anchor Bible Commentary linasema, “imeandikwa na Nabii Mkristo wa Kiyahudi aitwaye Yohana ambaye hakuwa Yohana mwana wa Zebedayo wala hakuwa Yohana wa Injili, wala si yule wa Waraka” (ukurasa 774).
- F. Katika namna nyingi uandishi una tiliwa shaka. Kuna mgongano wa usambamba na Maandiko mengine ya Mtume Yohana pia kutofautina sana. Msingi wa kukielewa kitabu hiki haipo katika kujua ubinadamu wa mwandishi bali katika Uungu wa Mwandishi! Mwandishi mwenyewe anajiamini kuwa nabii aliyevuviwa (rejea Ufunuo 1:3; 22:7, 10, 18, 19).

III. TAREHE

- A. Hii kwa hakika inatengeneza muunganiko katika ya uandishi na dhana ya utafsiri (rejea Nadharia za Kihistoria)
- B. Uwezekano wa baadhi ya tarehe
1. Tarehe za kienyeji ni wakati wa utawala wa Domitia (baada ya Kristo mwaka 81-96) kwakuwa inarandana na ushahidi wa ndani wa dhiki.
 - a. Irenaeus (alinukuliwa na Eusebius) katika *Against Heresies*, 5.30.3 “Hii dhiki ilionekana si miaka mingi iliyopita karibu na kizazi chetu, karibu na utawala wa Domitia”
 - b. Clement wa Iskandria
 - c. Asili ya Iskandria
 - d. Eusebius wa Kaisaria, *Church History*, iii.23.1
 - e. Victorinus, *Apocalypse* x.11
 - f. Jerome
 2. Epiphanius, mwandishi wa karne ya tatu, katika *Haer*, 51.12, 32, inasema kuwa Yohana aliandika baada ya kutolewa Patmos wakati wa utawala wa Klaudio (baada ya Kristo mwaka 41-54).
 3. Wengine yawezekana kuwa wakati wa utawala wa Nero (baada ya Kristo mwaka 54-68) kwasababu ya:
 - a. Historia ya mateso ya kidini Mfalme
 - b. *Caesar Nero*, kimeandikwa kwa lugha ya Kiebrania, ikitaja namba za mnyama, 666
 - c. Kama wenye mlengo wa kuwa matukio haya yalishatokea wako sawa kuwa Ufunuo wa Yohana unamaanisha uharibifu wa Yerusalemu, kwahiyo ili kitabu kuwa cha Unabii, lazima kiwe kimeandikwa mwaka 70 baada ya Kristo

IV. WAPOKEAJI

- A. Kutoka Ufunuo 1:4 ni wazi kuwa wapokeaji wa asili yalikuwa makanisa saba katika Jimbo la Rumi huko Asia. Makanisa haya yanaambiwa ujumbe katika namna inayomaanisha ramani ya muwasilishaji wa barua.
- B. Ujumbe wa Ufunuo kipekee una uhusiano na makanisa yote na waaminio wanaopitia hali ya dhiki kutoka katika mfumo ulioanguka wa utawala wa kidunia.
- C. Kama hitimisho la Kikanoni kwa Agano Jipya, kitabu hiki ni ukamilisho wa waaminio wote wa vizazi vyote.

V. MAZINGIRA

- A. Mazingira yalikuwa ni ya dhiki iliyosababishwa na kuachana kwa makanisa kutoka katika ulinzi wa kisheria wa Rumi uliorasmishwa kwa dini ya Kiyahudi. Mgawanyiko huu ulitokea rasmi katika miaka ya 70 baada ya Kristo wakati walimu kutoka Jamnia walirasmisha utaratibu wa kiapo kilichokuwa na sharti la waaminio wa masinagogi kumlaani Yesu wa Nazareti.
- B. Nyaraka za Kirumi zinaonyesha kuwa kumwabudu Mfalme kulileta mtafaruku mkubwa na makanisa kutoka katika kipindi cha utawala wa Nero (mwaka 54-68 baada ya Kristo) mpaka kipindi cha Domitia (81-96 baada ya Kristo). Ingawa hakuna nyaraka zinazoonesha kuenea rasmi kwa dhiki katika ufalme. Kwa uwazi kabisa Ufunuo unaaksi kichocheo cha kitendo cha dini cha kuabudu Mfalme katika Majimbo ya Mashariki ya ufalme wa Rumi (rejea "Biblical Archaeology Review", Mei/Juni 1993 ukurasa wa 29-37)

VI. SARUFI YA MANENO

- A. Kuna matatizo mengi ya kisarufi katika maandiko ya Kiyunani
- B. Baadhi ya sababu za matatizo haya.
 - 1. Mpangilio wa mawazo ya Yohana katika lugha ya Ki-aramaiki.
 - 2. Hakuwa na kitabu cha kuandikwa huko Patmos.
 - 3. Alikuwa na msisimko wa kupitiliza wa maono.
 - 4. Yalikuwa na kusudi ya kutokea kwake
 - 5. Staili ya uwasilishaji wake (juu ya matukio ya mwisho wa nchi) ilijaa sana mafumbo.
- C. Sarufi inayofanana kitabia zinapatikana katika maandiko mengine ya Kiyahudi juu ya mwisho wa nchi. Hivyo, Ufunuo haukuandikwa katika staili dhaifu ya kisarufi bali katika namna pekee kisarufi.

VII. UIDHINISHAJI

- A. Kilikataliwa mapema na kanisa la Mashariki; kitabu hakipatikani katika Peshitta (toleo la tano la Ki-Ashuru)
- B. Mwanzoni mwa karne ya nne ya Eusebius, akifuatiwa na Dionysius wa Alexandria mwishoni kabisa mwa karne ya tatu, ilisemekana kuwa Ufunuo haukuandikwa na Mtume Yohana. Alikitaja kama moja ya vitabu vuisivyoeleweka japo alinijumuisha katika idadi ya vitabu vya Kikanoni (rejea Ecclesiastical History, III.24.18; III.39.6).
- C. Baraza la Laodikia (miaka ya 360 baada ya Kristo) ilikiondoa katika orodha ya vitabu vya kikanoni. Jerome alikikataa kuwa hakiwezi kuwa kikanoni, lakini baraza la Carthage (mwaka 397 baada ya Kristo) likiingiza katika orodha. Ufunuo kiliingizwa na kukubaliwa kwa mapatano ya kishingo upande kati ya makanisa ya Mashariki na Magharibi ambapo vitabu vyote vya Waebrania na Ufunuo vilikubaliwa kuingia katika Agano Jipya kama azimio la Kikanoni.
- D. Lazima tutambue kuwa ni dhana ya imani ya Waaaminio kwamba Roho Mtakatifu alisimamia na kuongoza mchakato wa kihistoria wa kutengeneza Kanoni ya Kikristo.
- E. Wanathiolojia wakubwa wa mwanzo wa Mageuzi ya Kiprotestant walikataa nafasi yake katika mafundisho ya Kikristo.
 - 1. Martin Luther alikitaja kuwa hakikuwa cha kinabii wala kitume, kiuhalisia alikataa uvuvio wake.
 - 2. John Calvin, aliyeandika Mwongozo katika kila kitabu cha Agano Jipya isipokuwa Ufunuo, kiuhalisia alikataa uhusika wake.

VIII. DHANA ZA KIHISTORIA ZA UTAFSIRI

- A. Kinasifika kwa kuwa kigumu kutafsiri; hivyo, kulazimisha imani fulani ni jambo lisilofaa!

B. Ishara zake zimetolewa kutoka

1. Aya za siku za mwisho wa ulimwengu katika
 - a. Danieli
 - b. Ezeieli
 - c. Zakaria
 - d. Isaya
2. Maandiko ya kiyahudi ya siku za mwisho wa nchi ya maagano.
3. Mazingira ya kihistoria ya karne ya kwanza ya Wagiriki-Warumi (hasa Ufunuo 17)
4. Maelezo ya hadithi za kubuni za uumbaji katika Near Eastern kongwe (hasa Ufunuo 12).

C. Kwa ujumla kuna dhana nne za utafsiri

1. WENYE MLENGO KUWA MATUKIO HAYA YAMEKWISHA TOKEA – kundi hili linakiona kitabu hiki kama chenye kuweka msingi sana wa mahusiano na makanisa ya kwanza katika majimbo ya Kirumi ya Asia. Maelezo mengi na unabii ulitimilizika katika karne ya kwanza (angalia John L. Bray, *Matthew 24 Fulfilled*)
2. WENYE MLENGO KUWA MATUKIO YANAYOTUKIA YAKO JUU YA UWEZO WA BINADAMU – kundi hili linaangalia kitabu kama mapitio tu ya Kihistoria, kikazo ustaarabu wa Magharibi na katika hali Fulani pia Kanisa la Kirumi la Kikatolic. Mara zote barua kwa makanisa saba kwa sura za pili na tatu zinatumika kama kufunua vipindi fulani vya muda. Wengine wanaliona hili kama uonishaji wa muda mfupi tu na wengine wakitazama kuwa zinatoa utaratibu mzuri wa mpangilio wa matukio.
3. WENYE MLENGO WA BAADAE – kundi hili linaona kitabu hiki kuwa kinayazungumzia zaidi matukio yajayo yatakayotangu;lia na yatayofuatia *Parousia* (Kuja kwa Kristo mara ya pili) ambayo kimaandiko na kihistoria lazima itimie (rejea *Progressive Dispensationalism*, kilichoandikwa na Craig A. Blaising na Darrell Bock).
4. WENYE MLENGO WA NADHARIA – kundi hili linakitazama kitabu kama ishara kabisa ya mashindano kati ya wema na uovu kisicho na rejea za kihistoria (angalia Ray Summers, *Worthy Is the Lamb*; William Hendriksen, *More Than Conquerors*).

Wote hawa wanazungumza ukweli, ila wanashindwa kuuona utata wa kimakusudi unaosababishwa na taswira na aina ya njia aliyoichagua Yohana katika uwasilishaji wa ujumbe. Tatizo hapa ni uwasa wa kimizani, na sio nani yuko sahihi.

IX. KUSUDI LA KITABU HIKI

- A. Kusudi la kitabu cha Ufunuo ni kuonesha ukuu wa Mungu katika historia na ahadi ya kilele cha mambo yote katika Yeye. Waaminifu wanatakiwa kudumu katika imani na matumaini katikati ya dhiki na uchokozi wa mfumo wa dunia hii ulioanguka. Lengo la kitabu ni dhiki (kuabudu mfalme katika majimbo ya Mashariki) na uaminifu (walimu wa uongo na maridhiano ya kiutamaduni) wa waaminio katika karne ya kwanza na katika kila karne (rejea Ufunuo 2:10). Kumbuka, manabii walizungumza juu ya mambo yajayo katika jitihada za kufanya mageuzi ya wakati uliopo. Ufunuo haujakita tu juu ya itakavyomalizika, ila pia jinsi inavyoendelea. Katika makala yake katika *The Expositors Bible Commentary*, Vol I yenye kichwa cha habari “The Eschatological of The Bible,” Robert L. Sancy alisema, “Manabii wa kibiblia hawakujali sana kuhusu muda na upangiliaji mzuri wa matukio yajayo. Kwao hali ya kiroho waliyokuwa nayoo wakati huo ndiyo iliyobeba umuhimu mkubwa na kutembelewa na Mungu kwa ajili ya siku za mwisho na hukumu ya wasio haki na Baraka za Wacha Mungu zinachachawizwa kwa matokeo yake ya kimaadili ya wakati tulionao” (ukurasa wa 104).
- B. Kusudi kuu linawekwa vyema ki-muhtasari katika utambulisho mfupi wa matoleo ya tafsiri ya TEV na NJB.
 1. TEV, ukurasa wa 1122, “Ufunuo wa Yohana uliandikwa wakati ambapo Wakristo walikuwa wanapitia dhiki kwasababu imani ya kumkiri kwao Kristo Yesu kama Bwana. Kusudi kuu la mwandishi ni kuwapa wasomaji wake tumaini nakuwatia moyo, na pia kuwasih kuendelea kuwa waaminifu wakati wa mateso na dhiki”
 2. NJB, ukurasa wa 1416, “Biblia inajumuishwa katika muhtasari katika ujumbe wa tumaini na utajiri mkubwa wa ishara wa kitabu hiki. Ni maono ya ukombozi kutoka katika majaribu ambayo yanawapata

watu wa Mungu, na ahadi ya utukufu ujao. Ujumbe unawasilishwa kwa namna ya taswira zinazotokana na Biblia nziama, ili kila sifa ya mnyama, rangi, tarakimu, zinaamsha hisia na zimejaa vidokezo halisi kwa msomaji wa Agano la Kale. Katika namna hii ni siri na ni Ufunuo wa kudokeza yajayo, licha ya ishara ya asili kuwa ishara kubwa ya matendo yakuabudu na maono ya mwisho ya mg'ao wa kimasiya wa Mji Mpya Mtakatifu kuwa dhahiri kabisa. Kuliwahi kuwa na desturi ya uandishi wa namna hii katika Uyahudi kutoka kwa Daniel na kuendelea, hii ni kuimarisha watu wa Mungu katika dhiki kwa uhakika wa hatimaye kupata ukombozi na ushindi”

C. Ni muhimu sana kuwa mtafsiri atoe kipaumbele cha hoja ya ukombozi.

1. Mungu ameleta wokovu wa mtu, watu na ulimwengu mzima kupitia Kristo.
2. Ukombozi wa Mungu ni wa vyote yaani roho na mwili. Kanisa linaokolewa lakini si salama! Siku moja litakuwa salama!
3. Mungu bado anawapenda walioanguka, wakaidi, wabinafsi. Gadhabu ya Mungu katika muhuri na baragumu ni kwa ajili ya Ukombozi (rejea Ufunuo 9:20-21; 14:6-7; 16:9, 11; 21:6b-7; 22:17).
4. Sio tu kwamba Mungu anarejesha mwanadamu, lakini pia uumbaji ulioanguka (rejea Warumi 8:18-25). Uovu katika kiwango chochote kitasafishwa!

Hali ya Mungu kujaribu tena na tena kumfikia mwanadamu aliyepotea kwa Injili kunakuza tabia ya Kurehemu aliyonayo Mungu. Hukumu ya Kitasa ni matokeo ya uovu usiovumilika, na si kwamba Mungu amekosa upendo. Mungu yeye hutoa hukumu na kuutenga uovu pale tunapokataa kutubu tena na tena. Katika namna nyingi kitabu kinahalalisha hukumu ya Mungu kwa walioanguka, binadamu wasiokubali kupatanishwa! Kitabu kinahitimisha kwa ukaribisho wa Injili (rejea 22:17).

D. Kitabu hiki hakitakiwi kuonekana kama mchoro wa utaratibu wa matukio, nyakati, na namna ya Kuja kwa Mara ya Pili. Imekuwa mara kwa mara ikitafsiriwa kama “siri” kwa historia ya Magharibi (makanisa saba kuonekana kama nyakati). Kila kizazi kimelazimisha historia yake yenyewe kuwa ishara ya mwisho wa nchi; mpaka hapa kila mmoja amekosea.

Maelezo ya unabii huu yatakuwa dhahiri zaidi katika kizazi cha mwisho cha waaminio watakaoteseka chini ya Mpinga Kristo (rejea 2 Wathesalonike 2). Tafsiri za kawaida umesababisha kitabu hiki kususiwa na baadhi (Calvin), kutopewa thamani na wengineo (Luther, “si cha kitume wala cha kinabii”), na kupewa msisitizo uliopitiliza na baadhi (wenye mlengo wa kimelenia).

X. MWONGOZO WA BOB WA UTAFSIRI

A. Tunahitajika kuangalia baadhi ya vipengele vya Agano la Kale

1. Aina ya uandishi kuhusu mwisho wa nchi wa Agano la Kale umejaa ishara nyingi.
2. Vidokezo kadhaa vimepakuliwa kutoka katika Agano la Kale (wengine wanakadiria kuwa ni kati ya mistari 404, mistari 275 inajuisha madokezo kutoka katika Agano la Kale); maana ya ishara hizi zimetafsiriwa tena katika namna ya ufahamu wa hali ya karne yya Kwanza ya Kirumi.
3. Dalili ya unabii inachukua matukio ya sasa kuonyesha dalili ya matukio yajayo ya mwisho wa nchi. Mara nyingi kutimilizwa kwa matukio haya ya kihistoria ya karne ya kwanza kunapelekea kutimilizwa kwa siku za mwisho kihistoria.

B. Muundo mzima wa kitabu unatusaidia kuona makusudi ya mwandishi

1. Mihuri, baragumu, vitasa kimsingi vinachukua muda ule ule (Ufunuo 6-16). Ufunuo ni hadithi ya matendo yanayofululiza.
2. Inawezekana kuwa Ufunuo 17-19 ni sambamba na Ufunuo 20-22. Sehemu za sura ya 19 (kama vile 19:11-21) zinarudiwa katika Ufunuo 20: 7-10.
3. Angalia vipengele vya uandishi katika Maelezo ya Ufunguzi, C.

C. Mukadha wa kihistoria lazima uzingatiwe katika kila tafsiri ya kitabu

1. Uwepo wa kumuabudu Mfalme
2. Dhiki katika Majimbo ya Mashariki.

3. Biblia haiwezi kuwa na maana ambayo haikukusudiwa. Tafsihi ya Ufunuo lazima iwe na uhusiano na nyakati za kwanza za Yohana. Inaweza kutimilizwa kwa namna mbalimbali au kutumiwa, lakini lazima ijikite katika karne ya kwanza.
- D. Maana za baadhi ya maneno ya kimapumbo hatuyafahamu na yamepoteza maana kwetu kwasababu ya utamaduni, lugha na mazingira yetu. Inawezekana matukio ya mwisho yenyewe yatatupatia ufahamu juu ya tafsihi sahihi ya ishara hizi. Kuwa mwangalifu usije ukasukumia maelezo yote katika tamthiliya ya kutukia kwa mwisho wa nchi. Watafisi wa kisasalazima watafute kweli kuu katika kila maono.
- E. Naomba nijumuishe baadhi ya vipengele vya miongozo ya kutafsihi
1. Historia ya asili ya ishara
 - a. Mada za Agano la kale, madokezo ya Agano la Kale
 - b. Visasili vya Near Eastern ya kale
 - c. Maandiko kati ya agano la kale na agano jipya ya siku za mwisho
 - d. Mazingira ya karne ya kwanza ya Wagiriki-Warumi
 2. Njia za mwandishi za kutoa maana za ishara
 - a. Mazungumzo na malaika waongozaji
 - b. Tenzi za kwaya za kimbangu
 - c. Maana zinazotolewa na mwandishi mwenyewe
 3. Muundo wa kitabu (usambamba wa kitamthiliya)
- F. Msaada zaidi
1. Watoa maoni wawili wa Ufunuo ninaowapendelea zaidi ni George Eldon Ladd na Alan F. Johnson. Hawakubaliani. Kuna kutoelewana kwingi kati ya watu wa Mungu, wasomi, wanataaluma kuwa neno la tahadhari ni muhimu. Naomba kumnukuu Alan Johnson katika kazi yake ya *Commentary on Revelation*, iliyochapishwa na Zondervan:

“Katika maoni ya utumizi wa taswira na maono kutoka Ufunuo 4:1 mpaka mwisho wa Ufunuo na namna jambo hili linavyofanana na sura 1-3, haishangazi kwamba watoa maoni wanatofautiana sana wanavyozitazama sura hizi. Tatizo moja linalojitokeza ni utafsihi. Taswira na maono humaanisha *nini*? Tatizo lingine linahusisha mpangilio wa wa nyakati. Lini mambo haya yanatukia? Zaidi sana, je Yohana anatafisi taswira zakke za Agano la Kale katika mfanano uleule wa vyanzo vyake vya Agano la Kale, au anatoa tafsihi zake huru tu kwa taswira hizi? Kipi ni ishara na kipi sio? Majibu ya maswali hayo itaamua mtazamo wa mtafisi. Kwakuwa baadhi ya maswali haya machache yana uwezekano wa kupewa majibu ya kidini, kuna umuhimu wa kuvumiliana katika kugawanyika huku kwa mitazamo ya tumaini kuwa Roho anaweza kutumia majadiliano huru ya kiakili kutufikisha mali zaidi hata katika maana za nyakati za mwisho” (ukurasa wa 69).
 2. Kwa Utangulizi wa jumla wa uhusiano wa Ufunuo na Agano la Kale, napendekeza *Prophecy Interpretend* cha John P. Milton na *The Authority of The Old Testament* cha John Bright. Kwa ajili ya mjadala mzuri wa uhusiano wa Ufunuo na Paulo, napendekeza *A Man In Christ* cha James S. Stewart.
- XI. MANENO NA VIFUNGU VYA KUTAMBUA KWA MUHTASARI
1. “vitu ambavyo havina budi kutokea,” 1:1,3
 2. “anakuja mawinguni,” 1:7
 3. Amina 1:7
 4. “Alpha na Omega,” 1:8
 5. “katika kinywa kukatoka panga mkali ukatao kuwili,” 1:16
 6. “funguo za mauti na kuzimu,” 1:18
 7. “mmeuacha upendo wenu wa kwanza,” 2:4
 8. “Yeye ashindaye,” 2:7
 9. “mti wa uzima katika Paradiso ya Mungu,” 2:7

10. "sinagogi la shetani," 2:9; 3:9
11. "kifo cha pili," 2:11
12. "vitu vya ndani vya shetani," 2:24
13. "kitabu cha uzima," 3:5
14. "ufunguo wa Daudi," 3:7
15. Yerusalemu mpya, 3:12
16. "Nalikuwa katika Roho," 4:2
17. bahari ya kioo, 4:6
18. kitabu, 5:1
19. mihuri saba, 5:1
20. "mwanakondoo amesimama kama vile amechinjwa," 5:6
21. "pembe saba na macho saba," 5:6
22. "dhiki kuu," 7:14
23. "chetezo cha dhahabu," 8:3
24. "shimo lisilo na kitako," 9:2
25. Halleluya, 19:1
26. "ndoa bora ya mwanakondoo," 19:9
27. "shinikizo la mvinyo ya gadhabu," 19:15
28. "akafungwa miaka elfu," 20:2
29. Yerusalemu mpya, 21:2
30. "nyota ig'aayo ya asubuhi," 22:16

XII. WATU WA KUTAMBUA KWA MUHTASARI

1. "akizungumza kwa Malaika Wake," 1:1
2. Yohana, 1:1
3. "roho saba," 1:4
4. mwenye nguvu, 1:8
5. anayeelezewa katika 1:12-16?
6. maelezo haya yanatoka wapi?
7. Wanikolai, 2:6,15
8. Yezebell, 2:20
9. wazee, 4:4,10
10. Simba wa kabila la Yuda, 5:5
11. "farasi mweupe, na yeye akaaye katika upinde," 6:2
12. "chini ya madhabahu nafsi za wale waliokuwa wamechinjwa," 6:9
13. "wakawekewa mihuri. . .katika mapaji ya uso," 7:3
14. "kusanyiko kubwa," 7:9
15. "nyota kutoka mbinguni," 9:1
16. "malaika mwingine mwenye nguvu," 10:1
17. "mashuhuda wawili," 11:3
18. mwanamke, 12:1
19. "joka kubwa jekundu," 12:3
20. "mtoto, mwana wa kiume," 12:5
21. "mnyama akitoka katika bahari," 13:1
22. "mnyama mwingine akitoka katika nchi," 13:11
23. Babeli, 14:8
24. kahaba mkuu, 17:1
25. "farasi mweupe, na yeye akaaye juu yake," 19:11
26. Gogu na Magogu, 20:8

XIII. MAENEO YALIYOONYESHWA KATIKA RAMANI

1. Patmo, 1:9
2. Efeso, 1:11
3. Smirna, 1:11
4. Pergamo, 1:11
5. Thiatira, 1:11
6. Sardi, 1:11
7. Filadelfia, 1:11
8. Laodikia, 1:11
9. Mlima Sayuni, 14:1

XIV. MASWALI YA MJADALA

1. Aina gani ya uwasiishaji iliyotumika katika Ufunuo? Orodhesha tabia zake.
2. Kwanini kuna makanisa saba yanayotajwa katika sura ya 2 na 3?
3. Kwanini makabila yote ya nchi yataomboleza juu Yake? (1:7)
4. Orodhesha "saba" katika sura ya 1
5. Inamaanisha nini kwamba Yesu ataiondoa taa ya kanisa? (2:5)
6. Orodhesha vitu vinavyopatikana katika ujumbe wa kila kanisa katika makanisa saba.
7. Ni yapi mazingira ya sura za 4-5?
8. Nini uhusiano wa mihuri saba, baragumu saba na vitasa saba?
9. Wakina nani wanaotajwa kama wapanda farasi wa sura ya 6? Taswira hii inatoka wapi?
10. Wanaorejerewa kama 144,000 ni watu gani? Kwanini makabila ya Kiyahudi yanatajwa kimakosa?
11. Kwanini hukumu inaongezeka kutokea 1/4 katika mihuri mpaka 1/3 katika baragumu, kukamilisha uharibifu katika vitasa?
12. Jeshi la 200,000,000 linarejerea watu gani katika 9:13-19?
13. Elezea vita mbinguni katika 12:7-10.
14. Kwanini Mungu aliruhusu mnayama kufanya vita dhidi ya watakatifu? (13:7)
15. Ni kwa namna gani mnyama anamuigiliza Kristo?
16. Ni watu gani watakuwa sehemu ya ufufuo wa kwanza? (2:4-6) Watu gani watakuwa sehemu ya ufufuo wa pili?
17. Nini umuhimu wa 22:3?
18. Ni kwa namna gani 22:5 inahusiana na 20:4?
19. Elezea 22:18-19 kwa maneno yako mwenyewe.
20. Ni nini dhamira kuu ya Ufunuo?

KIAMBATISHO CHA KWANZA

UFAFANUZI/FAHARASA

Uasilishaji. Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (cf. Rum.1:4). Yesu aliyaiishi maisha haya kama mfano ambao Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama “mwana” Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresha hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!

Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyozawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

Shule ya Alexandria. Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nyingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebicho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

Ufuasi wa Iskandria. Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lililothibitishwa, pamoja na Agano Jipya. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipya zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama “A, na machapisho ya alama “B” (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiriwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

Istiari. Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikuwa katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

Uchanganuzi wa misamiati. Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipya. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

Ushabihiano wa Maandiko. Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

Utata. Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwezekanazo au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu. Inamaanisha kuwa na “tabia zinazohusiana na wanadamu.” neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekanalo, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo

yanahusiana na wanadamu (kama vile Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

Shule ya Antiokia.Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianza huko Antiokia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiari wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Ilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Ilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu walioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

Kutabaini. Hii ni moja miongoni mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waebraia. Unahusiana na misitari ya ushairi yenye kukinzana kimaana (kama vile Mit. 10:1; 15:1).

Fasihi ya mafunuo. Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inahaidi ushindi mkuu na kupitia juhudi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenye maneno ya mafumbo. Mara nyingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nyingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1)katika Agano la Kale, Ezeieli (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

Mtetezi.Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi “ulinzi wa kisheria.” Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kifika kwa imani za Kikristo.

Haki ya kutangulia.Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno “dhanio.” Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyosadikika kuwa kweli paspo uchambuzi au chunguzi.

Ufuasi wa Arius.Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (B.K. 318) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K.walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

Jamii ya watu wakuu. Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia chunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

Miandiko binafsi. Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebraia na Kiyunani.

Maandiko ya asili ya karne ya sita. Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama “D.” Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nyingi za maandishi yenye ueledi. Inaunda msingi wa “uundaji wa maandiko”ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

Upendeleo. Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

Mamlaka ya Kibiblia. Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenyewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafsiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

Orodha ya vitabu vya Agano Jipya. Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

Kristo kama kitovu. Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

Fasiri. Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafsiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

Itifaki. Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza: (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika: (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza: (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi: (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (cf. Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

Magombo ya Bahari ya Chumvi. Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossorettes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu K.K.

Mambo yaliyofasiliwa. Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

Mbinu pembuzi. Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-mapenzi huru, ulinzi-ustahimilivu, imani-kazi; uwamuzi-ufuasi; uhuru wa Mkristo-uwajibikaji wa Mkristo

Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine. Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

Mlinganyo wa nguvu. Hii ni nadhalia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali.

Katika nadharia hizi mbili ndipo pana “mlinganyo wa nguvu” unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi vya kisasa na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth*, uk. 35 na katika Robert Bratcher’s utangulizi katika Biblia ya TEV.

Kutofuata mfumo. Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

Kupotosha maana. Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni “kuondoa” kulingana na kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha “kuingiza” wazo la kigeni.

Elimu ya asili na historia ya neno. Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

Fasili ya maandiko. Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha “uondoaji nje” (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

Namna ya Uwasilishaji. Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

Maarifa ya utambuzi/mafunuo. Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafunuo ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawezi kuhusishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika) kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (kama vile 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (kama vile 1Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihiiitajika kupitia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*eons*); au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

Kanuni za ufasili. Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

Uhakiki juu ya maandiko. Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

Nahau. Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenye maana maalumu na sio vilivyohusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: “ilikuwa ni vizuri sana” au “umeniua”. Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

Nuru.Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezwa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

Kudukiza. Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majaribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenye hadhi ya juu.

Unasaba. Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweka tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na “misamiati ya kiuchunguzi” ambayi inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

Uvuvio.Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezwa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

Lugha ya maelezo. Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hata yakamaanisha kuwepo.

Ushikiliaji sana wa sheria. Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

Tafasili sisisi. Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiokia. Ina maana kwamba utafasili unahusika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

Fasihi tanzu. Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

Sehemu ya fasihi. Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.

Maandiko ya asili. Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno “MS” (umoja) au “MSS” (wingi).

Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi. Hii inarejerea karne ya nane B.K. maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

Mshabihiano wa neno. Huu ni namna ya msembo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano “ birika linachemka” ki uhalisia inamaanisha “maji yaliyeko kwenye birika yanachemka”.

Orodha ya vitabu vya Agano jipya. Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 B.K. Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa “kiutendaji” pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

Ufunuo wa asili. Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum 2:14-15). Umeongelewa katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Umatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolijia unasisitizwa tena na mwenendo wa “dunia ya zamani” kati ya wanasayansi wa Kikristo (cf. maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kiasili. Kwa maoni yangu , hii ni fursa mpya ya ajabu kushuhudiwa juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

Ufuasi wa Nestory. Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antiokia ya Syria na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyingine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtazamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha “mama wa Mungu” alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cylil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antiokia. Antiokia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

Mwandishi wa awali. Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

Mafunjo/Magombo. Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

Vifungu Mlinganyo. Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahsusi na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapojaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

Ufafanuzi/fasili. Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa “neon kwa neon” ambapo neon la Kiingereza laweza kuweka kwa kila neon la Kiebrania au Kiyunani kwenye “fasili” ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtazamo wa kawaida wa neon au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi “mlinganyo wa nguvu” ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth, Uk. 35.*

Aya. Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhania. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

Uparokia. Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

Fumbo. Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, nab ado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

Pilato. Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohani. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha “mtizamo/mawazo” ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

Dhanio. Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenyewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

Uhakiki wa maandishi. Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

Ualimu wa dini ya Kiyahudi. Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 K.K). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii “dini ya wandishi” ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalemu mwaka wa 70 B.K. muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kiutendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoielezwa katika tamaduni za Talmud.

Ufunuo. Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemazana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3)Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

Elimu-maana. Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

Maandiko ya kale ya Kiyunani. hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 K.K. (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili na tatu K.K. (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni “LXX”.

Machapisho ya asili. Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne B.K.. Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa “*eleph*” (Ϝ). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja.

Kujitakasa. Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

Visawe. Hii inarejerea maana yenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejeshwa mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (kama vile Zab. 103:3).

Sintaksi. Hili ni neno la Kiyunani linalirejeresha muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

Usanisi. Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. Neon hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwingine katika maana moja, wakati mwingine huitwa “taaluma ya mabadiliko ya hali” (k.v. Zab 19:7-9).

Thiolojia mpangilio. Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna (Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi. Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ulitolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

Uhakiki wa tofauti za kiuandishi. Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa “uhakiki wa asili ya neno”.

Upokeaji wa Maandiko. Usanifishaji huu ulianza kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633 B.K. Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament* uk. 27 cha A.T Robertson anasema “andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkono. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 B.K.

Sheria za Musa. Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya “ufundishaji”. Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

Uanishaji. Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analojia. Namna hii ya kanuni za ufasihi ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusi ulioandikwa katika Agano jipya.

Maandiko ya Vatican. Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne B.K. Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu

zingine zilipotea(Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa “B”.

Tafasili ya Biblia ya Kilatini. Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa “kawaida” wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 A.D.

Hekima ya Fasihi. Hii ni fasihi tanzu iliyozeleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi lilikuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipya juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezwa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyongana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia. Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno “picha ya ulimwengu” inarejerea “kwa namna gani” juu ya uumbaji wakati “mtizamo wa kidunia” unahusiana na “nani.” Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

YAHWE/YEHOVA. Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linaelezwa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania “kuwa” ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani “Adonai” likimaanisha “Bwana”. Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

KIAMBATISHO CHA PILI

UHAKIKI WA TOFAUTI ZA KIUANDISHI

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.

Mhutasari ufuatao utahusika

- I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
 - A. Agano la Kale
 - B. Agano Jipya
 - II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya “maoni dhaifu” pia yanaitwa “uhakiki wa maandiko”
 - III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye
- I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale

1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na “Herufi Aristeas.” Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao “ Esene”. Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
 - a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
 - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, “Kama vile wengi watakavyo shangazwa Naye.”
 - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, “Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa Nawe.”
 - (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
 - (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, “hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye”
 - (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, “hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi”
 - b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
 - (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, “ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama.”
 - (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, “ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana.....”
 - c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
 - (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), “Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.”

- (2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), “Ataona —ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki.”

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuwika. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili B.K., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne B.K.. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania \aleph (*aleph*) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alexandrianus, kijulikanacho kama “A” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alexandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama “B” au (03), iliyopatikana katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya “Maandishi ya Kialekzandria.”
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama “C” au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama “D” au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya kwanza ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama “Maandishi ya Magharibi.” Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
 - a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
 - (1) P⁷⁵, P⁷⁶ (yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
 - (2) P⁴⁶ (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
 - (3) P⁷² (yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
 - (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
 - (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
 - (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni \aleph , C, L, W, 33
 - b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
 - (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
 - (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
 - (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsiri za kale za Kisiria
 - (4) Andiko D la Machapisho ya kale “Baze” ilifuata aina ya maandishi haya
 - c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
 - (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

- (2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
- (3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
- (4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya
- d. aina ya nne iwezekanayo ni ya “Kikaizari” kutoka Palestina
 - (1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
 - (2) baadhi ya shuhuda zake ni P⁴⁵ na W

II. Matatizo na nadharia ya “ukosoaji dhaifu.”

A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea

1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
 - a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
 - (1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
 - (2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
 - b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
 - c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
2. makusudi
 - a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
 - b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
 - c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
 - d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi (kama vile I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
 - e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili (Yohana 5:4)

B. Mafundisho muhimu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)

1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
7. nukuu mbili ambazozinzaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
 - a. kitabu cha J. Harold Greenless, *Introduction to New Testament Textual Criticism*, “Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning’inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia” (uk. 68).

- b. W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* (Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo “angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri.” Criswell alisema “Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa...Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza...” Mababa wa uzao wa SBC wasio wakoaji walidai kuwa “kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu” pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda (Mt. 27 na Matendo 1): “Ni maoni tofauti ya kujinyonga,” Criswell alisema “Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia.”Criswell aliongeza, “Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu...”

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Criticism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

KIAMBATISHO CHA TATU

MAELEZO MAFUPI YA ISTILAHU ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Mediterania ilianzishwa na Alexandra mkuu (336-323 K.K) na ikadumu mpaka miaka ya (300 K.K-500 B.K.). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

I. NJEO

- A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
 1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukuelezwa.
 2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.
- B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
 1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
 2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA
 3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA TIMILIFU
 4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
 5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
 6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- “okolewa” (Rum 8:24)
 2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPIA- “ameokolewa na matokeo yake yanaendelea” (Efe 2:5,8)
 3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (kama vile 1Kor 1:18; 15:2)
 4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (kama vile Rum 5:9,10; 10:9)
- C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
1. NJEO YA WAKATI ULIOPIA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPIA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yaliyotendeka kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
 2. NJEO YA WAKATI ULIOPIA AINISHI. Hii ilikuwa kama njee ya WAKATI ULIOPIA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
 3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
 4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njee hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPIA na WAKATI ULIOPIA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongelea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt3:5)
 5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualagini wa tukio. Mfano: “Heri wale....wata...”(Mt 5:4-9).

II IRABU

- A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
- B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
- C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
 1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (kama vile Mt 1:22; Mdo 22:30)
 2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (kama vile Mt 1:22)
 3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
 4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
- D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitiza KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika

Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” (2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

III. DHAMIRA (au “NAMNA”)

- A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI YA UCHAGUZI).
- B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna pekee ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.
- C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno “ingalikuwa”, “ingaliweza”, “yawezekana” au “yenye uwezo”.
- D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. “yawezekana isiwe” (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano (kama vile Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo 8:20 na 1Thes 3:11
- E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitiza juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.
- F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezwa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.
- G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au “kisichotambulika” cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

- A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
- B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
- C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993
- D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950

- E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

V. NOMINO

- A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyesha na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
- B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI “kuwa” au “kufaa”
 2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, “aina gani?” mara nyingi ulielezwa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza “ya/za”
 3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezwa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza “kutoka”.
 4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezwa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ya”.
 5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezwa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na”
 6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezwa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno “kwa” au “enye”
 7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali “kwa umbali gani” au “kwa namna gani”
 8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

- A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra (vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.
- B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament
1. Viunganishi vya wakati
 - (a) *epei, epedē, hopote, hōs, hote, hotan* (TEGEMEZI)- “lini”
 - (b) *heōs*- “wakati”
 - (c) *hotan, epan* (TEGEMEZI)- “kila, wakati wowote”
 - (d) *heōs, achri, mechri* (Tegemezi)- “mpaka”
 - a. *priv* (kitenzijina)- “kabla”
 - b. *hōs*- “tangu”, “lini”, “kama”.

2. Viunganishi venye mantiki
 - a. Kusudi/dhumuni
 - 1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs* (TEGEMEZI) *hōs*- “ya kwamba”, “kuwa”
 - 2) *hōste*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
 - 3) *pros*(KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
 - b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
 - (1) *hōste*(ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
 - (2) *hiva*(TEGEMEZI)- “ya kwamba”
 - (3) *ara*- “kwa kiasi hicho”
 - c. Chanzo au sababu
 - 1) *gar*(chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
 - 2) *dioṭi, hotiy*- “kwa sababu ya”
 - 3) *epei, epeidē, hōs*- “tangu”
 - 4) *dia*(ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”
 - d. Maamuzi
 - (1) *ara, painun, hōste*- “kwa hiyo”
 - (2) *dio*(KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”
 - (3) *oun*- “kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”
 - (4) *tinoun*- “kufuatana na”
 - e. –a kinyume au tofauti
 - (1) *alla*(yenye KINYUME thabiti)- “lakini”, “isipokuwa”
 - (2) *de*- “lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwingine”
 - (3) *kai*- “lakini”
 - (4) *mentoi, oun*- “ingawa”
 - (5) *plēn*- “hata hivyo” (haswa katika Luka)
 - (6) *oun*- “ingawa”
 - f. Ulinganifu
 - (1) *hōs, kathōs* (ingiza vishazi linganifu)
 - (2) *kata*(kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper*)
 - (3) *hasos*(katika Kiebrania)
 - (4) *ē*- “kuliko”
 - g. Enye mlolongo au mtiririko
 - (1) *de*- “na”, “sasa”
 - (2) *kai*- “na”
 - (3) *tei*- “na”
 - (4) *hina, oun*- “kile”
 - (5) *oun*- “kasha”(katika Yohana)
3. Matumizi yenye mkazo
 - a. *alla*- “kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”
 - b. *ara*- “hakika”, agharabu”, “kweli”
 - c. *gar*- “lakini kweli”, “agharabu”, “hakika”
 - d. *de*- “hakika”
 - e. *ean*- “hata”
 - f. *kai*- “hata”, “hakika”, “kweli”

- g. *mentoi*- “hakika”
- h. *oun*- “kweli”, “kwa hali zote”

VII.

- A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.
- B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezwa kwa neno “kama.” Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa “tangu”(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)
- C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
 1. “kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
 2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
 3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)
- D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16
- E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

VIII. VIZUIZI

- A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani.....”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu.....” (Mt 6:25); “wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi.....”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo.....”(Ef 5:18)
- B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa.....”(Mt 5:17); “msisumbuke.....”(Mt 6:31); “msiuonee haya.....”(2Tim 1:8)
- C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali yeyote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti.....”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe.....”(1Kor 8:13)

XI

- A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno “wale, Yule,ile” kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya “muonyeshwaji”, ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai.

Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda

1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
 2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
 3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: “Mungu ni Roho” Yoh 4:24, “Mungu ni nuru” 1Yoh 1:5; “Mungu ni upendo” 4:8,16
- B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;
1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
 2. Mlengo juu ya aina ya kitu
- C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

- A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.
- B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)
- C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.
 - a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
 - b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
 - c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
 2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
 - a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
 - (1) KITENZI
 - (2) KIIMA
 - (3) SIFA
 - b. VITENZI elekezi
 - (1) KITENZI
 - (2) KIIMA
 - (3) KISHAMILISHI
 - (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
 - (5) KIRAI HUSISHI
 - c. Virai vya NOMINO
 - (1) NOMINO
 - (2) KIVUMISHI
 - (3) KIRAI HUSISHI
 3. Mpangilio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:

- a. “walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika” (Gal 2:9) kirai “mkono wa kuume wa shirika” imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
 - b. Pamoja na Kristo (Gal. 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
 - c. “ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi” (Ebr. 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.
- D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na
1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: “mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe.....”(Mt 28:20)
 2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
 - a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff (ikisisitizia orodha)
 - b. Yohana 14:1 (maada mpya)
 - c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
 - d. 2Kor 12:20 (inasisitizia orodha)
 3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: “usifwe utukufu wa neema yake” (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
 4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
 - a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama “lala” kwa kifo (Yoh 11:11-14) au “nyayo” kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
 - b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama “ufalme wa mbingu” (Mt 3:21) au “sauti toka mbinguni” (Mt 3:17)
 - c. Maumbo ya hotuba
 - (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
 - (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
 - (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
 - (4) Kejeli (Gal 5:12)
 - (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
 - (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
 - (a) “kanisa”
 - i. “kanisa” (Efe 3:21)
 - ii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
 - iii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
 - (b) “huru “
 - i. “Mwanamke huru” (Gal 4:31)
 - ii. “uhuru” (Gal 5:1)
 - iii. “huru” (Gal 5:1)
 - d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
 - (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno “chakula” (Yoh 4:31-34)
 - (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno “hekalu” (Yoh 2:19; Mt 26:61)
 - (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno “chukia” (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)
 - (4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.
 5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.
 6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*

- a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”
 - b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”
- E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.
 2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neni kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)
Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
 3. Utumiaji wa *The Emphasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
 4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
 - a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
 - b. *Young’s Literal Translation of the Bible* cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti na kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasih, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.